BISMILLAHI RAHMANI RAHIIM

{مَا أَفَاءَ اللهُ عَلَى رَسُولِهِ مِنْ أَهْلِ الْقُرَى فَلِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ وَلِذِي
الْقُرْبَى وَالْيَتَامَى وَالْمَسَاكِينِ وَابْنِ السَّبِيلِ كَيْ لاَ يَكُونَ دُولَةً بَيْنَ
الأَغْنِيَاءِ مِنْكُمْ وَمَا آتَاكُمْ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانْتَهُوا
وَاتَّقُوا اللهَ إِنَّ اللهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ - لِلْفُقَرَاءِ الْمُهَاجِرِينَ الَّذِينَ أُخْرِجُوا
مِنْ دِيارِهِمْ وَأَمْوَالِهِمْ يَبْتَغُونَ فَضْلاً مِنَ اللهِ وَرِضْوَانًا وَيَنْصُرُونَ اللهَ
وَرَسُولَهُ أُوْلَئِكَ هُمْ الصَّادِقُونَ - وَالَّذِينَ تَبَوَّءُوا الدَّارَ وَالإِيمَانَ مِنْ
قَبْلِهِمْ يُحِبُّونَ مَنْ هَاجَرَ إِلَيْهِمْ وَلاَ يَجِدُونَ فِي صُدُورِهِمْ حَاجَةً مِمَّا
أُوتُوا وَيُؤْثِرُونَ عَلَى أَنْفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ وَمَنْ يُوقَ شُحَّ
نَفْسِهِ فَأُوْلَئِكَ هُمُ الْمُفْلِحُونَ - وَالَّذِينَ جَاءُوا مِنْ بَعْدِهِمْ يَقُولُونَ رَبَّنَا
اغْفِرْ لَنَا وَلإِخْوَانِنَا الَّذِينَ سَبَقُونَا بِالإِيمَانِ وَلاَ تَجْعَلْ فِي قُلُوبِنَا غِلاًّ
لِلَّذِينَ آمَنُوا رَبَّنَا إِنَّكَ رَءُوفٌ رَحِيمٌ }

*"Mali aliyoileta Allah kwa Mtume wake kutoka kwa watu wa vijiji hivi (vilivyo karibu na Madina) ni kwa ajili ya Allah na Mtume wake na jamaa zake, na mayatima na maskini na msafiri aliyeharibikiwa, ili isiwe kinyanganyiro baina ya matajiri wenu tu, na anachokupeni Mtume basi pokeeni na anachokukatazeni jiepusheni nacho, na mwogopeni Allah kwa yakini Allah ni mkali wa kuadhibu - (Basi wapewe mali hiyo) mafukara wa kimuhajiri ambao walifukuzwa katika nyumba zao (wakakhiari kuacha hayo) kwa ajili ya kutafuta fadhla za Allah na radhi yake na kuinusuru dini ya Allah na Mtume wake, basi hao ndio waislamu wa kweli - Na (pia wapewe) wale waliofanya maskani yao hapa (Madina) na wakautakasa Uislamu wao barabara kabla ya kuja (hao muhajirina) na wakawapenda hao waliohamia kwao wala hawapati (hawaoni) dhiki nyoyoni mwao kwa hayo waliopewa (hao muhajirina) na wanawapendelea kuliko nafsi zao ingawa wenyewe wa hali ndogo, na waepushwao na ubakhili na nafsi zao hao ndio wenye kufaulu kweli kweli - Na (pia wapewe) waislamu wale waliokuja baada yao wakawa (wanapendana na waislamu waliotangulia) wanasema,"mola wetu! Tusamehe sisi na ndugu zetu waliotutangulia katika uislamu wala usijaalie katika nyoyo zetu chuki juu ya waumini ewe mola wetu hakika wewe ni mpole mwenye huruma"* [TMQ: 95:7 – 10]

**<u>YALIYOMO KATIKA KITABU</u>**

**AYA YA UFUNGUZI**

**UTANGULIZI WA CHAPA YA PILI**
**UTANGULIZI**

**BAITUL MALI NA IDARA ZAKE**
**IDARA ZA BAITUL MALI**
**MWAKA WA KUWEKWA KWA IDARA**

**VIGAWANYO VYA IDARA ZA BAITUL MALI**
**KITENGO (KIGAWANYO) CHA MAPATO**
IDARA YA NGAWIRA (FAI) NA KODI YA ARDHI
IDARA YA MALI YA UMMA
IDARA YA SADAQA
**KITENGO CHA MATUMIZI**
IDARA YA NYUMBA (OFISI) YA KHILAFA
IDARA YA USIMAMIZI WA SERIKALI
IDARA YA TUNU YA SERIKALI
IDARA YA JIHADI
IDARA YA MATUMIZI YA SADAKA
IDARA YA MATUMIZI YA MALI YA UMMA
IDARA YA MAMBO YA DHARURA
**IDARA YA BAJETI JUMLA NA IDARA YA HISABU JUMLA NA IDARA YA UANGALIZI (USIMAMIZI)**

**MALI YA SERIKALI YA KHILAFA**
**MALI**
**NGAWIRA (ANFAL, GHANIIMA, FAI) NA KHUMUS**
NGAWIRA (ANFAL NA GHANIIMA)
**KIGAWANYO CHA GHANIMA, JINSI YA KUITUMIA NA WANAOSTAHILI KUPEWA**
FAI
KHUMUS

**KODI YA ARDHI (KHARAJ)**
KODI YA ARDHI ILIYOPATIKANA KWA VITA
KODI YA ARDHI ILIYOPATIKANA KWA AMANI
KUCHANGANYA KODI YA ARDHI NA ZAKA ZA USHRI
UHAKIKA WA KIVITENDO AMBAO TUNASTAHILI KUUTEKELEZA HIVI LEO
NAMNA YA KUIWEKA KODI YA ARDHI
KIWANGO CHA KODI YA ARDHI
MATUMIZI YA KODI YA ARDHI
**VIWANGO VYA UREFU, MAENEO, VIPIMO NA UZITO**
UREFU NA UPANA
UZITO NA UZANI

**KODI YA KICHWA (JIZYA)**
KWA NINI INACHUKULIWA?
NI WAKATI GANI HAICHUKULIWI?
KIWANGO CHAKE
WAKATI WA KUIKUSANYA
MATUMIZI YAKE

**MALI YA UMMA NA SAMPULI ZAKE**
SAMPULI YA KWANZA
SAMPULI YA PILI
SAMPULI YA TATU
NAMNA YA KUITUMIA MALI YA UMMA, HIMA YAKE NA MAPATO YAKE
KUKOPA KUTOKA KWA NCHI NYINGINE

**MALI YA SERIKALI ARDHI, MAJENGO MASILAHI NA MAPATO YAKE**
SAMPULI ZA MALI YAKE
MATUMIZI YAKE
MAPATO (MANUFAA) YAKE

**KODI YA USHR**
JE HUCHUKULIWA WAPI NA LINI HUCHUKULIWA?
**MALI YA (KUPORWA) INAYOPATIKANA KUTOKA KWA VIONGOZI NA WATUMISHI WA SERIKALI NA MALI ILIYOPATIKANA KINYUME CHA SHERIA NA FAINI**
RUSHWA (HONGO)
ZAWADI NA TUNU
UWAKILI NA UDALALI
MALI ILIYOPATIKANA KIMAKOSA
FAINI

**ZAKA ZA KHUMUS, MALI ILIYOZIKWA NA MADINI**
**MALI ISOKUWA NA MRITHI**
**MALI YA WALIOACHA DINI**
**KODI**

**MALI YA ZAKA**

**ZAKA**
**ZAKA YA WANYAMA**
NGAMIA
NG'OMBE
MBUZI NA KONDOO

KINACHOHISABIWA, KUCHUKULIWA NA KISICHOCHUKULIWA KATIKA ZAKA YA MBUZI NA KONDOO
HUKMU YA USHIRIKA KATIKA MBUZI NA KONDOO

**ZAKA ZA MAKULIMA**
SAMPULI YA MAZAO NA MATUNDA YANAYOPASA KUTOLEWA ZAKA
KIWANGO MAALUM (NISAAB) CHA MAZAO NA MATUNDA
WAKATI WA KUKUSANYA ZAKA YA NAFAKA NA MATUNDA
MAKADIRIO YA MATUNDA

**ZAKA YA DHAHABU NA FEDHA**
KIWANGO CHA NISAB YA FEDHA
KIWANGO CHA ZAKA KINCHOPASWA KATIKA FEDHA
KIWANGO CHA NISAB YA FEDHA NA ZAKA INAOPASWA NDANI YAKE
ZAKA KATIKA SARAFU ZA KARATASI
**ZAKA KATIKA BIDHAA ZA BISHARA**
ZAKA YA DENI
**MAPAMBO**
**KUTOA ZAKA KUMPATIA KHALIFA**
HUKMU YA MWNYE KUZUIA ZAKA
**MATUMIZI YA ZAKA**

**SARAFU**

**SARAFU KATIKA UISLAMU**
UZITO WA DINARI NA DHAHABU
**NIDHAMU YA SARAFU**
**NIDHAMU YA MAADINI**
NIDHAMU YA MAADINI MOJA
NIDHAMU YA DHAHABU NA FEDHA ILIOYAYUSHWA
NIDHAMU YA VINOA VYA DHAHABU NA FEDHA
NIDHAMU UA KUBADILISHA DHAHABU AU FEDHA
NIDHAMU YA MAADINI MBILI
**NIDHAMU YA KARATASI**
**KUCHAPA SARAFU**
MAADILI YA DHAHABU NA FEDHA
MNASABA WA WA DHAHABU KWA FEDHA
**FAIDA ZA NIDHAMU YA DHAHABU NA FEDHA**
UTOSHELEZAJI WA DHAHABU ULIOKO KATIKA ULIMWENGU
VIPI TUTAWEZA KURUDILIA KATIKA MSINGI WA DHAHABU NA FEDHA

BISMILLAHI RAHMANI RAHIM

## UTANGULIZI WA CHAPA YA PILI

Baada ya kumalizika nakala zote za chapa ya kwanza na tukapata maombi kadhaa ya kuchapa kitabu ikaonelewa kurudilia kukichapa, na hasa baada ya kutujilia maongezeo na maelezo na marekebisho ya chapa.

Na yakachunguzwa maongezeo yote hayo na maelezo na marekebisho uchunguzi wa kina na ikachukuliwa kwa jicho la kuzingatia kila kilichokua na uzito kwetu sisi, na kitabu chote kikarudiliwa upya kwa ajili ya kukirekebisha, na hadithi zilizopokelewa zikapewa uzito wa hali ya juu ili kuzidhibiti kwa mujibu wa nusus ziizopokelewa vityabu vilivyo Sahihi, na kuweka mbali hadithi yoyote humo ilio dhaifu.

Hivyo basi hii itakua ni chapa ya pili - kwa shukrani za Allah - kilichosahihishwa na kurekebishwa na kilicho na hadithi madhubuti, na tunamuomba Allah ajaalie kheri katika kitabu hiki na manufaa kwa Uislamu na waislamu na awajalie waislamu wakiweke katika nafasi ya kutabikisha na kutekeleza katika Dola la Khilafa Rashida kwa hakika yeye ni mueza juu kila anachokitaka.

Jumatano 21 Rajabu 1408 Hijria
Sawa 9 March 1988 Miladi

Muandishi

**BISMILLAHI RAHMANI RAHIIM**

# UTANGULIZI

Kwa kua Uislamu ambao Allah alimtumiliza nao Mtume wake Muhammad (saw) kua ndio nidhamu ya maisha na ujumbe wa ulimwengu, hivyo basi imekua hamna budi kuwepo kwa Dola itakaoutabikisha na kuubeba katika ulimwengu, na Uislamu ikaifanya Dola hiyo ni (Dola la Khilafa) na kuifanya kuwa na muundo spesheli na umbile la kipekee inaotafautiana na miundo ya dola zote katika ulimwengu: katika nguzo ambazo inasimama juu yake, na viungo ambavyo inaojengwa nayo na katiba yake na kanuni zake zinazochukuliwa kutoka katika Kitabu na Sunnah za Mtume wake (saw) ambazo ni wajibu juu ya khalifa na Ummah kushikamana nazo na kuzitabikisha na kujifunga na ahkamu zake kwa sababu ni sharia za Allah na wala si tungo za wanadamu. Na Uislamu ukategemezea juu ya Dola kusimamia mambo ya watu na kutegemezea kwayo kusimamia mapato ya mali inaokuja kwa Dola na matumizi yake ili iweze kupatikanwa usimamizi na kubeba ujumbe, na dalili za kisharia zikabainisha mapato ya Dola ya kimali na sampuli zake na namna ya kuzipata na vile vile ikabainisha wanaoistahiki na upande wa matumizi yake.

Na katika Kitabu hiki tumefafanua mali katika Dola la khilafa na ahkamu zake na tukaelezea mapato yake na sampuli zake na sababu za kuchukuliwa kwake na huchukuliwa kutoka kwa kina nani na wakati wa kustahiki kwake na namna ya kuipata na namna ya kumilikiwa na kuhifadhiwa na pia tukafafanua wanaoistahiki na na njia ya matumizi yake.

Na kwa kua udhibiti wa hizi mali na kuzipata inalazimu kujua urefu na mapana na uzito na uzani pia tukaelezea yanaolazimu hayo ili iweze kuwa wazi vilivyo kwa sura ambayo inaofafanua hali yake halisi na kuondosha ujinga katika hayo, na pia tumelinganisha kwa urefu na mapana na vipimo na uzani inaotumika leo hii ili iweze kuwa sahali kuchukua mbali na utata karibu kufahamika.

Na kwa kua upande wa sarafu pia ina umuhimu maalum katika mali ya Dola la khilafa kwa kufungamana kwake na ahkamu za kisheria pia tumeelezea na kufafanua hali halisi yake na msingi inaosimama juu yake na kutu kinachonasibishwa nacho na uzito wake na matatizo yanaoikumba na namna kutatua matatizo hayo.

Na hukmu za mali katika Dola la khilafa zimechukuliwa kutoka katika Kitabu na Sunnah, na baada ya uangalifu na kudadisi maneno ya maswahaba na Tabiina na Tabiina wao na maneno ya maimamu na mujtahidia katika haya, kwa msingi wa kile kilichokua na uzito kwetu sisi kupitia dalili huku tukizingatia kua hukmu za kisheria huchukuliwa kua isio na dhana na wala sio lazima kukatikiwa na yakini kama vile ambavyo ni sharti katika Aqeeda.

Twamuomba Allah atukamilishie na kutusahalishia kuweka katika utabikishaji na utekelezaji katika Dola la khilafa nae ndie Mola wetu Mola mwema alioje na msaidizi mwema alioje.

16 Rabiuthani 1402 Hijri
10 February 1982 Miladi

Muandishi

**<u>BAITUL-MAAL NA USAJILI WAKE</u>**

**<u>BAITUL-MAAL</u>**

Baitul-maal ni muelekeo ambao ni hasa kwa kila kinachoingia katika Dola au kinachotoka humo katika mali wanaoyasahiki waislamu, hivyo basi kila mali iwe ni ardhi au jengo au mgodi au sarafu au bidhaa wanaoistahiki waislamu kwa mujibu wa ahkamu za kisheria na wala haikufafanua mtu mwenye kuimiliki hata kama imefafanua muelekeo wake hiyo basi ni haki ya waislamu iwe itaingia katika milki wa Baitu-maal au isiingie. Na kila mali inaopaswa kutumika juu wa wanaoistahiki

na watu wake au juu ya masilahi ya waislamu na kusimamia mambo yao au katika kubebe ujumbe basi hiyo ni haki ya Baitul-maal iwe itatumika kivitendo au isitumike, hivyo basi Baitul-maal kwa maana hii ni muelekeo.

Na Baitul-maal huitwa na kukusudiwa sehemu ambayo huwekwa humo na kutumiwa kutoka humo mali ambayo ni miongoni mwa mapato ya Dola.

Na kusimaishwa kwa kwanza kwa baitul-maal kwa maana ya muelekeo ilipatikanwa baada ya kushuka kwa kauli yake Ta'ala:
**{ يَسْأَلُونَكَ عَنْ الأَنْفَالِ قُلْ الأَنْفَالُ لِلهِ وَالرَّسُولِ فَاتَّقُوا اللهَ وَأَصْلِحُوا ذَاتَ بَيْنِكُمْ وَأَطِيعُوا اللهَ وَرَسُولَهُ إِنْ كُنتُمْ مُؤْمِنِينَ }**
*"Wanakuuliza juu ya mali yaliotekwa (ngawira; yagaiwe vipi?) sema mali yaliotekwa ni ya Allah na Mtume, basi muogopeni Allah na suluhisheni mambo baina yenu na mtiini Allah na Mtume wake iwapo nyinyi ni waumuini"* [TMQ:8: 1] katika Badr, baada ya kumalizika kwa vita, na wakatafautiana juu ya ngawira. Imepokewa kutoka kwa Said bin Jubeir amesema: "Nilimuuliza Ibn Abbas: Suratul Anfaal, akasema ilishuka Badr" Hivyo basi ngawira ya Badr ndio mali ya kwanza ilipatikanwa baada ya ngawira ya msafara wa Abdallah bin Jahsh, Alah akabainisha hukmu ya kuigawa na akaifanya ni haki ya waislamu na akamfanya Mtume (saw) kua ni mwenye kuisarifu vile anavyonelea kua ina masilahi kwa waislamu, hivyo basi ikawa ni haki ya baitul-maal na kiongozi wao ataisarifu katika yale ambayo yatakua ni yenye kuhakikisha masilahi yao.

Ama baitul-maal kwa maana ya sehemu ambayo huwekwa humo mali inaopatikanwa na kutoka humo hutumiwa mali inaotoka, sehemu hiyo maalum haikupatikanwa katika zama za Mtume (saw) kwani mali iliokua inapatikanwa haikua nyingi na wala kinachogawanywa hakikua kinatosheleza waislamu, na kilikua kinatumia katika kuyasimamia mambo yao. Na Mtume (saw) alikua anagawa ngawira na mafungu matano baada ya kumalizika vita na wala hakua anachelewesha ugawaji wa mali

au kuitumia mwa muelekeo wake. Ikapokewa na Handhala bin Sayfi - na alikua ni Muandishi wa Mtume (saw) - amesema: "Mtume (saw) aliniambia Kuwa nami na unikumbushe juu ya kila kitu katika siku yake ya tatu, akasema: ikawa hamna mali au chakula isipokua humkumbusha katika siku ya tatu, na ikawa halali Mtume (saw) huku akiwa hana kitu, na mara nyingi alikua anaigawa mali katika siku hiyo hiyo, imepokewa kutoka kwa Hassan bin Muhammad "Kua Mtume (saw) hakua anaizuia mali kwake wala kuilaza" yaani ikimjilia asubuhi basi haitafika mchana isipokua ameshaigawa na ikimjilia jioni basi hakua anailaza mali kwake, hivyo basi haikua mali inawekwa kiasi cha kuhitajia mahala au usajili.

Na hali ikaendela kuwa hivyo katika muda wote wa siku za Mtume (saw) na pindi alipotawazwa Abubakar hali ikaendelea kuwa hivyo katika mwaka wa kwanza wa khilafa yake, alikua anapopokea mali kutoka katika baadhi ya maeneo alikua anaileta katika msikiti wa Mtume (saw) na kuigawa kwa wanaoistahiki, na alikua amemtua Aba Ubeida bin Jarrah kama mwakilishi wake katika hilo, kwani Abu Ubeida alimuambia wakati wa kuteuliwa kwake: "Mimi nitakutosheleza katika mali" japo katika mwaka wa pili wa khilafa yake alianzisha viini vya baitul-maal na akatenga sehemu maalum katika nyumba yake na akawa anaweka kila mali inaoingia ndani ya Madina, na alikua anaitumia yote juu ya waislamu na masilahi yao, na wakti alipokufa Abubakar na Umar kutawala aliwakusanya wadhamini na akaingia katika nyumba ya Abubakar na akaifungua baitul-maal na hakupata humo isipokua dinari moja iliokua imeanguka kutoka katika gunia, na pindi futahi zilipokithiri katika zama za Umar na waislamu wakafungua ardhi ya Kisra na Kaisari na mali kuongezeka na ikamiminwa ndani ya Madina hapo Umar akaiwekea nyumba maalum na akaiwekea wasajili na kuiwekea makatibu na akawawekea mishahara na akaweka wanajeshi japo mara nyengine alikua anaweka fungu la tano la ngawira katika msikiti na kuligawa pasina kuchelewa, Imepokewa kutoka kwa ibn Abbas amesema:

"Umar aliniita na nikitahmaki nikaona mbele yake tambara juu yake lina dhahabu zimetawanyika mfano wa majani makavu, akasema: njoo tuigawe kati ya jamaa zako, kwani Allah ndie muelewa zaidi ni kwa nini aliizua kwa Mtume wake (saw) na Abubakar na akanipatia mimi, sijui amekusudia kheri au shari kwa hilo" Na imepokewa kutoka kwa Abdurrahman bin Auf amesema: "Umar aliitisha wakati wa adhuhuri na nikamuendea na nikaingia ndani ya nyumba na akaushika mkono wangu kisha akaniingiza ndani ya nyumba nikitahmaki nikakuta mifuko moja juu ya mwengine, akasema: hapa ndio jamii ya Al-Khattab imekua nyonge mbele ya Allah, naapa na Allah lau kama ni kapata utukufu kwa Allah jambo hili lingepewa masahibu zangu wawili mbele yangu ili iwe ni kielelezo kwangu katika jambo hili, akasema Abdurrahman: nilipoona aliokuja nayo nikasema: kaa ewe amirul-muminina ili tufukirie, akasema: tukaketi na tukawaandika watu wa Madina na kutawaandika wapiganaji katika njia ya Allah na tukawaandika wake za Mtume (saw) na tukawaandika wengine".

Hivyo basi waislamu wakawa na baitul-maal ambayo ndani yake hukusanywa mali na kuhifadhiwa na kusajiliwa, na kutoka humo inatoka mishahara na mali kupewa wanaoistahiki.

## DIWAN YA BAITUL-MAAL

Usajili (Dawawin) hiutwa na kukusudiwa sehemu inaokua ni mahali pa kuketi waandishi na kuhifadhi usajili na pia hukusudiwa usajili wenyewe na hupatikanwa kuweka maana mbili pamoja.

## KUBUNIWA KWA DIWAN YA KWANZA

Kuanzishwa kwa usajili wa kwanza na kupawekea sehemu maalum itakaohifadhiwa humo ilikua ni katika zama za Umar bin Al-Khattab mwaka wa (20) wa Hijria, ama katika siku za Mtume (saw) hapakuwa na usajili wa kuhifadhiwa japo Mtume (saw) alikua ameweka waandishi watakaoandika mali, kwani alikua amemteua Muaiqiib bin Abi Fatima Ad-Dawsiy kama

Muandishi wa ngawira, na Zubeir bin Al-Awaam Muandishi wa zaka, na Hudheifah bin Al-Yaman juu ya mazao ya Hijaz, na Abdallah bin Rawaha juu ya mazao ya Khaibar, na Mughira bin Shuubah Muandishi wa kukopeshana na muamalat, na Abdallah bin Arqam muadishi wa watu kwa makabila yao na maji yao, pamoja na hayo haikuwekewa usajili na wala haikutengewa sahamu maalum ya kuhifadhi na kuandika, na hali ikaendelea hivyo katika zama za khilafa ya Abubakar isipokua mambo yalibadilika baada ya kutawala kwa Umar na kuongezeka kwa futahi ambayo ikapalekea mali kuingia kwa uwingi Madina na kupelekea kuweka usajili, na madaftari ya kusajili na kutenga sehemu maalum, ya kuhifadhi ya kuziandika.

Na imepokewa kua sababu hasa ya kufikiria kuanzisha usajili ni kua Abu Hureirah alikuja na mali nyingi kwa Umar bin Al-Khattab kutoka Bahrain, na Umar akamuuliza umeleta nini? Akasema: nimeleta dirhamu laki tano, Umar akasema: wajua unasema jini? Wewe umechoka, nenda ukapumzike hadi kupambazuke, na alipojilia asubuhi siku ya pili, akamuambia: ni ngapi? Abu Hureirah akasema: dirhamu laki tano, Umar akasema: jee ni ya halili? Abu Hureireh akasema: sijui lolote ila hilo, hapo Umar akapanda Mimbar, na akamhimidi Allah na akamsifu, kisha akasema: enyi watu tumejiliwa na mali nyingi iwapo mwataka tatawapimia nyinyi kipimo, na ikiwa mwataka tutawahisabia, akasema mtu katika watu: ewe amirul-muminina wasajili watu na kuandika inachowapatia, na anasema Al-Waqidiy kua Umar bin Al-Khattab aliwashauri waislamu kuhusu kuweka usajili, ndiposa Ali akuamuambia: "Kila mwaka gawanya mali inaokujilia na wala usizuie chochote" na akasema Uthman: "Naona mali nyingi inaowafuata watu na ikiwa hawatahifadhiwa ili iweze kujuikanwa aliechukua na ambae hajachukua basi huenda mambo yakaharibika" hapoa akasema Wali bin Hisham Al-Mughira: "Mimi nilikua Sham na nikawaona wafalume wake wameweka usajili na kuweka wanajeshi, ndiposa Umar akayachukua maneno yake na

akamuita Aqil bin Abi Twalib na Makhramahbin Naufal na Jubeir bin Muti'im na walikua na nasaba ya kiqureshi, na akasema: waandikeni watu kwa majumba yao, na muanze na Banu Hashim na muwaandike na badae mufuatilizie na Abubakar na watu wake na badae Umar na watu wake na wakaandika makabila na wakampelekea Umar na alipoangalia humo alisema: sikupendelea iwe hivyo lakini anzeni na familia ya Mtume (saw) wakaribu awe karibu zaid mpaka mumweke Umar pale alipowekwa na Allah.

Hivi ndivyo ilivyo suala la usajili wa kupeana na uwanajeshi, na ilikua imeandikwa kwa kiarabu, ama usajili wa kulipa na ukusanyaji wa mali, hali humo ilikua tafauti na hivyo, kwani usajili wa Iraq ilikua imeandikwa kwa kifursi kama ilivyokua ikiandikwa wakati wa dola la kifursi, na vile vile usajili wa miji iliosalia ambyo ilikua chini ya utawala wa kifursi kwani usajili wa kulipa Kharaji yake na Jizya yake na ukusanyaji wa mali yake imeandikwa kwa kifursi. Ama Sham na sehemu ambazo zilizokua chini ya warumi usajili wake wa malipo ya Kharaji yake na Jizya yake na ukusanyaji wali yake ilikua kwa kirumi kama vile ilivyokua hali yake katika zama za utawala wa warumi. Na hali ya Iraq na Sham ikabakia kuwa hivyo kutoka katika zama za Umar bin Al-Khattab hadi katika zama za Abdul-Malik bin Marwan Al-Umawiy hapo usajili wa Sham ukageuzwa na kufanywa kwa kiarabu mwaka wa 81 Hijria.

Ikaelezewa kua kilichomfanya Abdul-Malik bin Marwan kuigeuza kutoka kwa kirumi na kuifanya kwa kiarabu ni kua Muandishi wa usajili wa kirumi alitaka maji katika kichupa chake cha wino, na badali ya kuweka maji alikitia mikojo ndani yake na badae hayo yakamfikia Abdul-Malik ndiposa akamtia adabu na akamuamuru Salman bin Sa'ad abadilishe usajili na kuifanya kwa kiarabu, na akamuomba amsaidie kwa Kharaji ya Jordan mwaka na akafanya hivyo na akampa usimamizi juu ya Jordan na Kharaji yake ilikua dirhamu laki moja elfu thamanini (180,000), na wala haikupita mwaka hatimae Suleiman

ameshamaliza kugeuza usajili, na akaja nayo kwa Abdul-Malik bin Marwan na akamuita Muandishi wake Sarjun na akamuonyesha na akashangaa hapo akatoka kwake huku akiwa na huzuni na akakutana na waandishi wa kirumi na akawaambia: tafuteni maisha kwa kazi isokua hiyo kwa Allah ameshawakatia.

Ama usajili wa Iraq Hajjaj ambae ni Wali wa Abdul-Malik juu ya Iraq alimuanrisha Muandishi wake Swaleh bin Abdurrahman aibadilishe kutoka kifurisi na kuifanya kwa kiarabu na Swale alikua anazijua vilivyo lugha mbili, ndiposa Swaleh akamkubalia hilo, na akammpa muda hatimae akaigeuza ni kuifanya kwa kiarabu na alipoyajua hayo muandishi wa Hajjaj wa kifursi, Muradnashah ibnu Zadan Faroukh alijaribu kuataka kumhonga Swaleh dirhamu kali moja ili aonyeshe uajizi wake lakuni hakufanya, na akamuambia: Allah akuvunje vunje duniani kama vile ulivyoikata asili ya kifursi.

## VIGAWANYIKO VYA DIWAN YA BAITUL-MAAL

Diwan ya baitul-maal husimama juu ya vigawanyiko viwili muhimu, kigawanyiko cha kwanza: inahusiana na mali inaoingia ndani ya baitul-maal, na mali yake inaostahiki. Na kigawanyo cha pili: inahusiana na mali inaotumika, na waostahiki mali.

## KIGAWANYO CHA MAPATO.

Ama kigawanyo cha kwanza hii inakusanya usajili wa yanaokuja ikifuata aina ya mali.

## DIWAN YA FAI NA KHARAJI

Nayo ni diwan ambayo inakua ndio sehemu ya kuhifadhi madaftari ya mapato ya Dola na usajili wake ambao unazingatiwa kuwa ni Fai ya waislamu wote, vile vile mapato ya Ushuru ambao huenda ukawapasa waislamu katika hali ya uhaba wa mapato ya baitul-maal ili kukimu yale ambayo ni

wajibu juu ya baitul-maal kuyasiamamia, hii ikiwa ni katika matumizi ya wajibu kwa sura ya badali, au ni wajibu kwa sura ya masilahi na sikitiko pasina badali. Mali inaopatikanwa aina hii hutengewa sehemu maalum na usajili katika baitul-maal, wala haichanganywi na mali nyengine yoyote kwa sababu mali hiyo matumizi yake inakua ni ya kusimamia mambo ya waislamu na katika masilahi yao kwa mujibu wa rai ya khalifa na ijitihadi yake.

Idara ya usajili wa Fai na Kharaji inabuniwa kulingana na mapato yanaopatikanwa na mali ianostahiki, nayo ni:

1 - Idara ya ngawira: Na inajumuisha Ngawira na Anfaal na Fai na Khums
2 - Idara ya Kharaji
3 - Idara ya ardhi: Na inajumuisha ardhi za kimabavu na za Ushri na Swawafi na milki ya Dola na ardhi za milki ya jumuia na ardhi za Hima.
4 - Idara ya Jizya
5 - Idara ya Fai na inajumuisha usajili wa mapato ya Swawafi na Ushuru na Khums ya Rikaz na maadini na ardhi au nyumba ya Dola inaouuzwa au kukodishwa au Swawafi na mali isio na mrithi.
6 - Idara ya Ushuru

**<u>DIWAN YA MILKI YA JUMUIA</u>**

Ni usajili ambao inakua ni sehemu ya kuhifadhi mali za milki ya jumuia na kuisajili kiutafiti na kiuchunguzi na kuichimba na kuitafutia soko na kimapato na kimatumizi. Na mali ya milki ya jumuia hutengewa sehemu maalum ndani ya baitul-maal na wala haichanganywi na nyengine, kwa sababu ni milki ya waislamu wote, Khaliaf ataitumia kulingana vile anaona kua ni masilahi kwa waislamu kwa mujibu wa rai yake na ijtihadi yake ndani na mipaka ya ahkamu za sharia.

Idara za usajili wa milki ya jumuia zinakua kwa mujibu wa mali ya milki hizi na yale yanaolazimu ni yafuatayo:

1 - Idara ya mafuta na gasi
2 - Idara ya umeme
3 - Idara ya maadini
4 - Idara ya bahari na mito na maziwa na chemichemi
5 - Idara ya Hima/Hifadhi

## DIWAN YA ZAKA/SADAKA

Nayo ni Usajili wa zaka ambao ni sehemu ya kuhifadhi na kusajili mali ya zaka ambayo ni faradhi.

Idara za zaka zinakua kwa mujibu wa aina ya mali ya zaka iliowajibu, nayo:

1 - Idara ya zaka ya sarafu na bidhaa za biashara
2 - Idara ya zaka ya mimea na matunda
3 - Idara ya zaka ya ngamia ngombe na mbuzi/ kondoo

Na mali ya zka hutengewa sehemu maalum ndani ya baitul-maal na wala haichanganywi na mali nyengine yoyote, kwa sababu Allah Ta'ala ameshakwisha kuwafunga wanaoistahiki kwa mafungu manane yaliokuja katika kauli yake:

**{ إِنَّمَا الصَّدَقَاتُ لِلْفُقَرَاءِ وَالْمَسَاكِينِ وَالْعَامِلِينَ عَلَيْهَا وَالْمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمْ وَفِي الرِّقَابِ وَالْغَارِمِينَ وَفِي سَبِيلِ اللهِ وَابْنِ السَّبِيلِ }**

*"Hakika zaka ni ya mafukara na masikini na wenye kuitumikia na wenye kulainishwa mioyo yao na katika kukomboa watumwa na wenye madeni na katika njia ya Allah na aliyeharibikiwa na safari"[*TMQ:]na wala haifai kupewa mwengine asiekuwa katika hawa.

## KIGAWANYO CHA MATUMIZI

Hii ni kuhusiana na kigawanyo cha kwanza katika usajili wa baitul-maal, ama kigawanyo cha pili ambacho ni kwa mujibu wa namna ya matumizi na mali ianostahiki juu ya baitul-maal

inajumuisha matumizi ya usajili na Idara na namna zinazostahiki ni ifuatavyo:

**DIWAN YA NYUMBA YA KHILAFA**

Na inajumuisha:
1 - Nyumba ya khilafa
2 - Afisi ya washauri
3 - Afisi ya Muawin Tafwidh
4 - Afisi ya Muawin Tanfidh

**DIWAN YA MASILAHI YA DOLA**

Na inajumuisha:
1 - Idara ya Amiri wa Jihad
2 - Idara ya mawali
3 - Idara ya makadhi
4 - Idara ya masilahi ya Dola na Idara na afisi za Ummah zinazohusiana na hayo.

**DIWAN YA KUTUNUKU**

Ni sehemu ya kusajili yoyote yule anaona khalifa kumpatia katika mafukara na masikini na wenye mahitaji na wenye madeni na walioharibikiwa na safari na wakulima na wenye viwanda na wengineo, na yoyote yule anaeona khalifa kua ni masilahi kwa waislamu katika kumpatia, na hutumiwa juu ya usajili hizi tatu mapato ya usajili wa Fai na Kharaji.

**DIWAN YA JIHAD**

Na inajumuisha:
1 - Usajili wa jeshi, katika kulibuni na muundo wake na vifaa vyake na mafunzo yake.
2 - Idara ya silaha
3 - Idara ya viwanda vya silaha

Na diwan hutumiwa juu yake mapato ya diwan zote za kigawanyo cha kwanza, hivyo basi hutumiwa mapato kutoka Fai na Kharaji kwa sababu ni katika yale yanaostahiki juu ya

baitul-maal kwa badali, na pasina badali, vile vile hutumiwa juu yake mapato ya diwan ya zaka kwa sababu ni katika mafungu manane yaliokuja katika aya:

**{ إِنَّمَا الصَّدَقَاتُ لِلْفُقَرَاءِ وَالْمَسَاكِينِ وَالْعَامِلِينَ عَلَيْهَا وَالْمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمْ وَفِي الرِّقَابِ وَالْغَارِمِينَ وَفِي سَبِيلِ اللهِ وَابْنِ السَّبِيل }**

*"Hakika zaka ni ya mafukara na masikini na wenye kuitumikia na wenye kulainishwa mioyo yao na katika kukomboa watumwa na wenye madeni na katika njia ya Allah na aliyeharibikiwa na safari"[*TMQ:]

## DIWAN YA MATUMIZI YA ZAKA

Hutumiwa mapato ya diwan ya zaka katika hali ya kuwepo.

## DIWAN YA MATUMIZI YA MILKI YA JUMUIA

Hutumiwa mapato ya diwan ya milki ya jumuia vile anavyoonelea khalifa kwa mujibu wa ahkamu za sharia.

## DIWAN YA MAAFA

Hutumiwa juu ya kila janga linalowafika waislamu katika matukio ya ghafula, kama mitetemeko na tufani na ukame na mifano yake, na diwan ya maafa hutumiwa juu yake mapato ya diwan ya Fai na Kharaji na mapato ya diwan ya milki ya jumuia, na ikiwa hamna mali katika mbili hizi hutumiwa mali ya waislamu juu yake.

## DIWAN YA BAJETI JUMLA DIWAN YA UHASIBU JUMLA NA DIWAN YA UCHUNGUZI

Ama diwan ya bajeti jumla hiyo ni diwan inaosimamia utayarishaji wa bajeti ya Dola ya siku za mbeleni kwa mujibu wa vile anavyoona khalifa, kuanzia kukadiria mapato ya Dola na matumizi ya mali yake na kulinganisha na mapato na matumizi jumla ya kivitendo kulinganishwa na bajeti hiyo, na kufuatilizia mapato ya Dola na matumizi yake kivitendo, na diwan hii itakua chini ya nyumba ya khilafa.

Ama diwan ya uhasibu jumla, ni diwan ambao inadhibiti mali ya Dola ya yaani kuhisabu akiba yake matakwa yake na yaliokamiishwa nayo na yale yanaostahiki.

Ama diwan ya ufuatiliziaji ni diwan ambayo itasimamia kurudia na kuchunga maelezo ya uhasibu wa mali ya Dola na masilahi yake, na kuhakikisha kilichoko na ukweli ya kuwepo kwake na matakwa na mapato na matumizi na kuwahisabu wahusika katika kukusanya na kupokea na kutumia mali hizo vile vile itakuwa inatekeleza ufuatiliziaji na kuzihisabu diwan zote na Idara za Dola na watumishi wake na katika masuala ya kiidara.

Hizi ndizo diwan za mali ya Dola la Khilafa kwa sura ya kijumla, ama dalili ya kusimamishwa kwake ni mbinu miongoni mwa mbinu za Idara, na njia miongoni mwa njia za kutekeleza kazi, na Mtume (saw) alisimamia idara yeye mwenyewe na akaziwekea waandishi, iwe ni katika inaohusiana na mali na nyengineo, na tumekiwisha tangulia kuelezea katika mlango (mwanzo wa kuweka diwan) wale walioteuliwa na Mtume (saw) kama waandishi katika upande wa mali. Juu ya hayo aya na hadithi zilizokuja kuruhusu (mubah) Anfaal na Ghanima na Fai na Jizya na Kharaji na kuifanya ni yenye kuwastahiki waislamu kutoka kwa makafiri, na aya na hadithi ambazo ni dalili ya uwajibu wa zaka na wanaofaa kupewa na ambazo ni dalili juu ya milki jumla zaonyesha wazi ulazima kua ni ruhusa (mubah) kuweka mbinu za kiidara ambazo kutatumika kuchukua na kuandika na kuhifadhi na kutumia mali hizo, kwa sababu mbinu hizi ni mitagaa katika mzizi hivyo basi inakua ni ndani yake, na inakua ni katika yalioruhusiwa (mubah), hivo basi khalifa anaweza kutumia na kuzitabanni ile anaoonelea kutumia katika kukusanya mali hizi na kuzidhibiti na kuzihifadhi na kuzigawa, na ikapatikanwa kuweka Diwan na zikatabanniwa katika zama za makhalifa waongofu huku maswahaba wakiona na kusikia na wala hakuna miongoni mwao aliepinga.

## MALI YA DOLA LA KHILAFA

## MALI

Mali ya kwanza walioiteka waislamu - baada ya Allah kuwaruhusu wao kupigana baada ya Mtume (saw) kuguria Madina na kujenga msikiti wake na akaanza kujenga Dola la kiislamu jiwe baada ya jiwe - na ghanima ya kikosi cha Abdallah bin Jahsh, na baadhi za ngamia za maqureshi zilikua zimebebeshwa ngozi na biashara, ilipatikanwa katika mwezi wa Jamadul Akhira katika mwaka wa pili wa Hijra, na katika mwezi wa Ramadhani mwaka huo huo vikazuka vita vya Badr hapo wailsmu wakapata ngawira mali na silaha, na wakatafautiana katika kuigawanya kwake ndiposa Allah Akaiteremsha Suratul Anfaal na akateremsha ndani yake kauli yake Ta'ala:

**{ يَسْأَلُونَكَ عَنِ الأَنْفَالِ قُلِ الأَنْفَالُ للهِ وَالْرَسُولِ }**

*"Wanakuuliza kuhusu anfal waambie anfal ni ya Allah na Mtume"* (TMQ: 8:1) na Allah akaifanya kuigawa kwake ni kwa Mtume (saw) na akaigawa pasina kuigawa mafungu matano, kisha waislamu wakapata ngawira mali ya mayahudi wa banu Qainuqa'a pale walipovunja ahadi, na Mtume (saw) akawafukuza hadi Adhra'at Sham, na hii ilikua ni mwezi mmoja baada ya Badr na Mtume (saw) akaigawa mafungu matano kulingana na aya ya ngawira ambayo ilikua imeshuka baada ya Badr:

**{ وعلموا أنما غنمتم من شيء فَأن لله خمسه وللرَسُوْلِ وَلِذي القُربَى وَاليَتامَى وَالمَساكِين وابن السبيل }**

*"Na jueni kua ngawira yoyote munaoipata basi sehemu yake ya tano ni ya Allah na Mtume na jamaa zake na mayatima na masikini*" [TMQ: 8: 41]

Na ardhi ya kwanza aliyoifunguwa Mtume (saw) ni ardhi ya banu Nadhir, baada ya kwenda kinyume na ahadi, kutokamana na ayhari ya vita vya Uhud, na akawazingira kwa muda wa masiku kumi na tano na baadae akakubaliana na wao kwa sharti watoke Madina na watachukua kile tu

kitakachowezekanwa kubebwa na ngamia isipokua vifaa na silaha zote, hapo Mtume (saw) akagawa mali yao isipokua ardhi kwa waliogura wa kwanza pasina Answaar isipokua Sahl bin Hanif na Abu Dujana Samak bin Kharshah kwani wao walielezea kuhusu ufukara wao ndiposa akawapatia, na akazizuia ardhi na ikawa anawatumilia familia yake kutokamana nazo matumizi ya mwaka na inaobaki anaiweka katika kununua wanyama na silaha kama maandalizi kwa ajili ya Jihad, na katika vita hivi ikashuka Suratul Hashr na ikashuka kauli yake Ta'ala:

**وَمَا أَفَاءَ اللهُ عَلَى رَسُولِهِ مِنْهُمْ فَمَا أَوْجَفْتُمْ عَلَيْهِ مِنْ خَيْلٍ وَلاَ رِكَابٍ وَلَكِنَّ اللهَ يُسَلِّطُ رُسُلَهُ عَلَى مَنْ يَشَاءُ وَاللهُ عَلَى كُلِّ شَيْءٍ قَدِيرٌ**

*"Na mali alioyoileta Allah kwa Mtume wake kutoka kwao pasina kutoa farasi wa vipando lakini Allah anapatia nguvu Mtume wake juu ya yoyote amtakae na Allah ni mweza juu ya kila kitu"* [TMQ: 59:6] hivyo basi akaifanya ni spesheli kwa Mtume. Kisha vikaja vita vya banu Quraidha baada ya kuvunja ahadi na kuwafanyia khiyana waislamuna wakaungana na makundi katika vita vya Khandaq, na Mtume (saw) akagawa mali yao kwa waislamu na kupeana kwa mwenye farasi mafungu matatu na fungu moja kwa mwenye miguu, kisha vikaja vita vya Khaibar baada ya Mtume (saw) kufunga mkataba wa kusitisha vita pamoja na maqureshi katika Hudeibiya, na Allah akamapa ushindi Mtume wake na waumini kimabavu na kuwamilikisha ardhi zao majumba yao na mali yao, akaigawa ngawira na ardhi baada ya kugawa mafungu matano, na akazifanya ardhi kuwa vigawanyo alfu moja na mia nane, ziligawanywa mafungu kumi na nane kila fungu lina hisa mia moja, kisha, kisha akakubaliana na wenyewe juu ya nusu ya mazao yanaopatikanwa ya matunda na nafaka. Na baada ya futahi ya Khaibar wakaja watu wa Fadak na wakafanya suluhu na Mtume (saw) kwa sharti kua yeye atachukua nusu ya ardhi zao na mitende yao kwayo ataamiliana nao na wao watapata nusu nyengine, hivyo basi nusu ya Fadak ilikua ni spesheli ya Mtume (saw) kwa sababu aliipata pasina farasi na vipando, na sehemu ya kinachopatikanwa alikua anakitumia katika zaka. Vile vile

akafanya suluhu na watu wa Wadil-Quraa baada ya kuufungua mji wao kimabavu kwa sharti ya kua waziwache ardhi zao katika mikono yao mfano wa vile alivyokubaliana na watu wa Khaibar, ama Timaa wao walifanya suluhu na Mtume (saw) juu ya kua watampatia yeye Jizya na kua biladi yao na ardhi zao ni yao.

Na baada ya futahi ya Makka vikaja vita vya Hunein na Mtume (saw) akaigawa mali yao na akawasamehe mateka wao wakiwemo wanawake wao na watoto wao pale alipojiliwa na ujumbe wa Hawazin na kumuomba hilo, na Tabuk Yahna bin Ru'ba mwnye Al-Aqabah akafanya suluhu – alikua ni mnasara – kwa sharti ya kua watowe Jizya kama vile watu wa Adhraj na Jarbaa na Maqna – na wao walikua mayahudi- kwa sharti ya kuwa watowe Jizya, pia Akaydar mwenye Daumatul-Jandal mnasara alifanya suluhu kwa sharti atowe Jizya baada ya kusamehewa pale alipochukuliwa mateka na Khalid.

Kisha wakaja wajumbe wa Najran na Yaman na yule aliesilimu miongoni mwao alifaradhishiwa atowe zaka na yule alibakia katika unasara wake au uyahudi wake alifaradhishiwa atowe Jizya na aya ya Jizya ilikua imekwisha teremka na zaka imeshafaradhishwa na wakati wa vita hivi Mtume (saw) aliitenga ardhi ya Naqi'i kwa ajili ya ngamia wa zaka, na kwa ajili ya ngamia na farasi wa jihadi, kama vile alivyofanya maadini na maji na malisho kuwa ni milki ya jumuia ya waislamu wote, na wakti Mtume (saw) alipofariki na Abubaka kutawala baada yake na baada yake Umar zikaja futahi nyingi na zikaja mali nyingi pamoja nazo, ikiwemo Ghanima Jizya na Kharaji zinamiminika ndani baitul-maal ya waislamu katika Madina.

Na kwa maelezo haya ya haraka tunaweza kutafakari mali ambayo iliyokua inaingia ndani ya baitul-maal ya waislamu na ile ambayo Allah aliyowaruhusu (mubah) na kuifanya kuwa ni haki ya baitul-maal itakayotumika katika njia ambazo ahkamu

za kisheria imekuja nazo kwa mujibu wa ijtihadi ya khalifa katika lile alionalo kuwa ni masilahi kwa waislamu na kusimamia mambo yao.

Hivyo basi mali ndani ya Dola la Khilafa ni muundo wa makundi manane:
1 – Anfaal na Ghanima na Fai na Khums
2 – Kharaji
3 – Jizya
4 – Milki ya jumia kwa sampuli zake
5 – Milki ya Dola ikiwemo ardhi na majengo na masilahi na mapato yake
6 – Ushur
7 – Mali ya Ghulul kutoka kwa watawala na watumishi wa Dola na mali ilitomwa kwa njia isiokua ya halali na mali za faini
8 – Khums ya Rikaz na maadini
9 – Mali isio na mrithi
10 – Mali ya walioritadi
11 – Ushuru
12 – Mali ya swadaqa – zaka

Na tutavielezea vigawanyiko hivi ili tuvijue hali halisi zake na yule ambaye amepewa uwezo wa kutumia na namna ya kutumia na sehemu ya kutumia na wanaoistahiki.

**<u>ANFAL GHANIMA FAI NA KHUMS</u>**
**<u>ANFAL NA GHANIMA</u>**

Neno anfal hutamkwa kumaanisha mali ya ngawira Allah Subhana anasema:
**{ يَسْأَلُونَكَ عَنِ الأَنْفَالِ قُلِ الأَنْفَالُ للهِ وَالْرَسُولِ }**
*"Wanakuuliza kuhusu anfal waambie anfal ni ya Allah na Mtume"* (TMQ: 8:1) na wakaulizwa ibn Abbas na Mujahid kuhusu anfal katika kauli yake Ta'ala wakajibu: anfal ni ngawira, vile vile anfal huitwa kile ngawira anaoipata Imam – katika mali ya makafiri iliotekwa – kabla ya vita na baada yake. Hivyo basi anfal na ngawira ni kitu kimoja, nayo ni ile mali inaotekwa na

waislamu katika mali ya makafiri kwa vita katika uwanja wa vita, ikiwemo pesa na silaha na bidhaa vyakula na mengineo, na hii ndio maana ya kauli yake Ta'ala:

{ وَاعْلَمُوا أَنَّمَا غَنِمْتُمْ مِنْ شَيْءٍ فَأَنَّ للهِ خُمُسَهُ وَلِلرَّسُولِ وَلِذِي الْقُرْبَى }

*"Na juweni kua chochote katika ngawira basi khums ni ya Allah na Mtume"* (TMQ: 8:41) na ngawira ikahalialishiwa Mtume baada ya kua ilikua ni haramu kwa Umma zilizotangulia, akasema Mtume (saw):

« أُعْطِيتُ خَمساً لم يُعْطَهُنَّ أحدٌ قبلي" وذكر منها "وَأُحِلَّتْ لِيَ المَغانِمُ »

"**Nimepewa matano hayakupewa yoyote kabla yangu**" **na akataja miongoni mwake "na nimehalalishiwa mimi ngawira",** na ikapokelewa na Abu Huraira amesema: amesema Mtume (saw):

« لَمْ تَحِلَّ الْغَنَائِمُ لأحَدٍ سُودِ الرُّؤوسِ مِنْ قَبْلِكُمْ كانَتْ تَنْزِلُ نَارٌ مِنَ السَّمَاءِ فَتَأْكُلُهَا »

"**Ngawira haikua imehalalishiwa yoyote mwenye nyele nyeusi katika waliowatangulia, moto ulikua unashuka na kuichoma**"

Hii ndio hali halisi ya anfal na ngawira na Allah akapeana uwezo wa kuigawa na kuisarifu kwa viongozi wa waislamu, na hili imekuja wazi katika kauli yake Ta'ala:

{ يَسْأَلُونَكَ عَنِ الأنْفَالِ قُلِ الأنْفَالُ للهِ وَالْرَسُولِ }

*"Wanakuuliza kuhusu anfal waambie anfal ni ya Allah na Mtume"* (TMQ: 8:1) na kauli yake Ta'ala:

{ وما أفاءَ الله على رسولهِ }

*"Na kila Allah alichompa ngawira Mtume wake"* (TMQ: 59:6) pia ikaja wazi kupitia matendo ya Mtume (saw) katika kuigawa ngawira na kupitia matendo ya makhalifa waongofu baada yake, kwani Mtume (saw) alikua ndie anasimamia kugawa ngawira na kuisarifu na makhalifa pia walikua hali kadhalika, ima wao wenyewe au yule wanaemuwakilisha katika kuigawa. Hivyo basi khalifa wa waislamu anakua ndie mwenye uwezo wa kuigawa ngawira na kuisarifu.

Ama kuhusu njia ya kuisarifu hii itakua kwa mujibu wa vile anavyoona kua ni masilahi kwa waislamu vile ilivyokuja katika sharia, kwa kua sharia imemtegemezea khalifa usimamizi wa ya waislamu na kutatua matatizo yao kwa mujibu wa ahkamu za

kisharia kulingana na rai yake na ijtihadi yake madamu yatapatikanwa masilahi ya Uislamu na waislamu.

**<u>KIGAWANYO CHA NGAWIRA NA MUELEKEO WA MATUMIZI YAKE NA WANAOISTAHIKI.</u>**

Ama kuhusu ngawira na mtazamo wa kuisarifu na wanaostahiki, hakika Mtume (saw) aligawa ngawira za Badr kati ya wapiganaji pasina kutoa fungu la tano (khums) na akampatia mwenye farasi mafungu matatu na wa miguu fungu moja, lakini katika vita vya na mapigano mengine alikua anatoa fungu la tano, hii ikiwa ni dalili kua kuisarifu kwake kwa ngawira haikua juu ya mtindo mmoja bali ilikua tafauti, kwani alikua anapeana ngawira kabla ya kuigawanya na baada yake, mara nyengine alikua anapeana kabla ya kutoa fungu la tano na mara nyengine baada ya kulitoa fungu la tano, na mara nyengine alikua anaahidi katika anfal katika ngawira inaoletwa na futahi, na anaisarifu katika kila ambalo anaona kua kuna masilahi ya Uislamu na waislamu. Na aya ya kwanza ilioteremka kuhusiana na anfal na ngawira iliifanya usimamizi wake na kuisarifu kwake ni kwa Allah na Mtume, na ikifuatiwa na kiongozi wa waislamu baada ya Mtume, anasema Ta'ala:

**{ يَسْأَلُونَكَ عَنِ الأَنْفَالِ قُلِ الأَنْفَالُ للهِ وَالرَّسُولِ }**

*"Wanakuuliza kuhusu anfal waambie anfal ni ya Allah na Mtume"* (TMQ: 8:1) hivyo basi aya ikafanya suala la ugawaji wa ngawira na anfal na namna ya kuisarifu nayo ni kwa Mtume, yaani kwa kiongozi wa waislamu. Imepokewa kutoka kwa Abi Umamah amesema: nilimuuliza Ubadah bin Swamit kuhusu anfal na akasema:

**« فينا معشر أصحاب بدر نزلت حين اختلفنا في النفل وساء□ فيه أخلاقنا، فانتزعه الله من أيدينا وجعله إلى رسول الله صلى الله عليه وسلم، فقسّمه رسول الله صلى الله عليه وسلم بين المسلمين عن بواء, يقول: على السواء - »**

**"Tulipata fai wa mkusanyiko wa watu wa Badr na ikashuka pale tulitafautiana kwa sababu ya mgao na ikadhihirika humo tabia zetu mbaya, ndiposa Allah akaiondosha kutoka katika mikono yetu na kumpatia Mtume (saw), na Mtume (saw) akaigawa baina ya waislamu kwa usawa**" na aya ni Amm

inaojumuisha kila ngawira na wala sio maalum ya vita vya Badr.

Na usimamizi wa Mtume (saw) katika ngawira inabainika kua uamuzi wake inategemea rai ya kiongozi, na ataisimamia vile anavyoona kua masilahi ya Uislamu na waislamu ni yenye kupatikanwa humo. Kwani Mtume (saw) aligawa thuluthi katika ngawira, na pia aligawa kutokamana nayo robo baada ya khumusi. Imepokewa kutoka kwa Abi Umamah kutoka kwa Ubadah bin Swamit amesema:

« غزونا مع رسول الله صلى الله عليه وسلم فنفلنا في بدأته ربع, وحين قفلنا ثلث »

"**Tulipigana pamoja na Mtume (saw): na akatupatia robo mwanzoni mwake na thuluthi pindi tulipofunga safari ya kurudi nyumbani**" vile vile alipeana ngawira ya alieuwawa kwa aliemuuwa. Imepokewa kutoka kwa Abi Qatada kua Mtume (saw) alisema siku ya Hunein:

« من قتل قتيلا ه عليه بينة فله سلبه »

"**Yoyote atakaeuwa na ana ushahidi basi atapewa mali yake**" na pia akaigawa ngawira za banu Nadhir na kuwapatia Muhajirun pasina na Answaar" isipikua Sahl bin Hanif na Aba Dujana kwani aliwapatia kwa sababu ya ufukara wao, na Allah akaelezea sababu ya kupeana huku katika sura ya Al-Hashr kwa qauli yake:

{ كَي لا يكُونَ دُو ةً بين لأغنياء مِنكُم }

*"Ili isiwe ni mzunguko kati ya matajiri miongoni mwenu"* [TMQ: 59: 7] na siku ya Hunein akawapatia wenye kulainishwa mioyo yao zawadi nono, na akaigawa ngawira za banu Nadhir kuwapatia muhajirina tu pasina Answaar, imepokewa kutoka kwa Anas bin Malik amesema: "Mtume (saw) aligawa ngawira za Hunein na akampatia Aqra'a bin Habis ngamia mia moja, na akampatia Uyeinah bin Husn ngamia mia moja, na akampatia Abu Sufyan ngamia mia moja, na akampatia Hakim bin Hizaam ngamia mia moja, na akampatia Harith bin Kaldah ngamia mia moja, na akampatia Harith bin Hisham ngamia mia moja, na akampatia Suheil bin Amru ngamia mia moja, na akampatia Huweitib bin Abdul Uzza ngamia mia moja, na akampatia A'laa bin Jariya

Ath-thaqafi ngamia mia moja, na akawapatia wasiokuwa hawa wenye kulainishwa mioyo yao kichache kuliko hiki, na Answaar wakaona vibaya katika nafsi zao, kwa sababu Mtume hakumpatia yoyote miongoni mwao ndiposa Mtume (saw) akakutana nao na akawahutubia na akawaliza na kuwaridhisha.

Hali kadhalika kwa makhalifa waongofu baada yake, kwani walikua wanatoa ngawira kabla ya vita na kabla haijapigwa mafungu, kwani Umar bin Al-Khattab alimpatia Jarir bin Abdalla Al-Bijliy na kabila lake la Bijliya thuluthi ya ardhi ya Sawad baada kuigawa mafungu matano baada ya kumkubalia pale alipomuomba aende upande wa Iraq, na akaendelea kula thuluthi ya ardhi ya Sawad kwa muda wa miaka miwili au mitatu, na baadae akaichukua tena kutoka kwake, kwa kumuambia: "Ewe Jarir lau kama mimi sie mgawaji mwenye kuulizwa basi ningeliwaachia kile nilichowapatia, lakini naona kua watu wamekuwa wengi kwa naonelea uwarudishie" Jarir akafanya hivyo na Umar akampatia zawadi ya dinari thamanini.

Hivyo basi aya zote hizi na matendo ya Mtume (saw) na makhalifa baada yake yeye inabainika kua suala la ngawira limetegemzwa kwa Imam ataisarifu vile anavotaka katika yale ambayo anaona kuwa ni kheri kwa Uislamu na waislamu, iwapo ataonelea ni bora aigawe au aigawe sehemu yake kwa wapiganaji ambao walishiriki katika vita basi atafanya, na ikiwa ataonelea kua aiweke katika Baitul-maal ili ipate kuwa pamoja na mali iliyopo ya Fai na Jizya na Kharaji ili aweze kuituimia katika yale ambayo ni masilahi ya waislamu basi atafanya hivyo, na hasa kwa kuwa siku hizi Dola ndio ambayo inaosimamia maandalizi ya kijeshi kivitendo na wa akiba na kuwalipa, na kuwatosheleza na kuwapa wao mishahara na familia zao, na kuandaa silaha, na leo hii silaha nzito haiwezi kumilikiwa na mtu binafsi mwenye kupigana na pia maandalizi kama hai ilivyokua hapo kale, na hasa kwa kua leo hii silaha zimeendelea na kubadilika kuwa ni silaha nzito na kuwa ni

milki ya Dola na wala haiwezekani silaha hizi nzito kumilikiwa na watu binafsi.

Kwa hivyo hukmu ya ngawira inakua sawa na hukmu ya mali ya Fai na Kharaj na Jizya na Ushr: huwekwa katika Baitul-maal ya waislamu na kutumiwa katika kusimamia mambo yao na kutimiza mahitaji yao, na khalifa ana haki ya kuigawa ngawira hizi kwa wale walioshiriki katika vita kwa sura ile ambayo anaona kua ni yenye masilahi kwa Uislamu na wailsmu.

**FAI**

Fai huitwa na kukusudiwa ile ambayo wameipata waislamu katika mali ya makafiri kwa msamaha pasina kutowa farasi wala vipando, yaani pasina kulitoa jeshi na kufanya safari na pasina kupigana, kama ilivyopatikanwa kwa banu Nadhir, au makafiri watoroke kwa sababu ya kuwaogopa waislamu, huku wakiwa wamewacha majumba yao na mali zao na waislamu waje waichukue, au ni makafiri waogope na waje kwa waislamu ili wafanye suluhu na wao, na watoe sehemu za ardhi zao na mali zao ili wasipigwe vita, kama ilivyopatikanwa kwa mayahudi wa Fadak, na maana ya hii ya Fai ndio iliokusudiwa katika kauli yake Ta'ala katika suratul Hashr:

**{ وَمَا أَفَاءَ اللهُ عَلَى رَسُوْلِهِ مِنْهُمْ فَمَا أَوْجَفْتُمْ مِنْ خَيْلٍ وَلا رِكَابٍ }**

*"Na mali alioileta Allah kwa Mtume wake kutoka kwao hamukuyaendesha mbio farasi wala ngamia"* [TMQ: 59: 6] na mali ya banu na Fadak ilikiua ni katika Fai hii ambayo waislamu hawakuwaendesha mbio farasi wala ngamia. Hivyo basi hii ilikua ni spesheli kwa Mtume (saw), na Mtume (saw) alikua akitumia sehemu katika uhai wake juu ya wakeze matumizi ya mwaka, na kinachobakia alikua anakiweka katika kununulia farasi na silaha kwa ajili ya maandalizi ya jihad, na baada ya kufariki kwake Abubakar na wale waiokua baada yake walikua wanafanya hivyo kama vile alivyokua anafanya Mtume (saw).

Amesimulia Bukhari katika mlango wa Khums kua Athman na Abdurtrahman bin A'uf na Zubeir na Sa'ad bin Abi Waqqas

walitaka ruhusa ya kuingia kwa kwa Umar na akawaruhusu, na wakakaa kidogo na wakaja Ali na Abbas wakataka ruhusa na wakapewa ruhusa na wakaingia na wakasalimia na wakakaa, na Abbas akasema: Ewe Amirul-Mumin, hukumu baina yangu na huyu, na wao walikua wanazozana kuhusu Fai ilioletwa na Allah katika mali banu Nadhir, kipote kikasema: Athman na wenzake: Ewe Amirul-Muminin hukumu baina yao, na mmoja wao akamtuliza mwengine, Umae akasema: fanyeni subra, nawaomba kwa jina la Allah ambae imesimama mbingu na ardhi kwa idhni yake, jee mwajua kua Mtume (saw) alisema: haturithiwi, kile tunachokiwacha ni sadaka, akimkusudia Mtume (saw) mwenyewe? Kikundi kikasema: ndio alisema hivyo: hapo Umar akamuelekea Ali na Abbas na akasema: nawaomba kwa jina la Allah jee munajua kua Mtume (saw) alisema hivyo? Wakasema: ndio alisema hivyo: akasema: basi mimi nawazungumzia jambo hili kua Allah alimpatia Mtume (saw) kitu katika Fai hii na wala hakumpatia mwengine asiekua yeye, kisha akasoma:

**{ وَمَا أَفَاءَ الله عَلَىَ رَسُوْلِهِ مِنْهُمْ }**

*"Na mali alioileta Allah kwa Mtume wake kutoka kwao"* [TMQ: 59: 6] hadi kauli yake:

**{ قَدِير }**

*"Mweza"* [TMQ: 59: 6] hivyo basi hiyo ikawa ni spesheli kwa Mtume (saw), na Wallahi hakuiondosha kutoka kwenu na hakuwanyanganya, kwani aliwapatia na akaisambaza miongoni mwenu mpaka ikasalia katika mai hii, na Mtume (saw) akawa anaitumia juu ya wakeze matumizi yao mwaka mmoja katika mali hii, na baadae anachukua iloibakia na kuiweka katika sehemu ya mali ya Allah, na hayo Mtume (saw) akayatekeleza katika uhai wake, nawaomba kwa jina kwa Allah jee mwajua hayo? Wakasema: ndio, akasema Umar: kisha Allah akamfisha Mtume wake (saw) na Abubakar akasema: mimi ndie badali wa Mtume (saw) na Abubakar akasihika: na akafanya sawa na vile alivyofanya Mtume (saw), na Allah anajua kua yeye alikua mkweli mwema muongofu na mwenye kufuata haki, kisha Allah akamfisha Abubakar na mimi ndie nikawa ndie badali ya

Abubakar, na nikashikilia utawala miaka miwili huku nikifanya aivoyfanya Mtume (saw) na alioyafanya Abubakar, na Allah anajuka kua mimi katika hili ni mkweli mwema muongofu na ni mwenye kuifuta hadi mwisho wa hadithi ambayo ni ndefu.

Hivyo basi hukmu ya kila Fai wanayoipata waislamu kutoka kwa adui wao pasina kulitoa jeshi na pasina kupigana inakua ni hukmu ya mali iliochukuliwa kutoka kwa makafiri kama Kharaj na Jizya, huwekwa katika Baitul-maal itatumiwa katika masilahi ya waislamu na kusimamia mambo yao kwa mujibu wa rai ya khalifa vile anavyoona kua masilahi ya waislamu ni yenye kupatikanwa.

Pia Fai huitwa na kukusudiwa ardhi iliofunguliwa kimabavu au suluhu na yanaofuata kama ardhi ya Kharaji na Jizya ya vichwa na Ushri wa biashara, na hayo ndio yale yaliodokezewa katika kauli yake Ta'ala:

**{ مَا أفَاءَ الله عَلىَ رَسُوْلِهِ مِنْ أهل القُرَى فلله و للرَسُوْلِ وَلِذي القُربَى وَاليَتامَى وَالمَساكِين وَابنِ السَبِيل كَي لا يكُونَ دُولةً بين الأغنياء مِنكُم }**

*"Mali aliyoileta Alah kwa Mtume wake kutoka kwa watu wa vijiji hivi ni kwa ajili ya Allah na kwa ajili ya Mtume na jamaa zake na mayatima na masikini na alieharibikiwa na safari, ili isiwe ni mzunguko kati ya matajiri miongoni mwenu"* [TMQ: 59: 7] na hayo ndio alioyafahamu Umar kutokamana na aya hii na akaifanyia kazi katika Sawad ya Iraq na katika ardhi ya Sham na ardhi ya Misr, pale Bilal na wenzake walipomtaka fungu katika Fai ya Iraq, kwa sababu wao waliifungua kimabavu kwa panga zao, na hayo yamekuja wazi katika mazungumzo yao pindi walipokua wanajadiliana na Umar pale walipomuambia: "Watunyima Fai tuliopewa na Allah kupitia panga zetu kwa sababu ya watu ambao hata hawakukuwepo wala hawakushuhudia na kwa sababu ya watoto wa watu na kwa ajili ya watoto wa watoto wao na wala hawakuhudhuria" kama yalivyokuja wazi katika maneno ya Umar pindi alipokua anazungumza na kikundi cha maswahaba ambao aliowaitisha kwa ajili ya kushauriana nao kua Kharaj na Jizya ni katika Fai, pale aliposema: "Na

nimeonelea nizuzuie ardhi pamoja na miti yake na nizitoze Kharaji na Jizya juu ya mashingo yao, watakaoilipa na itakua Fai ya waislamu, waliopigana na watoto wao, na wale watakaokuja baada yao" na mali yote hii ya Fai na inaoifuata kama Jizya na Kharaji na Ushri na nyenginezo itakua ni yenye kuwanufaisha waislamu wote, tajiri wao na fukara wao, na itawekwa katika Baitul-maal na kutumia katika kusimamia mambo yao na kukidhi masilahi yao na ndani yake muna haki ya kila muislamu, na Umar aliyasema hayo baada ya kuweka Kharaji juu ya ardhi ya Iraq na Sham na Misr: "Hamna muislamu hata mmoja isipokua ana fungu katika mali hii na Umar akasoma:

**{ مَا أَفَاءَ الله عَلىَ رَسُوْلِهِ مِنْ أهل القُرَى }**

*"Mali aliyoileta Allah kwa Mtume wake kutoka kwa watu wa vijiji"* [TMQ: 59: 7] mpaka akafika:

**{ وَالذِينَ جَاءوا مِن بَعدِهِم }**

*"Na wale ambao waliokuja baada yao wanasema ewe Mola tusamehe sisi na ndugu zetu waliotangulia katika Iman"* [TMQ: 59: 10] kisha akasema: "Hii imewajumuisha waislamu wote, na lau nitaishi na nijiliwe na mchungaji kutoka Cypress na Himyar pia atakua na fungu katika mali hii hata kama hakutokwa na jasho"

**<u>KHUMS</u>**

Kinachokusudiwa katika Khums ni ngawira ambayo hugawanywa iliokuja katika kauli yake Ta'ala:

**{ وعلموا أنما غنمتم من شيء فَأن لله خمسه وللرَسُوْلِ وَلِذي القُربَى وَاليَتامَى وَالمَساكِين }**

*"Na jueni kua ngawira yoyote munaoipata basi sehemu yake ya tano ni ya Allah na Mtume na jamaa zake na mayatima na masikini"* [TMQ: 8: 41] na katika zama za Mtume (saw) Khums ilikua inagawanywa mafungu matano, sehemu ni ya Allah na Mtume, na sehemu ya jamaa za Mtume, na mafungu matatu yaliosalia ni ya mayatima na masikini ya walioharibikiwa na safari.

Na Mtume (saw) alikua analitumia fungu lake katika Khums juu ya waislamu, na sehemu akiitumia katika Jihad katika kununua farasi na silaha na kuwaanda wapiganaji, kwani imepokelewa kutoka kwake kua pindi aliporegea kutoka Hunein alinyanyua

manyoa ya ngamia kutoka katika ardhi na kusema: "**Mimi nina ni nini katika Fai alioileta Allah - hata mfano wa haya - isipokua Khums na Khums pia inawarudi kwenu**"

Ama kigawanyo cha jamaa, katika zama za Mtume (saw) ilikua ikipewa banu Hashim na banu Abdul-Muttalib, na hakuna aliepewa asiekuwa katika hawa katika jamaa za Mtume (saw), na hisa ya jamaa ilikua inatumiwa kama lishe ya Mtume na kwa ajili ya kuwanusuru banu Hashim, na banu Abdul-Muttalib kwa ajili ya usaidizi wao kwa Mtume na Uislamu, na kwa sababu hiyo ikafungika tu kwao kama jamaa, imepokewa kutoka Jubeir bin Muti'im amesema: "Wakati Mtume (saw) alipoligawa fungu la jamaa kati ya banu Hashim na banu Abdul-Muttalib, mimi na Athman tulimuendea na nikamuambia: Ewe Mtume wa Allah hawa banu Hashim hakuna anaeweza kukataa fadhla zao kwa sababu ya hadhi yako aliyoiweka Allah kwao, lakini mbona unawapatia banu Abdul-Muttalib na unatunyima sisi, ilihali sisi na wao kwako wewe ni daraja moja! Akasema: hakika wao hawakututenga sisi katika ujahiliya wala katika Uislamu, bali banu Hashim na banu Abdul-Muttalib ni kitu kimoja, na akavishikanisha vidole vyake"

Na baada ya Allah kumfisha Mtume wake (saw) na akaja Abubakar, fungu la Mtume na fungu la jamaa katika Khums yalikua yanawekwa katika Baitul-Maal, na yalikua yanatumiwa katika masilahi ya waislamu na sehemu yake kuwekawa katika jihadi na hali ikaendelea kuwa hivyo. Ibn Abbas aliulizwa kuhusu fungu la jamaa baada ya kufariki Mtume (saw) na akajibu: sisi tulikuwa tunadai kua ni letu, na watu wetu wakatukatalia sisi, na akasema kumjibu Najda Al-Haruriy pindi alipoulizwa kuhusu hisa ya jamaa: "hiyo ni yetu na Umar alituita ili aitumie katika kuwaozesha waume wasiokua na wake na wake wasiokua na waume na kuitumia katika kusimamia wagonjwa wetu na tukalikataa hilo isopokua atukabidhi kamili, na yeye nae akutukatalia hilo"

Na tulikua tumekiwisha kuelezea katika mlango wa ngawira kua ngawira leo hii huwekwa katika Baitul-maal na usimamizi wake upo kwa khalifa ataisarifu kwa kuitumia juu ya masilahi ya waislamu kwa mujibu wa rai yake na ijtihadi yake na kwa kua Khums ni sehemu yake basi nayo pia itachukua hukmu hiyo hiyo na itawekwa sehemu yake na viwili hivi vitakua sawa na Jizya na Kharaji na Ushri.

## KHARAJI

Kharaji ni haki ya waislamu inaowekwa juu ardhi ambayo imepatikanwa kama ngawira kutoka kwa makafiri iwe ni kwa vita au kwa suluhu, na kuna Kharaji ya kimabavu na Kharaji ya suluhu.

## KHARAJI YA KIMABAVU

Ni Kharaji ambayo huwekwa juu ya kila ardhi waliyoinyakua waislamu kutoka kwa makafiri kimabavu kwa vita, kwa mfano ardhi ya Iraq na Sham na Misr, na asli yake ni neno lake Ta'ala:

**{ مَا أَفَاءَ اللهُ عَلَى رَسُولِهِ مِنْ أَهْلِ الْقُرَى فَلِلَّهِ وَلِلرَّسُولِ وَلِذِي الْقُرْبَى وَالْيَتَامَى وَالْمَسَاكِينِ وَابْنِ السَّبِيلِ كَيْ لاَ يَكُونَ دُولَةً بَيْنَ الأَغْنِيَاءِ مِنْكُمْ وَمَا آتَاكُمْ الرَّسُولُ فَخُذُوهُ وَمَا نَهَاكُمْ عَنْهُ فَانْتَهُوا وَاتَّقُوا اللهَ إِنَّ اللهَ شَدِيدُ الْعِقَابِ - لِلْفُقَرَاءِ الْمُهَاجِرِينَ الَّذِينَ أُخْرِجُوا مِنْ دِيارِهِمْ وَأَمْوَالِهِمْ يَبْتَغُونَ فَضْلاً مِنْ اللهِ وَرِضْوَانًا وَيَنْصُرُونَ اللهَ وَرَسُولَهُ أُوْلَئِكَ هُمْ الصَّادِقُونَ - وَالَّذِينَ تَبَوَّءُوا الدَّارَ وَالإِيمَانَ مِنْ قَبْلِهِمْ يُحِبُّونَ مَنْ هَاجَرَ إِلَيْهِمْ وَلاَ يَجِدُونَ فِي صُدُورِهِمْ حَاجَةً مِمَّا أُوتُوا وَيُؤْثِرُونَ عَلَى أَنْفُسِهِمْ وَلَوْ كَانَ بِهِمْ خَصَاصَةٌ وَمَنْ يُوقَ شُحَّ نَفْسِهِ فَأُوْلَئِكَ هُمْ الْمُفْلِحُونَ - وَالَّذِينَ جَاءُوا مِنْ بَعْدِهِمْ يَقُولُونَ رَبَّنَا اغْفِرْ لَنَا وَلأَخْوَانِنَا الَّذِينَ سَبَقُونَا بِالإِيمَانِ وَلاَ تَجْعَلْ فِي قُلُوبِنَا غِلاًّ لِلَّذِينَ آمَنُوا رَبَّنَا إِنَّكَ رَءُوفٌ رَحِيمٌ }**

*"Mali aiyoileta Allah kwa Mtume wake kutoka kwa watu wa vijiji hivi ni kwa ajili ya Allah na kwa ajili ya Mtume na jamaa na mayatima na masikini na msafiri aliyeharibikiwa ili isiwe ni mzunguko baina ya matajiri miongoni mwenu tu na anachukupeni Mtume basi pokeeni na anachokukatazeni jiepusheni nacho na muogopeni Allah kwa yakini Allah ni mkali wa kuadhibu, - wapewe mafakiri waliogura ambao walifukuzwa kutoka katika majumba yao na mali zao kwa ajili ya kutaka fadhila za Allah na radhi na kumnusuru Allah na Mtume wake basi hao ndio wakweli, - na wale waliofanya maskani yao ya hapa na wakautakasa Uislamu kabla ya kuja hao na wakawapenda wale walioguria kwao na wala hawapati hawaoni dhiki nyoyoni mwao kwa*

*hayo waliopewa na wanawapendelea kuliko nafsi zao ingawa wenyewe wana hali ndogo, na waepushwao na ubakhili wa nafsi zao hao ndio wenye kufaulu kweli kweli - na wale ambao waliokuja baada yao wanasema ewe Mola tusamehe sisi na ndugu zetu waliotangulia katika Iman"* [TMQ: 59: 7 -10]

Na aya hii ndio ambayo Umar bin Al-Khattab aliitumia kama hujja ya rai yake katika kutozigawa ardhi ya Iraq na Sham na Misr kwa waliopigana, baada ya kufuatwa na Abdurrahman na Zubeir kwa ajili ya kuzigawa ardhi hizi ambazo Allah alizozileta kupitia panga zao kama vile Mtume (saw) alivozigawa ardhi ya Khaibar kwa waliopigana pindi alipozifungua, na katika yale alioyasema kuwaambia Answaar ambao aliowakusanya ili kuwataka ushauri kwao juu ya rai yake: "Mimi nimeonelea nizizuie ardhi pamoja na miti yake na niziwekee Kharaji na Jizya uu ya mashingo yao watailipa na itakua ni Fai ya waislamu waliopigana na watoto na kwa wale watakaokuja baada yao, mwaiona hii mipaka ni lazima iwekwe wanaume watakaoilinda, mwaiona miji hii makubwa kama Sham na Jazira na Kufa na Basra na Misr ni lazima ijazwe wanajeshi na wapewe mishahara, basi watapewa kutoka wapi iwapo ardhi hizi na kiti ikigawanywa? Kisha akawajengea wao hujja rai yake kwa kuisoma aya hii ya Faihadi akafika katika neno lake Ta'ala:

**{ وَالَّذِينَ جَاءُوا مِن بَعدِهِم }**

*"Na wale ambao waliokuja baada yao wanasema ewe Mola tusamehe sisi na ndugu zetu waliotangulia katika Iman"* [TMQ: 59: 10] hakika hii imewakusanya watu wote mpaka siku ya Qiyama, na hamna muislamu yoyote isipokua ana haki na hisa" na wakamuafiki katika rai yake na wote Wakasema: rai yako ndio ya sawa na ni uzuri uioje wa yale ulioyasema, iwapo mipaka na miji hii haitajazwa kwa wanaume na kuwekewa pato basi makafiri watairudilia miji yao, baadae akasema: "Kwa hakika mambo yamekuwa wazi kwangu, basi ni mtu gain ambae anajua na kuelewa aziweke ardhi mahala pake na miti ikadiriwe? Na wote wakakubaliana juu ya Uthman bin Hanif na Wakasema: huyu waweza kumtuma kwa muhimu zaidi kuliko hili kwani yeye

ana maono na akili na ujuzi, hapo Umar akamkimbilia na kupitia kazi ya kupima ardhi ya Sawad"

Uthman akaenda na akapima ardhi ya Sawad na akaiwekea Kharaji maalum na akampelekea Umar na Umar akakiri, na mapato ya Sawad ya Kufa pekee kabla ya kufa kwa Umar ilifikia Dirhamu milioni mia moja, na siku hizo Dirhamu ilikua na uzito wa mithqal, hivyo basi Umar akaziwacha ardhi katika mikono ya wenyewe na akawa anawatoza Kharaji watakaoilipa kwa Baitul-maal ya waislamu, na akaifanya kuwa ni Fai ya waislamu hadi siku ya Qiyama, na itabaki kuwa ni Kharaji mpaka ile siku Allah atairithi ardhi na vilivyo juu yake na wala haitageuka kuwa ni Ushri hata kama wenye kuimiliki wakasilimu, au watamuuzia muislamu kwa sababu ndio sifa iliowekwa juu ya ardhi na kwa sababu asli yake ilifunguliwa kimabavu na ikawekewa Kharaji hayo yatabakia na wala hayatobadilika. Imepokewa kutoka kwa njia ya Twariq bin Shihab amesema: Umar bin Al-Khattab aliniandikia barua kuhusu kabila Dahaqna wa mto wa Malik - na lilikua limeshasilimu - aliandika: "Kua wapewe ardhi zao na walipishwe Kharaji" na ipo wazi kua Umar bin Al-Khattab hakuwasamehe Kharaji juu ya ardhi iliofunguliwa kimabavu na ambao wenyewe wamesilimu bali aliwalazimisha waendelee kulipa Kharaji baada ya kusilimu kwao.

**KHARAJI YA SULUHU**

Ni Kharaji inaowekwa juu ya kila ardhi ambayo watu wake wamefanyiwa suluhu, na itafuata kama vile ambavyo watakavyokubaliana baina ya waislamu na wale wataokafanya nao suluhu, na ikiwa imeafikiwa kua ardhi ni yetu lakini tuziwache kwa wenyewe kwa Kharaji watakaoilipa basi Kharaji hiyo itabakia milele juu ya ardhi hizo, na ardhi hizo zitabakia kua ni za Kharaji hadi siku ya Qiyama, hata lau kama zitagura kwenda kwa waislamu kwa kusilimu au kwa kununua au kwa namna nyengine.

Ama ikiwa suluhu imepitishwa kua ardhi ni zao na zitakua katika mikono yao na ikaamuliwa kua watakua wanalipa kiwango Fulani cha Kharaji basi Kharaji hiyo itachukua nafasi ya Jizya na itaondolewa kwa kusilimu kwao au kwa kuiuza ardhi kwa muislamu, hayo ni kwa neno lake Ta'ala:

**{ وَأَوْفُوا بِالْعَهْدِ إِنَّ الْعَهْدَ كَانَ مَسْئُولاً }**

*"Na timizeni ahadi kwani ahadi kwa hakika ahadi itaulizwa"* [TMQ: 17: 34] na kwa kauli yake (saw):

**« المؤمنون عند شروطهم »**

"**Waumini wanawajibika kutekeleza masharti yao**" na ikiwa wataiuza ardhi kwa kafiri basi Kharaji itakua ni yenye kubakia na wala haitaondoka kwa sababu kafiri ni mtu wa Kharaji na Jizya.

Na Kharaji si Ushri kwani Ushri huchukuliwa juu ya mazao ya ardhi ya Ushri, na ardhi za Ushri ni:

A: - Bara Arabu, kwa sababu wakazi wake walikua wanaabudu masanamu (washirikina), kwa hivyo wao hawakua wanatakiwa kitu chengine isipokua ni kusilimu, na kwa sababu Mtume (saw) hakuwalazimishia Kharaji yoyote juu yao pamoja na kua yeye alipigana na akazifungua sehemu kadhaa.

B: - Kila ardhi ambayo watu wake walisilimu kwa mfano Indonesia na kusini mashariki ya Asia, amesema Mtume (saw):

**« أُمرت أن أقاتل الناس حتى يقولوا لا إله الا الله, فمن قال لا إله الا الله فقد عصم مني نفسه وماله ألا بحقه, وحسابه على الله »**

"**Nimeamrishwa niwapige vita watu mpaka waseme hapana mola apasae kuabudiwa isipokua Allah, na yoyote atakasema basi atakua ameihifadhi nafsi yake na mali yake kutokamana na mimi isipokua kwa haki yake, na hisabu yake ni kwa Allah**" na ardhi ni kama mali.

C: - Kila ardhi ambayo imefunguliwa kimabavu na khalifa akaigawa kwa wapiganaji kwa mfano ardhi ya Khaibar, au aliwakubalia wapiganaji wamiliki sehemu yake kama vile Umar alivyowakubalia wanajeshi wa Sham kumiliki ufuo wa mto wa Irbid ndani ya Hums, na Marj Barada ndani ya Dimishq.

D: - Kila ardhi ambayo imefanywa makubaliano watu wake kua ardhi zitabakia katika mikono yao na ni milki yao kwa Kharaji watakaoilipa, hapo itakua ni ardhi ya Ushri pindi watakaposilimu au watakapomuuzia muislamu.

E: - Kila ardhi ambayo ni maiti na ikafufuliwa na muislamu amesema (saw):

**« من أحيا أرضاً ليست لأحد فهو أحق بها »**

"**Yoyote atakaefufua ardhi isio ya mtu basi yeye ana haki nayo zaidi**" na Bukhari akaipokea kwa maneno:

**« من أعمر أرضاً ليست لأحد فهو أحق »**

"**Yoyote atakaeamirisha ardhi isio ya mtu basi yeye ana haki zaidi**"

NA Ushri hii itabakia kuwa ni Ushri na wala haitabadilika kuwa ni Kharaji isipokua katika hali ambayo iwapo kafiri atainunua ardhi ya Ushri kutoka kwa muislamu katika ardhi za kimabavu, hapo itakua ni wajibu juu yake kuilipia Kharaji na wala hatoilipia Ushri kwa sababu Ushri ni zaka na kafiri katika watu wa kutoa zaka kwa sababu ni sadaqa na ni kitakaso kwa muislamu. Na ikiwa kafiri atanunua ardhi ya Ushri kutoka kwa muislamu katika ardhi zisizokua za kimabavu basi hapo hatakua ni mwenye kutoa Kharaji na Ushri kwa sababu ardhi ya Ushri haina Kharaji juu yake na pia kwa sababu kafiri hastahili kutoa zaka vile vile lau akanunua mifugo kutoka kwa muislamu pia hapo hana zaka juu yake katika hiyo.

## KUKUTANA KWA KHARAJI NA USHRI

Kwa hakika Kharaji huwekwa mwanzo katika ardhi za kimabavu ambazo zilikua zinamilikiwa na makafiri wakati wa kuzifungua, na iwapo ardhi zitaendelea kuwa katika mikono ya makafiri basi hapo zitakuwa na Kharaji, ilimwe au isilimwe na wala hamna Ushri juu yake kwa sababu Ushri ni zaka na makafiri hawastahili kuitoa, na iwapo watasilimu au kuiuza kwa muislamu basi hapo Kharaji yake haitaondolewa kwa sababu ndio sifa yake kwani asli ilifunguliwa kimabavu na itabakia hivyo miliele, na pia itakua ni wajibu juu yao kutoa

Ushri pamoja na Kharaji kwa sababu Kharaji ni haki ya wajibu juu ya ardhi na Ushri na haki ya wajibu juu ya mazao ya ardhi ya muislamu kwa aya na hadithi, na wala hamna mgongano kati ya haki mbili hizi, kwani zimewajibika kwa sababu mbili tofauti, kwa mfano lau aliehirimia akauwa kiwinjo kinachomilikiwa katika Haram basi hapo itamlazimu juu yake thamani yake kwa mmiliki wake na kulipa haki ya Allah, ama kuhusu yale walioyategemea mahanafi kuhusu kutokutana kwa Ushri na Kharaji kupitia hadithi wanaisimulia kutoka kwa Mtume (saw):

« لا يجتمع عشر وخراج في أرض مسلم »

"Hikutani Ushri na Kharaji katika ardhi ya muislamu" hiyo si hadithi na wala wadhibiti wa hadithi hawajaithibitisha kua ni katika maneno ya Mtume (saw).

Na ataanza kulipa Kharaji na iwapo baada ya kulipa Kharaji itabakia katika yale ambayo ni wajibu kutolewa zaka katika makulima na matunda na ikafika Nisab basi hapo itatolewa zaka, na iwapo haitafikia Nisab basi zaka haitakua ni wajibu juu yake.

## <u>HALI HALISI YA KIVITENDO AMBAYO NI WAJIBU KUFUATWA LEO</u>

Na baada ya futahi kuwa mbali na sisi kwa muda na jumla ya watu wamekuwa na waislamu katika ardhi zote ambazo zilifunguliwa kimbavau au suluhu, na baada jumla ya usajili na kumbukumbu kupotea ambazo zinazobainisha ardhi zilizopeanwa na ardhi zilizofufuliwa na ardhi iliofanyiwa makubaliano na ardhi ya kimabavu na ardhi ya suluhu, twaweza kufuata taratibu zifuatazo: kuzizingatia jumla ya ardhi vile inavokulikanwa kua imefunguliwa kimabavu au watu wake wamesilimu au ilichukuliwa kwa hali maalum.

Hivyo basi ardhi zote za Iraq ikiwemo Kuwait na Iran na India na Pakistan na Afghanistan na Turkistan na Bukhari na Samarqand na ardhi za Sham na Uturuki na Misr na Sudan

kaskazini mwa Afrika zote hizi ni ardhi za Kharaji kwa sababu zilifunguliwa kimabavu, hivyo basi ni wajibu zitolewe Kharaji na wenyewe wakiwemo waislamu na makafiri na pia Ushri juu ya waislamu ikiwa mazao ya ardhi zao ni katika yale yanaopaswa kutolewa zaka na ikafika Nisab baada ya kutolewa Kharaji, isipokua ikiwa itathibitika kutoka kwa muislamu na ushuhuda wa stakbadhi kua ardhi yake ni ardhi ya Ushri basi hapo hatatozwa Kharaji na inatosheleza kuitolea zaka.

Ama bara Arabu ikiwemo Yemen na Indonesia na kusini ya mashariki ya Asia na mifano yake hizo ni ardhi za Ushri na wala hamna Kharaji juu yake na haipaswi kutolewa illa Kharaji nayo ni zaka ya mazao ambayo yanaopaswa kutolewa zaka.

**<u>NAMNA YA KUWEKA KHARAJI</u>**

Ni lazima kwa khalifa ateuwe watu walio na ujuzi wa kupima ujuzi wa namna ya kukisia na namna ya kukadiria mazao wakati wa kuweka Kharaji hayo ni kama vile hali ilivyokuwa kwa Umar bin Al-Khatttab pndi alipokuwa anataka kupima ardhi ya Sawad, kwani aliwashauri waislamu juu ya yule ambae anaefaa kuteuiwa katika kazi hiyo, kwa kuwaambia: "Kwa hakika mambo yamekuwa wazi kwangu, basi ni mtu gani ambae anajua na kuelewa aziweke ardhi mahala pake na miti ikadiriwe? Na wote wakakubaliana juu ya Uthman bin Hanif na Wakasema: huyu waweza kumtuma kwa muhimu zaidi kuliko hili kwani yeye ana maono na akili na ujuzi, hapo Umar akamkimbilia na kupitia kazi ya kupima ardhi ya Sawad"

Na ni lazima kwa yule alieteuliwa kwa ajili kuweka Kharaji kuchunga ahli haisi ya ya ardhi na asili ya ile ardhi kama ni nzuri yenye rutuba ilio na mazao mazuri na inatoa kwa uwingi, au sio nzuri na mazao yake ni machache, au inanyeshewa na mvua au kwa maji ya chemichemi au visima au mikondo au mito, na jee hunyeshewa na mvua au inanyunyiziwa au kupitia mashine kwa sababu juhudi ya hizo haziko sawa, na katika upande wa mazao na matunda ambayo hupandwa na

kuvunwa, kwa sababu katika yanaopandwa na matunda kuna ambayo ni ghali na thamani yake iko juu na miongoni mwake kuna ya rahisi na thamani yake ni ndogo, na katika upande wake wa sehemu ilioko, jee ni karibu na miji na masoko yake na mbali nayo na jee kuna njia inaopitika ya sahali ya kufikisha huko na kusafirisha mazao yake hadi masokoni na ni ya taabu na shida.

Ni lazima mambo yote hayo yawe ni kuchungwa na kuyaangalia kwa makini ili ardhi isate kudhulumiwa na wala isitozwe zaidi ya uweza wake, na Umar bin Al-Khattab alimuliza Uthman bin Hanif na Hudheifah bin Al-Yaman baada ya jurudi kutoka kupima ardhi ya Sawad na kuiwekea Kharaji juu yake: "Mumeweka vipi juu ya ardhi pengine mumewawekea watu wasichokiweza? Hudheifah akasema: nimewabakishia zaidi, na Uthman akasema: nimewawachia maradufu na lao kama unataka ningelikichukua. Na pia ni lazima watu wenye ardhi waangaliwe na waachiwe kitakachowatosheleza katika hali ya mikasa na kuharibika kwa mimea, kama vile alivyoamrisha Mtume (saw) katika kukadiria matunda wakati wa zaka ili watu wenye mitende waachiwe thuluthi robo na akasema:

**« وخففوا الخرص فإن في المال الوصية والعرية والواطئة والنائبة »**

**"Na mufanye ukhafifu katika kukadiria kwani katika mali kuna aliusiwa na alieathirika na baridi na mimea kuanguka na mikasa"**

Na inawezekana kua Kharaji ikawekwa juu ya ardhi na inawezekana ikawekwa juu ya mimea na matunda, na ikiwa itawekwa juu ya ardhi basi mwaka wake utahisabiwa kwa mwaka wa mwezi (moon) kwa sababu ndio mwaka ambao kisheria huqadiriwa wakati wa zaka Diyyah na Jizya na mengineo, na ikiwa imewekwa juu mimea na matunda basi itazingatiwa kwa kutimia kwa mimea na matunda na kulisafisha kwake, na huo ndio utakua mwaka wake na wakati wake, na Kharaji inaweza pia kuwa kwa sarafu, au sarafu na

nafaka na matunda, na pia inaweza kuwa mchanganyiko wa mimea na matunda, kwani mwaka wake utakuwa kwa kukamilika kwa mimea na matunda na kulisafisha kwake, na kwa siku hizi inaweza kuwa kwa uwepesi zaidi Kharaji ya ardhi iwe ni sarafu kwa mujibu wa kinachopandwa.

**KIWANGO CHA KHARAJI**

Bila shaka uwekaji wa Kharaji juu ya ardhi linahitajia wajuzi ambao wanajua namna ya kuweka kama ilivyofafanuliwa katika mada ilitangulia kama vile alivyofanya Umarbin Al-Khattab pindi alipomtuma Uthman bin Hanif baada ya watu kumshauri na kumpendekeza kwa sababu ya ujuzi wake na akili na uzoefu, na Umar akamteua aende Kufa katika ufuo wa mto wa Furat na kama vile alivyomteua Hudheifah bin Al-Yaman aende nyuma ya mto wa Dajla (Tigris) na wakapima Sawad na wakakadiria Kharaji inaowezekana na wakampelekea Umar nae akakubali, imepokewa kutoka Amru bin Maimun amesema: "Nilimshuhudia Umar bin Al-Khattab na kijana wa Hanif akamjilia na akawa anamzungumzia na nikamsikia anasema: Wallahi lau nikiweka dirhamu moja na Qafiz moja ya chakula juu ya kila Jarib moja ya ardhi basi hilo halitakua uzito kwao na wala haitowaumiza" Na katika hadithi ya Muhammad bin Ubeid Ath-Thaqafiy amesema: "Umar bin Al-Khattab aliweka dirhamu moja na Qafiz ya chakula juu ya watu wa Sawad juu ya kila Jarib ilioamiriwa au iliojaa maji na dirhamu tano juu ya kila Jarib ilio na rutuba" na Ash-Sha'abiy akaeleza kutoka kwa Umar" "Kua alimtuma Uthman bin Hanif juu ya Sawad na akaweka dirhamu mbili juu ya kila Jarib ya shayiri na dirhamu nne juu kila Jarib ya ngano na dirhamu sita juu ya kila Jarib ya miwa na dirhamu nane juu ya kila Jarib ya mitende na dirhamu kumi juu ya kila Jarib ya mizabibu na dirhamu kumi na mbili juu ya kila Jarib ya mizeituni".

Hivyo basi inabainika kua kiwango cha Kharaji alichokiweka Uthman bin Hanif juu ya ardhi ya Iraq na Umar kukubali ni kua haikua ni moja bali ilikua tafauti huku ikizingatiwa ardhi na

uzuri wake na kunyunyiziwa kwake maji na kinachopandwa na ni ardhi iliamiriwa inaolimwa au ni ardhi iliojaa maji na pia ilikua inachukuliwa juu yardhi kwa mimea na matunda na pia alikadiria kwa sarafu na kwa nafaka na pia makadirio ilikua ni kwa mujibu wa uweza na wala haikua ni ya kulazimisha na kuwatoza wenye ardhi wasichokiweza na pia aliwabakishia wao sehemu.

Na kwa kuwa makadirio hayo yaliwekwa katika wakati fulani na ikajengwa juu ya ijtihadi, hivyo basi hayo sio makadirio ya wajibu kisheria ambayo haifai kuenda kinyume nayo kwa kuzidisha au kupubguza bali inajuzu kwa khalifa kuongeza na kupunguza kwa mujibu wa rai yake na ijtihadi yake na kwa mujibu wa mabadiliko ya hali juu ya ardhi ima kwa kuzidi uzuri au kuharibika, au ardhi kukosa mahitajio yake au kuzidiwa na maji au kwa uhaba wake au kukosa kabisa au kwa sababu ya ugonjwa au kuangamia kwake au kwa sababu ya kupanda kwa bei au kushuka kwani mabadiliko yote hayo yana tathira katika kukadiria na ni lazima yachungwe na makadirio yarudiwe tena mara kwa mara ili isiwe ni dhulma kwa mwenye ardhi na wala kwa Baitul-Maal.

## MATUMIZI YA KHARAJI

Miongoni mwa maneno yaliopokewa kutoka kwa Umar bin Al-Khatttab katika majadiliano yake na wale waliokuwa wakimjadili kuhusu kuigawa ardhi ya Iraq na Sham na Misr yanaonyesha wazi juu matumizi ya Kharaji na pia yamekuja maneno yake katika majadiliano hayo: "Lau nitaigawa basi hakutabakia kitu kwa ajili yale watakaokuja baada yenu, basi itakuaje kwa waislamu watakaokuja na wakute kua ardhi zimeshagawanywa na zikarithiwa kutoka kwa mababu na zimeshamilikiwa, kwa hakika huo sio ushauri mzuri na mipaka hii tutaijaza na nini? Na watapata nini watoto na wajane wa biladi hii na nyenginezo kama Sham na Iraq? Na maneno yake kuwaambia Answaar waliomshauri: "na nimeonelea nizizuie ardhi pamoja na miti yake na niziwekee Kharaji na Jizya katika

mashingo yao, watakua wanalipa na itakuwa ni Fai ya waislamu walipigana na watoto na kwa ajili wa wale watakaokuja baada yao, mwaiona mipaka hii ni lazima wapatikane watu watakaoilinda, mwaiona miji hii makubwa: Sham na Jazira na Kufa na Basra na Misr ni lazima ijazwe wanajeshi na kuwatumilia juu yao, na lau ardhi na miti yake itagawanywa basi watapewa kutoka wapi? Na akasema: baada ya kuisoma aya ya Fai na akasoma aya:

**{ وَالَّذِينَ جَاءُوا مِن بَعْدِهِم }**

*"Na wale ambao waliokuja baada yao"* [TMQ: 59: 10] aya hii imewakusanaya watu na hamna muislamu aliesalia isipokua ana haki katika mali hii, na lau nitaishi nitampatia kila muislamu haki yake hata akija mchungaji kutoka Suru na Himyar na sehemu yake hata kama hakutokwa na jasho"

Hivyo basi inaonyesha wazi kua Kharaji ni haki ya waislamu wote na kwamba inatumiwa sehemu yake juu ya masilahi yote ya waislamu katika Dola, na kutokamana nayo hutumiwa katika kuwalipa na kuwasimamia watumishi wa Ummah na wanajeshi, na kwayo huandaliwa majeshi na kuandaliwa silaha, na hutumiwa juu ya wajane na wene matatizo na kutatuiwa masilahi ya watu na kwasimamia mambo yao, na khaifa ataitumia kwa mujibu wa rai yake na ijtihadi yake vile anavyoonelea katika yalio na masilahi kwa Uislamu na waislamu.

## MAADILI/VIPIMO YA UREFU NA UPANA NA UZANI NA UZITO

Kwa hakika kujua kwa hukmu nyingi za kisheria zinazohusiana na Kharaji Jizya zaka kukata na Kaffarah yanahitajia ufahamu wa urefu uzani na uzito ambazo zilikua zinatumika katika zama za Mtume (saw) katika zama za maswahaba watukufu radhi za Allah ziwashukie wao. Na pindi zama zilipoweka mbali urefu huu na uzani na uzito na ikawa jumla yake leo hii – ikiwa sio yote – hazitumiki, imekua sio sahali kufahamu, na kufahamu viwango vinavyolingana na urefu na uzani na uzito

vinavyotumika leo hii, ambazo zimekua sahali kujua na rahisi kufahamu na kuelezea kwa makini.

Hivyo basi tutaelezea urefu huu na uzani na uzito ili kufafanua hali yake halisi, na mahusiano yake na urefu na uzani na uzito zinazotumika leo hii kwa sura ambayo itaweka wazi na sahali kujua na rahisi kufahamu maelezo ya kina.

**UREFU NA UPANA**

Jarib ndicho kilichokua kipimo msingi cha upana, kilicokua kinatumika katika kupima ardhi ya makulima, na mpaka wa kumiliki na ambayo juu ya msingi wake ilikua inakadiriwa Kharaji. Imepokewa kutoka Ash-Sha'abi amesema: "Umar bin Al-Khattab alipima Sawad na ikafikia jarib milioni mia sita na thalathini (630,000,000)" na katika Al-Ahkam As-Sultaniya amesema: "Ama Jarib ni Qasba kumi kwa Qasba kumi" na Qafiz ni Qasba kumi kwa Qasba moja, na Qasba moja ni dhiraa sita, hivyo basi Jarib ni dhiraa vipande alfu tatu na mia sita, na Qafiz ni dhiraa mia tatu na sittini, nayo ni fungu la kumi la Jarib" na ikaeleza kua Ja'afar bin Qudama alisema kuhusu Farsakh:"nakua ni dhiraa kwa upana nayo ni dhiraa ya kihashimu dhiraa alfu tisa" na Qalshandi akaeleza: "kua dhiraa ya kihashimu ni sawa na dhiraa moja na thuluthi mbili sawa na dhiraa ya mkono ambayo ni dhiraa ya mursala, na dhiraa ya mkono ni sawa na mishiko sita kwa mishiko ya mtu wa wastani, na kila mshiko ni vidole sita kuanzia kidogo hadi cha shahada, na kila kidole ni nywele sita kwa upana"

Na waislamu walitumia urefu unaofuata:
Mshiko = vidole 4
Dhiraa mursala = mishiko 6 au vodole 24
Dhiraa ya kihashimu = mishiko 8 au vidole 32
Qasba = dhiraa 6 za kihashimu
Jarib = qasba 10 kwa qasba 10

Hivyo basi Qasba 10 = 10 mara 6 dhiraa urefu wa Qasba = 60 dhiraa urefu wa ubavu wa Jarib
Urefu wa Jarib: 60 dhiraa urefu wa ubavu mara dhiraa 60 = dhiraa 3600 za kihashimu mraba
Qafiz = 1/10 urefu wa Jarib yaani ni sawa na dhiraa 360 za kihashimu mraba

Na twaweza kutumia vipimo vya mita vinavyotumika leo hii katika kujua hali halisi ya urefu urefu huu, na ambayo inachozingatiwa kua ni kipimo cha urefu na upana sahali zaidi na fafanuzi zaidi ikiwa tutajua upanawa wastani wa kidole kwa centimita.

Na kupitia hisabu inabainika kua upana wa wastani wa kidole ni sawa na centimita 1,925, hivyo basi urefu wa vipimo hivi ni kama ifuatavyo:

Kidole = 1,925 centimita
Mshiko = vidole 4 mara 1,925 centimita upana wa kidole = 7, 7 centimita
Dhiraa mursala = vidole 24 mara 1,925 centimita upana wa kidole = 42,2 centimita
Dhiraa ya kihashimu = vidole 32 mara 1,925 centimita upana wa kidole = 61,6 centimita
Qasba = dhiraa 6 za kihashimu mara 61,6 centimita urefu wa dhiraa ya kihashimu = 3,696 mita urefu wa qasba
Hivyo basi qasba 10 = 10 mara 3,696 mita urefu wa qasba = 36,96 mita urefu ubavu wa Jarib
Upana wa Jarib = 36,96 mita urefu wa ubavu wa Jarib mara 36,96 mita = 1366 mita mraba
Yaani ni sawa Dunum moja na thuluthi mbili ya Dunum
Upana wa Qafiz = 1/10 Jarib Yaani 132,6 mita mraba

Haya yanahusiana na vipimo vya upana ama vipimo vya urefu ni Barid, na Farsakh na Maili, na hupimwa kwa dhiraa mursala ambayo huitwa dhiraa ya asli na dhiraa ya kisharia, na urefu

wake ni mishiko sita au vidole ishirini na nne, kama vile ilivyotangulia katika vipimo vya upana, na muandishi wa Ahkam As-Sultwaniya ameleza kua Maili ni dhiraa alfu nne kwa dhiraa za mursala, na vitabu vya kifiqhi vikaafikana kua Farsakh ni Maili tatu, na Barid ni Farsakh nne, hivyo basi vipimo vyake vitakua kama vile ilivyotangulia na kwa mujibu wa kilomita inaotumika leo hii, na ndio ambayo inaozingatiwa kuwa ndio vipimo vya masafa ya urefu sahali zaidi na wazi, kama ifuatavyo:

Dhiraa mursala = mishiko 6 au = vidole 24
Maili = 4000 dhiraa mursala
Farsakh = maili 3
Barid = Farsakh 4

Na kwa hisabu za mita na kilomita itakua:
Dhiraa mursala = vidole 24 mara 1,925 centimita upana wa kidole = 46,2 centimita urefu wa dhiraa mursala
Maili = 4000 dhiraa mursala mara 46,2 centimita urefu wa dhiraa mursala = 1848 mita au 1,848 kilomita urefu wa maili
Farsakh = 3 maili mara 1848 mita urefu wa maili = 5544 mita au 5.544 kilomita urefu wa Farsakh
Barid = 4 Farsakh mara mita 5544 urefu wa Farsakh = 22176 mita au 22,176 kilomita urefu wa Barid
Na kwa kuwa masafa ya kukusuru ni Farsakh 16 au Maili 48 basi kwa kilomita itakua kama ifuatavyo:
Kukusuru = 16 Farsakh mara 5,544 kilomita urefu wa Farsakh = 88,704 kilomoita urefu wa masafa ya kukusuru
Au = 48 Maili mara 1,848 urefu wa Maili = 88,704 kilomita urefu wa masafa ya kukusuru.

Na kwa kuwa kujifunga katika vipimo ya urefu upana na masafa kwa vipimo hivyo hivyo ambavyo vilivyokua vinatumika hapo awali si wajibu wa kisharia, kwa sababu ni mbinu na vyombo ambayo vinatumiwa kwa ajili ya kutekeleza matendo na kusahalisha katika kuyatekeleza hivyo basi

inaruhusiwa kutumia na pia inaruhusiwa kutumia nyengine huku tukifuata ilio rahisi na sahali zaidi na bayana na yenye kudhibiti, pamoja na kujua kua asli ya Jarib ni kipimo cha kifursi na Fadan (ekari) ilikua na bado ndicho kipimo kinachotumika ndani ya Masri, na upana wake unatafautiana na upana wa Jarib.

Na kwa kua vipimo vya mita na kilomita na dunum vinavyotumika leo hii ndivyo vinavyozingatiwa kuwa ndivyo vipimo sahali zaidi na fafanuzi basi inawezekana kuwa dunum ndio kipimo cha kupimia ardhi, na mita ndio kipimo cha kupimia vitambaa na majumba, na kilomita ndicho kipimo cha kupimia masafa, na Jarib aliyoiweka Umar bin Al-Khattab kama msingi wa kukadiria ardhi ya kharaji inalingana na mita 1366 mraba na ni inakurubiana kuwa sawa na dunum moja na thuluthi mbili kwa sababu upana wa dunum ni mita 1000 mraba.

**UZANI NA UZITO**

Ikapokewa na Abu Said Al-Khudhriy amesema: "Tulikua tunatoa zaka ya Fitri Swaa moja ya chakula au Swaa ya shayiri au Swaa ya tende au Swaa ya Jibini au Swaa ya zabibu" na imepokewa kutoka kwa Jabir bin Abdallah amesema: "Mtume (saw) alikua anaoga kwa Swaa na kujitaharisha kwa Mudd" na ikapokewa na Abi Said Al-Khudhriy – akaifanya marfuu – amesema: "Haina zaka chini ya wasaq tano" na wasaq ni makhtum sittini, Yaani Swaa kwa dalili kama ilivyopokewa kutoka kwa Hassan na ibn Sirin wamesema: "Wasaq ni Swaa sittini" imepokewa na Ash-Sha'abiy kua Mtume (saw) alisema kumuambia Ka'ab bin U'jra: "Unacho cha kuchinja? Akasema: la, akasema: basi funga siku tatu au utowe sadaka Swaa tatu ya tende kuwapa masikini sita, Swaa moja kwa masikini wawili" na ikapokewa kutoka kwa Muhammad bin Ubeidullah Ath-Thaqafiy amesema: "Umar bin Al-Khattab aliwatoza watu wa Sawad juu ya kila Jarib iliyoamirishwa au iliyojaa maji dirhamu moja na Qafiz" na akasema Abu Ubeid katika kitabu Al-

Amwaal: “Swaa moja ni mudd nne, na mudd ni ratili moja na thuluthi kwa Baghdad, hivyo basi Swaa moja ni ratili tano na thuluthi mbili, na ndio Swaa ya Mtume (saw) kama vile anavyosema Malik na watu wa Hijaz”.

Na kwa kuzifuatilizia hadithi na maneno ya wanavyuoni wa fiqhi na wa hadithi wa maimamu wa lugha kuhusiana na uzito na uzani inabainika kua Swaa ndicho kipimo cha kupimia uzito wote ambao ulikua unatumika, na kwamba Swaa ni sawa na mudd nne, na kua mudd moja ni ratili moja na thuluthi kwa Baghdad, nakua ratili ya Baghdad ni dirham 128 3/7, na ukikadiria dirham hii kwa uzani wa gramu inaotumika leo hii uzito wake ilikua gramu 3,17, - na diramu hii sio sarafu, kwani dirhamu sarafu ya fedha ya kisheria uzito wake ni gramu 2,975 – hivyo basi uzito wa ratili ya Baghdad ni gramu 408.

Na kwa haya inabainika vipimo vya uzito na uzani wake kwa gramu na kilogramu kupitia ngano kwa sura ifuatayo:

Mudd = 1 1/3 ratili ya Baghdad
Mudd = 1 1/3 ratili mara 408 gram uzito wa ratili = gramu 544 uzito wa mudd ya ngano.
Swaa = mudd 4 uzani
Swaa = 4 mudd mara 544 gramu uzito wa mudd = 2176 gramu uzito wa Swaa ya ngano au 2,176 kilogramu uzito wa Swaa ya ngano.
Qafiz = 12 Swaa uzani
Qafiz = 12 Swaa mara 2176 gramu uzito wa Swaa = 26112 gramu uzito wa Qafiz ya ngano au 26,112 kilogramu uzito wa Qafiz ya ngano.
Wasaq = Swaa 60 uzani
Wasaq ya ngano Swaa 60 mara 2176 gramu uzito wa Swaa = 130560 gramu uzito wa Wasaq ya ngano au = 130,56 kilogramu uzito wa Wasaq ya ngano.

Na kutokamana na haya inabainika yanaofuata:

Kwa kua nisab ya zaka na Wasaq tano basi uzito wake unakua ni 652,8 kilogramu ya ngano, na kwa kua Wasaq ya tende au jibini au zabibu uzito wake unatafautiana na uzito wa Swaa ya tende hata kama itakua sawa katika uzani, kwa hivyo uzani wa nisab ya zaka ya tende au zabibu au jibini zitatafautiana uzani wake na nisab ya ngano, kwa sababu bidha hizi haziko sawa kwa uzani wake japo zitakua sawa katika uzito wake.

Na kwa kua zaka ya fitri ni Swaa basi uzito wake ni 2,176 gramu ya ngano.

Na kwa kua fidia ya kuchinja ni Swaa tatu basi uzani wake itakua 6,528 kilogramu ya ngano.

Vile vile inabainika kua uzito wa Qafiz ambayo aliiweka Umar bin Al-Khattab pamoja na dirham kama Kharaji juu ya Jarib katika ardhi ya Iraq ni sawa na kilogramu 26,112 ya ngano.

Na dirhamu aliyoiweka uzito wake ilikua ni Mithqal yaani 4,25 gramu ya fedha, na kwa kua upana wa Jarib ni sawa 1,366 dunum basi kiwango chake ndicho kile alichokiweka Umar bin Al-Khatttab juu ya dunum kama Kharaji 19,116 kilogramu ya ngano na 3,11 gramu ya fedha.

## **<u>JIZYA</u>**

Jizya ni haki ambayo Allah amewapatia waislamu kutoka kwa makafiri, kwa ajili ya kuwa chini ya utawala wa kiislamu, na waislamu hawatakuwa ni wenye kuwaingilia na wao na kuwalinda wao, ili wawe katika amani kwa kutowaingilia na salama kwa kuwalinda, na asili ya Jizya ni kauli yake Ta'ala katika sura Tauba:

{ قَاتِلُوا الَّذِينَ لاَ يُؤْمِنُونَ بِاللهِ وَلاَ بِالْيَوْمِ الآخِرِ وَلاَ يُحَرِّمُونَ مَا حَرَّمَ اللهُ وَرَسُولُهُ وَلاَ يَدِينُونَ دِينَ الْحَقِّ مِنْ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ حَتَّى يُعْطُوا الْجِزْيَةَ عَنْ يَدٍ وَهُمْ صَاغِرُونَ }

*"Piganeni na wale ambao hawaamuamini Allah na wala siku ya mwisho na wala hawaharimishi aliyoyahramisha Allah na Mtume*

*wake na wala hawafuati dini ya haki wakiwemo walioteremshiwa kitabu mpaka watowe Jizya kwa mikono wakiwa madhalili"* [TMQ: 9:29]

**<u>HUCHUKULIWA JIZYA KWA NANI</u>**

Huchukuliwa Jizya kutoka kwa watu wa kitabu (ahlul kitab) kutoka kwa mayahudi na kutoka kwa wakristo kwa dalili ya aya iliyotangulia:

{ مِنْ الَّذِينَ أُوتُوا الْكِتَابَ }

"*Wakiwemo walioteremshiwa kitabu mpaka watowe Jizya kwa mikono wakiwa madhalili*" [TMQ: 9:29] Ni sawa sawa mayahudi au manasara hao wawe ni waarabu au wasiokuwa waarabu kwa sababu Mtume (saw) aliichukua kutoka kwa mayahudi wa Yaman na kutoka kwa manasara wa Najran, imepokelewa kutoka kwa Urwa bin Zubeir amesema: Mtume (saw) aliwaandikia barua watu wa Yaman: " … na yoyoye atakebakia katika uyahudi wake au unasara wake basi huyo hatosumbuliwa ni ni juu yake atowe Jizya" na ikapokewa kutoka kwa ibn Shihab amesema: "Wakwanza kutoa Jizya ni watu wa Najran na walikua wakristo" na pia Abubakar aliichukua kutoka kwa manasara wa Hira na walikua ni waarabu, vile vile Umar aliichukua kutoka kwa manasara wa Sham wakiwemo waarabu na wasiokua waarabu.

Pia huchukuliwa kutoka kwa wasiokua ahlul kitab: kutoka kwa majusi na maswabai na mabanyani na wakomunisti, kwa sababu Mtume (saw) aliichukua kutoka kwa wamajusi wa Hajar, imepokewa kutoka kwa Hassan bin Muhammad amesema: "Mtume (saw) aliwaandikia barua majusi wa Hajar akiwalingania katika Uislamu na yoyote atakaekubali basi utakubaliwa kwake Uislamu wake na atakaekataa basi atatozwa Jizya, pia kichinjo chao hakitaliwa na asiolewe mwanamke wao" na ikapokewa kutoka kwa ibn Shihab kua Mtume (saw) alichukua Jizya kutoka kwa majusi wa Hajar, na Umar akachukua Jizya kutoka kwa majusi wa Faris, na Athman akachukua Jizya kutoka kwa Barbar, na ikapokewa kua Umar

bin Al-Khattab aliwacha kuchukua Jizya kutoka kwa majusi mpaka Abdurrahman bin Auf akatoa ushahidi kua Mtume (saw) aliichukua kutoka kwa majusi wa Hajar, vile vile ikapokelewa kua Mtume (saw) alisema:

**« سنوا بهم سنة أهل الكتاب »**

**"Muwafanyie kama vile munavyowafanyia watu wa kitab"**

Ama waarabu wenye kuabudu masanamu kwao wao haikubaliwi isipokua Uislamu ama sivyo ni upanga, kwa kauli yake Ta'ala":

{ فَاقْتُلُوا الْمُشْرِكِينَ حَيْثُ وَجَدْتُمُوهُمْ }

*"Wauweni washirikina popote mutapowapata"* [TMQ: 9:5] na neno lake:

{ سَتُدْعَوْنَ إِلَى قَوْمٍ أُوْلِي بَأْسٍ شَدِيدٍ تُقَاتِلُونَهُمْ أَوْ يُسْلِمُونَ }

*"Karibuni hivi mtaitwa kwenda kupigana na watu wenye mapigano makali mtapigana nao au watasilimu"* [TMQ: 48:16] na haya yalikua katika mwaka wa Tabuk mwaka wa tisa wa hijra, na katika mwaka huo ndio iliposhuka suara ya Bara'ah ambayo ikfaradhisha kuchukua Jizya kutoka kwa watu wa kitab, na kupigana na washirikina wa kiarabu wenye kuabudu masanamu, na ikakoma kuwepo kwa kuabudu masanamu kwa waarabu tangu mwaka wa kumi wa Hijra.

Ama watu binafsi au makundi ambayo yalikua ni waislamu na yakaritadi na ambayo yap oleo hii basi hapo itaangaliwa hali yao halisi leo hii, ikiwa walizaliwa wakiwa wamesharitadi na wala wao wenyewe hawakuritadi bali walioritadi ni mababa zao au mababu zao au mababu wa mababu wao kwa mfano kama waduruz na mabahai na ismaili na nasirin ambao wanmfanya Ali kuwa ni Mungu hawa hawatapelekwa kwa walioritadi bali watapelekwa kama wanvyopelekwa majusi na sabai hawa watawekewa Jizya na wala kichinjo chao hakitaliwa na hawataolewa wanawake wao, isipokua ikiwa wataurudisha upya Uislamu wao na wakaingia tena upya katika Uislamu basi wakati huo watatabikishiwa juu yao hukmu za waislamu.

Na ikiwa wao wenyewe wataritadi kwa mfano wakawa mayahudi au wakristo au wakomunisti au katika fikra yoyote inaokanusha Uislamu kama dini ilioshuka kutoka kwa Allah na kukanusha kua Muhammad ni Mjumbe wa Allah au kukanusha kua Uislamu sio wajibu kutabikishwa au kukanusha baadhi za aya kwa mfano wakomunisti au mfano wao basi hao wataamiliwa muamala wa waliorotadi sawa kwa sawa.

Na Jizya huchukuliwa kutoka kwa wananume wenye akili walio baleghe, na wala haichukuliwi kutoka kwa watoto na na wala wanawake, kwani Mtume (saw) wakti alipomtuma Mudha kwenda Yaman "alimuamrisha achukue dinari moja kutoka kwa kila aliebaleghe" na Umar akawaandika barua viongozi wa kijeshi "wawe wakitoza Jizya na wala wasiatoze wanawake na watoto, na wala wasiitoze ila kwa yule ambae ameshapitisha wembe" Yaani waliobaleghe, na wakti mtoto anapobaleghe au mwandazimu kupona basi Jizya itakua ni wajibu juu yake, na iwapo kubaleghe au kupona itakua katika mwanzo wa mwaka wa watu wake basi hapo atalipa juu ya mwaka mzima pamoja na wao na ikiwa kubaleghe au kupona katikati ya mwaka pamoja basi hapo atalipa kiwango chake pamoja na watu wake ili mwaka wake na mwaka wao uwe umeshikana, na pia ni wajibu juu ya makasisi katika ………….. na watu wa masinagogi na wagonjwa na vipofu na waze ikiwa wanajiweza, kwa sababu aya ya Jizya na hadithi zake ni jumla na inawakusanya, na wala hamna nass inaowachuja, na ikiwa na mafukara basi watatolewa sadaka, kwani Jizya inawaondokea wao na wala haichukuliwi kutoka kwao kwa sababu wao hawana uwezo wa kulipa, na aya inasema:

{ لاَ يُكَلِّفُ اللهُ نَفْسًا إِلاَّ وُسْعَهَا لَهَا }

*"Allah haikalifishi nafsi yoyote ila yalio sawa na uweza wake"* [TMQ: 2:286] na ikapokewa na Umar bin Al-Khattab kua alimuona mzee katika dhimiy anaomba kwa kuwabishia watu milango, akamuliza ni lipi limekufanya ufanye haya ninayoyaona? Akasema: Jizya na uzee shida, akasema: itakua tumekukosea ikiwa tulichukua Jizya kutoka kwako katika ujana wako na

baadae tukupuze katika uzee wako" na akamchukua hadi nyumbani kwake na akampatia chakula na baadae akamitisha mweka hazina wa baitul-maal na akamuamrisha amuondoshee Jizya na ampatie mali kutoka baitul-maal.

**WAKATI UPI JIZYA HUONDOKA.**

Jizya huondoka kwa Uislamu, kwani yoyote anaesilimu Jizya humuondokea katika kichwa chake, sawa sawa atasilimu mwanza wa mwaka au katikati yake au mwisho wake au baada ya kumalizika kwake, hivyo basi haitakua wajibu juu yake kitu chochote kabisa kwa kauli ya Ta'ala:

**{ قُلْ لِلَّذِينَ كَفَرُوا إِنْ يَنتَهُوا يُغْفَرْ لَهُمْ مَا قَدْ سَلَفَ }**

*"Waambie wale waliokufuru kama watawacha basi watasamehewa yaliopita"* [TMQ: 8:38] na kwa yaliopokewa na ibn Abbas kutoka kwa Mtume (saw) kua alisema: **"Hamna Jizya juu ya muislamu"** na Jizya ni kwa sababu ya ukafiri na huondoka kwa Uislamu, kwa hivyo haiwezi kukutana na Uislamu kwa namna yoyote, na ikiwa Uislamu huvunja yaliotangulia kabla yake ikiwemo shirki ukafiri na maasi basi iweje isiweze kuvunja Jizya na dogo lake? Na pia imepokewa kutoka kwa Mtume (saw) kauli yake: **"Uislamu unayayusha yaliokua kabla yake"** imepokewa kutoka kwa Masruq kua mmoja katika waajemi alisimu na ikawa Jizya inachukuliwa kutoka kwake, na akaja kwa Umar bin Al-Khattab na akasema: "Ewe amirul-muminina mimi nimesilimu, akasema: pengine umesilimu kwa kujilinda, akasema: kwani katika Uislamu hamna kitu cha kunilinda? Akasema: kipo, akasema: hapo Umar aliandika Jizya isichukuliwe kutoka kwake.

Na Jizya haiondoki kwa kifo iwapo mtu atakufa baada ya mwaka kupita kwa sababu wakati huo itakua imeshakuwa wajibu juu yake na deni, hivyo basi ni lazima lilipwe kutoka katika alichokiwacha kama madeni mengineo, na ikiwa hamna alichokiwacha basi hapo humuondokea na wala haitakuwa wajubu juu ya warithi wake, kwa sababu huenda akawa katika hukmu ya wenye shida fakiri.

Na wala Jizya hatosamehewa yoyote katika madhimiy katika wale ambao ni wajibu juu yao, kwa sababu aya na hadithi zinawajibisha kuchukua na wala sio kusamehe, na hatasamehewa isipokua wale waliotajwa katika hadithi wasamehewe, hata kama dhimiy atakua mwanajeshi katika jeshi la kiislamu, na akapigana na makafiri pamoja na waislamu au akaajiriwa katika kazi yoyote, hayo hayatamuondoshea yeye Jizya madamu atabakia katika ukafiri wake, na kwa sababu atakua anachuku mshahara kwa kujinga na jeshi au kazi.

Na huwekwa daftari maalum la madhimiy wote kulingana na dini zao na vikundi vyao na kuwekwa sehemu maalum katika idara ya Jizya itakokusana maelezo yote ya muhimu, kuanzia tarehe zao za kuzaliwa na miaka yao na vifo vyao na hali yao ya kiuchumi ili iweze juu ya msingi wake kukisia kiwngo cha kuchukua Jizya.

**<u>KIWANGO CHA JIZYA</u>**

Kiwango cha Jizya kilichokua kinachukuliwa katika zama za Mtume (saw) na makhalifa baada yake hakikuwa kimoja bali kilitafautiana kutoka sehemu moja hadi nyengine, kwani Mtume (saw) alimuamuru Muadh pale alipomtuma Yaman achukuwe "Dinari moja au kitambara cha thamani yake kutoka kwa kila aliebaleghe katika watu wa dhimiy" na Umar akawatoza watu wa Sham na Misr juu ya tajiri dinari nne na mtu wa kati na kati dinari mbili na maskini mwenye kutuma dinari moja, pia akawatoza juu ya hicho kama chakula cha wanajeshi na kuwakaribisha waislamu, na akawatoza watu wa Iraq dirhamu arubaini na nane juu ya tajiri na dirhamu ishirini na nne kwa wa kati na kati, na dirhamu kumi na mbili juu ya maskini mwenye kutuma, na pia akawatoza zaka ya maradufu juu ya wakristo wa bani Taghlab pale walipokataa kutozwa Jizya, imepokewa na Na'aman bin Zar'ah "kua alimuuliza Umar bin Al-Khattab na kuzungumza nae kuhusu wakristo wa bani Taghlab na ilikua Umar ameazimia kuchukua Jizya kutoka kwao ndiposa wakatawanyika katika nchi, na Na'aman

akasema kumuambia Umar: Ewe amirul-muminina bani Taghlab ni watu waarabu na wanaipuza Jizya na wao hawana mali bali wao ni wakulima na watu wa mifugo na wana nguvu za kupambana na adui basi usiwape nafasi maadui wako kuwatumia dhidi yako, akasema: ndiposa Umar akafanya suluhu na wao ya kwamba awatoze zaka maradufu".

Na katika Swahih Bukhari kutoka kwa Abi Najih amesema: nilimuuliza Mujahid, ni kwa nini watu wa Sham walitozwa dinari nne na watu wa Yaman wakatozwa dinari moja? Akasema: iliwekwa hivyo kwa sababu ya uweza.

Na kiwango cha dinari aliyoiweka Umar kama Jizya juu ya vichwa vya watu dhimiy kwa gramu ambayo inazingatiwa kama kiungo cha makadirio ya dhahabu leo hii ni kama ifuatavuo:

| | Dinari | uzito wa dinari kwa gramu | gramu za dhahabu |
|---|---|---|---|
| Tajiri | 4 mara | 4,25 | gramu 17 |
| Kati na kati | 2 mara | 4,25 | gramu 8,50 |
| Muajiriwa | 1 mara | 4,25 | gramu 4,25 |

Na mpaka inafahamika kua kiwango cha Jizya sio kimoja na wala hakikufungiwa kiwango kimoja ambacho haifai kukibadilisha kama vile nisab ya zaka, bali hilo amewachiwa khalifa na rai yake na ijtihadi yake, na huangaliwa humo usahali na uzito ili isiwe kuwa ni uzito juu ya madhimiy, na wala hawatozwi juu ya uwezo wao, na pia huchungwa humo isije ikadhulumiwa baitul-maal na isije ikanyimwa mali yake inaostahiki katika mashingo za madhimiy.

Na kipimo cha kiwango cha tajiri na kati na kati na fakiri hurudiliwa ada, na ufahamu wa watu wenye ujuzi katika suala hilo, hivyo basi khalifa atawateuwa watu wenye ujuzi ili kupambanua matajiri na wa kati na kati na mafukara, na ili kuweka mipaka ya tajiri na wa kati na kati na mafukara na kutoa mapendekezo ambayo yatakaowezekana kwa tajiri na wa kati na kati na mfanyikazi mwenye kuchuma, ili kiweze kiwango cha khalifa cha Jizya kuwa sawa na kile atakachofikia rai yake na ijtihadi yake juu ya msingi wa hilo, kwa kiasi ambacho hatowapeleka mbio watu madhimiy na kuwatoza juu ya uweza wao na wala isidhulumiwe baitul-maal na kupunguziwa haki yake.

**WAKATI WA KUCHUKUA JIZYA**

Jizya inastahli kwa kuingia kwa mwaka, kwani huchukuliwa mara moja katika mwaka, na mwaka huanza mwanzo wa Muharram na kumalizika mwisho wa Dhul-Hijjah na ili iweze kulipwa kabla ya kuingia kwa Muharram ya mwaka unaokuja, twaweza kuiweka miezi mitatu ya mwisho ya mwaka yaani Shawal na Dhul-Qa'ada na Dhul-Hijjah kama wakati wa kulipa Jizya ili mwaka uweze kuwa sawa mwanzo wake na mwisho wake kwa wote, na wala sio kila mtu awe na mwaka wake, na ili iweze kupatikanwa udhibiti na usahali wa kulipa.

Na watateuliwa wakusanyaji maalum wa kupokea Jizya na kuikusanya, hawa watatengewa kitengo maalum chao katika idara ya Jizya katika diwan ya Fai na Kharaji, na mishahara yao na pato lao itatoka katika Baitul-maal na wala sio kutoka kwa madhimiy.

Na wakusanyaji watazuiwa kuchukua chochote cha kuzidi kiwango kilichopangwa juu ya mtu kwa kumuadhibu kwa sababu ziada ni dhulma na dhulma ni viza siku ya qiyama, na kwa sababu itakua ni ghulul inaotokamana na wakusanyaji na ghulul ni katika moto, vile vile wakusanyaji watazuiwa kupiga au kudhibu madhimiy wakati wa kukusanya Jizya, kwa sababu Mtume (saw) alikataza hayo, imepokewa kutoka kwa Hisham

bin Urwah kutoka kwa babake kua Umar bin Al-Khattab alipita katika njia ya Sham na alikua anaregea kutoka Sham aliona watu wamesimamshwa juwani huku wanamiminiwa mafuta katika vichwa vyao, Umar akasema: wamefanya nini hawa, wakasema: wanadaiwa Jizya na hawajalipa, ndiposa wanaadhibiwa hadi watakapolipa, Umar akasema: kwani wao wanasema nini, wametoa sababu gani kuhusiana na Jizya? Wakasema : wanasema: hatuna, akasema, basi waacheni musiwakalifishe wasichokiweza, kwani mimi nilimsikia Mtume (saw) akasema:
Musiwaadhibu watu kwani wale wanaoadhibu watu katika dunia Allah atawaadhibu wao siku ya Qiyama) na akawaamrisha waachiliwe, ni ikapokewa kutoka kwa Mtume (saw) kua alimteuwa Abdallah bin Arqam kukisanya Jizya kwa madhimmi, na pindi tu alipokua anampa mgongo alimuita na akasema:

(Juweni kua yoyote atakaemdhulumu muahid au kumkalifisha zaidi ya uwezo wake au akamnyanyasa au akachukua kitu kutoka kwake pasina ridha ya nafsi yake basi mimi nitakua mpinzani wake siku ya Qiyamah).

Na yoyote katika madhimiy atakae dai hali ngumu basi atatakiwa athibitishe ugumu wa hali yake, na iwapo atathibitisha baasi atasubriwa hadi katika hali ya uepesi, na iwapo hatothibitisha na ikathubutu kua anafanya madharau basi atatiwa gerezani na atawachwa gerezani hadi atakapolipa Jizya, kwani Mtume (saw) aliwahi kumtia gerezani mwenye kupuuza deni na wala haziingiliani, na iwapo itapita miaka miwili au zaidi pasina kulipa basi haziingiliani, na inapasa kulipa zote kama vile ambavyo ni wajibu kulipa madeni yote, na wala haviuzwi bidhaa za dhimmiy kwa ajili ya kulipa Jizya.

Na dhahabu na fedha hazifanywi kuwa ndio pekee katika Jizya, bali inafaa Jizya iwe ni dhahabu na fedha na pia inafaa iwe visivyokua hivyo kwa mfano bidhaa au mnyama, pia inafaa

ikadiriwe kwa thamani na kchukuliwe chengine badali yake, kwani imepokewa katika hadithi ya kumtuma Muadh huko Yemen kua Mtume (saw) alimuamrisha achukuwe dinari moja kutoka kwa kila aliebaleghe kwa madhimiy au muafir yaani nguo, vile vile aliweka mkataba wa suluhu na watu wa Najran kwa sharti kulipa vitambaa elfu mbili nusu watakua wanalipa katika mwezi wa Safar na nusu ya pili katika mwezi wa Rajab, na Umar alikua anachukua wanyama hoa na nafaka badali ya dinari na dirham, hali kadhalika makhalifa wengine, na ili kusahalisha kulipa na kuhifadhi na ugawaji katika siku hizi Jizya inaafaa iwe ni sarafu inaozunguka.

## MATUMZI YA JIZYA

Hamna katika waislamu waliotafautiana kua matumizi ya Jizya ni matumzi ya mali ya Fai kama Kharaji na Ushur, yaani huwekwa katika Baitul-maal na kutumiwa katika masilahi wa waislamu na pia kuwekwa katika njia ya Allah (jihad) vile anavyoonelea khalifa kulingana na rai yake na ijtihadi yake katika kusimamia mambo ya waislamu na kukimu masilahi yao.

## MILKI ZA JUMUIA NA AINA ZAKE

Milki za jumia ni aina ambayo mteremsha sharia akaifanya umilikaji wake ni wa waislamu wote na akaifanya kuwa ni shirika baina yao, na kuifanya mubah kwa watu binafsi kunufaika nayo na kuwakataza kuimiliki.

Na aina hizi zinawakilishwa na aina tatu kuu nazo:
1 – Masilahi ya jumuia ambayo watu jumla hawana budi nayo katika maisha yao ya kila leo.
2 – Aina ambazo asili yake zinakua ni zenye kuwazuia watu binafsi kumiliki.
3 – Maadini mengi yasiokatika.

Hivyo basi aina hizi tatu kuu na vitanzu vyake na mapato yanapatikanwa kutokamana nazo zinakuwa ni milki ya waislamu wote ni shirika baina yao na inakuwa ni mapato

miongoni mwa mapato ya baitul-maal ya waislamu khalifa atakuwa ni mwenye kugawa kati yao vile alivyofikishwa na ijtihadi yake ndani ya ahkamu ya kisharia katika yale ambayo ndani yake muna masilahi kwa Uislamu na waislamu.

## AINA YA KWANZA YA MILKI YA JUMUIA

Ni masilahi ya watu wote, ambayo hawana budi nayo katika maisha yao yao kila leo na hutawanyika wakati wa kukosekanwa kwake, na Mtume (saw) ameshabainisha sifa za masilahi yake, na kufafanua vilivyo, katika hadithi iliopokewa kutoka kwake kuhusiana nayo, kwani imepokewa kutoka kwa Abi Kharash kutoka kwa baadhi ya maswahaba wa Mtume (saw) amesema: amesema Mtume (saw):

**{المسلمون شركاء في ثلاث, الماء والكلأ والنار }**

**"Waislamu ni shirika katika vitatu: katika maji na malisho na moto"** na katika mapokezi mengine:

**{الناس شركاء في ثلاث, الماء والكلأ والنار }**

**"Watu n shirika katika vitatu: maji na malisho na moto"** na imepokewa kutoka kwa Abi Hureira kua Mtume (saw) amesema:

**{ ثلاث لا يمنعن, الماء والكلأ والنار }**

**"Vitatu havinyimwi: maji na malisho na moto"** vile vile imepokewa kutoka kwake (saw) neno lake:

"Muislamu ni ndugu ya muislamu

Maji na malisho na moto ndivyo vya kwa katika vilivyoruhusiwa na Mtume (saw) kwa watu wote na kuwafanya ni washirika katika hivyo, na akakataza mtu yoyote kunyimwa, kwa sababu ni haki ya waislamu wote, hii ni kwa sababu watu wanakuja kutoka katika safari zao na mabedui wanaishi katika ardhi zenye mazao ambayo Allah amewaekea wanyama na kua hamna mtu anaefanya kazi ya kulima wala kupanda wala kunyunyizia maji hivyo basi ni ya yule alietangulia kuifikia, na wala haifai kwa yoyote kuifanya ni yake tu na kuwatenga watu wengine, lakini wanalisha wanyama wao na vipando vyao kwa

pamoja, na wanatumia maji yaliomo humo pia, hivyo basi watu ni shirika katika hivi.

Na suala sio tu limefungika katika vitu hivi vitatu vilivyotajwa katika hadithi zilizotangulia, bali zinakusanya kila ambavyo vimeweza kupata sifa ya asili ya masilahi ya jamii, kwa dalili kua Mtume (saw) pindi aliposema hayo:

**{الناس شركاء في ثلاث, الماء والكلأ والنار }**

**"Watu n shirika katika vitatu: maji na malisho na moto"** aliwakubalia watu binafsi ndani ya Khaibar na Taif wamiliki kisima chao umilikaji wa kibinafsi, wantumia maji yake kwa kunywa na kuwanywesha mifugo yao, na wanyama wao na mabustani yao na wala hakuwazuia kumiliki, na visima hivi vilikua vidogo na wala havikua vinahusiana na mahitaji ya jumuia, na kwa kuziweka pamoja hadithi mbili inabainika kua maji pindi yanapokua yanahusiana na mahitaji ya jumuia basi hapo yanakua ni milki ya jumuia na huzuiwa mtu binafsi kumiliki, na wakti yatakapokua hayahusiani na mahitaji ya jumuia basi yanakua ni milki ya mtu binafsi, na inaruhusiwa watu binafsi kumiliki, muhimu ni kua asli ya kitu kiwe kinahusiana na mahitaji ya jumuia, na kua jamii hawana budi nacho kitu hicho katika maisha ya kila siku, na kua lau kitakosekanwa basi jamii itatawanyika katika kukitafuta kitu hicho, kama vile kabila lilivyokua linatawanyika pindi linapokosa maji au pindi linapokosa malisho ya mifugo yao na wanyama wao, hivyo basi kila aina ambayo inahusiana na mahitaji ya jumuia na kua hawana budi nayo katika maisha ya kila siku na hutawanyika pindi kinapokosekanwa basi hiyo inakua ni milki ya jumuia.

Na kila aina ya chombo ambacho kinachotumika katika milki hiyo pia hufuata hukmu yake, na inakua ni milki ya jumuia mfano wake, hivyo basi mashine inaotumika katika kuyatoa maji ya jumuia yakiwemo ya chemichemi na visima na mito na bahari, na mashine ya kuvuta maji hayo na mabomba ya kuyafikia hadi katika majumba ya watu ni milki ya jumuia,

sawa sawa na asili ya maji yanaotolewa na kuyavuta na kuyafikisha ni milki ya jumuia, isipokua mashine hizi iwapo zitawekwa katika mito mikubwa kama Nile na Furat basi wakati huo inafaa mashine hizo kuwa ni milki ya mtu binafsi na kunufaisha mtu binafsi.

Pia mashine za kuzalisha umeme ikiwemo mishuko ya maji ya jumuia kama mapito yake na mito na nguzo zake na nyaya zake na vituo vyake ni milki ya jumuia, kwa sababu ya vitu hivi vimezalisha umeme ambao ni aina ya milki ya jumuia, ndiposa vinachukua hukmu yake, vile vile vifaa vya kuzalisha umeme na vituo vyake na nguzo zake na nyaya zake ni milki ya jumuia – hata kama vitakua ni vyenye kuzalisha umeme kwa njia ya mashine – isipokua ikiwa umeme ni ule unaotumia kwa ajili ya mafuta hata kama ni kwa uwingi na hata kwa kuangazia inafuatilia, kwa mfano uwe unatumika katika kupika au kufanya joto kuendesha mashine za viwanda au kuyayusha maadini kwa sababu wakati huo utakuwa ni moto na moto ni miongoni mwa milki za jumuia vile vile vyenye kuuzalisha na vituo vyake na vifaa vyake na nguzo zake na nyaya zake vitafuata hukmu hiyo ya mulki ya jumuia.

Vile vile vyenye kuzalisha umeme na vituo vyake na nguzo zake na nyaya zake ni milki ya jumuia, na iwapo vifaa hivi vitawekwe katika barabara jumla view vitatumia mafuta au vitatumia kwa kuangazia kwa sababu barabara jumla haifai kwa yoyote mtu binafsi au mashirika kujitengea sehemu yake na kujiwekea yeye mwenyewe na kuwazuia watu nayo, kwa sababu kuhifadhi katika milki ya jumuia haifai isipokua kwa sirikali, ama ikiwa umeme umezalishwa kupitia mashine na vyenye kuzalisha umeme huo na vituo vyake na nguzo zake na nyaya zake zikawekwa katika njia isiokua ya jumla, kwa mfano vikawekwa katika milki ya mwenyewe basi itakua ni milki ya mtu binafsi na inaweza kumilikiwa na watu binafsi umilkikaji wa kibinafsi.

Pia inafaa viwanda vya gasi na makaa ya chuma kuwa ni milki ya jumuia kwa mujibu wa asili ya gasi na makaa ya chuma ni milki ya jumuia kwa sababu hivi na maadini na katika moto na maadini nyingi na moto na katika milki ya jumuia.

## AINA YA PILI YA MILKI YA JUMUIA

Nayo ni katika aina ambayo asli ya umbile lake inazuia watu binafsi kuimiliki, na aina hii ni katika milki ya jumuia, na ikiwa ni katika masilahi ya jumuia mfano wa aina ya kwanza na inajumuishwa na dalili ya masilahi ya jumuia, isipokua asili ya umbile ya aina hii inazuia watu binafsi kuifanya kuwa ni yao kinyume na ile aina ya kwanza kwani asili ya umbile lake inazuia watu Fulani kuifanya kuwa ni yao, na kwa sababu hiyo visima vidogo ambayo havitoshelezi mahitaji ya jumuia viliweza kumilikiwa umilikaji wa kibinafsi.

Na dalili kuhusiana na asili ya aina hii kua ni katika milki ya jumuia mbali na dalili za ile aina ya kwanza ni neno la Mtume (saw):

**{مِنى مناخ من سبق}**

**"Mina ni sehemu ya mapumziko ya alietangulia"**na kama ilivyopokewa kutoka kwa Mtume (saw) kwa kunyamazia kwake watu katika kuimilki njia jumla, na kutooruhusu mtu kuifanya kuwa ni yake pekee, na Mina ni sehemu inaojulikanwa nje ya Makka tukufu, na ni sehemu ambayo mahujaji wanashukia baada ya kumaliza kusimama Arafah, ili waweze kutekeleza matendo maalum ya Hija, kama kurusha mawe na kuchinja na kuchinja mnyama na kulala, na asili ya maana yake kua ni mapumziko ya alitangulia ni kua ni milki ya waislamu wote, hivyo basi yoyote atakaetangulia sehemu yoyote humo na akapumzika basi ni yake, kwa sababu ni shirika kati yao na wala si milki ya mtu yoyote mpaka iwe mtu atazuiwa nayo, na vile vile njia jumla kwani Mtume (saw) alikubalia watu washiriki katika hilo, na wote wana haki ya kuipita, na akafanya

kuondosha chenye kudhuru ni swadaqa, kama ilvyokuja katika hadithi:

**{ تميط الأذى عن الطريق صدقة }**

**"Kuondosha chenye madhara katika njia ni swadaqa"** na akakataza kukaa njiani kwa kusema:

**{ إياكم والجلوس في الطرقات }**

**"Jiepusheni kukaa katika njia"** kwa sababu kukaa huenda ikawazuia watu kupita na kuwadhiki wao.

Na kwa mwenye kudadisi hali halisi ya watu ndani ya Mina na hali halisi ya barabara jumla atakuta kua asili ya umbile lake inazuia mtu maalum kuifanya ni yake na kuimiliki, hivyo basi Mina watu hushukia huko ili watekeleze baadhi ya amali za Hija, na asli ya umbile lake kwa kua ni sehemu ya kutekeleza matendo ya hija kwa waislamu wote ndiposa ikazuiwa mtu binafsi kuifanya ni yake pekee au watu binafsi, na mfano wake ni Arafah na Muzdalifa, na barabara jumla pia ni ya wote, na njia za kupitia wote, na wala haiwezekani kuifanya ni ya mtu binafsi au watu binafsi, kwa hivyo dalili zilizopokewa kuhusiana nazo zinaingiliana na kila aina ambayo asili yake huzuia kuifanya kua ni ya mtu fulani, au watu fulani na inakua ni milki ya jumuia, hivyo basi bahari na maziwa na visiwa njia na kanali mfano wa Suez kanal na sehemu jumla za matambezi na misikiti ni milki ya jumuia ya kila mmoja katika raia.

Pia zinazohusiana na milki ya aina hii ya jumuia ni magari moshi na barabara na nguzo za umeme na mabomba ya maji na mabomba ya maji taka ambayo hupitia katika mabarabara jumla kwani zote hizi zinakua ni milki ya jumuia sambaba na asili ya njia kua ni milki ya jumuia, na wala haifai kuwa ni milki ya mtu binafsi kwa sababu haifai kwa mtu binafsi kuitengea kitu ambacho ni katika milki ya jumuia kwa sura ya milele, na wala kuhifadhi katika kile ambacho ni cha watu wote kwa mujibu wa kauli ya Mtume (saw):

**{ لا حمى إلا لله ولرسوله }**

**"Hamna kuhifadhi isipokua kwa ajili ya Allah na Mtume wake"** yaani hamna kuhifadhi isipokua kwa sirikali, na maana ya hadithi ni kua haifai kwa yoyote kujhifadhia nafsi yake kile ambacho ni cha watu jumla, na yule aliefanya magari moshi na mabarabara na nguzo ya umeme na mabomba ya maji na mabomba ya maji taka ambayo yapo katika njia ya jumuia ni milki ya jumuia, huchukua sehemu asili ya asili ya barabara jumla kwa sura ya daima, na hifadhiwa kwa sura ya daima ndiposa ikawa ni hima, na hima haifai kwa isiokua sirikali, hivyo basi inakua ni milki ya jumuia.

## AINA YA TATU YA MILKI YA JUMUIA

Nayo ni maadini mengi yasiokatika, isiokua na kiasi cha kukadiriwa, ama maadini kidogo inaoweza kukisiwa kiwango chake hiyo inakua ni milki ya kibinafsi na inafaa kumilkiwa na watu binafsi kama vile ambavyo Mtume (saw) alivyommilikisha Bilal bin Al-Harith Al-Muzni maadini kidogo ya upande wa Al-Far'a huko Hijaz, na Bilal alimuomba Mtume (saw) ampatie, ndiposa Mtume (saw) akampatia na kummilikisha , hivyo basi akiba ya dhahabu na fedha na maadini mengineo yaliopo ya kiasi kidogo isiokua ya biashara inakua ni milki ya kibinafsi na pia inafaa kumilkiwa watu binafsi, vile vile inafaa kwa Dola kuwapatia, lakini ni wajibu wao watoe Khums ya kile wanachikitoa humo kuipatia Baitul-Maal kiwe kinachotoka ni kidogo au kwa uwingi.
Ama maadini mengi isikua na kiasi hiyo inakua ni milki ya jumuia ya waislamu wote, na wala haifai mtu binafsi kuifanya kuwa ni yake tu au watu binafsi au kumilikshwa, au kupewa mtu au watu binafsi, vile vile haifai kuwapatia watu fulani tu wawe ni wenye kuitoa au shirika bali ni wajibu ibakie kuwa ni milki ya jumuia ya waislamu wote shirika baina yao, na Dola itasimamia kuitoa na kuisafisha na kuiyayusha na kuiuza kwa niaba yao na kuweka pato lake katika baitul-maal ya waislamu, na hamna tafauti iwe maadini hayo yawepo waziwazi watafikiwa pasina shida au kazi kubwa, kama vile chumvi na makaa ya chuma au yawe yapo ndani ya ardhi na chini na wala

hayawezi kutolewa isipokua kwa na mashaka na kazi na juhudi kubwa kama vile dhahabu na fedha na chuma na shaba na risasi Na Bati na kauri na Urenium na fosfati na madini mengine,sawa yatakuwa makavu kama dhahabu na chuma au yenye kububujika kama mafuta/petrol na gesi ya kawaida

**والقصدير، والكروم، واليورانيوم، والفوسفات**

ama dalili juu ya kuwa madini haya ni mengi si yenye kupangiwa kiwangu hayo ni katika Umiliki wa jumla /wa watu wote,ni yale waliopokelewa toka kwa Abyadh bin Jamal Al-maaziniy kwamba yeye alifika kwa Mtume (S.a.w)akamuomba amkatie chumvi basi akamkatia,punde alipoondoka akasema Mtu Fulani katika kikao hichoUnajua kile ulihcomktia ?bila shaka umemkatia maji/kisima kisichokatika.akasema :akakirejesha toka kwake,kule kuwa Mtume (S.a.w)amekirejesha kile alichompa Abyadh bin Jamal katika Chumvi baada ya kujua kuwa ni nyingi haikatiki,haifai kumilikiwa na mtu mmoja kwa sababu ni milki ya Waislamu wote,na jambo hili sio khasa/maalum kwa chumvi,bali inaenea hukmu hii kwa kila madini ya aina yeyote ile,na kwa kile kilichopo katika sharti la maji yasiokatika yaani yasiokatika.

Na pamoja kwamba madini ambayo hayakatiki ni katika miliki ya umma kwa raia wote,kwa ajili hii hairuhusiwi kwa dola kuwamilikisha watu Fulani,au mashirika na wala kuruhusu watu na mashirika kuyachimba kwa hesabu zao,bali ni wajibu serikali isimamie yenyewe uchimbaji wa maadini kwa niaba ya waislamu,na kusimamia mambo yao na yawe yote yanayochombwa ni yenye kumilikwa na umma kwa raia wote.

Na kuchimba madini ,khasa yale yanayokuwa ndani ya Ardhi,sawa ni yenye kububujika au yale makavu,yanahitaji vyombo na viwanda,na dola katika kila hali ,itachimba madini haya kwa hesabu za raia kwa kuwa ni miliki ya umma,na huku kuchimba ima kutafanywa moja kwa moja na dola kwa vyombo na viwanda inavyovimiliki au viwanda vya umma au inaweza ikaifanya kazi hii kwa njia ya watu itakaowalipa kwa kule

kufanya kazi au kwa manufaa au kwa vyombo wanavyovimiliki.
Na ikiwa dola itatoa madini haya kwa vyombo na viwanda inavyovimiki,hakika umiliki wa viwanda viwanda hivi na vyombo inajuzu kubaki ni milki ya Dolan a inajuzu kwa dola kuvigeuza kuwa ni milki ya Ummah,na hili ni bora kuliko ikabaki kuwa ni milki ya Dola,ili ichukuwe hukmu ya umiliki wa madini,yaani viwe ni milki ya umma kwa kufuata umiliki wa madini ambayo inayazalisha kwa kuchukua uharamu wa kutengeneza pombe au uharamu wa kumiliki viwanda vya pombe,kwa kufuata kuharamishwa kwa pombe kunakochukuliwa toka hadithi ya Anas

**من حديث أنس " لعن رسول الله صلى الله عليه وسلم في الخمرة عشرة: عاصرها ومعتصرها..."**

Anas (r ) Amemlani Mtume wa Mwenyezi Mungu katika pombe watu kumi,mgemaji na mgemewa…..Hadithi,na kutoka katika hadithi iliopokelewa toka kwa Ibn Omar;

**ومن الحديث المروي عن ابن عمر" لعنت الخمرة على عشرة وجوه: لعينها، وشاربها، وشاقيها، وبائعها، ومبتاعها، وعاصرها، ومعتصرها..."**

Imelaniwa pombe kwa namna kumi:pombe yenyewe,na mnywajiwake,na mmiminaji wake ,na muuzaji wake na mnunuzi wake na mgemaji wake na mgemewa wake.Hadihti.
Basi hadithi hizi zimeharamisha kugema pombe na kuitengeneza,pamoja kwamba kukamua zabibu si kwa ajili ya pombe ni jambo lenye kuruhusiwa,lakini kukamua zabibu kwa ajili ya pombe ni haramu na kwa ajili hii imeharamishwa kutengeneza pombe,na imeharabishwa kufatana na hilo kumiliki viwanda vya kutengeneza pombe na kutoakana na haya imekuja ruhusa ya kuweka vyombo na viwanda ambavyo vinamilikiwa na dola kwa ajili ya kuchima madini yanayopatikana kwa wingi kuwa milki ya umma kwa kule kufuatana na kwamba madini haya ni milki ya umma,na kwa ajili hii inakuwa thamani ya vyombo na viwanda hivi ni katika mali za milki ya umma.
Ama dola kuchimba madini haya kupia watu binafsi kwa kuwalipa mshahara kwa kazi waliofanya,au kuwapa manufaa au kwa vyombo ambavyo wanavimiliki ,kwa hakika vitabaki

vyombo hivi na viwanda hivi ni milki binafsi kwa wanavimiliki,kwa kuzingatia kuwa viwanda vyenyewe kama venyewe ni katika mali za milki binafsi,na alikubali Mtume (S.a.w) kwa watu binafsi kumiliki viwanda milki binafsi na alitengeneza kwao minbari yake na pete yake.
Isipokuwa umilki binafsi wa vyombo na viwanda hivi hauwaruhusu wamiliki kuvitumia kuchimba madini yanayopatikana kwa wingi kwa ajili yao,kwa sababu madini haya ni milki ya waislamu wote,na wala haijuzu mmoja wao akayafanya ni binafsi yake pasina wengine,lakini wanaruhusiwa kuikodisha dola kwa malipo maalum yaliopangwa,ili ivitumie katika kuchimba madini haya,na yote yanayochimbwa ni milki ya umma kwa waislamu wote,na yatawekwa mapato yake katika Baitil Mali ya waislamu katika ofisi ya milki ya umma kwa sababu Baitil mali ndio hifadhi yake,na ijapokuwa inamilikiwa na waislamu wote.
Kwa ajili ya haya inajuzu kuwa vyombo na viwanda vya kuchimba madini yanayopatikana kwa wingi na mafuta ni milki ya dola,au inamilikiwa milki ya umma,kama vile inajuzu kwa vyombo na viwanda hivi kuwa milki binafsi kwa watu au makampuni yatakayoikiodisha dola.

## NAMNA YA KUNUFAIKA NA VITU VYA UMMA NA MAPATO YAKE

Pamoja kwamba vitu vyenye kumilikiwa kama mali ya umma,na mapato yake ni milki ya waislamu wote,wakishirikiana baina yao,kwa hakika kila mmoja katika raia ana haki ya kunufaika na mali ya umma na mapato yake,hakuna tofauti ya kuwa ni mwanamme au mwanamke,mdogo au mkubwa,mwema au mwovu.
Na vitu vilivyo mali ya umma haviko sawa katika namna ya kunufaika navyo,vingine inakuwa wepesi kwa mwanaadamu kunufaika navyo moja kwa moja,na vingine si rahisi kunufaika navyo moja kwa moja.

**Ama sehemu ya kwanza**:ni kama vile maji na majani na moto na njia za watu wote na bahari na mito na mabwawa na na Mifereji mikubwa.
Mtu anaweza kunufaika navyo moja kwa moja yeye mwenyewe kwa kuyatumia maji na majani na moto,ataingia katika visima na chemchem na mito ili anywe,na abebe maji toka humo na awanyweshe wanyama wake na mifugo yake,na ataingia katika machungio ili achunge/alishe humo wanyama na mifugo yake na anaingia sehemu za kukata kuni ili akate kuni humo.
Na anaweza kuchomeka chombo chake katika mito mikubwa,ili amwagilie mimea na miti yake,kwa sababu mito mikubwa inawatosha watu wote,na kuchomeka vyombo vyake khasa hakuwadhuru waislamu wengine/hakumdhuru muislamu yeyote,kama vile kila mtu ana haki ya kunufaika na njia ya watu wote na bahari na mito na mifereji mikubwa kama vile mfereji wa Suwez,ana haki ya kupita katika njia ya wote yeye mwenyewe,na wanyama wake na gari yake na ana haki ya kukatiza baharini na kwenye mito na kwenye mifereji mikubwa kwa kutumia merikabu na meli zake kwa sababu hamdhuru muislamu yeyote,na wala hamzuii yeyote kwa ule upana na ukubwa wa njia ya wote,bahari,mito na mifereji .

**Na amma sehemu ya pili**:katika vitu vya milki ya uma,navyo ni vile ambavyo si rahisi kunufaika navyo moja kwa moja na inahitajika mashaka na kushoka na kuvitoa,kama mafuta/petrol na gesi na madini,hakika dola ndio ambayo inasimamia vitu hivi na kuvitoa kwa niaba ya waislamu,na itaweka mapato yake katika baitil mali ya waislamu,na anakuwa khalifa ndio mwenye uwezo/maamuzi ya kugawa mapato yake kwa mujibu inavyopelekea ijtihadi yake kwa mujibu wa hukmu za sheria,kwa yale anayoyaona yanahakikisha maslahi ya waislamu.
Na inawezakana kufuatwa katika ugawaji mapato ya milki ya umma kwa sura ifuatayo:
**Kwanza** : kuhudumia vile vinavyohusiana na milki ya umma,basi ihudumie :

1- Diwani/ofisi ya milki ya umma,majengo yake,ofisi zake,madaftari/sijili zake ,tafiti zake na wafanyakazi wake.
2- Wataalamu bingwa,washauri wa kitaalamu,wabunifu,wafanya kazi ambao wanafanya kazi ya utafiti na ugunduzi na utafutaji wa mafuta/petrol,gesi na madini,na kuyachimba,kuyadhalisha,kuyatengeneza na kuyafanya yafae kutumika na wale wanaofanya kazi ya kuyachimba maji na kuyafikisha kwa watu na wale wanaozalisha umeme na kuufikisha kwa watu.
3- Kununua vyombo na viwanda,na vyombo vya usafiri vya lazima vya kuchimbia mafuta,gesi na kuisafisha,na kuzalisha madini na kuyasafisha na kuyafanya yafai kutumika,na vyombo na viwanda vya lazima vya kutengenezea vitu vya milki ya umma na kunufaika navyo.
4- Na vyombo vya kuchimbia maji na kuyakusanya na kuyasafisha na mabomba ya kuyafikisha(kwa watu)
5- Na vyombo vya kuzalishia umeme.na vituo vya kusambaza umeme na nguzo pamoja na nyaya zake.
6- Na Treni/magari moshi na viberenge.

Matumizi yote haya yanahusiana na milki ya umma na uendeshaji wake na kuhudumia njia za kunufaika nayo,kwa ajili hii imekuwa mahitaji ya matumizi yake yatoke katika mapato ya milk ya umma,kama vile wanalipwa wale wanakusanya zaka toka katika mali ya zake

**{والعاملين عليها}**

[…Na wanaozitumika TMQ 9:60 ]

Kwa hakika Mwenyezi Mungu amewawekea fungu lao kutoka katika zaka ikiwa ni malipo ya kule kufanya kwao kazi ya kukusanya zake.

**Pili** :kuwagaia raia ambao ndio wanamiliki hizi milki ya umma,na mapato yake,na ugawaji huu hatofungwa khalifa na aina Fulani maalum,yeye anaweza kuwagaia toka katika vitu vya milki ya umma kama maji,na umeme na mafuta/petrol na gesi,yote wanayoyahitaji katika matumizi yao binafsi katika majumba yao na masoko yao pasina

kulipia.na yeye anaweza akawauzia vitu hivi kwa bei ya uletaji /gharama za kuvileta au kwa bei ya sokoni,kama vile anaweza kuwagaia hela toka faida ya milki ya umma,atafanya katika yote hayo yale anayoyaona yana kheri na maslahi kwa raia.

**Tatu** :pamoja kwamba matumizi ya dola siku hizi yamekuwa ni makubwa mno ,baada ya kupanuka majukumu yake,na kuzidi matumizi yake,na pamoja kwamba mapato ya umma yanayosthiki baitil mali miongoni mwa ghawira,jiz'yah,kharaji,ushuur na khumsi hunda visitosheleze matumizi ya dola,kama hali ilivyokuwa zamani,siku za Mtume (S.a.w) na Makhalifa baada yake,na siku za utawala wa Bani Umayah na Abasiya mpaka siku za utawala wa Uthmaniyah,baada ya kundelea njia za maisha na namna mbali mbali za madaniyah kuendelea kukubwa hasa yale yanayohusiana na silaha za kivita nay ale yaliofikiwa katika maendeleo yenye kutisha jambo ambalo linahitaji matumizi ya ziada,kwa sababu hii imekuwa hapana budi dola iwe na njia nyingine (ya kupata hela) ili kuweza kukidhi matumizi yake ya lazima katika baitil mali,katika hali ya kuwepo hela au kutokuwepo,na ambayo utahama uwajibu wa kuhudumia kwa waislamu wakati inapokuwa hakuma mali katika baitil mali,nayo ni kama huduma na gharama za ofisi mbali mbali na ofisi za dola,na kama badala/posho za watawala na vyakula vya askari na mishahara ya wafanya kazi na gharama za kuleta maji na ujenzi wa bara bara,shul,vyuo vikuu,misikiti na mahospitali ambavyo vinahesabika na vitu vya lazima na umma hauwezi kuepukana navyo na utafikwa na madhara vinapokosekana.

Na kama vile kuhudumia masikini na mafakiri,wasafiri,mayatima,wajane na vikongwe wenye haja,na kama kuhudumia faradhi ya Jihadi na kutayarisha jeshi lenye nguvu na kuleta yale yanayohitajiwa na jihadi ikiwemo viwanda vizito vya kuzalisha silaha za kisasa,makombora na nyinginezo,miongoni mwa makombora ya masafa marefu,ndege,vifaru,Makombora ya

kujihami NA Manuari NA NYINGINEZO Ikiwa ni kuitikia kauli ya Allah Mtukufu :-

{وأعدوا لهم ما استطعتم من قوة ومن رباط الخيل ترهبون به عدو الله وعدوكم وآخرين من دونهم لا تعلمونهم الله يعلمهم}.

[basi waandalieni(wawekeeni tayari) nguvu mziwezao (silaha) na mafarasi yaliofungwa (kufunga) ,tayari tayari(mipakani )ili kwazo (nguvu hizi )muogopeshe maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui zenu,(mnaowajua) na pia (maadui zenu)wngine wasiokuwa wao,msiowajua nyinyi (lakini)Mwenyezi Mungu anawaju.TMQ 9:60]

Basi sehemu zote hizi zinahitaji vyanzo vikubwa vya kuhudumi,na wala hana njia khalifa ya kukidhi gharama za vitu hivi isipokuwa kwa moja ya njia tatu,zaidi ya yale yanayotokea na kupatikana katika kufungua miji,na njia hizi ni :-

1-kukopa toka dola za kigeni na mshirika ya mali ya kimataifa.

2-kuhifadhi baadhi ya vitu vya milki ya umma ,miongoni mwa mafuta,gesi na madini.

3-kuweka kodi kwa raia.

**1- <u>KUKOPA TOKA DOLA ZA KIGENI</u>**

Ama kukopa tola dola za kigeni,ku na mshirika ya mali ya kimataifa hairuhusiwi kisheria,kwa sababu kukopa toka huko hakutimii mpaka kwa faida zenye riba,na kama si hivyo basi kwa masharti.na faida za riba ni haramu kisheria,sawa ni kwa watu mmoja mmoja au kwa dola,na masharti yanazifanya dola na mashiriki yenye kukopesha yatawale waislamu,na kufanya uongozi wa waislam na matumizi yak yako rehani/yamedhibitiwa kwa matakwa ya dola na mashirika yenye kukopesha,na hili hairuhusiwi kisheria,na kwa hakika imekuwa mikopo ya kimataifa ni hatari na balaa kwa miji ya kiislam,na imekuwa ni sababu ya makafiri kutawala waislamu,na mara nyingi umma umetatizika na maangamivu yake,kwa ajili hii mikopo ya kimataifa haruhusiwi khalifah kuilkea ili kukidhi mahitaji ya sehemu hizi za dola.

2- KUHIFADHI BAADI YA VITU VYA MILKI YA UMMA

Ama kuhifadhi baadhi ya vitu vya milki ya umma ,miongoni mwa mafuta,gesi na madini,kama kutenga Khalifa visima maalum vya mafuta/petrol na gesi na machimbo maalum katika machimbo ya madini kama vile machimbo ya fosfati,dhahabu na shaba kwa mfano,akayahifadhi,na akahusisha mapato yake kwa kuhudumia sehemu hizi ambazo tumezitaja,kuhifadhi huku ni ruhusa kisheria,nayo ni njia yenye kufaulu kwa kuongeza hudumu/mahitaji ya lazima ya kuhudumia sehemu hizi,na ni ruhusa kwa Khalifah kufanya hivyo kwa kutegemea haya yafuatayo :-

**1-** Hakika Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) na Makhalifah baada yake ,walihifadhi mahala/sehemu maalum ambazo ni katika milki ya umma.toka kwa Ibn Abbas,toka kwa Asswa'ab bin Juthamah amesema:amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w)

**(لا حمى إلا لله ولرسوله)**

( haifai kuhifadhi/kuhami isipokuwa kwa ajili wa Mwenyezi Mungu na kwa ajili ya Mtume wake) yaani hakuna kuhifadhi isipokuwa kwa dola kwa mfano wa alivyohifadhi Mwenyezi Mungu na Mtume wake kwa ajili ya Jihadi ,mafakiri na Masikini,na kwa maslahi ya waislamu wote,hapana si kwa mfano wa walivyokuwa wakihifadhi katika zama za kijahilia kwa kuwa kujihifadhia mtu mtukufu kwa ajili yake binafsi.

Toka kwa Nafi'i toka kwa Inb Umar :"kwama Mtume (S.a.w) alihifadhi eneo la ANNAQI'IA-Ni sehemu maarufu katika mji wa madina- kwa ajili ya farasi wa Waislamu" na kadhalika alihifadhi Abubakar eneo la ARRABADHA kwa ajili ya ngamia wa sadaka na akamfanya kiongozi wa hapo ni ndugu yake Abu usama,na pia Omar kadhalika aliifadhi eneo la ASHARAF ndani ya eneo la ARRABADHA na akamfanya kiongozi wake ni ndugu yake akiitwa HUNAYYU.

Na kwa hakika ilikuwa kuhifadhi huku ni sehemu za majani na machungio/malisho,nayo ni katika milki ya umma.eneo la ANNAQI'IA ambalo alilihifadhi Mtume (S.a.w) lilikuwa nje ya Mji Wa Madina,lilikuwa likibubujisha maji na pindi yakikauka huona hapo majani,yaani eneo hilo ni milki ya waislamu wote,na alisema Abuubaida katika kubainisha hilo baada ya kutaja kwake hadithi "( haifai kuhifadhi/kuhami isipokuwa kwa ajili wa Mwenyezi Mungu na kwa ajili ya Mtume wake)"akasema "na ta'awili ya kuhifadhi kulikokatazwa kama tunavyoona-na Mwenyezi Mungu ndio Mjuzi – ni kuhifadhi vitu ambavyo Mtume wa Mwenyezi Mungu amevifanya kwa watu ni vya kushirikiana .navyo ni maji,majani na moto"

Na kwa hakika alihusisha Mtume (S.a.w) na Abubakari na Umar sehemu ambazo wamezihifadhi kwa ajili ya farasi ambao walikuwa wanabeba silaha na askari katika njia ya Mwenyezi Mungu,na ngamia na mifugo ya sadaka na walikuwa wakizuia kuchungia mifugo mingine katika sehemu hizo.

Toka kwa A'mir bin Abdillah bin Zubeir toka kwa Baba yake amesmea "Bedui mmoja alimjia Umar bin Khatwa'b akasema : Ewe Amirul muuminina,Miji yetu tumepigana juu yake katika ujahilia,na tukasilimu juu yake katika Uislamu,kwa nini unaihifahdi/unatenga sehemu maalum?! Amesema :akanyamaza Umar na akawa akipuliza na akivuta sharubu zake – na alikuwa akizidiwa na jambo alikuwa akivuta sharubu zake na akipuliza – na yule Mbedui alipoona hivyo basi akawa anakariri kauli yake ,akasema Umar :Mali ni mali ya Mwenyezi Mungu na waja ni waja wa Mwenyezi Mungu ,Wallah lau kuwa si haya niliohifadhi katika njia ya Mwenyezi Mungu nisingehifadhi tena hata shubiri moja kwa shubiri moja" na toka kwa Aslama amesema: "Nimemsikia Umar bin Khata'b na hali kuwa akimwambia HUNAYYU Wakati alipomfanya ni

kiongozi katika hifadhi ya ARRABADHA : Ew Hunayyu Kunja ubawa wako kwa watu,na Ogopa dua ya Mwenye Kudhulumiwa,kwa sababu ni yenye kukubaliwa,na mungize mwenye ngamia na mbuzi wachache na cha kuwaingiza ngamia wa Ibn Affan na Ibn Aufi kwa sababu ikiwa itakufa mifugo yao watarudi katika( kazi ya) kilimo na kwenye mitende,lakini masikini huyu ikiwa itakufa mifugo yake atarudi halikuwa anapiga kelele/analia,Ewe Amirul-muuminana ,hivi majani/malisho ni rahisi kwangu au kulipa deni la dhahabu na fedha?na kwa hakika hiyo ni ardhi yao ,walipigana juu yake katika zama za ujahilia,na wamesilimu juu yake katika Uislamu,na hakika wao wanatuona kuwa tunawadhulumju,na lau kuwa sio ngamia wanabebeshwa katika njia ya Mwenyezi Mungu,nisingehifadhi kwa watu sehemu yeyote katika miji yao kamwe.

Hadithi na athari hizi zinaonyesha ushahidi wa wazi kuwa serikali inaweza kuhifadhi katika milki yaumma yale inayoyahitaji kwa ajili ya jihadi nay ale yanayohusiana nayo na mengineyo katika maslahi ya waislam kwa kiasi chochote kitakachofikia.

2- Hakika Mwenyezi Mungu Mtukufu amefaradhisha jihadi kwa waislamu wote,matajiri wao na masikini wao,na amewafaradhishia wapigane kwa mali zao na nafsi zao,amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu :-

{لكن الرسول والذين آمنوا معه جاهدوا بأموالهم وأنفسهم وأولئك لهم الخيرات، وأولئك هم المفلحون}

[Lakini Mtume na wale walioamini pamoja naye walipigania (dini) kwa mali zao na nafsi zao na hao ndio watakaopata kheri ,na hao ndio wenye kufuzu (kufaulu ) TMQ :9 88]

Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu :-

{إن الذين آمنوا وهاجروا وجاهدوا بأموالهم وأنفسهم في سبيل الله}

[Hakika wale waliaomini na wakahama na wakapigania dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na nafsi zao..TMQ :8 72]

Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu :-

{إنما المؤمنون الذين آمنوا بالله ورسوله، ثم لم يرتابوا، وجاهدوا بأموالهم وأنفسهم في سبيل الله أولئك هم الصادقون}

[Wenye kuamini kweli kweli ni wale waliomuamini Mwenyezi Mungu na Mtume wake,kisha wakawa si wenye shaka,na wakaipigania dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zao na nafsi zao .Hao ndio wenye kuamini Kweli .TMQ 49: 15 ]

{وقاتلوا في سبيل الله}

[Na piganeni katika njia ya Mwenyezi Mungu ….TMQ 2: 190 ]

Na amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu :-

{قاتلوا الذين لا يؤمنون بالله ولا باليوم الآخر}

[Piganeni na wale wasiomuamini Mwenyezi Mungu wala siku ya mwisho TMQ 9:29]

{وقاتلوا المشركين كافة، كما يقاتلونكم كافة}.

[Na nyote piganeni na makafiri kama wao wote wanavyopigana nanyi TMQ 9:36 ]

Basi aya hizi ziko wazi kabisa katika uwajibu wa waislamu kupigana jihadi kwa nafsi na kwa mali,na kwa hakika walikuwa waislamu siku za Mtume (S.a.w),na Makhalifa baada yake wakitoka kwenda jihadi kwa mali zao na nafsi zao,na walikuwa wakifanya maandalizi ya jihadi wenyewe kwa yale wanayaoyahitaji katika jihadi,miongoni mwa silaha,farasi,ngamia na akiba za safari pasina kusubiri matayarisho ya dola iwatayarishie,kwa sababu hayo ni katika walifaradhishiwa na Mwenyezi Mungu juu yao.

Kwa kutokana na hayo,kwa hakika kuhudumia jihadi nay ale yanayohitajika unahamia kwa waislam pale wanapokuwa waislamu hawana katika Baitil'mali mali za kutosha kuhudumia,na juu ya khalifah azipate mali hizi za lazima kwa jihadi kwa waislamu,au achuku katika mapato ya mali ya milk ya umma ambayo ni milki ya waislama,kwa kuhifadhi kile kitakachoziba /kitakachokidhi huduma hizi badala ya kuzikusanya kutoka kwa waislamu.

3- Hakika Umar bin Khata'b alikataa kuigawa ardhi ya Iraqi na Sham na Misri kwa wale ambao waliozifungua kwa panga zao baada ya kumtaka awagaie,pamoja na kujua kuwa wao wamezikomboa kwa panga zao,na zimekuwa ni ngawira zao,na aikijua kuwa ngawira hugaiwa kwa wale waliozipata/zileta na kwamba mafungu manne kati ya matano ni ya wale wapiganaji ambao walishiriki vita,na akijua kuwa Mtume (S.a.w) aliigawa ardhi ya Khaybara kwa wapiganaji ambao walishiriki vita hiyo,pamoja na haya alikataa kuwagaia ardhi kwa kuegemea ufahamu wake wa aya ya ghawira,na kujua kwake kuwa hapana budi kuwepo na vyanzo vya kudumu na vyenye kuthubiti hutolewa humo malipo na kuhudumia maslahi ya dola,majeshi na kulinda mipaka,na mafakiri na masikini,mayatima na wajane,na atalipwa yule anayesimamia maslahi ya waislamu.na hili limejitokeza wazi katika majadiliano yake na wao wakati walipomtaka awagaie ardhi hiyo,na katika kuonyesha hoja zake mbele ya Answar ambao aliwakusanya wote kuwataka ushauri,kiasi alisema :- "itakuwaje kwa waislamu watakaokuja baada yao,watakapoikuwa ardhi yote imegaiwa na imrithiwa toka kwa Baba na Mababa na imekusanywa kwa wenyewe,hii sio rai nzuri" na akasema : "pindi nitakapoigawa ardhi na mali asili zake Iraq,ardhi ya shamu na maliasili zake,ni kipi kitakidhi mahitaji ya mipaka,na watoto na wajane wa miji hii watapata nini,na pia ni vipi kwa ardhi nyingine zisizokuwa za shamu na Iraq ? "na akawaambia Maanswar : "name nimeona nihifadhi ardhi za nchi zote mbili pamoja na maliasli zake na niwawekee wakazi wake kodi ya mazao na katika shingo zao kodi ya kichwa(Jiz'yah) watazitoa itakuwa ni ngawira kwa waislamu.wapiganaji na watoto/vizazi.hivi hamuoni mipaka hii ? hapana budi wawepo wanamume wa kuilinda,hivi hamuoni miji hii mikubwa kama Shamu,Jazira,Kufa,Basra na Misri hapana budi ijazwe Majeshi,na kuwapatia huduma hao wanajeshi,ni kutoka wapi watapewa huduma ikiwa ardhi na mali ghafi zitagaiwa?"Mazungmzo haya,na hoja

hizi,zinabainisha kuwa Umar alikuwa akitambua kuwa hapana budi kuwepo vyanzo vya kudumu na vyenye kuthibiti kwa ajili ya kuhudumia jihadi,na sehemu ambazo ni wajibu kwa dola kuzihudumia,akaona kwamba ardhi hizi zilizofunguliwa katika Iraq ,Shamu na Misri ndio vyanzo vinavyohitajika,kwa sababu hii hakuvigawa kwa wale ambao walizikomboa,nao ni waislamu wachache ,na kuzibakisha kwa wenyewe kwa makubaliano ya kutoa kodi ya mazao ili ij ihudumie maslahi ya waislamu wote.na kutokana na haya inachukuliwa kuwa ni ruhusa kwa Khalifah kwa njia bora ahifadhi vile ambavyo ni milki ya umma,ili vihudumie sehemu ambazo ni wajibu kwa waislamu kuzihudumia katika hali ya kutokuwepo Baitil'mali kwa waislamu.

## MALI ZA DOLA IKIWEMO ARDHI,MAJENGO NA KILA VINAVYOHUSIANA NA MAPATO YAKE

Kila kitu katika ardhi,au jengo linalohusiana na haki ya waislamu wote na wala halikuwa ni katika milki ya umma,inakuwa ni milki ya Dola,milki ya Dola ni vile vitu vyote vinavyokubali Milki binafsi,kama vile Ardhi na Majengo na vitu vyenye kuhamishika,lakini vina mahusiano na haki za waislamu imekuwa ndio inayopangilia,na kusimamia mambo yake na matumizi yake yametegemezwa kwa Khalifa,kwa sababu yeye ndio mwenye uwezo wa kupanga matumizi kwa kila kinachohusiana na haki za waislamu.na zama vilipokuwa vitu hivi havipo katika milki ya umma – kwa sababu anaruhusiwa Khalifa amiliki asili yake na kumiliki manufaa yake kwa watu,pindi ambapo haruhusiwi kwake kumilikisha yeyote,si mtu mmoja na wala si kikundi cha watu wengi,asili ya miliki ya umma – kwa sababu hii vimekuwa viyu hivi ni milki ya Dola,kwa sababu Dola ndiyo yenye uwezo juu yake katika matumizi, na hii ndio maana ya kumiliki.

Na kwa hakika ijapokuwa Dola ndio ambayo inasimamia na kupangilia milki ya umma,na inasimamia milki ya

Dola,isipokuwa kuna tofauti kati ya milki hizi mbili.kila kilichopo ndani ya milki ya umma,
mfano :Mafuta,gesi,madini yanayotoka kwa wingi,bahari,Mito,Chemchem,Viwanja vya wazi,Mapori,malisho/machungio,na Misikiti hakika hivi haifi kwa Khalifa kummilisha yeyote,sawa ni mmoja au ni kikundi cha watu kwa sababu ni milki ya waislamu wote,na ni juu ya khalifa kuweka mpangilio maalum wa kuwawezesha watu wote kunufaika na hivi vitu,kwa mujibu wa vile inavyopelekea jitihada yake katika kusimamia mambo yao na kukidhi maslahi yao.ama vile ambavyo vipo ndani ya milk ya Dola,ikiwepo ardhi na majengo kwa hakika anaweza kumikisha yeyote katika raia,kwa kumpa chote na manufaa,au kwa kumpa atumie manufaa yake pasina kumilikishwa kitu chote,au kwa kumruhusu kukihuisha na kukimiliki,atafanya (khalifah) katika hivi kile anachokiona kinafaa na kina kheri kwa waislamu.

## AINA ZA MILKI YA DOLA

1- **Majangwa**,Milima,Fukwe za Bahari na Ardhi maiti(zisizoendelezwa) ambazo hazimilikiwi na yeyote.
   Kila jangwa,na kila mlima au Kichuguu au Bonde au Ufukwe wa bahari,au ardhi maiti,sawa itakuwa ni maiti kutokana na kupitiwa na Muda mrefu sana na haijapata kulimwa hata kidogo,au ilipata kulimwa , kasha ikabadilika kuwa maiti kwa kuangamia watu wake,kwa hakika ardhi zote hizi ikiwemo majangwa,milima,fukwe za bahari na ardhi maiti zinahesabiwa kuwa ni ardhi maiti na zilikuwa ni milki ya Dola atasimamia Khalifa matumizi yake kwa mujibu wa rai na jitihada yake kwa kile anachokiona kina maslahi kwa waislamu.yeye ana haki ya kumkatia mtu katika hizo na anahaki ya kuchukuwa kwa ajili ya kuhuisha na kuzuia kitu humo.toka kwa Bilali bin Harithi Al-muzani “kwamba Mtume (S.a.w) alimkatia Bonde lote la Aqiqa” na katika mapokezi mengine

“kwamba Mtume (S.a.w) alimkatia Bilal bin Harith kati ya Bahari na kwenye Mawe/Mlima wa mawe mawe” na toka kwa Amri bin Shu’aib toka kwa Baba yake amesema : “Mtume (S.a.w) aliwakatia watu toka kabila ya Muzainah au Juhainah “

**وعن عمرو بن شعيب عن أبيه قال: "أقطع رسول الله صلى الله عليه وسلم أناساً من مزينة، أو جهينة".**

Na toka kwa Adi’I bin Hatim “Hakika ya Mtume (S.a.w) alimkatia Furata bin Hayan Al-aj’lii ardhi katika eneo la Yamama “

**وعن عدي بن حاتم "أن رسول الله صلى الله عليه وسلم قطع فرات بن حيان العجلي أرضاً باليمامة".**

Na toka kwa Ab’yadh bin Hammal Al-maazini “kwamba yeye alifika kwa Mtume (S.a.w) akamuomba amkatie eneo la kulima chumvi akamkatia.pindi alipoondoka akasema Mwanamme mmoja katika Kikao hicho :unajua ni kipi umemkatia ?bila shaka umemkatia maji yanayotoka kwa wingi,akasema: akarejesha alichomkatioa Yule mtu “

**وعن أبيض بن حمّال المازني "أنه وفد إلى رسول الله صلى الله عليه وسلم فاستقطعه الملح فقطع له، فلما أن ولّى قال رجل من المجلس: أتدري ما قطعت له؟ إنما قطعت له الماء العدّ، قال: فانتزعه منه"**

Na toka kwa Amri bin Dinar amesema : “wakati alipofika Mtume (S.a.w) Madina alimkatia eneo Abubakar na alimktia Omar “ kama vile Mtume (S.aw) alimkatia ardhi pana Zubeir bin Al-awwam,kwa hakika alimkatia zizi la farasi wake katika ardhi maiti ya Naqi’I na alimkatia ardhi ambayo ndani yake kuna miti na mitende.

**وعن عمرو بن دينار قال: "لما قدم رسول الله صلى الله عليه وسلم المدينة أقطع أبا بكر، وأقطع عمر"، "كما أقطع الرسول الزبير بن العوام أرضاً واسعة، فقد أقطعه ركض فرسه في موات النقيع، وأقطعه أرضاً فيه شجر ونخل".**

Hadithi hizi – ambazo zimebainisha kwamba Mtume (S.a.w) alimkatia ardhi Abubakar,Omar,Zubeir,Bilali Al-mazini,Ab’yadhwa bin Hammal,Furata bin Hayan,watu wa kabila la Muzani na watu wa kabila la Jahani na wengineo –zinafahamisha kuwa Majangwa,Milima,Mabonde,na Ardhi Maiti kuwa sio

milki ya yeyote bali ni milki ya Dola,Khalifa atapanga matumizi yake kwa vile atakavyoona vina maslahi kwa waislamu.Mtume (S.a.w) kupanga matumizi ya ardhi hizi na kuwakati awatu hawa na hiyo milki yake khasa,si kwa mirathi na wala si kwa kuikomboa kivita inaonyesha ushahidi wa wazi kwamba hizo ni milki ya Dola,na lau ingekuwa sio milki ya Dola basi asingekuwa na uwezo/maamuzi juu yake,na wala asingemkatia yeyote ardhi hiyo,kwa sababu hakuwa ni mwenye kumiliki chochote katika ardhi hiyo umiliki khasa.

Na Milki ya Mwenyezi Mungu na Mtume wake inakusudiwa kuwa ni milki ya Dola,na Umiliki wa Mtume (S.a.w)kwa sehemu hizo unamfanya awe na utawala juu yake,na haki ya kutumia,na kwa hakika umehama utawala wake na haki ya kutumia kwa Makhalifah baada yake,kwa sababu hiyo Alikuwa Abubakar,Omar,Othmani,Ally na Makhalifah waliokuja baada yao wakiwakatia watu kama alivyokuwa Mtume (S.a.w) akiwakatia,kwa kule kuelewa kwao kuwa Majangwa,Milima na Ardhi maiti ni miliki ya Dola na wao wana utawala juu yake na wao ndio wenye uwezo wa kisheria kupanga utumiaji wake.kama vile walifahamu maswahaba na waislamu kwamba Majangwa,Milima na ardhi maiti kuna haki ya waislamu wote.na kwamba utawala wake upo juu ya Dolan a Kwamba Mtume (S.a.w) na Makhalifah baada yake kuwa ndio wenye uwezo wa kupanga matumizi yake na upangiliaji wake na kupanga mambo yake na katika kuikata kwake,na kutoa ruhusa ya kuzihuisha na kuziimarisha.kwa sababu hiyo hakika Zuberi bin Al-awwam,Ab’yadhwa bin Hammal,Bilali bin Harithi Al-mazini,Abu tha’labah Al-khushani,Temimi Ad-daariy na wengineo walimtaka Mtume (S.a.w) awakatie ardhi,na pia Na’afi Abu Abdillah Mwenyeji wa Basra toka kabila la Thaqif alimtaka Omar bin Khatwab amkatie ardhi katika mji wa mji wa Basra – si katika ardhi ya Kharaji na wala

hatamdhuru Muislamu yeyote – ili ailime ikiwa ni malisho ya farasi wake.

Kama alivyopokea Kuthair bin Abdillah toka kwa Baba yake toka kwa Babu yake amesema :Tulifika pamoja na Omar bin Khaatwab katika Ibada ya Umra mwaka kumi na saba Hijri wakazungumza nae watu wa njiani kuwa wanataka wajenge nyumba kati ya Makkah na Madina ambazo hazikuwepo kabla ya hapo,akawaruhusu,na akawapa sharti kuwa wasafiri wana haki ya kupata maji na kivuli"

**كما روى كثير بن عبد الله عن أبيه عن جده قال: "قدمنا مع عمر بن الخطاب في عمرته سنة سبع عشرة فكلمه أهل المياه في الطريق أن يبنوا بيوتاً فيما بين مكة والمدينة، لم تكن قبل ذلك، فأذن لهم، واشترط عليهم أن ابن السبيل أحق بالماء والظل".**

Na kama alivyopokea Abubakar bin Abdillah bin maryam toka kwa Atwiyah bin Qaisi " kwamba watu walimuomba Omar bin Khatwab awape ardhi katika ardhi za Adhrikistan maeneo ya Damasca kwa ajili ya kuvungia farasi wao".

**وكما روى أبو بكر بن عبد الله بن مريم عن عطية بن قيس "أن أناساً سألوا عمر بن الخطاب أرضاً من أرض أنذركيسان بدمشق لمربط خيلهم".**

Na kwa yote haya inabainika wazi kuwa Majangwa,Milima na Ardhi maiti ni miliki ya Dola,anapanga Khalifah matumizi kwa mujibu wa anavyoona jitihada yake kuhusu namna ya kukata,au kuihuisha,au kuiuza,au kuikodisha,au kuizaliza,au kuihifadhi,au matumizi mengine yasiokuwa hayo kwa vile anavyoona kuwepo kwa khei na maslahi kwa waislam.

## 2- MABONDE

Mabonde ni ardhi zenye kufikiwa ambazo zinajaa maji,mfano wa Mabonde ambayo yalikuwa yapo kati ya mji wa Kufa na Basra,na ambazo zimejaa maji ya Mto wa Dijla na Furat baada ya kuporomoka baadhi ya vizuizi vyake ambavyo vinaazuia mapitio/njia ya maji ya miti mito miwili,hali iliyoyafanya maji yakibubujika toka mahala pa maporomoko na kuzama katika ardhi hizi na

kuzifanya hazifai tena kwa kilimo pamoja kwamba zilikuwa ni mabostani,mashamba na makazi.na yalipatikana mabond haya siku za **QUBADHI BIN FEIRUZ**,Na baadaye yakazidi na yakapanuka kwa kughafilika na jambo lake na kushughulika na vita baina ya waislamu na wafursi,mpaka ukafika upana wake ni farsakha Thalathina mara Thalathini yaani yanalingana na kilometa za mraba 27225 kwa sababu Farsakh moja ilingana na km 5.5 kwa karibu.basi ardhi hizi ambazo zimemezwa na maji,na zikawa tena hazifai kwa kilimo kwa kuzamishwa na maji zinakuwa na hukmu ya ardhi maiti,na ijapokuwa ilitanguliwa na kuwa ni ardhi yenye kuimarishwa kwa kilimo na majengo,na inakuwa ni milki ya Baitil-mali,na ni milki ya Dola,muda wa kuwa si yenye kumilikiwa na yeyote,na inaingia katika maana ya mabonde,Mabonde,mapori,Ardhi ya Chumvi chumvi na ardhi ya maji maji/Bwawa,kwa sababu yanafanana,na inachukuwa hukmu yake.

3- ASSWAWAF

Asswawaf : ni kila ardhi anayoagiza Khalifa iingizwe katika baitil-maali miongoni mwa ardhi zilizokombolewa,ambazo zimebakia pasina mmiliki yeyote baada ya kuondoka watu wake,au zilikuwa zinamilikiwa na dola ambazo zimekombolewa,au ni za watawala wake,au ni za wale waliouawa vitani,au aliokimbia vita na akaiacha ardhi yake,au ni kwa Yule ambaye ameiingiza katika Baitil-mali,na akaifanya ni khasa/maalum kwa baitil-mali ni Omar bin Khatwab.

**قال أبو يوسف: حدثني عبد الله بن الوليد عبد عبد الله بن أبي حرة قال: " أصفى عمر بن الخطاب من أهل السواد عشرة أصناف: أرض من قتل في الحرب، وأرض من هرب، وكل أرض كانت لكسرى، وكل أرض كانت لأحد من أهله، وكل مغيض ماء، وكل دير بريد، قال: ونسيت أربع خصال كانت للأكاسرة، وقال: وكان خراج ما استصفاه عمر سبعة ألف درهم ".**

Amesema Abu Yusuf :amenielezea Abdullah bin Al-walid Abdullah bin Abii Hurrah amesema : Aliingiza /alitenga Omar Bin Khatwab kwa watu wengi aina kumi za

ardhi:Ardhi ya wale waliouawa vitani,Ardhi ya wale waliokimbia vitani,na ardhi iliokuwa ni Kisra /mfalme na ardhi ya familia yake,na kila Bonde la maji,na kila Jengo la Posta, Amesema :na nimesahau sifa nne walizokuwa Makaisar,na akasema :ilikuwa Kharaji ya vile alivyovyiingiza Omar katika Baitil-mali ni Dirham alf saba"

Kwa sababu hiyo ,kwa hakika Dola ya Khilafah wakati inapokomboa mji basi inayompasa Khalifah aingize katika milki ya baitil-mali au miliki yeyote ya Dola kila Jengo,na kila ardhi,iliokuwa ni milki ya Dola iliokombolewa au ni milki ya watawala wake au milki ya makamanda wake,au ni ya wale waliouawa katika viwanja vya vita,au ni ya wale waliokimbia vitani wakaacha ardhi zao,na atapanga Khalifa namna ya matumizi yake kwa namna anayoiona ina Kheri na Maslahi kwa Uislamu na Waislamu.

4- MAJENGO NA VITU VYA WAQFU

Ni kila Ghorofa au Jengo au Jengo la waqfu,linalotawaliwa Dola katika miji ambayo imiteka,na yalikuwa ni maalum kwa vyombo vya Dola ambazo zilizofunguliwa na Ofisi zake,au ni za mashirika yake na vile vinavyohusiana,au ni za vyuo vikuu vyake na mashule yake,au za Mahospiali yake,au sehemu zake za Makumbusho yake,au zi wale walioua vitani au ni za wale waliokimbia vita,au ni za wale ambao wamekimbia wenyewe kwa kuwaogopa waislam na wakaziacha,Maghorofa yote,Majengo,na Majengo ya Waqfu zinakuwa ni ghawira na faia kwa waislamu na zinakuwa zinastahiki kuwa ni za Baitil-mali,na ni milki ya Dola.na kadhalika kila jengo linakuwa ni milki ya Dola,au jengo la waqfu/huduma lililojengwa na Dola,au linainunua kutokana na mali za Baitil-mali na kuvikhusisha na vyombo vya Dola,na maslahi yake au kwa Ofisi zake au kwa vyuo vyake vikuu na mashule yake,au kwa Hospitali zake au kwa kila kitu ambacho inaisimamisha/jenga.na kadhalika itakuwa ni milki ya

Dola kila jengo au jengo la waqfu/huduma wanalopewa zawadi au kupewa hiba au kuusiwa au inarithi toka kwa wale waliokuwa na hawana warithi au toka kwa aliyerutadi au akauawa kwa kule kuritadi kwake.

## KUZALISHA MALI ZA DOLA

Pamoja kwamba sheria immkabidhi Khalifah kusimamia mambo ya Waislam,na kutatua mambo yao,na kukidhi haja zao,yakiwemo ndani yake mambo ya kheri na shari kwa mujibu inavyopelekea Jitihaada yake,kwa ajili hiyo ana haki Khalifah ya kuzalisha mali za Dola kwa wasaa unaowezekana,mpaka yazidi mapato ya Baitil-mali,kwa kile kinakachosambaza manufaa kwa waislamu wote na ili zisibaki mali za Dola hazina kazi na manufaa yake ni yenye kupotea,na mapato yake ni yenye kukatika.

Na kwa hakika alikuwa Mtume (S.a.w) na Makhalifah baada yake wakizalisha mali hizi za Dola,kwa mujibu walivyokuwa wakiona kuna Maslahi kwa waislamu.

Na kuzalisha mali za Dola hakuna ya kwamba Dola inakuwa inafanya Biashara au inazalisha au watu wa kazi/Watu wa mipango ya Kibiashara,ikafanya kama utendaji wa wafanya biashara na wazalishaji na wenye utendaji wa kazi za kibiashara,bali Dola ni Mchungaji,kwa sababu hii inapasa uzalishaji wa Dola kwa mali zake uwe ni uzalishaji unaonyesha/onekana ndani yake usimamizi wa mambo ya ummah.na kutatua maslahi yao na kutimiza haja zao,asili ni uhungaji na wala si kuchuma.

NAMNA YA KUZALISHA MALI ZA DOLA

Na kuzalisha mali za Dola kunakuwa kwa njia nyingi miongoni mwazo ni :-

1- Kuuza,au kukodisha,basi kila kinachopelekea kupata maslahi ya kuwamilikisha watu,au kuwamilikisha manufaa ya kutumia hiyo ardhi,au jengo katika milki za Dola,ina haki ya kuuza,au

kukodisha kwa watu kwa mujibu inavyoona,kwa kuhakikisha maslahi yao,sawa ardhi hiyo itakuwa ipo ndani ya mji kwa kuweka masoko au makazi au sawa itakuwa ardhi hiyo ipo nje ya mji au kijijini,kwa ajili ya kuweka maghala au Mazizi ya Ng'ombe,Ngamia,Mbuzi na Kondoo,au ndege wa Kufungwa(Kuku,Bata,Khanga nk) au zimkuwa zipo katika Fukwe za Bahari au Mito kwa ajili ya kuweka Viwanda au vitega uchumi,au itakuwa ni ardhi ya kilimo inayofaa kwa kilimo au kuotesha miti,pamoja kwamba ardhi ya kilimo inauzwa na wala haikodishwi.

2- Kuizalisha ardhi yenye miti,yote au sehemu yake kubwa,inayomilikiwa na Dola kwa kuifanyia kazi juu yake kwa sehemu/kiasi ya kile kinachotoka humo kama robo,au theluthi,au nusu,kama vile alivyowatendea Mtume (S.a.w) watu wa Khaybarah na Fadak.

3- Kuizalisha ardhi ya kilimo yenye kuimarika,kwa kuajiri wafanyakazi wa kuiendeleza na kuilima na kuisimamia mambo yake.

4- Kuhuisha Mabonde,chemchem,visima vilivyokauka na ardhi za chumvi chumvi,kwa kuzuia/kukusanya maji juu yake,na kuanzisha njia za kupitia maji hapo,na kujaza maji kisha kuyakausha mpaka ziweze kufaa kwa kilimo na kuotesha miti.

5- Kuikata/kuigawa ardhi ,na kunakuwa kwa khalifah kuwakatia watu ardhi inayomilikiwa na Dola,kwa mujibu wa vile anavyoona kuna maslahi kwa Uislamu na waislamu,ana haki ya kumkatia mwenye uwezo katika Uislamu,au ana ziada,kama vile anaweza kumkatia anayemuona katika kuunganisha nyoyo(aliyesilimu) kama vile ana haki ya kuwakatia wakulima wenye kuhitaji sababu ya kupata rizki kama vile anakata kwa kuimarisha ardhi na kutokuiasha haina kazi,kwa kuzidisha uzalishaji,mazao na matunda.na anaweza kumkatia kila mara atakapoona

kuna maslahi ya kufanya hivyo.na kwa hakika alikata ardhi Mtume (S.a.w) ,kama vile Makhalifah walikata ardhi baada yake kama ilivyopokelewa katika hadithi zilizopokelewa katika maudhui hii.

Na kuikata ardhi ima kutakuwa katidhi ya Ushru,na ima kutakuwa katika ardhi ya Kharaji,ikiwa kutakuwa ni katika ardhi ya Ushru nayo ni ardhi ya bara arabu(Mfano wa kisiwa cha arabuni),na kila ardhi waliosilimu watu wake wakiwa humo,kama Indonesia.kwa hakika anaruhusiwa Khalifah kummilikisha moja kwa moja au manufaa yake Yule anayekatiwa,au ammilikishe manufaa yake,pasina kummilikisha yote moja kwa moja,umiliki wa moja kwa moja,au wa muda maalum,kwa mujibu wa anavyoona kuwa kuna maslahi kwa waislamu,sawa itakuwa ni ardhi maiti,haijapata kulimwa hata mara moja,au ilipata kulimwa na kisha ikaachwa na ikawa ni ardhi maiti,au itakuwa ni ardhi yenye kuimarika inafaa kwa kilimo na kuotesha miti.na katika hali zote hakika umeliki haupatiakani/hauthibiti katika kukata huku isipokuwa kwa kuhuisha ardhi iliokatwa katika ardhi maiti,na kwa kuilima ardhi ilioimara kwa kulima na kutoa matunda.na kukutiwa kunampa haki,na wala haipaswi katika ardhi hizi zilizokatwa isipokuwa Ushru/Moja ya Kumi ya mapato ya ardhi ikiwa ni zaka katika wajibu unaopaswa wa zaka,na pale inapofikia kiwango na si wajibu kutoa Kharaji hata kidogo,kwa sababu ardhi ya Ushru si wajibu kutoa Kharaji.ama ikiwa kukata ni katika ardhi ya Kharaji- nayo ni kila ardhi aliokombolewa kwa nguvu mfano wa Iraq,Shamu na Misri- itaangaliwa : ikiwa kukata ni katika ardhi ilioimara,sawa ilishapata kupangiwa Kharaji juu yake,au haijapata kupangiwa Kharaji juu yake,hamiliki anaekatiwa isipokuwa manufaa ya ardhi peke yake,na wala hamiliki umiliki wa moja kwa moja,kwa sababu umiliki wa moja kwa moja ni milki ya waislamu

wote.na Khalifah ana nafasi ya kufanya kummilikisha mwenye kukatiwa akafanya manufaa ni ya moja kwa moja,au ni kwa muda maalum uliopangwa,kwa mujibu anavyoona kuna maslahi kwa waislamu, na ni wajibu katika ardhi hii iliokatwa kutoa Kharaji ya Ardhi, na kutoa Ushru/Moja ya kumi ya mazao na matunda ambayo ni wajibu kutoa zaka,pindi vitakavyofikiwa kiwango baada ya kutoa Kharaji.

**عن موسى بن طلحة قال:" إن عثمان بن عفان أقطع خمسة من أصحاب النبي صلى الله عليه وسلم، الزبير، وسعداً، وابن مسعود، وأسامة بن زيد، وخباب بن الأرت، قال: وكان جاري منهم ابن مسعود وخباب". قال أبو يوسف: وحدثنا أبو حنيفة عمن حدثه قال: "كان لعبد الله بن مسعود أرض خراج، وكان لخباب أرض خراج، وكان للحسين بن علي أرض خراج، ولغيرهم من الصحابة أرض خراج، وكان لشريح أرض خراج، فكانوا يؤدون عنها الخراج".**

Toka kwa Mussa bin Twalha amesema :"hakika Othman bin Affan aliwakatia watano kati ya Maswahaba wa Mtume (S.a.w) Zubeir,Sa'ad,Ibnu Masoud,Usaba Bin Zaid na Khabbab bin Aratti,amesema :na alikuwa jirani yangu katika hao ni Ibnu masoud na Khabbat" amesema Abu yusuf : na ametueleza Abu hanifa toka kwa wale waliomueleza amesema : "alikuwa Abdallah bin Masoud ana ardhi ya Kharaj,na alikuwa Khabbab ana ardhi ya Kharaj,na Alikuwa Hussein Bin Ally ana ardhi ya Kharaj,na maswahaba wengine nao walikuwa na ardhi ya Kharaj,na alikuwa Shuraih ana ardhi ya Kharaj,walikuwa wakitoa Kharaji."

Ama ikiwa kukata ni katika ardhi maiti basi itatazamwa :ikiwa ardhi iliokatwa na maiti toka miaka mingi,au ilipata kuimarika na kulimwa,kisha ikawa ni ardhi ya Kharaji,na ikawa ni maiti kabla ya kupangiwa Kharaji,kama ardhi ya mabonde ya Iraq,yaliopo kati ya Kufa na Basra,hakika anayo Khalifah nafasi ya kummilikisha Yule mwenye kukatiwa umiliki wa moja kwa moja na manufaa yake,na anaweza kummilikisha manufaa peke yake.na kuimiliki ardhi hii hakuwi/hakutimii isipokuwa kwa kuihuisha baada ya

kukatiwa,ijapokuwa kukatiwa kunampa haki humo mwenye kukatiwa.lakini kumiliki hakutimii isipokuwa kwa kupatikana kuhuisha,na hapana budi kupatikan kuhuisha kabla ya miaka mitatu baada ya kukatiwa,

**كما ورد في الأثر الذي رواه طاووس أن عمر بن الخطاب قال:"ليس لمحتجر حق بعد ثلاث". عن محمد بن عبد الثقفي قال:" استقطع رجل من أهل البصرة يقال له نافع أبو عبد الله عمر بن الخطاب أرضاً بالبصرة ليست من أرض الخراج، ولا تضر بأحد من المسلمين ليتخذ فيها قضباً لخيله، فكتب عمر إلى أبي موسى الأشعري، إن كانت كما يقول فأقطعها إياه". وأقطع عثمان بن عفان عثمان بن أبي العاص الثقفي، أرضاً بالبصرة كانت سباخاً وآجاماً، فاستخرجها وأحياها.**

kama ilivyopokelewa katika athari ambayo amipokea Twaus kwamba Omar bin Khatwab alisema :"Hana haki aliyezuiliwa/pewa ardhi baada ya miaka mitatu" Toka kwa Muhamad bin Abdutaqafii amesema : "Mtu mmoja wa Basra alimuomba Omar amkatie ardhi katika mji wa Basra na wala sio ardhi ya Kharaji,na wala haitamdhuru muislamu yeyote ili aifanye kuwa ni malisho ya farasi wake,akaandika Omar kwa Abu Musa AL-ash'ariy,ikiwa ni kama alivyosema basi mkatie"na Othman bin Affan alimkatia Othman bin Al-a's Athaqafiy ardhi katika mji wa Basrah ilikuwa ni ya chumvi chumvi na mabori,basi akamtolea na akaihuisha.na ardhi hizi ikiwa atakatiwa Muislamu atawajibika atoe Ushru yake,na wala si wajibu juu yake kutoa Kharaji,kwa sababu hukmu yake ni hukmu ya ardhi maiti ambayo hukatwa na kuhuishwa katika ardhi ya Ushru,kwa zile hadithi zilizopokelewa katika jambo hili,

**عن عمر بن الخطاب عن رسول الله صلى الله عليه وسلم أنّه قال: "من أحيا أرضاً ميتة فهي له". وعن عمرو بن شعيب عن أبيه عن جده عن النبي صلى الله عليه وسلم "من أحيا أرضاً مواتاً فهي له".**

Toka kwa Omar bin Khatwab toka kwa Mtume (S.a.w) kwamba yeye amesema : " Yeyete mwenye kuhisha ardhi maiti basi hiyo ni kwake"

Na toka kwa Amru bin Shuaib toka kwa baba yake toka kwa babu yake toka kwa Mtume (S.a.w) amesema : " Yeyete mwenye kuhisha ardhi maiti basi hiyo ni kwake"

Na ikiwa atakatiwa ardhi hii kafiri dhimmiy basi ni wajibu juu yake atoe Kharaji mfano wa ardhi ambayo wambakishwa watu wake juu yake baada ya kukombolewa kwa mkabala wa Kharaji watakaoitoa.

Na ikiwa imetangulia kuimarika kwa ardhi hizi maiti ambazo wamekatiwa watu ,na zikapangiwa Kharaji basi ni wajibu kutoa Kharaji,sawa amekatiwa Muislamu au kafir dhimmiy,kwa sababu zile ardhi ambazo zimepangiwa Kharaji katika ardhi zilizokombolewa zitabakia zimethibiti hivyo hivyo mpaka atakapoirithi Mwenyezi Mungu ardhi na vilivyomo juu yake.

6- Ruhusa ya kuhuisha ardhi maiti,na kulihimiza hili,nayo ni kwa Khalifah kuwaruhusu watu kuhuisha ardhi maiti,na kulihimiza jambo hili,nako ni kwa Khalifah kuruhusu watu wahuishe ardhi maiti,na awahimize wafanye kazi ya kuhuisha ardhi maiti,sawa itakuwa ni ardhi ya Ushru,au itakuwa ni katika ardhi ya Kharaj,sawa itakuwa ardhi maiti toka siku nyingi haijapata kuimarishwa hata mara moja,au ilipata kuimarishwa na kufanywa ya Kharaji na sasa imekuwa ni ardhi maiti.

Na kuhuisha ardhi ikiwa ni ya makazi,au kujenga Maghala,au viwanda,au mazizi ya wanyama au ndege,hakika itatimia kwa kujengwa na kusakafiwa,kwa sababu ndio hatua ya mwanzo ambayo inaweza kuishi ndani yake,au kutumia kwa maghala au viwanda au kuhifadhi wanyama au kuwaweka ndege,na ikiwa kuhuisha ni ajili ya kulima na kupanda,kwa hakika linatimia hili kwa kuzungurushia (uzio/ukuta)ili kuizuia,na kuitofautisha na nyingine na kuipelekea maji au kuchimba kisima humo,ikiwa ardhi ni kavu na mimea yake inaishi kwa kumwagiliwa maji,na kuyazuia maji hapo,na kuyakausha ikiwa ardhi yake imejaa maji,na kuilima ardhi na kuisawazisha yenye muinuko na kuizawazisha yenye mabonde na kwa kutimia kuihuisha kunatimia kuimiliki kwa dalili za hadithi zilizopita zinazozungumzia kuhuisha ardhi,

وحديث عمر رضي الله عنه، عن رسول الله صلى الله عليه وسلم قال: "من أحيا أرضاً ميتة فهي له".

na hadithi ya Ibn Omar,toka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) amesema : “Yeyote mwenye kuhuisha ardhi maiti basi hiyo ni yake wake”

ama kuizuia ardhi hakika yake haitimii kwa hiyo kumiliki,na inathibisha haki ya Mwenye kuzuia kwa sehemu alioizuia,na ikiwa itapitiwa na miaka mitatu pasina kuhuisha kile alichokizuia ,itaanguka haki yake katika ardhi ambayo ameizuia.

عن طاووس أن عمر قال: "ليس لمحتجر حقّ بعد ثلاث".

Toka kwa Twausi amesema kwamba amesema Omar : “hana haki Mwenye kuzuia ardhi baada ya Miaka mitatu “ na mwenye kuhuisha ardhi maiti katika ardhi ya Ushru atakuwa amemiliki ardhi hiyo na manufaa yake,sawa atakuwa ni muislamu au ni kafiri,na ni wajibu kwa muislamu katika ardhi hiyo atoe Ushru(Moja ya kumi ) ikiwa ni zaka ya mazao na matunda yanayopaswa kutolewa zaka,ikiwa yatafikiwa na kiwango,na wala si wajibu kwake kutoa Kharaj,kwa sababu ardhi ya Ushru haina Kharaji,ama kafiri si wajibu kwake kutoa Ushru na Kharaj,kwa sababu yeye si katika watu wa kutoa zaka na kwamba Kharaj si wajibu katika Ardhi ya Ushru.na mwenye kuhuisha ardhi maiti katika adhi ya Kharaji haijapata kupangiwa kharaji,atamiliki ardhi yenyewe na manufaa yake ikiwa ni Muislamu,na manufaa peke akiwa ni akfiri,ni ni wajibu kwa Muislamu kutoa Ushru na wala hana Kharaji juu yake,naa ni wajibu kwa kafiri kutoa kharaji ,kama vile ilivyowekwa kwa watu wake wakati walipokubaliwa kukaa hapo wakati wa kuikomboa kwa kutoa kharaji toka ardhi hiyo.

Na mwenye kuhuisha ardhi maiti katika ardhi ya Kharaji,iliopata kuwekewa Kharaji kabla haijageuka kuwa ardhi Maiti,atamiliki manufaa yake peke yake pasina kuimiliki ardhi sawa ni muislamu au ni kafiri,na atawajibika kutoa Kharaji kwa sababu imewafikana kuwa ni ardhi iliokombolewa na imepangiwa Kharaji,kwa ajili hiyo ni wajibu ibaki Kharaji juu yake,sawa kaimiliki Muislam au kafiri mpaka pale Mwenyezi

Mungu atakapoirithi ardhi na vilivyomo juu yake. Hii ni pale inapokuwa kuhuisha ni kwa Mimea,ama ikiwa kuhuisha ni kwa jili ya makazi,au kujenga viwanga viwanda au Maghala au mazizi kwa hakika hakuna humo kutoa Ushru wala Kharaji,hakuna tofauti katika hilo baina ya ardhi ya Ushru na ardhi ya Kharaji,kwa hakika maswahaba ambao waliikomboa Iraq na Misri waliingia Mji wa Kufa ,Basra na Fustat na wakaingia siku za Omar na wakaingia pamoja na wao watu wengine,na wala hawakupangiwa Kharaj na wala hawakutoa zaka,kwa sababu Zaka si wajibu kwa Makazi na Majengo,na bila shaka ni wajibu kwa Mazao na Matunda.

**VYENYE MANUFAA**

Vyenye manufaa ni wingi wa Chenye Manufaa nacho ni kila kitu kinachonufaisha,ikiwemo Nyuma,mji na dola,inatokana na neon RAFAQA BIHI –PINDI ANAPOMNUFAISHA NA AKAMSAIDIA.na vyenye manufaa kiujuma/kwa wote ni vile vinavyowekwa na dola katika vyenye manufaa na huduma ili wanufaike navyo raia wote,na vinakusanya hivi vifuatavyo:-

1- Hudma za posta,ikiwemo Barua,simu,telegram,telefax na mawasiliano ya Televishen kupitia satalight na vinginevyo.

2- Huduma za Benk ,ikiwemo hiwala,kuhifadhi,kubadilisha hela na kufua hela za dhahabu na fedha au kuzibadilisha kuwa zenye kufuliwa,na benk za dola zitatoa huduma hizi nazo ni huduma zisizokuwa na riba,inaruhusiwa kuzifanya.

3- Huduma za Usafiri wa wote,na usafiri wa wote nazo ni kama Treni zipitazo katika njia zisizokuwa za watu wengi,kwa sababu treni zinazopita katika njia za watu wengi zinamilikiwa na uma,kwa kule kufuata njia ya uma,na kama vile ndege na usafiri wa baharini na vyombo hivi ni milki binafsi,wanaruhusiwa raia kuvimiliki,na kwa wakati huo huo dola inaruhusiwa kuvimiliki vyombo hivi ikiwemo Ndege,Treni,na Meli ikiona kufanya hivyo kuna maslahi kwa waislamu na kuwepo dharura ya kuwahudumia na kufanya wepesi usafiri wao.

4-Viwanda : navyo ni kwamba Dola inawajibu kuanzisha aina mbili ya viwanda kwa kuzingatia usimamizi wake kwa mambo ya watu :-

**Aina ya kwanza** : Viwanda ambavyo vinahusiana na mambo ya uma,kama vile viwanda vya kuchimba madini na kuyasafisha na kuyaunganisha,na kama vile viwanda vya kuchimba na kusafisha mafuta,na aina hii ya viwanda inaruhusiwa kuwa vinamilikiwa milki ya uma kwa kufuatana na maa ambayo inatengeneza na inayohusiana nayo na pamoja kwamba vitu vya milki ya uma vinakuwa ni milki ya waislamu wote,inajuzu/inaruhusiwa viwe viwanda vyake vinamilikiwa milki ya uma na waislamu wote,na Dola inachukuwa jukumu la kuvianzisha kwa maslahi ya Waislamu wote.

**Aina ya pili** :Ni vuwanda vinahusiana na kutengeneza vitu vizito,na vya kutengeneza silaha,na aina hii ya viwanda wanaruhusiwa watu binafsi kuwa nayo,kwa sababu ni katika ya watu binafsi,lakini pale ilipokwa viwanda hivi vinahitaji mali nyingi sana,na huenda ikawa ni uzito kupata uwezo huu baadhi ya raia,na muda wa kuwa zimekuwa silaha nzito siku hizi hazihesabiki kuwa ni milki binafsi kama ilivyokuwa hali wakati wa simu za Mtume (S.a.w) na siku za Makhalifa baada yake,bali zimekuwa ni milki ya Dola,Dola ndio yenye jukumu la kuzileta kwa wingi,kwa sababu ule uwajibu wa kuchunga/;kusimamia ambo ya uma kuwajibisha hayo,khasa baada ya kuendelea silaha maendeleo yenye kutisha,na zimekuwa malighafi zake nazo ni nzito,na zenye Gharam kubwa mno,kwa ujili kimekuwa ni wajibu kwa dola kuanzisha viwanda vya silaha na viwanda vya vitu vizito na hii haina maana kwamba Raia wazuiliwe kuanzisha viwanda hivi.

**Hivi ndio vitu vine vyenye manufaa ambavyo ni wajibu kwa dola kuvifanya viwepo kwa wingi kwa kule kusimamia kwake mambo,na vile amabvyo vinaweza kuletwa kwa wingi,na vitu hivi vyenye manufaa vinamilikiwa na dola basi mapato yake na faida zake nazo vinakuwa ni milki ya dola,na yanakuwa mapato yake ni mapato ya baitil mali,yatawekwa**

**katika diwani la Faui na Kharaji,na dola itatumia katika matumizi yake.**

**Ama yasiokuwa haya katika mambo yenye faida kwa watu ambayo ni wajibu kwa dola kutengeneza kwa wingi na kuwajengea watu kwa kuwafanyia mambo yenye manufaa nayo na ikiwa ndio kusimamia mambo yao,kama vile kujenga Mashule na Vyuo Vikuu,Mahospitali na nja za uma,na mengineyo katika vyenye faida za lazima kwa kusimamia mambo yao,kwa sababu vitu hivyo haviji kwa wingi vyenyewe bali vinahitaji huduma/Gharama za kudumu,na wala hazina njia zozote za mapato.**

**USHURU/MOJA YA KUMI**

Ushuuru : ni haki ya waislamu huchukuliwa toka kwa ahludhima (makafiri wanaishi kwa amani katika dola ya kiislamu) na bidhaa zao za biashara ,na watu wa vita(Makafiri waliopo vitani dhidi ya Uislamu) wanaopita katika mipaka ya dola ya khilafah,na Yule ambaye anasimamia kuchukua anaitwa Al-aashiru.(Mshukuwa Ushuru)

Na pamoja kwamba zimepokelewa hadithi nyingi zinazotaja vibaya kuchukuwa kodi,na kutia uzito kwa mchukuaji,mfano wa hadithi iliopokelewa na Uq'bah bin A'mir kwamba yeye amemsikia Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) akisema :-

**ما رَوَى عقبة بن عامر أنه سمع رسول الله صلى الله عليه وسلم يقول: "لا يدخل الجنة صاحبُ مَكْس"،**

"Haingii peponi mwenye kutoza kodi "

Na "Maksu" (Kodi) Ni mali ambayo inachukuliwa toka kwa wafanya biashara wakati wanapopita katika mipaka ya dola, na ile iliopokelewa na Kuraiz bin suleyman amesema :

**وما روي عن كريز بن سليمان قال: "كتب عمر بن عبد العزيز إلى عبد الله بن عوف القاري أن اركب إلى البيت الذي برفح، الذي يقال له بيت المكس فاهدمه، ثم احمله إلى البحر فانسفه فيه نسفاً.**

" Aliandika Omar bin Abdul-aziz kumuandikia Abdallah bin Auf Al-qaari kwamba :panda (chombo)uende katika nyumba ambayo ipo eneo la "Rafaha" ambayo inaitwa ni nyumba ya Ushuru/kodi ukaivunje,kisha ibebe mpaka baharini na uzamishe kisawasawa.

**كما كتب إلى عَديّ بن أرطأة أن ضع عن الناس الفدية، وضع عن الناس المائدة، وضع عن الناس المكس، وليس بالمكس ولكنه البخس الذي قال الله فيه: {ولا تبخسوا الناس أشياءهم، ولا تعثَوا في الأرض مفسدين} فمن جاءك بصدقة فاقبلها منه، ومن لم يأتك بها فالله حسيبه".**

Kama vile alimuandikia Adiyy bin Artwa'ah kwamba : waondolee watu vidia,waondolee watu meza,waondolee watu ushuru.kodi,na wala sio ushuru lakini hiyo ni kupunja ambako Mwenyezi Mungu amesema kuuhusu : [na wala msiwapunguzie watu vitu vyao,na wala msieneze uovu katika nchi mkafanya uharibifu-TMQ :11:85) basi yeyote atakayekuja na sadaka mkubalie sadaka yake,na Yule ambaye hakukuletea basi Mwenyezi Mungu anamtosha'.

Hadithi na athari zote hizi zinataja vibaya kuchukuwa ushuru/kodi,na kutia mkazo na ugumu kwa mchukuaji hali ambayo inaonyesha kutokufaa kwa jambo hili,na pia zimepokelea athari nyingine zinaonyesha kuwa Ushuru/kodi haikuchukuliwa toka kwa Waislamu,na wala kwa biashara za watu wa dhimma ambao wanapita na biashara zao katika mipaka ya dola ya kiislam,na bila shaka ushiru ukichukuliwa toka kwa wafanya biashara watu wa vita peke yao,

**مثل ما روي عن عبد الرحمن بن معقل قال: "سألت زياد بن حدير: من كنتم تعشرون؟ قال: تجار الحرب كما كانوا يعشروننا إذا أتيناهم".**

mfano ni yale alioyapokea Abdurrahmani bin Ma'qili amesema :Nimemuuliza Ziyad bin Haidar: "ni kina nani mlikuwa mkichukuwa Ushuru kwao ?akasema : wafanya biashara watu wa vita kama vile ambavyo wakitushika ushuru tukipita kwao"

**وما روي عن عمرو بن دينار قال: "أخبرني مسلم بن المصبح أنه سأل ابن عمر: أعلمت أن عمر أخذ من المسلمين العشر؟ قال: قال: لا، لم أعلمه".**

na yale yaliopokelewa toka kwa Amru bin Dinar amesema :kanielezea Muslim bin Al-muswbih kwamba yeye alimuuliza Ibn Omar :Je unajua kuwa Omar alichukuwa ushuru toka kwa Waislamu?akasema :Hapana ,sijapata kulijua jambo hili.(sifahamu)athari hizi zinaonyesha kwamba haikuwa ikichukuliwa ushuru toka kwa waislamu,na wala toka kwa watu wa dhima,na bila shaka ilikuwa ushuru ikichukuliwa toka kwa watu wa vita(Darul harbi)ikiwa ni kuwatendea kwa mfano ule ule wanaowatenda waislamu.

Lakini zimepokelewa athari nyingine zikibainisha kuwa Omar Bin Khatwab na Makhalifah wa baada yake Othman na Ally na Omar Bin Abdul-aziz walikuwa wakichukuwa Ushuru toka kwa wafanya biashara ambao walikuwa wakipitisha bidhaa zao katika mipata ya Dola,walikuwa wakichukuwa toka kwa wafanya biashara waislamu robu ya ushru(robo ya moja ya kumi) Na toka kwa wafanyabiashara wa Ahlu dhimma nusu ya ushuru(nusu ya moja ya kumi)

**عن زياد بن حدير قال: "استعملني عمر بن الخطاب على العشر فأمرني أن آخذ من تجار المسلمين ربع العشر". وقال ف أثر آخر: "أمرني عمر بن الخطاب أن آخذ من نصارى بني تغلب العشر، ومن نصارى أهل الكتاب نصف العشر".**

Toka kwa Ziyadi Bin Hudair amesema :"Alinipa kazi Omar ya kukusanya Ushru akaniamrisha nichukuwe toka kwa wafanya biashara wa Kiislamu robo ya Ushru,"na amesema katika Athari nyingine : "Ameniamrisha Omar Bin Khatwab nichukue Ushru toka kwa Manaswara wa Bani Taghlubi,na Nusu ya Ushru toka kwa Manaswara wa Ahlul kitab"

**وفي رواية عبد الرحمن بن معقل عن زياد بن حدير السابقة، أنه كان يأخذ من تجار أهل الحرب العشر.**

Na katika mapokezi ya Abdur rahmani Bin Maa'qili toka kwa Ziyad ni Hudairi( Athari )iliopia kwamba alikuwa akichukua Ushru toka Watu wa vita (Ahlul Harbi)

**عن السائب بن يزيد قال: "كنت عاملاً على سوق المدينة في زمن عمر قال: فكنا نأخذ من النبط العشر".**

Toka kwa Saib Bin yazid amesema: "Nilikuwa mfanyakazi katika soko la Madina wakati wa utawala wa Omar,akasema :Tulikuwa tunachukuwa Ushru toka wa Nebti"

**وروى عبد الله بن عمر قال: "كان عمر يأخذ من النبط من الزيت والحنطة نصف العشر، لكي يكثر الحمل إلى المدينة (أي لكي يُرغِّبَ الأنباط في جلب الزيت والقمح إلى المدينة) ويأخذ من القطنيّة العشر".**

Na amepokea Abdullah Bin Omar amesema : "Alikuwa Omar anachukuwa nusu ya Ushru toka wa wa Nebti ya Mafuta na Ngano ili wazidi wachukuzi katika mji wa madina (yaani ili awapendezeshee wa Nebti kuleta Mafuta na Ngano katika Mji wa Madina) na akichukuwa Ushru toka kwa vifaa vya Pamba ."

**وعن زريق بن حيان الدمشقي –وكان على جواز مصر- أن عمر بن عبد العزيز كتب إليه: "من مرّ بك من أهل الذمة فخذ مما يديرون ف التجارات من أموالهم من كل عشرين ديناراً**

**ديناراً، فما نَقَصَ فبحساب ذلك، حتى تبلغ عشرة دنانير، فإن نقصت ثلث دينار فلا تأخذ منها شيئاً".**

Na toka kwa Zurayq Bin Hayyan Addamashqiy – na alikuwa katika mpaka wa misri – kwamba Omar Bin Abdul-aziz alimwandikia kuwa " Yeyote atakaepita kwako katika watu wa Dhimma chukuwa kile wanachozungurusha katika Biashara,miongoni mwa mali zao toka kila Dinari Ishirini Chukuwa Dinari moja,na kile kitakachopungua basi ni kwa hesabu hiyo hiyo,mpaka zifike dinari kumi,na ikiwa zitapunguwa theluthi Dinari basi usichukuwe chochote.".

Basi athari hizi ziko wazin kwamba Omar bin Khatwab na Makhalifah baada yake,walikuwa wakichukuwa ushur toka kwa biashara ambazo zikipita katika mipaka toka kwa wafanya biashara wasilamu wakichukua robo ya Ush'rru na toka kwa wafanya biashara Ahlu dhimmah Nusu ya Ush'ru na wafanya biashara Harbiyu Ush'ru kamili,na hili lilikuwa mbele ya macho na masikio ya maswahaba,inakuwa hii ni ij'maa toka kwao ya kujuzu kushuchukuwa huo ushru na kwamba Omar bin Abdul-aziz - ambaye alimuamrisha Adiyyu bin Artwa'a awaondelee watu kodi na akamuamrisha Abdallah bin Aufi Al-qaarii aliivunje nyumba ya kodi iliokuwa eneo la Rafah- alimuamrisha mfanyakazi wake wa Ushur katika nchi ya Misri Zurayq Bin Hayyan Addamashqiy achukuwe toka kwa Ahlu Dhima Nusu ya Ush'ru,na kwamba Ziyad Bin haydar ambaye amesema : " Hatukuwa tukichukuwa Ush'ru kwa Muislamu na wala kwa Muahidi/anaishi kwa mkataba katika Dila ya kiislamu", amesema katika mapokezi mengine "Kwamba omar alimuamrisha achukuwe Robo ya Ushru toka kwa waislamu na toka kwa Ahlu Dhimmah nusu ya Ush'ru" .Hadithi na Ahtari hizi kwa uwazi zinaonekana kupingana na Hadithi zilizopita,ambazo zinataja ubaya wa juchukuwa kodi,na kumuwekea ngumu anaechukuwa kodi,na ambazo ndani zinasema kuwa Omar na Ziyad bin Haidar hawakupa kumchukulia Ush'ru muislam wala dhimmiy yeyete Yule .

Na kwa kutazama kwa kina katika namna ya kukusanya Hadithi na athari hizi zilizopokelewa katika maudhui haya

inabainika kuwa hakuna kupinzana ndani yake hata kidogo,hakika ya Kodi ambayo imetajwa vibaya na kutiliwa mgumu mchukuaji wake ni katika ambali ambazo zinachukuliwa kwa waislamu pasina haki,kama vile kuchukuliwa kwao Ush'ru au kuchukuliwa katika biashara zao zipitazo katika mipaka ya kiislamu zaidi ya robo ya ush'ru,Muislamu si wajibu juu yake kutoa Ush'ru na wala si wajibu kwa Biashara yake isipokuwa kutoa zaka tu basi.na wala si wajibu humo isipokuwa robo ya ush'ru na hiyo sio kodi,na wala sio Ush'ru (Ten percent ) na kutokana na hayo inakuwa wazi kuwa makusudio ya hadithi ya Ibn Omar na hadithi ya Ziyad bin haidar kwamba omar hakuchukuwa Ushru , isipokuwa alikuwa alikuwa akichukuwa kwao zaka na ilikuwa kiwango chake ni Robo ya ush'ru na wala sio Ush'ru.

Amma Ahludhimmah,nao kadhalika walikuwa hawachuliwi Ush'ru,na bila shaka wakichukuliwa Nusu ya Ush'ru,na kile kilichokuwa kinachukuliwa kwao katika hiyo nusu ya ush'ru kilikuwa kimewekewa sharti kwao katika makubaliano/mikataba ya kuweka sulhu ambayo ilifungwa pamoja nao wakati wa Omar bin Khatwab wakati alipoifunguwa Iraq ,Shamu na Misri.kwa ajili hiyo inakuwa kodi ambayo alikataza na akatilia ngumu kwa mchukuaji kwani imechukuliwa pasina haki,sawa toka kwa waislamu au Ahlu dhima au Ahlul Harbi,kwani imechukuliwa kwao zaidi ya vile walivyoshurutishwa au zaidi ya vile wanavyochukuliwa wafanya biashara wetu pindi wanapokwenda katika miji yao.

Na zimepokelewa Athari zinaondosha mkindano huu wa wazi,

**أورد أبو عبيد في كتاب الأموال حديثاً مرفوعاً حين ذكر العاشر، فقال: "هو الذي يأخذ الصدقة بغير حقها"**

amepokea Abuu Ubeidi katika kitabu cha Al-amuali hadithi ambayo ni marfuu wakati akutaja AL-A'ASHIRU-MTOZA USHURU akasema : " Ni Yule ambaye anachukuwa sadaka pasina haki yake " .

Na ametafsiri hivyo Abu ubeida kwa kusema :" Ikiwa atazidisha zaidi ya asili katika kuchukuwa zaka,kwa hakika ameichukuwa pasina haki yake "

وفسر ذلك أبو عبيد قائلاً: "فإذا زاد في الأخذ على أصل الزكاة، فقد أخذها بغير حقها". ثم تابع قائلاً: "وكذلك وجه حديث ابن عمر حين سُئل: هل علمت أن عُمر أخذ العشر من المسلمين؟ فقال: لا، لا أعلمه.

na akaendelea kusema : " kadhalika ndio ilivyo upande wa hadihi ya Ibn Omar wakati alipoulizwa : Je unajua kuwa Omar alichukuwa Ushru toka kwa waislamu ? akasema Hapana,hapana silitambui hilo.

Bila shaka tunaona alikusudio hili,Yaani kuchukuwa ziada juu ya asili ya zaka,na wala hakukusaudia kuchukuwa zaka, na vipi alipinge hilo Ibn Omar ? na alikuwa Omar na Makhalifah wengine wakichukuwa zaka wakati wa kupewa,na ilikuwa Rai ya Ibn Omar kuwapa hao,kisha akaendelea kusema :"na kadhalika hadithi ya Ziyad bin Hudayr amesema :hatukuwa tukimtoza ushuru Muislam wala huahad,bila shaka alikusudia kwamba sisi tulikuwa tunachukuwa toka kwa waislam robo ya Ush'ru,na kwa ahlu dhimma tukichukuwa nusu ya Ush'ru,kama ilivyopokelewa hivyo kwa uwazi katika mapokezi mengine zilizopokelewa kwake".

Na amesema Abu Ubaeid kwamba kuchukuwa kwa watu wa dhimma kulimpa matatizo/mishkili,kwa sababu wao sio waislam mpaka ichukuliwe zaka toka kwao,na wala si watu wa vita mpaka wachukuliwe kama wanavyochukuliwa kwa waislamu,kisha akasema : " mpaka likatukia tukio ikaonekana kwamba Omar alipatana nao juu ya hilo,isipokuwa Jizyah/kodi ya kichwa,na Kharaji ya Ardhi", kama ilivyokelewa katika Mapokezi ya Qatadah toka kwa Abi Majlaz wakati Omar alipomtuma Othman Bin Hanif aende Iraq katika hadithi ndefu na imepokelewa humo :

"وجعل في أموال أهل الذمة التي يختلفون بها من كل عشرين درهماً درهماً، وجعل على رؤوسهم الجزية",

"na akaweka katika mali za Ahlu dhima ambazo hutofautiana kwazo kwenye kila Dirham ishirini Dirham moja,na akawawekea Jizyah ya vichwa vyao" kicha akaendelea kusema " Naomba kuchukuliwe katika biashara zao katika utaratibu wa asili ya sulhu,nayo hivi sasa ni haki ya waislam juu yao" na kadhalika alikuwa Malik bin Anas akisema :-

"إنما صولحوا على أن يُقرّوا ببلادهم فإذا مرّوا بها للتجارة أخذ منهم كلما مرّوا".

“Bila shaka walipewa sulhu juu ya kubakia katika miji yao.lakini pindi wakipitisha humo biashara zao watachukuliwa kwao kama walivyopita”
Kutokana na haya inakuwa kuwa hakuna kupingana katika hadithi hizo,na kwamba Kodi iliotajwa vibaya ni kule kuchukuwa mali pasina haki yake.
Na kwa kuzingatia hayo itachukuliwa Robo ya Ushru ikiwa ni zaka toka kwa wafanya biashara waislamu kwa zile biashara zao ambazo wanapita nazo mipakani mwa dola ,kwa sababu vifaa vya biashara zaka yake ni kama zakaya hela,kwa sababu zinathaminiwa kwa thamani yake,na cha wajibu kw zaka ya hela ni robo ya Ushru 10%,basi kadhalika ndiyo inavyokuwa zaka ya vifaa vya biashara.na wala haizidishwi juu yake,na wala haipunguzwi ni haki katika mali ya Muislamu,imeiwajibisha Mwenyezi Mungu juu yake kwa asina makundi manane yaliotajwa ikiwa ni zaka na takazo,na itawekwa katika ofisi ya zaka na itatumika katika matumizi yake.

Na itachukuliwa Nusu ya Ush’ru toka kwa wafanya biashara wa Ahludhimma juu ya biashara zao ambazo wanapita nazo katika mipaka ya dola kwa mujibu wa sulhu na makubaliano ambayo yaliwekwa pamoja na wao zama za Omar bin Khatwab,na ikiwa patawekwa mkataba mipya  na Ahlul kitab na wengineo patawekwa kiwango cha Ush’ru au Theluthi au Robo au Nusu au zaidi ya hayo au chini ya hicho kitakachochukuliwa katika biashara zao ambazo wanapita nazo katika mipaka ya Dola kwa sababu ni wajibu/lazima kutekeleza yale yaliokubaliwa.

Na ilikuwa ikichukuliwa Ush’ru 10% toka kwa wafanya biashara wa kivita kwa biashara zao ambazo wakipita nazo katika mipaka ya dola ikiwa ni kuwatendea kwa mfano ule ule wanaowatendea waislam,kama wanavyochukuwa toka biashara zetu basi tunachukuwa toka katika biashara zao,sawa kiwe ni kitu kidogo au kingi,na ilikuwa ush’ru 10% ndio kiwango walichokuwa wakichukuwa watu wa vita toka kwa wafanya biashara waislam ikiwa watapita katika miji yao zama za Omar

na makhalifah baada yake,kwa sababu hii wamechukuliwa watu wa vita Ush’ru 10% kuwaanyi sawa kwa sawa.toka kwa ziadi bin Hudayr amesema :Mtu wa mwanzo kutumwa na Omar bin Khatwab kukusanya Ush;ru ni mimi,akaniamrisha nisimchunguze Muislamu yeyote na atakaepita kwangu kwa kitu chochote nitakachochukuwa katika hesabu ya Dirhamu Arubaini dirhamu moja,na kwa Ahlu Dhimma kwa kila Ishirini nichukuwe moja na wale wasio na dhima watoe Ush’ru 10%”

**وعن أنس بن مالك قال: "بعثني عمر بن الخطاب على العشور، وكتب لي عهداً أن آخذ من المسلمين مما اختلفوا فيه لتجاراتهم ربع العشر، ومن أهل الذمة نصف العشر، ومن أهل الحرب العشر".**

Toka kwa Anas bin Malik amesema :amenituma Omar bin Khatwab kukusanya Ush’u,na akaniadnikia mkataba kwamba nichukuwe toka kwa waislamu kwa biashara zao tofauti tofauti robo ya Ush’ru,na toka kwa Ahlu dhima nusu ya Ush’ru na watu wa vita Ush’ru.

Na aliandika Abu mussa Al-ash’ariy kwa Omar akisema :Hakika wafanya biashara toka kwetu ni waislamu wanaokwenda ardhi ya vita huchukuliwa kwao Ush’ru,amesema :akaandika Omar : Chukuwa wewe kwa hao (makafiri) kama wanavyowachukuliwa wafanyabiashara wa kiislamu”.

Na wakaandika watu wa Manbij kwa Omar:”Turuhusu tuingie ardhi yako na utupangie kodi,amesema :Omar akawataka ushauri maswahaba wa Mtume (S.a.w)katika hilo na wakamshauri juu ya jambo hilo”kwa sababu hii kilikuwa kiwangio kinachochukuliwa kwa watu wa vita ndio hicho hicho wanachowachukulia wafanya biashara wetu ikiwa ni kutendeana usawa,basi ikiwa leo tutaweka makubaliano mapya/mikataba mipya na baadhi ya Dola itakayopanga kiwango itakachochukuwa toka kwa wafanya biashara wetu,hakika sisi ni wajibu kutekeleza kwa kuchukuwa kiwango toka kwa wafanya biashara wao kiwango kile kile kilichopangwa na makkubaliano /mikataba na wala haifai kuzidisha juu ya hapo.

Kwa hakika kile kinachochukuliwa katika Ush'ru toka kwa wafanya biasha wa Ahlu Dhimmah,na wafanya biashara wa Vita hizo ni Faiu/ngawira kwa waislamu na kitawekwa katika diwani/ofisi ya Faiu na Kharaji.

Na hakika kiwango kinachochukuliwa toka kwa Ahlu Dhimmah,na toka kwa wafanya biashara wa vita jambo lake limetegemezwa kwa Khalifah,yeye ndiye mwenye haki ya kuzidisha au kupunguza,kwa mujibu wa makubaliano/mikataba ya sulhu iliofungwa,au ambayo inafungwa,na kwa mujibu wa kutenda kwa mfano kama wanavyotendewa wafanya biashara waislamu,kwa mujibu wa vile anavyoona vina maslahi kwa uislamu na waislmu,na kuibeba Da'wah.toka kwa Abdallah bin Omar amesema : "alikuwa Omar akichukuwa toka kwa wa-Nebti mafuta na ngano nusu ya Ush'ru ili usombaji/uhemeaji chakula na bidhaa uwe kwa wingi katika mji na akichukuwa kwa QATNIYAH USh'ru"

**<u>USH'RU HUCHUKULIWA JUU YA NINI NA LINI HUCHUKULIWA</u>**

Ush'ru huchukuliwa katika mali zote za Biashara,kwa vyovyote zitakvyokuwa aina zake,sawa ziwe ni bidhaa,wanyama,mimea na matunda,na wala haichukuliwi katika zisizokuwa za biashara.haichukuliwi katika nguo za mtu,wala juu ya vyombo vyake na vifaa vyak binafsi kwa matumizi yake.na wala haichukuliwi kwa chakula chake.na ikiwa mtu atadai kuwa bidhaa alizobeba si za biashara,pamoja kwamba mfano wa vitu kama hivyo hufanywa vya biashara,hatokubaliwa isipokuwa kwa ushahidi,unaothibitisha madai yake.

Hautachuliwa Ush'ru kwa wafanya biashara wa Ahlu dhima au Ahlul harbi isipokuwa katika biashara zao zinazopita mipakani,na wala Hautachuliwa Ush'ru kwa wafanya biashara wa Ahlu dhima au Ahlul harbi katika biashara zao za ndani isipokuwa pale mkataba wa sulhu utakapokuwa umeleza hivyo,au mikataba ya kibiashara pamoja Dola nyingine ikiwa iko hivyo,kwa sababu wao hawana zaka juu yao.

Na wala si wajibu kwa Ahlu dhima walioko ndani ya dola isipokuwa Jizyah kwa vichwa vyao na Kharaj juu ya ardhi zao,isipokuwa yale yalioelezwa na mikataba ya Sulhu,kama kulisha wanajeshi na kuwapokea wageni wa kiislamu kwa mfano,kama ilivyopokelewa katika mkataba wa Omar(Al-ahdil Umariyah).Ahlul harbi hapana budi kujilazimisha kuwatendea vile wanavyotutendea,na kwa makubaliano ya mikataba,na masharti ya ruhusa ya kuingia katika Dola ya kiislam,ikiwa kitapatikana katika hivyo chochote juu ya biashara zao za ndani basi kitachukuliowa toka kwao,na kam hakuna basi hakitachukuliwa kwao chochote.ama waislamu wao wana wajibu wa kutoa zaka ya mali na bidhaa zao za biashara.

Na wala hauchukuliwi Ush'ru isipokuwa mara moja kwa mwaka juu ya bidhaa moja.hata kama biashara itapita mara nyingi kwa mtoza ush'ru.Toka kwa Ziyad bin Hudayr amesema : "hakika baba yake alikuwa anachukuwa toka kwa nasara kila mwaka mara mbili,akamwendea Omar bin Khatwab akasema : Ewe Amirul munina hakika Mfanya kazi wako anachukuwa toka kwangu mimi Ush'ru kila mwaka mara mbili.akasema Omar : hana haki ya kufanya hivyo,na haki yake ni kuchukuwa kila mwaka mara moja,kisha akamwendea akasema mimi ni mtu mzima wa kinaswar,akasema Omar : na mimi ni Mtu mzima wa Hanif(Nimetakasika na mila zote,nikawa Muislamu) nishaandika juu ya haja yako.

Na ikiwa atapita Zaidi ya mara moja Dhimiy na Harbiy na Bidhaa tofauti,ikiwa kila mara anapita na bidhaa mpya tofauti na biashara ya mwanzo,hakika tachukuliwa Ush'ru kwa kila biashara mpya atakayopita nayo,kama vile ambavyo huchukuliwa kwa muislam zaka kwa kila biashara yake anayopita nayo.ikiwa Muislam atasema kwamba tayari keshato zaka basi atakubaliwa kwa kutoa kiabu,au kwa maandishi atakayoyaonyesha kuwa tayari ametoa zaka ya biashara yake,kwa sababu zi wajibu kwa mwaka isipokuwa mara moja,na kila biashara anayopita nayo na ikiwa haijatolewa zaka basi itachukuliwa kwake Robo ya Ush'ru ikiwa ni zake yake.

Na itachukuliwa Robo ya Ush'ru toka kwa Mfanya biashara Muislamu pindi ikifikia biashara yake kiwango cha kutolewa zaka na ikapitiwa na mwaka,yaani imfikia thamani ya Dinar ishirini za Dhahabu,yaani Gram 85 za Dhahabu,au Dirhamu 200 za Fedha ,yaani thamani ya Gram 595 za Fedha.na wala haitachukuliwa kwake chochote ikiwa biashar a yake haikufikia kiwango cha zaka.na ama Dhimiyu na Harbhiyu watachukuliwa kwao wawili kwa kila mali ya biashara wanayoibeba sawa iwe ni nyingi au kidogo.

Na ilipokuwa kituo cha Mtoza Ush'ru ni hisia,kwa sabau Mtoza Ush'ru yupo katika hatari ya kuwadhulumu watu,kuhadaiwa na Rushwa,kwa sababu hii ni wajibu awe Mtoza Ush'ru ni katika watu wema na wacha mungu,ili asiwadhulumu watu,na akakosea kuwatendea watu,au akachukuwa zaidi ya kile cha wajibu kuchukuliwa kwao,na asije kudhoofika mbele ya hadaa,na mpaka asiwe mpokea Rushwa ili asije akafanya wepesi kwa njia hiyo pamoja na wafanya biashara akawapunguzia kile kiwango cha wajibu kuchukukiwa kwao kwa kupokea hadaa au Rushwa,akapoteza haki ya maitil mali haki ya waislamu.kama ni wajibu kukagua hali za Mtoza Ush'ru,atakaepatina ni muovu,ataadhibiwa au kuadabishwa au kuuzuliwa.

## <u>MALI YA HADAA YA WATAWALA NA WAFANYA KAZI WA DOLA,NA MALI ILICHUMWA PASINA NJIA YA KISHERIA NA MALI YA GHARAMA/FIDIA.</u>

Mali ya hadaa ni kila mali inayochumwa na watawala (wakuu wa wilaya),na watawaka wa Maeneo (Umaali)na wafanya kazi wa dola kwa njia zisizo za kisheria,sawa wamezipata kwa njia ya Dola,au kutoka katika mali za watu.si halali kwao isipokuwa vile wanavyopangiwa na dola miongoni mwa malipo au mshahara.na kila mali walioichuma kwa nguvu za kupora,au utawala au cheo na madaraka sawa itakuwa ni katika mali ya Dola au mali za watu inahesabika ni Hadaa,na ni chumo la haramu na ni mali isiyofaa kumilikiwa kwa sababu ni chumo kwa njia isiokuwa ya kisheria,na ni wajibu kuirejesha kwa wenyewe ikiwa watajulikana na kama hawakujulikana basi ni

wajibu kuitaifisha na kuiweka katika Baitil mali ya waislamu.amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu :-

**{ومن يغلل يأت بما غلّ يوم القيامة}.**

[Na atakayefanya Khiyana,atavileta siku ya kiama alivypvifanyia Khiyana.TMQ 3:161]

**وعن معاذ بن جبل قال: "بعثني رسول الله صلى الله عليه وسلم إلى اليمن، فلما سرت أرسل في أثري، فرددت، فقال: أتدري لم بعثت إليك؟ لا تصيبنّ شيئاً بغير إذني، فإنه غلول، ومن يغلل يأت بما غلّ يوم القيامة، لهذا دعوتك، فامض لعملك"، رواه الترمذي.**

Na toka kwa Muadhi bin Jabal amesema :"Amenituma Mtume wa Mwenyezi Mungu katika nchi ya Yemen,Pindi nilipoondoka alituma mjumbe nyuma yangu nikarudishwa,akaniambia : hivi unajua kwanini nimekutumia Mjumbe akurejeshe ? usichukue kitu pasina idhini yangu,kwani kufanya hivyo ni hadaa,na atakaehadaa atakuja na kile alichohadaa siku ya kiama,kwa sababu hii nimekwita,sasa nenda kaendelee na kazi yako."ameipokea Thirmidhii.

**وعن ابن مسعود قال: "بعثني رسول الله صلى الله عليه وسلم ساعياً، ثم قال: انطلق أبا مسعود، لا ألفينّك يوم القيامة تجيء على ظهرك بعير من إبل الصدقة له رغاء قد غللته، قال: إذاً لا أنطلق، قال: إذاً لا أكرهك".**

Na toka kwa Ibn Masoud amesema :-alinituma Mtume wa Mwenyezi Mungu nikiwa ni Mkusanyaji wa zaka,kisha akaniambia : Nenda Ibn Masoud,nisije kukuta siku ya kiama ukajaa mgongoni mwako una ngamia katika ngamia wa sadaka huku analia /anatoa sauti umemchukuwa kwa hadaa,akasema:kwa hiyo siondoki( kwenda kazini) akasema : kwa hiyo sikukarahishi.

NA NJIA ZA KUCHUMA ZISIZO ZA KISHERIA TOKA KWA MA-LIWALI NA UMALI NA WAFANYAKAZI WA DOLA NI HIZI:-

RUSHWA

RUSHWA:ni kila mali anayopewa Wali au A'amili au Kadhi au Mfanyakazi kwa ajili ya kukidhi na kutatua mambo ya watu,ambayo ni wajibu kuyakidhi pasina kutoa chochote.

Rushwa zote ni haramu,kwa vyovyote itakavyokuwa aina yake,iwe nyingi au kidogo,na kwa njia yeyote iliotolewa na kwa utendaji wowote ule iliotolewa.

**روى أبو داود عن أبي هريرة قال: "قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: لعنة الله على الراشي والمرتشي في الحكم".**

Amepokea Abudawda toka kwa Abu hurairah amesema :amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w)" Laana ya Mwenyezi Mungu Inamshukia Mtoa rushwa na mpokea Rushwa katika hukmu/maamuzi."

**وروى الترمذي عن عبد الله بن عمرو قال: "قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: لعنة الله على الراشي والمرتشي".**

Na amepokea Tirmidhii toka kwa Abdallah bin Omar amesema : Amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) " Laana ya Mwenyezi Mungu Inamshukia Mtoa rushwa na mpokea Rushwa ."

**وروى أحمد عن ثوبان قال: "لعن رسول الله صلى الله عليه وسلم الراشي والمرتشي والرائش بينهما".**

Na amepokea Ahmad toka kwa Thawban amesema : "Amemlani Mwenyezi Mungu Mtoa Rushwa na Mpokea Rushwa na Mtu wa kati yao"

Hadithi hizi ziko wazi katika kuthibisha uharamu wa Rushwa uharamu wa moja kwa moja.

Na Rushwa inaweza ikachukuliwa kwa ajili ya kukidhi/kupata Maslahi ambayo ni wajibu kuyatenda pasina kupewa chochote kwa Yule ambaye ni wajibu wake kutekeleza,na huenda ikachukuliwa ikiwa ni badala ya kutokufanya kazi ambayo ni wajibu kuifanya,na huenda ikachukuliwa ikiwa ili kufanya kazi ambayo dola inazuia kufanya kazi kama hiyo,na wala hakuna tofauti katika maslahi hayo kuwa ni ya kuleta maslahi au kuondoa madhara,na sawa itakuwa ni haki au batili,na mali yoyote itakayochumwa kwa njia ya rushwa inahesabika ni mali ya haramu,na inahesabika si yenye kumilikiwa kisheria,na ni wajibu kuitaifisha na kuiweka katika Baitil mali kwa sababu imechumwa kwa njia isiokuwa ya kisheria,na ni wajibu kumuadhibu aliyechukuwa,aliyetoa na mtu wa kati yao.

## ZAWADI NA HIBA

Zawadi na Hiba : Ni kila mali wanayopewa watawala wa Wilaya,Maeneo au Makadhi au wafanya kazi wa Dola kwa njia

ya Zawadi,au hiba nayo ni mfano wa Rushwa,si halali kwa Wali/kiongozi wa Wilaya au wa Eneo au kadhi au Mfanya kazi kuchukuwa Rushwa,na hata hakuna maslahi yajayo ayatakayo kwa mtoa zawadi au hiba ,kwa sababu anakuwa na tama ya kupata hadhi Fulani,au kupata maslahi kwa siku za baadaye.

Zawadi na Hiba kwa Ma-wali na watawala wa maeneo,na makadhi,na wafanya kazi wa Dola inazingatiwa ni khadaa,na Khadaa mafikio yake ni Motoni.

Na limepokelewa katazo la wazi la kukubali zawadi toka kwa Mtume (S.a.w)

**روى البخاري ومسلم عن أبي حميد الساعدي قال: "استعمل النبي صلى الله عليه وسلم رجلاً من بني أسد، يقال له ابن الأتبيّة على الصدقة، فلما قدم، قال: هذا لكم، وهذا أُهْدِيَ إليّ. فقام النبي صلى الله عليه وسلم على المنبر، فحمد الله وأثنى عليه، ثم قال: ما بال العامل نبعثه فيأتي يقول هذا لكم، وهذا أُهْدِيَ لي، فهلا جلس في بيت أبيه وأمه فنظر أَيُهْدَى له أم لا، والذي نفس محمد بيده، لا ينال أحد منكم منها شيئاً إلا جاء به يوم القيامة يحمله على عنقه، بعير له رغاء، أو بقرة لها خوار، أو شاة تيعر، ثم رفع يديه حتى رأينا عفرتي إبطيه، ثم قال: اللهم هل بلغت؟ مرتين".**

amepokea Bukharin a Muslim toka kwa Abii humaid Assa'idiy amesema : Mtume (S.a.w) alimpa kazi ya kukusanya sadaka mtu mmoja toka kabila la Bani Asadi,akiitwa Ibn Lutabiyyah,wakati aliporudi akasema : hii ni ya kwenu nahii ni kwangu nimepewa zawadi, akasimama mtume (S.a.w) juu ya minmbar akamshukuru Mwenyezi Mungu na kumsifia kisha akasema :ana nini Mfanyakazi tunamtuma halafu anakuja anasema : hii ni ya kwenu nahii ni kwangu nimepewa zawadi,basi kwa nini asikae nyumbani kwa baba yake na mama yake aangalie atapewa zawadi au hata pewa,namuapa Yule ambaye nafsi yangu ipo mkononi kwake,Hachukui mmoja wenu chochote isipokuwa atakuja nacho siku ya kiama huku akibebe juu ya shingo yake,(ikiwa ni )Ngamia anatoa sauti,au ng'ombe analia au Mbuzi analia,kisha kanyanyua mikono yake mpaka tukaona weupe wa makwapa yake,kisha akasema Mara Mbili : Ewe Mwenyezi Mungu Je Nimefikisha ?

na kutokana na haya basi kila kinachotolewa zawadi au hiba kwa Watawala wa Wilaya na wa Maeneo na makadhi na wafanyakazi wa Dola kinazingatiwa ni chumo la haramu,na si lenye kumilikiwa kisheria,na ni wajibu kulitaifisha na kuiweka

katika baitil mali ya waislamu kwa sababu ni chumo lisilokuwa la kishria.

MALI AMBAZO ZIMATAWALIWA NA WATAWAKA KWA NGUVU

Hizo ni mali ambazo zinataliwa na watawala,na watawala wa Wilaya na wa maeneo,au jamaa zao wa karibu,na wafanya kazi wa Dola,miongoni mwa mali za Dola,au ardhi zao, au katika mali za watu,au ardhi zao kwa nguvu,na kutwaa/kuvamia,na kushinda kwa nguvu za utawala na cheo,na kila mali inayovamiwa/twaliwa pasina haki,na kila ardhi inayovamiwa katika mali za dola na ardhi zake,au mali za watu na ardhi zao kwa sababu imechumwa kwa njia isiokuwa ya kisheria,na kila kutwaa kwa njia yeyote katika njia hizi inazingatiwa ni chumo la haramu,na wala hamiliki kwa njia yoyote katika njia hizi ila atahesabika ni dhalimu,na dhulma ni haramu na kiza siku ya kiama,kama vile anahesabika njia hiyo ni Khadaa,na khadaa ni njia ya Motoni,

**عن النبي صلى الله عليه وسلم:" من أخذ من الأرض شيئاً بغير حق خسف به يوم القيامة إلى سبع أرضين"، وفي رواية: "من أخذ شبراص من الأرض ظلماً فإنه يطوقه يوم القيامة من سبع أرضين"، رواه الشيخان.**

Toka kwa Mtume (S.a.w) amesema : “Yeyote Mwenye kuchukuwa chochote katika ardhi pasina haki atazamishwa siku ya kiama mpaka ardhi ya saba” na katika mapokezi mengine “yeyote mwenye kuchukuwa Shubiri moja ya ardhi kwa dhulma basi kwa hakika atazamishwa siku ya kiama katika ardhi saba” Imepokewa na Sheikhani/Masheikh wawili.

**وعن عائشة أن النبي صلى الله عليه وسلم قال:" من ظلم شبراً من الأرض، طوقه الله من سبع أرضين"، متفق عليه.**

Na toka kwa Aisha ( R ) kwamba Mtume (S.a.w) amesema : “yeyote mwenye kudhulumu shubiri moja ya ardhi,atazamishwa katika ardhi saba”Muttafaqu alayh.

Na mali na ardhi ambazo zinaporwa ikiwa zitakuwa ni mali za watu basi ikiwa watajulikana wenyewe ni wajibu warejeshewe,na ikiwa hawajulikani basi ni wajibu ziwekwe katika baitil mali.na ikiwa ni katika mali za dola basi ni wajibu kuzirjesha katika baitil mali kwa kauli moja.kama

alivyopkelewa kwa Omar bin Abdul-aziz wakati alipotawala Khilafah alikusanya mali zote pamoja ardhi zilizoporwa na utawala wa Bani Umayyah kwa nguvu katika milki ya watu na milki ya dola zirejeshwe katika Baitil mali,isipokuwa zile ambazo walijukana wenyewe akawarudishia.

Na kwa hakika aliwasafisha bani umayah kwa maeneo waliyoyakata na waliokhusika nayo,na vyote walivyotaa/vamia,kwa sababu alivihesabu kuwa wamevimiliki kwa nguvu ya utawala wa bani umayyah,na kwa njia isiokuwa ya kisheria,haifai kumiliki kwa njia hiyo,na alijianza yeye mwenyewe akajivua na mali zake zote na anavyovimiki,na vipando vyake vyote na manukato yake na bidhaa zake,kisha akaviuza kwa Dirham Ishirini na tatu elf na akaziweka katika Baitil mali.

UDALALI NA KUWA KIBARAKA/MTUMISHI

Hizo ni kila mali wanazozichuma watawala wa wilaya au wa maeneo na wafanyakazi wa dola kwa udalali au kuwa ni watumishi vibaraka wa mashirika ya kijeni,au ya kimaeneo/kitaifa au watu mmoja mmoja kwa mkataba wa mauziano au mikataba kati ya dola na wao,na kila wanachokichuma kwa njia hii kinahesabika ni Khadaa na chumo haramju,na wala haifai kumiliki kwa njia hii na ni wajibu iwekwe katika bailtil mali ya waislam,kwa sababu imechumwa kwa njia isiokuwa ya kisheria.

**عم معاذ بن جبل قال: "بعثني النبي صلى الله عليه وسلم إلى اليمن، فلما سرت، أرسل في أثري، فرددت، فقال: أتدري لم بعثت إليك؟ لا تصيبن شيئاً بغير أذني فإنه غلول، ومن يغلل يأت بما غل يوم القيامة، لهذا دعوتك، فامض لعملك".**

Na toka kwa Muadhi bin Jabal amesema :"Amenituma Mtume wa Mwenyezi Mungu katika nchi ya Yemen,Pindi nilipoondoka alituma mjumbe nyuma yangu nikarudishwa,akaniambia : hivi unajua kwanini nimekutumia Mjumbe akurejeshe ? usichukue kitu pasina idhini yangu,kwani kufanya hivyo ni hadaa,na atakaehadaa atakuja na kile alichohadaa siku ya kiama,kwa sababu hii nimekwita,sasa nenda kaendelee na kazi yako."ameipokea Thirmidhii.

Udali na ukibaraka kwa mashirika,watu,watawala wa mikoa,watawala wa maeneo na wafanyakazi wa dola,hupewa wao pasina dola kufahamu na ndani yake na hiyo ni Rushwa,wanapewa ili mashirika yaweze kumakinika au watu wamekinike waweze kupata mikataba ya kibiashar au kupata mikataba ya lazima ya kufanya miradi kwa sura ambayo itawathibitishia kupata maslahi yao,na wala sio maslahi ya Dola.
BISMILLAHI RAHMANI RAHIIM

VILIVYOPORWA
Nazo ni mali ambazo zinaporwa na Watawala wa Wilaya na watawala wa maeneo na wafanyakazi wa Dola katika mali zilizowekwa katika matumizi ya uangalizi wao,au kwa kusimamia kazi zake,au kusimamia juu ya uanzishwaji wake au miradi au nyinginezo katika mambo ya Dolan a vile vinavyoambatana navyo,na yanaunganishwa na haya yale anayochukuwa wafanyakazi wa Posta,Umeme,Simu na Mawasiliano na Ofisi Nyingine za Serikali miongoni mwa watu kuchukuwa zaida ya malipo yaliopangwa (wakachukuwa ) kwa njia ya kutokujulikana,na hadaa na uongo.
Mali zote hizi ambazo zinachumwa kwa njia ya kupora katika mali ya Dola,au kwa njia ya Kughafilika na kuwahadaa watu inazingatiwa ni chumo la haramu na haifai kumiliki kwa njia hiyo,nayo ni katika Khadaa ni wajibu kuitaifisha na kuiweka katika Baitil-mali.

Na alikuwa Omar Bin Khatwab pindi akiwa na kutokulewa/Shubha juu ya kiongozi wa wilaya au wa neo humtafisha mali zake amabazo zinazidi rizki yake aliopangiwa, au mgao wake juu yake,na alikuwa akizihesabu mali za watawala wa Wilaya na wa maeneo kabla hajawateua kuwa watawala na baada ya kutawala,ikiwa atawakuta wana mali ya ziada au kakuta shubha katika hilo,basi ataitaifisha mali hiyo au atawagaia na anaweka zile alizozichukuwa toka kwao katika bailil mali.

Kama vile alitaifisha toka kwa Abusufiani wakati aliporudi toka kwa mwanawe Muawiyah,na alikuwa wali wa Omar katika mji wa Sham,na alikuwa Abusufiani amekuja kumsalimia Omar,Omar akamwambia – na alikuwa ametokewa katika moyo wake kwamba mwanawe atakuwa amempa mali baba yake wakati wake wa kurudi- akasema : Tupe zawadi ewe Abusufiani ,akasema :hatukupa kitu ili tukupe zawadi,akanyooosha omar mkono wake kwenye pete iliopo mkononi mwa Abusufini akaichukuwa,na akamtuma Mjumbe kwa Hindu Mke wa Abusufiani ,na akamuarisha mjumbe ambaye amemtuma amwambie kwa sauti ya Abusufiani :angalia ile mifuko miwili ambayo nimekuja nayo unitumie,mara punde akarudi mjumbe na mifuko miwili ndani yake kuna Dirham alf kumi,basi Omar akazirusha katika Baitil mali.

Yote yaliopita katika vile wanavyovichuma watawala wa wilaya na wa maeneo na wafanya kazi wa Dola,kwa njia isiokuwa ya kisheria vinakuwa ni katika mapato ya Baitil mali,na inaunganishwa na hayo vitu ambavyo navyo vitakuwa katika mapato ya baitil mali,kila kitu kinachochumwa na watu kwa njia miongoni mwa njia zilizozuia kisheria kwa kukuza umiliki kwavyo,kwa sababu vinakuwa ni chumo la haramu,na wala haipaswi kuviliki.

Yeyote mwenye kuchuma kitu kwa njia ya Riba kinakuwa ni haramu na si chenye kumilikiwa,kwa sababu Mwenyezi mungu Mtukufu ameharamisha Riba na ameharamisha kuiendeleza/kuikuza mali kwa njia ya hiyo,amesema Mwenyezi Mungu mtukufu :-

**( الذين يأكلون الربا لا يقومون إلا كما يقوم الذي يتخبطه الشيطان من المس، ذلك بأنهم قالوا إنما البيع مثل الربا، وأحل الله البيع وحرم الربا، فمن جاءه موعظة منن ربه فانتهى فله ما سلف، وأمره إلى الله، ومن عاد فأولئك أصحاب النار هم فيها خالدون).**

Wale wanaokula riba,hawasimami (Kuendesha yao ) ila kama anavyosimama yule ambaye shetani kamzuga kwa kumsawaa;(wako mbioni tu,hawana kituo).(Na)haya ni kwa sababu wamesema “Biashara ni kama riba”,hali Mwenyezi Mungu amehalalisha biashara na kuharamisha riba.na

aliyefikiwa na mauidha kutoka kwa Mola wako (ya huku kukatazwa riba),kisha akajizuia,basi yamekwisha mthibitikia yale (mali)yaliopita (aliyokwisha yapata ) na hukumu yake iko kwa Mwenyezi Mungu.Lakini wanaorejea (kula riba) basi hao ndio watu wa motoni,humo watakaa milele.(TMQ 2:275)

Na ni wajibu kuirejesha mali ya riba kwa wenyewe ambao imeliwa kwao ikiwa wanajulikana,na ikiwa si wenye kujulikana basi itataifishwa na itawekwa katika Bait mali,amesema Mwenyezi Mungu mtukufu :-

**(يا أيها الذين آمنوا اتقوا الله وذروا ما بقي من الربا إن كنت مؤمنين، فإن لم تفعلوا فأذنوا بحرب من الله ورسوله، وإن تبتم فلكم رؤوس أموالكم لا تظلمون ولا تظلمون)**

Enyi Mliamini ! Mcheni Mwenyezi Mungu ,na achni yaliobaki katika riba,ikiwa mmeamini.Na kama hamtafanya (hivyo) basi fahamuni mtakuwana vita na Mwenyezi Mungu na mtume wake.na mkiwa mmetubu ,basi mtapata raslimali zenu,msidhulumu na wala msidhulumiwe.(TMQ 2:278-279)

Na yeyote atakayechuma mali kwa nia ya kamari linakuwa chumo lake ni la haramu,na si lenye kumilikiwa ,na itarejeshwa kwa mwenyewe,na ikiwa hajulikani mwenyewe,itataifishwa na kuweka katika Baitil mali,kwa sababu kuendeleza milki kwa njia ya kamari ni haramu na wala haifai kisheria,kamari ni haramu,amesema Mwenyezi Mungu mtukufu :-

**( يا أيها الذين آمنوا إنما الخمر والميسر والأنصاب والأزلام رجس من عمل الشيطان فاجتنبوه لعلكم تفلحون. إنما يريد الشيطان أن يوقع بينكم العداوة والبغضاء في الخمر والميسر ويصدكم عن ذكر الله، وعن الصلاة هم منتهون).**

Enyi mliomini Bila shaka ulevi na kamari na kuabudiwa (na kuombwa) asiyekuwa Mwenyezi Mungu na kutazama kwa mishare ya kupigia ramli (na kwa vinginevyo),(yote haya) ni uchafu (Ni) katika njia ya shetani.Basi jiepusheni navyo, ili mpate kufaulu (kutengenekewa)Hakika shetani anataka kukutieni uadui na bughudha baina yenu kwa ajili ya ulevi na kamari na anataka kukuzuilieni kumkumbuka Mwenyezi Mungu na (kukuzuilieni) kuswali.basi je,mtaacha (Mabaya hayo)? (TMQ 5:90-91)

<u>GHARAMA- FIDIA</u>

Kadhalika miongoni mwa mapato ya Baitil mali ni Gharama/fidia ambazo dola huwatoza wale wanaofanya baadhi ya madhambi,au kwa wale wanaofanya mambo kinyume na kanuni zilizowekwa,au taratibu za kiiidara au mipango(iliowekwa).

Na kutoza Gharama ni jambo lililothibiti katika sunnah.

Amepokea Omar bin Shuayb toka kwa Baba yake,toka kwa babu yake Abdallah bin Amr Bin A'si toka kwa Mtume (S.a.w) kwamba aliulizwa juu ya thamani ya Matunda yalioning'inizwa,akasema:

**عمرو بن شعيب عن أبيه عن جده عبد الله بن عمرو بن العاصعن رسول الله صلى الله عليه وسلم، أنه سئل عن الثمرالمعلق، فقال:" من أصاب بفيه من ذي حاجة غير متخذ خبنة، فلا شيء عليه، ومن خرج بشيء منه فعليه غرامة مثلية والعقوبة"**

"Yeyote mwenye kupata kwa Mdomo wake toka kwa mwenye haja si mwenye kufanya Kuficha/Khadaa hana lawama juu yake,na mwenye kutoka na kitu chochote basi juu yake (atoe) gharama/fidia ya mfano wake na(apewe) adhabu"

**كما روي عن النبي صلى الله عليه وسلم أنه قال: " ضالة الإبل المكتومة غرامتها ومثلها معها"**

Kama ilivyopokelewa toka kwa Mtume (S.a.w) kwamba amesema : "ngamia aliopotea ambaye gharama zake zimefichikana na mfano wake pamoja"

Kadhalika kuchukuwa kwake toka kwa wale waliozuia kutoa zaka (alichukuwa)nusu ya mali yake,zaidi ya zaka ya wajibu ikiwa ni Ta'azir/adhabu kwake,kwa kauli yake Mtume (S.a.w)

**"......ومن ومنعها فأنا آخذها وشطر ماله"**

……..Na mwenye kuizua(zaka) hakika sisi tutachukuwa zaka na nusu ya mali yake"

Na yote haya yanaonyesha juu ya sheria ya ulazima wa gharama ikiwa ni adhabu na maonyo,Khalifah ana haki ya kupanga aina za madhambi na makosa ambayo yatawekewa gharama/fidia na kiwango cha gharama na fidia hizi akibainisha kiwango cha juu na cha chini,na awalazimishe ma-wali na ma-umali na ma-kadhi kuyatekeleza hayo,kama vile anapaswa asiache jambo la kupanga kiwango kwa jitihada za ma-wali,na ma-umali na ma-kadhi na wafanya kazi kwa mujibu wa kanuni maalum kwa hayo,afanye kile anachokiona kinafaa katika

kuchunga mambo ya waislamu kwa mujibu wa vile inavyompelekea jitihada yake.

**KHUMSI YA HAZINA NA MADINI**

**Hazina(Arrakaizu) Ni mali iliozikwa/fukiwa katika ardhi,sawa imekuwa ni Fedha,au Dhahabu,au Vito vya Thamani,au Lulu,au mengineyo miongoni mwa mapambo na silaha,sawa itakuwa ni hazina ilizikwa/fukiwa na watu wa zamani,kama vile wa-Misri,wa-Bablioni,wa-Ashour,wa-Sasaniyina,wa-Rumi,wa-Giriki,na wengineo,kama vile hela,mapambo na vito vilivyopatikana katika makaburi ya wafalme wao na watukufu wao,au katika mapori ya miji yao ilioharibika,au hela za dhahabu au fedha zilizowekwa katika vyungu au kwingineko,zimefichwa katika ardhi toka zaka za kijahilia,au zama za Dola ya kiislama iliopita,vyote hivyo vinahesabika ni hazina.**

**Na neno (Arrikazi)limetoholewa toka neno la Rakaza yarkizu,mfano wa Gharaza Yaghrizu(maana yake ) pindi inapofichika,inasemwa :Rakazar Rumha(ameuchomeka mkuki) Pindi atakapouchomeka katika ardhi,na katika maana hii Rikzu ;sauti ya chini .ameseama Mwenyezi Mungu Mtukufu "au unasikia hata mchakato wao ? TMQ 19:98"**

**(أو تسمع لهم ركزا).**

Ama madini : hayo ni yale alioyaumbwa Mwenyezi Mungu katika ardhi,siku alipoumba mbingu na ardhi,miongoni mwa dhahabu,fedha,shaba,risasi na mengineyo.

Neno madini limetoholewa kutoakana na neno "adanal-makana,Ya'dinu yaani pindi atakaposimamia mahahala hapo,na kutokana na neno hilo imeitwa pepo ya Adni kwa sababu ni nyumba ya kukaa milele,basi madini ni katika alivyoviumba Mwenyezi Mungu,na wala si katika vilivyizikwa/fukiwa na viumbe,kwa sababu hii yanatofautiana na hazina kwa sababu hazina ni katika vilivyozikwa/fukiwa na wanaadamu.

Na asili ya hazina na madini ni yale yalipokelewa na Abuhurairah,toka kwa Mtume (S.a.w) amesema " Jeraha la Al-

amau(Mnyama alimtoroka mwenyewe)kujeruhi kwake hakuna fidia,na katika hazina kuna Khumsi"

**هريرة عن رسول الله صلى الله عليه وسلم أن قال: " العجماء جرحها جبار، وفي الركاز الخمس"**

Na yale yaliopokelewa toka kwa Abdillah Bin Omar ( R ) kwamba Mtume (S.a.w) aliulizwa juu ya mali ambayo inapatikaana katika Magofu ya kawaida akasema"hayo ni hapo na katika Hazina ni kutoa Khumsu" na yale yalipokelewa toka kwa Ally Bin Abitwalib ,toka kwa Mtume (S.a.w) hakika yeye amesema : " na katika Suyubu Kuna khumsu,amesema : Na Assuyubu ni mizizi (Vyanzo) ya dhahabu na fedha ambazo zipo chini ya Ardhi".

**وماروى عن بعد الله بن عمرو أن النبي صلى الله عليه وسلم سئل عن المال الذي يوجد في الخرب العادي فقال: " فيه وفي الركاز الخمس" وماروى عن علي بن أبي طالب عن النبي صلى الله عليه وسلم أنه قال: " وفي السيوب الخمس، قال: والسيوب عروق الذهب والفضة التي تحت الأرض".**

Na kutokana na hayo basi kwa hakika kila mali ilizikwa/fukiwa ,miongoni mwa dhahabu,au fedha,au mapambo,au vito au vinginevyo,yamepatikama makaburini au maporini,au katika miji ya watu wa zamani,na ikapatikana katika ardhi maiti,au katika magofu ya kawaida,au ni ya zamani kwa upande wa watu wa a'di ,katika vilivyozikwa/fukiwa zama za kijahilia au vimefukiwa na waislamu,katika zama za dola ya kiislamu iliopita,vinakuwa ni milki ya aliyevipata atoe khumsi kwa Baitil mali.

Kwa sababu hiyo basi kila madini machache,si yenye kuhesabika,miongoni mwa dhahabu au fedha,sawa itakuwa ni miziz au mchanga/Tibran yaliopatikana katika ardhi maiti isiokuwa milki ya yeyote nasi hichi kitakuwa ni milki ya aliekipata atoe khumsi katika Baitil mali.

Na Khumsi ambayo inachukuliwa toka kwa aliyepata hazina,na toka kwa aliepata madini inakuwa na hadhi ya kama ghawira,na inachukuwa hukmu yake,na inawekwa katika Baitil mali,katika Diwani.ofisi ya Ghawira na Kharaji na inatumika katika matumizi ya Ghawira na Kharaji,na linakuwa jambo lake limetegemezwa kwa Khalifah inaitumia katika kusimamia

mambo ya uma,na kutatua maslahi yake kwa mujibu wa rai yake na jitihada zake,kwa yele yenye Kheri na uzuri.

Toka kwa Mujahid,toka kwa Ash'sha'bii "Kwamba Mwanamme mmoja alipata Dinar alfu moja zilizozikwa nje ya Madina,akamelekea Omar Bin Khatwab,akachukuwa Khumsi Dinar mia mbili,na akampa Yule mwanamme thamani yake,na akawa Omar anagawa zile mia mbili kwa wale waliokuwepo miongoni mwa Waislamu,mpaka kilipobaki kiasi kidogo,akasema Omar yuko wapi mwenye Dinar(Aliokota) akasimama mbele yake ,akamwamboa Omar; chukuwa hizi Dinar ni zako

**عن مجالد عن الشعبي " أن رجلا وجد ألف دينار مدفونة خارجا من المدينة، فأتى بها عمر بن الخطاب، فأخذ منها الخمس مائتي دينار، ودفع إلى الرجل بقيتها، وجعل عمر يقسم المائتين بين من حضره من المسلمين، إلى أن أفضل منه فضلة.فقال عمر: أين صاحب الدنانير؟ فقام إليه، فقال له عمر: خذ فهذه الدنانير فهي لك"**

Na toka kwa Alharithi bin AbilHarith Al-azdiy"kwamba baba yake alikuwa ni mjuzi wa Madini kuliko watu wote,na kwamba yeye alimuendea mtu alitoa/chimbamadini akanunua kwake kwa mbuzi mia moja wenye kufuatana,akasema:akayachukuwa na akayayeyusha,akatoa k=humo thamani ya Mbuzi alfu moja,akamwambia Muuzaji,nirejeshee Biashara yangu,akasema :sifanyi,akasema:wallah nitamuendea Allya na nitakuaibisha,-akawendea Ally-yaani Ally bin Abii twalib-akasema : hakika Abal-harithi kapaya Madini,akaniletea,akasema :iko wapi hazina ambayo umeipata ?akasema sikupata hazina bali nimenunua kwake kwa Mbuzi Mia moja wenye kufuatana. Ally akamwambia:sioni Khumsi isipokuwa ipo juu yako,akasema:akatoa Khumsi ya Mbuzi mia moja.

**وعن الحارث بن أبي الحارث الأزدي " أن أباه كان من أعلم الناس بمعدن، وأنه أتى على رجل قد استخرج معدنا، فاشتراه منه بمائة شاة متبع، قال: فأخذه فأذابه، فاستخرج منه ثمن ألف شاة، فقال له البائع: رد علي البيع، فقال لا أفعل، فقال: لآتين عليا فلأثين عليك - أي لأشين- فأتى عليا- يعني علي بن أبي طال- فقال: إن أبا الحارث أصاب معدنا، فأتاه علي، فقال: أين الركاز الذي أصبت؟فقال: ما أصبت ركازا، إنما أصابه هذا فاشتريته منه مئة بمائة شاة متبع. فقال له علي: ما أرى الخمس إلا عليك، قال: فخمس مائة الشاة.**

Na kutokana na hadithi ya Ash'sha'abii,na hadithi ya Alharith inabainika kuwa kiwango ambacho alichukuwa Omar toka kwa aliepata Hazina,na kile alichochukuwa Ally toka kwa aliepata

Madini,bila shaka hicho ni khumsi peke yake,na hakika Khumsi tano zilizobaki zilireejeshwa kwa aliepata Hazina,na aliepata madini,na kwamba Khumsi iliochukuliwa haikuwa zakkah,na waha hakumpa Omar katika hiyo kwa aliyeapata zaka kwa sababu yeye ni tajiri na zaka haifai kupewa tajiri.

Na kila mwenye kupata hazina,au madini itachukuliwa kwake Khumsi sawa atakuwa aliepata ni mwanamme au mwanamke,mdogo au mkubwa,mwenye akili au mwandawazimu,muislamu atakuwa au kafiri dhimiyi,na itachukuliwa Khumsi kwa kiwango chochote kilichopatikana,sawa kitakuwa ni kidogo au kingi,naa mwenye kupata hazina au madini katika milki yake miongini mwa ardhi au majengo basi yeye ataimiliki ,sawa atairithi ardhi hiyo au jengo,au aliinunua toka kwa mtu mwingine,na mwenye kukuta hazina au madini katika ardhi ya mtu mwingine au jengo lake itakuwa ni hazina,au madini ambayo yamepatikana kwa mwenye ardhi au mwenye jengo na wala si ya Yule aliepata hazina au madini.

Na mwenye kupata hazina au madina katika mji wa vita ataimiliki na itakuwa ni ghawira,na juu yake atapaswa kutoa Khumsi kama vile /Yule anaeipata katika ardhi maiti na magofu ya zamani katika mji wa Usilamu.

Na ni wajibu kutoa Khumsi kwa kule kupata hazina tu,au madini,na wala haifai kuchelewesha kuitoa na kuipa Baitil mali.

Na madini ambayo anayamiliki mwenye kuyapata hayo ni madini machache,ama madini mengi hakika haya hayamilikiwi na anayeyapata kwa sababu hayo ni katika milki ya uma ambayo haifai kumilikiwa na watu binafsi,bali hayo ni milki ya waislamu wote.

**Mali isiokuwa na Mrithi wake**

**Kila mali sawa itakuwa ni yenye kuhamishika au si yenye kuhamishika,wenyewe wamekufa,na hakusitahiki yeyote kuirithi kwa Fardhi(fungu maalum)au kwa Ta'asib (kuchukuwa mali iliobaki baada ya wenye mafungu maalum)kama vile mtu fulani akafa,na wala hukuwa na mrithi miongoni mwa mke,au watoto,au mababa.au ma-**

**mama,au ma-kaka,au ma-dada,au asaba,(wanaochukuwa mali baada ya wenye mafungu) hakika mali hii itahamia Baitil mali ikiwa ni Mirathi.**

**عن المقدام الكندي عن النبي صلى الله عليه وسلم قال: أنا أولى بكل مؤمن من نفسه، فمن ترك دينا، أو ضيعه فإلي، ومن ترك مالا فلورثته، ، وأنا مولى من لا مولى له، أرث ماله، وأفك عانيه" رواه الشيخان والترمذي.**

Toka kwa Al-miqdadi Alkindy toka kwa Mtume (S.a.w) amesema :Mimi ni bora kuliko Muumini na Nafsi yake,basi yeyote mwenye kuacha deni au Familia basi ni juu yangu(Kulipa na kuitazama ),na mwenye kuacha mali basi ni ya warithi wake,nami ni Msimamizi kwa asiye na msimamizi,narithi mali yake na nitamuokoa mateka wake kwa kumfidia .Ameipokea Sheikhani na Tirmidhii.

Na hadithi hii iko wazi na wazi kiushahidi katika kwamba mtu pindi akifa na hana wa kumrithi,hakika mrithi wake anakuwa ni Mtume (S.a.w),kwa sababu ni kiongozi wa waumini wote,na ni msimamizi wa Yule asiyekuwa na msimamizi,na baada yake umehama uongozi kwenda kwa Khalifah,na amekuwa Khalifah ndio kiongozi wa waumini wote,na msimamizi wa Yule aisyekuwa na msimamizi,na ni mrithi wa Yule asiyekuwa na mrithi,na kurithi kwake khalifah hakuwa kwa nafsi yake,na bila shaka si vinginevyo ila ni kwa baitil-mali ya waislamu,kwa sababau hii inabadilika mirathi ya Yule asiyekuwa na mirathi toka milki Khasa na kuwa milki ya Dola,na inawekwa katika Baitil-mali,katika diwani/ofisi ya Ghawira na Kharaji,na atatumia Khalifah hizo kwa mujibu anavyoona katika mambo ya waislam,yale yenye kheri na kutengeneza,ana haki ya kuviuza,na kuvikodisha,kuviweka wakfu,kuvitoa zawadi na kuwakatia watu,na kuvitoa kuhudumia jambo lolote katika mambo ya waislamu anayoyaona.

Na inaunganishwa na mali za waislamu ambao hawana wa kuwarithi,mali ya Dhimmiy ambaye hana wa kumrithi,Dhimmiy yeyote ataekufa na akaacha mali yenye kuhamishika au isiohamishika,na hakuwa na mrithi,itakuwa mali yake ni Ghawira kwa Waislamu,na pia mali ya Muislamu itakayobaki baada ya warithi kupewa mafungu yao,kama vile

mtu akifa na hana wa kumrithi isipokuwa mume au mke,kwa sababu mke na mume hawarudishiwi kile kinachobaki baada ya kuchukuwa mafungu waliopangiwa,basi kile kilichobaki baada ya mirathi yao kinakuwa ni Ghawira kwa waislamu,na kitawekwa katika baitil-mali ya waislamu,kwa sababu ni mali ambayo haina mtu maalum mwenye kustahiki basi imekuwa ni Ghawira kama vile mali ya muislamu ambaye hana wa kumrithi.

**MALI YA WALIORITADI/WALIOTOKA KATIKA UISLAMU**

**Murtadi: Ni aliyetoka katika didi ya kiislamu na kwenda katika ukafiri,amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu :**

**( ومن يرتدد منكم عن دينه فيمت وهو كافر فأولئك حبطت أعمالهم في الدنيا والآخرة، وأولئك أصحاب النار هم فيها خالدون).**

[Na watakaotoka katika dini yao katika nyinyi,kisha wakafa hali kuwa makafiri,basi hao ndio ambao amali zao zimeharibika katika dunia na akhera.Na hao ndio watu wa motoni;humo watakaa milele. TMQ 2:217]

Basi mtu ambaye anaritadi/anatoka katika Uislamu- sawa awe ni mwanamme au mwanamke- akaenda katika dini nyingine kama vile Uyahudi au Unaswara,au Umajusi ,au Ubudha,au dini nyingine,kama Ukomonist,( au Demokrasia ) Damu yake inakuwa haijahifadhika,na kinachofuata na mali yake inakuwa haijahifadhika,kwa sababu utukufu wa kuhifadhika mali yake unafuatana na kuhifadhika damu yake,basi pindi ukaharibika kuhifadhika damu,basi inafuata kutokuhifadhika mali,kwa sababu utukufu wa mali hufuatana na utukufu wa damu,ukiharibika utukufu wa damu kwa kuritadi,unakuwa utukufu wa mali ni mwepesi kuharibika kuliko daku,amesema Mtume (S.a.w) :

**قال صلى الله عليه وسلم " أمرت أن أقاتل الناس حتى يقولوا لا إله إلا الله فمن قال لا إله إلا الله فقد عصم مني نفسه وماله إلا بحقه وحسابه على الله "**

“Nimeamrishwa kupigana na watu,mpaka waseme hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu Mmoja,(atakayesema Hivyo)basi kwa hakika amehifadhi kwangu mimi nafsi yake na mali yake isipokiwa kwa haki yake na hesabu yake ipo juu ya Mwenyezi Mungu”

Na kumwaga damu kwa ajili ya kuritadi si sawa na kumwaka damu kwa ajili ya kufanya ujambazi,au kwa zinaa ya mtu mzima au kuua kwa makusudi,kwa sababu ujambazi,zinaa ya mtu mzima,na kuua kwa makusudi,hakufurishwi muislamu kwa kuyafanya hayo maovu,na wala hakuharibu utukufu wa mali yake,isipokuwa anabaki jambazi,mzinifu mtu mzima,na kuua kwa makusudi wote hawa wanabaki kuwa ni waislam,ni wenye kuruthi na kirithiwa,ama kuriyadi kwa hakika anakufuru mwenye kuritadi na unaharibika utukufu wa damu yake na mali yake.

Na Murtadi kwa kule kuritadi tu wanamiliki waislamu kumwaga damu yake,na wanamiliki haki ya kutwaa mali yake,isipokuwa kumuua na kutwaa mali yake kusimamiwa juu ya kumtaka atubue,ikiwa atatakiwa atubie ndani ya siku tatu na wala hakutubia,na wala hakurudi katika Uislamu,ni wajibu kumuua muda huo huo,na kuitwaa mali yake na itakuwa ni ghawira kwa waislamu,itawekwa katika Baitil mali ya waislamu katika Diwani/ofisi ya Ghawira na Kharaji na itatumika katika matumizi yake ,na wala haitarithiwa mali yake,kwa sababu ameritadi,ikiwa ataritadi mmoja wana ndoa kabla ya Dukhuli(kungia Kwa mume)ndoa itaharibika saa hiyo hiyo,na kwa jili hiyo hakuna kuruthiana,pia ikiwa kuritadi kumetokea baada ya Dukhuli itaharibika ndoa baina yao,na yeyote atakayekufa hatarithiwa na mwingine(Mwenzie) kwa sababu mmoja ni Muislamu na Mwingine ni Kafiri,kama vile ikiwa murtadi atafiwa na mrithi wake muislamu,na kafiri hamrithi muislamu,na litakuwa fungu lake ni la warithi wengine waliobaki ikiwa huko kuna warithi wengine,na ikiwa hakuna warithi wengine basi itakuwa mirathi yake yote ni Ghawira kwa Waislamu na itawekwa katika Baitil-mali ya waislamu,na ikiwa murtadi ana warithi miongoni mwa watoto,au ma-baba,au ma-mama,au makaka na madada,hakika wao hawamrithi,kwa kwa sababu muislamu hamrithi kafiri,na inakuwa mali yake yote ni ghawira kwa waislamu,na utawekwa katika Baitil-mali ya waislamu.

عن أسامة بن زيد قال رسول الله صلى الله عليه وسلم" لا يرث الكافر المسلم، ولا المسلم الكافر" متفق عليه

Na toka kwa Usama Bin Zaid amesema : amesema Mtume (S.a.w) "Hamrithi kafiri Muislamu,na wala Muislam hamrithi kafiri" Muttafaqun Alayh

وروى عبد الله بن عمرو قال: قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: " لا يتوارث أهل ملتين"

Na amepokea Abdallah bin Omar amesema : amesema Mtume ( S.a.w) : " Hawarithiani watu wa Mila(Dini ) Mbili "

Kadhalika ikiwa wataritadi warithi wake wote,basi mali inakuwa haina tena utukufu na inakuwa ni ghawira kwa waislamu,na hawarithiani baadhi ya o kwa baadhi.

Na kama kundi la watu litaritadi,na wakajizuia katika mji Fulani,na wakamuweka mtawala wao,na hukmu khasa za kwao wanakuwa ni watu wa kivita (Darul harbi) na panaondoka hifadhi ya damu na mali zao,na inakuwa ni wajibu kuwapiga vita na wanakuwa ni kama makafiri wa asili,bali wao ni wabaya na bora kupambana nao,kwa sababu makafiri wa asili wanakubaliwa kusilimu,au sulhu,au kutoa kodi(jizyah) ama walioritadi hawakubaliwi isipokuwa Uislamu tu,na wala hawkaubaliwi sulhu,na wala Kodi,ima Uislamu au kuuawa.

Kama alivyowapiga Abubakar ( R.a) na Maswahaba (Kuwapiga)waliritadi,na wala hakukubali kwao isipokuwa warudi katika Uislamu kiukamilifu au wauawe,amesema Mtume (S.a.w) : "Yeyote Mwenye kubadilisha dini yake Muueni"Bukhari na Annasai

قال صلى الله عليه وسلم: " من بدل دينه فاقتلوه".

Na kila atakachokichuma Murtadi katika hali ya kuritadi kwake basi hukmu yake ni hukmu ya mali yake ambayo alikuwa akiimiliki kabla ya kuritadi kwake inakuwa ni Ghawira kwa waislamu.na hakika ya matumizi yeyote ya Murtadi wakati wa kuritadi kwake – ikiwemo kuuza,au kutoa zawadi, au kuusia, au mengineyo hasiokuwa hayo – ikiwa ni baada ya kutwaliwa mali yake basi inakuwa ni batili,na ikiwa ni kabla ya kutwaliwa mali yake itasimamishwa (matumizi yake) ikiwa atarudi katika

Uislamu itahesabiwa ni matumizi sahihi na ikiwa hakurudi katika Uislamu itahesabiwa ni matumzi batili.

Na ikiwa atarudi murtadi katika Uislamu basi atarejeshewa mali yake ambayo ilitwaliwa,na ikiwa kurudi kwake katika Uislamu kulikuwa baada ya kufa mrithi wake na kabla ya kugaiwa mali za marehemu atarithi na atachukuwa fungu lake,na ikiwa kurudi kwake katika Uislamu ni baada ya kugaiwa mali za Marehemu,basi hatastahiki chochote na wala hatapewa fungu lolote katika mali hiyo.

**KODI**

**Hizo ni mali ambazo ameziwajibisha Mwenyezi Mungu kwa Waislamu ,kwa kusimamia kuhudumia juu ya haja na sehemu za lazima juu yao ,katika hali ya kutokuwepo mali katika Baitil-mali ya waislamu kwa ajili ya kutoa huduma.**

**Na asili ziwe mali za mapato ya Baiti-mali ni za kudumu,ambazo Mwenyezi Mungu amezifanya ni haki kwa waislamu ,na ni haki ya Baitil-mali,miongoni mwa Ghawira na Jizyah na Kharaji na Ushoor,na mali za mapato ya kuhifadhi (kulinda) ambako dola inahifadhi miongoni mwa milki ya uma,ziwe ni zenye kutosheleza kuhudumia yale wajibu kwa Baitil-mali katika hali ya kuwepo mali na kutokuwepo humo,huduma za yale yanahusiana na kusimamia mambo ya raia,na kutatua mambo yao,pasina kuhitaji Dola kuweka kodi kwa waislamu kwa ajili yake.**

**Na pamoja na hayo hakika sheria imeweka jukumu la kuhudumia juu ya haja/matatizo na sehemu ambazo ni wajibu kwa Baitil-mali kuhudumia wakati wa hali ya kuwepo mali humo au kutokuwepo ni faradhi kwa waislamu kuhudumia.**

**Isipokuwa yale majukumu makubwa yalitupiwa Dola ya Khilafah hivi leo ,huenda yakayafanya mapato kudumu ya Baitil-mali si yenye kutosheleza kukidhi huduma zote za lazima kwa Baitil-mali, kwa ajili ya haja na sehemu zinazostahiki kuhudumiwa,katika hali ya kuwepo mali katika Baitil-mali na katika wakati wa kutokuwepo mali katika Baitil-mali,pindi itakapokuwa mapato haya hayatoshelezi,na hakuna katika baitil-mali cha kuhudumia haja hizi na sehemu**

**zinazistahiki kuhudumiwa toka Baitil-mali,katika hali ya kuwepo mali na kutokuwepo kwake,na wala waislamu hawkujitolea wenyewe kuziba pengo la kuhudumia haja na sehemu hizi,utahama wakati huowajibu wa kuhudumia juu ya haja hizi na sehemu hizi toka baitil-mali na kwenda kwa waislamu,kwa sababu Mwenyezi Mungu amewaradhishia juu yao kutoa huduma juu ya haja na sehemu hizi,kwa sababu kutokusimama kuhudumia haja na sehemu hizi hupelekea kupatikana madhara kwa waislamu,na Mwenyezi Mungu amewajibisha kwa Dola na kwa Uma kuondoa Madhara kwa Waislamu,amesema Mtume (S.a.w) : -**

**قال صلى الله عليه وسلم " لا ضرر ولا ضرار"**

**"Haifai kujidhuru na wala kumletea Mtu madhara"- Ameipokea Imama Ibn majah na Ahmad.**

**Na amejaalia Mwenyezi Mungu Dola ina haki ya kupata mali kwa wailamu ili kukidhi na kuziba pengo la kutoa huduma hizo kutatua haja na mambo ya Waislamu.**

**Pindi ikitokea hali hii Dola inasimamia kuweka kodi kwa waislamu kwa kiwango ambacho kinahitajika kukidhi huduma za lazima kwa haja na sehemu hizi pasina kuzidisha,na Dola inachukua mali /kodi hizi kutoka zile ziada za watu za kukidhi haja za watu za lazima nay a ukamilifu kwa wema.**

**Ama haja na sehemu ambazo ni wajibu kwa Baitil-mali kuhudumia juu yake ,na ambazo zinastahiki kuhudumiwa katika hali ya kukosekana mali humu,na ambazo zitawekwa kodi kwa ajili ya kuzihumia ni hizi zifuatazo :-**

**Huduma za Jihadi na yale ya lazima ,miongoni mwa kutengeneza Jeshi lenye nguvu na kulipatia mafunzo ya kiwango cha juu,na kuliandalia silaha za kisasa,kwa ukubwa na kiwango kwa daraja ambayo itawatisha maadui na kuwaogopesha,na kuweza kuwatenza nguvu maadui zetu,na kukomboa ardhi zetu,na kuangalia nguvu za makafiri katika miji ya Waislamu,na pia kuweza kuibeba Da'wah ya kiislamu kwa Ulimwengu,kule kustahiki kuhudumia Jihadi na yale ya lazima ndio haki za lazima kwa Baitil-mali,sawa kutakuwa**

**katika Baitil-mali kuna mali au hakuna mali,mali ikiwepo humo basi itatumika kuhudumia Jihadi na yalea yanayolazimika katika jihadi,na ikiwa hakuna mali humo,basi utahama uwajibu wa kuhudumia – muda wa kuwa Jihadi ni wajibu na ni lazima-toka Baitil-mali kwenda kwa waislamu,kwa sababu jihadi kwao**

1- **Huduma za Jihadi na yale ya lazima ,miongoni mwa kutengeneza Jeshi lenye nguvu na kulipatia mafunzo ya kiwango cha juu,na kuliandalia silaha za kisasa,kwa ukubwa na kiwango kwa daraja ambayo itawatisha maadui na kuwaogopesha,na kuweza kuwatenza nguvu maadui zetu,na kukomboa ardhi zetu,na kuangalia nguvu za makafiri katika miji ya Waislamu,na pia kuweza kuibeba Da'wah ya kiislamu kwa Ulimwengu,kule kustahiki kuhudumia Jihadi na yale ya lazima ndio haki za lazima kwa Baitil-mali,sawa kutakuwa katika Baitil-mali kuna mali au hakuna mali,mali ikiwepo humo basi itatumika kuhudumia Jihadi na yalea yanayolazimika katika jihadi,na ikiwa hakuna mali humo,basi utahama uwajibu wa kuhudumia – muda wa kuwa Jihadi ni wajibu na ni lazima-toka Baitil-mali kwenda kwa waislamu,kwa sababu jihadi kwao ni wajibu kwa kutoa mali na nafsi,amesema Mwenyezi Mungu :-**

**(انفروا خفافا وثقالا  وجاهدوا بأموالكم وأنفسكم في سبيل الله ذلكم خير لكم إن كنتم تعلمون)**

**[ Nendeni (Vitani) mkiwa wepesi na mkiwa wazito (wazima au wagonjwa) na piganieni dini ya Mwenyezi Mungu kwa mali zenu na nafsi zenu.Haya ni bora kwenu;mkiwa watu mnaojua (jambo) TMQ 9:41]**

**Toka kwa anas ( R ) amesema :amesema Mtume ( S.a.w) :**

وعن أنس قال: قال رسول الله صلى الله عليه وسلم "جاهدوا المشركين بأموالكم، وأيديكم، وألسنتكم"

**"Piganeni Jihadi na Washirikina kwa mali zenu na mikono yenu na ndimi zenu" ameipokea Annasai.**

**Na zipo aya na hadithi nyingi ambazo zinafaradhisha kwa waislamu kupigana Jihadi kwa mali na nafsi.**

**Kwa sababu hiyo katika hali ya kutokuwepo mali katika Baitil-mali kwa ajili ya kuhudumia Jihadi na yale yanayolazimiana na Jihadi ikiwa ni kuwahimiza waislamu kujitolea kwa ajili ya Jihadi.**

أخرج أحمد عن عبد الرحمن بن خباب السلمي قال: "خطب النبي صلى الله عليه وسلم فحث على جيش العسرة، فقال عثمان بن عفان:علي مائة بعير بأحلاسها وأقتابها" وعن حذيفة بن اليمان قال: " بعث النبي صلى الله عليه وسلم " إلى عثمان يستعينه في جيش العسرة، فبعث إليه عثمان بعشرة الآف دينار، فصب بين يديه، فجعل فجعل النبي صلى الله عليه وسلم يقلبها بين يديه ظهرا لبطن، ويدعو له ويقول: غفر الله لك يا عثمان ما أسررت وما أعلنت، وما أخفيت، وما هو كائن إلى أن تقوم الساعة، ما يبالي عثمان ما عمل بعد هذا".

**Ametoa Imam Ahmad toka kwa Abdur rahman Bin Khabbab Assulamiy amesema : alihutubia Mtume ( S.a.w) akahimiza (Jihadi ) katika Jeshi la Usrah ( Zito) akasema Othman Bin Affan Mimi natoa Ghamia Mia moja wakiwa na Matandiko yake na mifuko yake(anakusudia Ghamia na zana zake zote)"**

**Toka kwa Hudhefah Bin Al-yaman amesema : Mtume (S.a.w) alituma Ujumbe kwa Othaman akimtaka msaada katika Jeshi la Usrah,Othman Akamtumia Mtume ( S.a.w) Dinari alfu kumi,akazimwaga mbele yake,basi akawa Mtume (S.a.w) anazibusu mbele yake mbele na nyuma,na anamuombea dua na anasema :"Mwenyezi Mungu akusamehe Ewe Othman yale ulioyafanya kwa siri na ulioyafanya kwa wazi,na yale uliyaficha,na yale yatakayokuja mpaka siku ya kiama,hatojali Othman yale atakayoyatenda baada ya haya.**

**Ikiwa sadaka/kujitolea kwa waislamu hakutatosheleza kuhudumia Jihadi na ikawepo jihadi ,Dola itaweka kodi kwa waisalamu kwa kiwango cha**

lazima kwa kuhudumia jihadi jihadi nay ale yanayoambatana na jihadi ,pasina kuzidisha,na wala si halali kuweka kodi zaidi ya ile haja ya lazima kwa ajili yake.

2- Huduma ya Viwanda na zana za Kivita na yale ya lazima miongoni mwa zana na viwanda,ili kuweza kutengeneza silaha za lazima,kwa sababu jihadi inahitaji Jeshi,na Jeshi mpaka liweze kupigana hapana budi liwe na silaha,na silaha mpaka ziweze kupatikana kwa wingi na kwa kutimia kwa wanajeshi,na kwakiwango cha juu,hapana budi zitengenezwe(kuwepo viwanda)kwa sababu hii vimekuwa viwanda vya kivita vina mahusiano kamili na jihadi,na vimefungamana na jihadi kufungamana kuliko madhubuti,na Dola mpaka iwe inamiliki uwezo wa mambo yake,pasina kuathirika na dola nyingine na kudhibitiwa,hapana dola isimamie kutengeneza silaha zake,khasa zile za kuihai katika silaha na kuziendeleza yenyewe,mpaka imiliki silaha za kisasa na zenye nguzu zaidi,kwa namna yeyote ile zitakapoendelea silaha na kupanuka,na iwe chini ya matumizi yake kila imnachokihitaji katika silaha,kwa ajili ya kuwatisha maadui,sawa wawe ni maadui wa wazi au waliojificha,kwa mujibu wa hali ya kilimwengu ambayo ipo.

Na kutokuwepo viwanda hivi kwa uma,kutawafanya waislamu wategemee kwa dola za makafiri katika mambo ya silaha,hali hii huenda ikafanya matakwa na maamuzi ya waislamu yapo mikononi mwa dola za kikafiri,kwa sababu wao (makafiri) hawauzi silaha ila kwa masharti yatakayo hakika maslahi yao na haya ni madhara makubwa sana kwa uma.

**Kwa sababu hii,hakika kuweka viwanda hivi ni wajibu kwa waislamu,kwa dalili ya aya na hadithi ambazo zinawajisha waislamu kupigana jihadi kwa mali na nafsi,kwa dalili ya kulazimiana,kwa sababu jihadi imesimamia juu ya silaha,na silaha zinahitaji kutengenezwa,na pia kwa dalili ya kauli yake Mwenyezi Mungu :-**

**( وأعدوا لهم ما استطعتم من قوة، ومن رباط الخيل ترهبون به عدو الله وعدوكم وآخرين من دونهم لا تعلمونهم الله يعلمهم)**

**[Basi waandalieni (wawekeeni tayari)nguvu mziwezao (silaha) na mafarasi yaliofungwa (kufunga) tayari tayari (Mipakani) .ili kwazo ( nguvu hizi) muogopeshe maadui wa Mwenyezi Mungu na maadui zenu, (mnaowajua) na pia (maadui zenu ) wengine wasiokuwa wao ,msiowajua nyinyi (lakini ) Mwenyezi Mungu anawajua…..TMQ : AL-anfal 60]**

**Maandalizi ambayo ameyawajibisha Mwenyezi Mungu kwa waislamu ni maandalizi ambayo patahakikikika kupatikana kuwatisha maadui,wa wazi na walijificha,na wanaotarajiwa,na maandalizi haya ya kutisha husimamia juu ya kupatikana silaha zilizokuwa hai na zilizoendelea (mpya) katika mfumo wa juu kabisa,na silaha hizi hutegema kuzipata kwake kwa kujenga viwanda.kwa sababu hii hakika ayah ii inajulisha juu ya wajibu wa kujenga viwanda vya silaha kwa umma,na kuondoa madhara kwa umma ni jambo la wajibu,na wala hakuwezi kupatikana kuondoa madhara haya isipokuwa kwa kujenga viwanda vya silaha za kivita,nay ale yanayolazimiana nayo miongoni mwa viwanda na silaha.**

**Na viwanda hivi inajuzu kwa watoto wa uma kuvijenga,na kujenga baadhi yake vya silaha za lazima,ikiwa hawakuvijenga au ikiwa waajenga baadhi yake,inakuwa wajibu kwa dola kujenga viwanda hivi,kwa kiwango cha lazima cha kuzalisha**

silaha zote za lazima na za maandalizi,na inakuwa kujenga viwanda hivini katika haki za lazima,sawa itakuwa mali ipo katika baitil-mali au haipo,ikiwa mali ipo basi itatumika katika kujenga viwanda hivi,na ikiwa katika baitil-mali hakuna mali ya kujenga viwanda hivi,kutahama uwajibu wa gharama za kujenga viwanda kwa umma,na Dola itaweka kodi za lazima kwa ajili hii kwa kiwango kinachotosha,kwa vyovyote itakavyofikia.

3- Huduma za Mafakiri na masikini na wasafiri,kuwahudumia hawa kunastahiki katika hali ya kuwepo mali katika Baitil-mali na katika hali ya kutokuwepo mali,ikiwa mali ipo katika Baitil-mali watahudumiwa,na ikiwa mali haipo katika Baitil-mali utawahamia uwajibu huu kwa waislamu,kwa sababu kuwahudumia Mafakiri na masikini na wasafiri ni faradhi ambayo Mwenyezi Mungu ameifaradhika kwa waislamu katika Zaka,na sadaka na vinginevyo,

قال رسول الله صلى الله عليه وسلم فيما يرويه عن ربه: " ما آمن بي من بات شبعان، وجاره جائع إلى جنبه وهو يعلم به"

amesema Mtume ( S.a.w) katika yale anayoyapokea toka kwa mola wake "Hajaniamini mimi (Kikweli) Yule ambaye atalala hali ya kuwa ameshiba na jirani yake pembezoni mwake ananjaa na hali ya kuwa analijua hilo" ameipoea Al-bazzar toka njia ya Anas.

Kwa ajili hiyo,ikiwa katika baitil-mali kuna mali ya kuhudumia mafakiri na masikini na wasafiri,watahudumiwa,na ikiwa hakuna utahama wajibu wa kuwahudumia kwa waislamu,na Dola itaweka kodi kwa waislamu kwa ajili ya hilo,kwa kiwango kinachotosha kwa kuwahudumia.

4- Mishahara ya askari,na wafanyakazi,na makadhi,na walimu na wengineo miongoni mwa wale wanaotoa huduma wanazifanya katika maslahi ya

waislamu,kwa sababu wao kwa kukabala wa huduma zao wanastahiki mshahara toka Baitil-mali,na kustahiki kupewa ni katika haki za lazima,sawa katika Baitil-mali kuna mali au hakuna mali,ikiwa katika Baitil-mali kuna mali basi watalipwa,na ikiwa hakuna mali basi utahama wajibu huo kwa waislamu,kwa sababu Mwenyezi Mungu amejaalia uongozi ni wa uma,na ukauwajibishia umtawaze Khalifah,utakaompa Ba'ia ya kusikia na kutii kwa kufanyia kazi kitabu cha MwenyeziMungu na sunnah za Mtume wake,ili aismame kiongozi kwa niaba ya ummah na ayachunge/asimamie mambo yao kwa mujibu wa kitabu na sunnah,na kusimamia mambo ya umah hakutimii isipokuwa kwa kwa kuweka muundo/ofisi za Dola,wakiwemo watawala,makadhi,askari,walimu,wafanya kazi ,na wengineo,na kuwaweka hawa kuemsimamia juu ya badala/mishahara na malipo wanayopewa.

Na muda wa kuwa Mwenyezi Mungu amewajibisha kwa waislamu kuwaweka hawa,basi kwa hakika inakuwa amewajibisha kwa waislamu kuwapa badala zao,na malipo yao,kwa njia ya kulazimiana,kwa hakika Mtume (S.a.w) aliweka maliwali(wakuu wa wilaya) na ma-ummali (watawala wa Maeneo)na waandishi na akawapangia (Mishahara ya ) Kuwapa,kama vile ambavyo makhalifa baada yake waliweka maliwali(wakuu wa wilaya) na ma-ummali (watawala wa Maeneo)na makadhi,na waandishi,na askari,na wakawapangia mishahara toka katika Baitil-mali.

Kwa sababu hii,ikiwa katika Baitil-mali kuna mali basi watapewa,na ikiwa katika Baitil-mali hakuna

**mali ,Dola itawapangia waislamu kodi kwa ajili ya huduma hizi kwa kiwango kinachohitajika.**

**5- Huduma zinastahiki juu ya maslahi ,na kuonea huruma uma,na ambazo hutolewa kuhudumia mambo yanahusiana na maisha yao,ambayo yanahesabika kuwepo kwakoni dharura miongoni mwa dharura,na uma utapata madhara kwa kutokuyasimamia hayo, mfano njia za uma,mashule ,vyuo vikuu,mahospitali,misikiti,huduma za maji ,na yenye kufanana na haya,kustahiki kuhudumia mambo haya kunahesabika ni katika haki za lazima,sawa kumepatikana mali katika Baitil-mali au hakukupatikana,ikiwa mali itapatikana katika Baitil-mali basi itatumika kuhudumia mambo haya,na ikiwa haikupatikana mali katika Baitil-mali ,utahamia uwajibu wa kuhudumia mambo haya kwa uma,kwa sababu kuyahudumia ni wajibu kwa Waislamu,kwa sababu kutokuyafanya haya kunapelekea madhara kwa uma,na madhara ni wajibu kuyaondoa kwa dola na uma,kwa kauli ya Mtume (S.a.w)**

**لقول الرسول صلى الله عليه وسلم: "لا ضرر ولا ضرار". وقوله: "ما ضارّ أضرّ الله به، ومن شاقّ شاقّ الله عليه".**

**"Haifai kujidhuru na wala kumletea Mtu madhara"- Ameipokea Imama Ibn majah na Ahmad.**

**Na kauli yake (S.a.w) "Na Mwenye kufanya uzito naye Mwenyezi Mungu atamfnyia Uzito juu yake." -Ameipokea Imama Abu Daud na Ahmad na Ibn majah .**

**Na wala haifai kwa dola kuweka kodi kwa uma kwa ajili ya kutoa huduma mbali mbali ambazo ni za wajibu kwa Baitil-mali katika hali ya kuwepo mali humo,si wakati inapokuwa hakuna,navyo ni kama vile huduma ambazo hutolewa kuhudumia mambo ambayo yanafanywa na dola na kuwapatia watu katika njia ya maslahi na**

kutengeneza,na wala hakuna madhara kwa waislamu kwa kutokufanya hivyo na kutokufanya hivyo,kwa mfano kufungua njia ya pili,au kuimarisha pamoja na kuwepo nyingine inayotosheleza,na inakidhi mahitaji yake,na mfano wa kujenga Shule,au Chuo kikuu au Hospitali,inapatikana nyingine inayokidhi mahitaji yake,na inatosheleza,au mfano wa kupanua bara bara ambazo hakuna dharura ya kuzipanua,na mfano wa kujenga miradi ya uzalishaji ambayo haipelekei kutokuijenga kuleta madhara yoyote kwa uma, kama vile kujenga kiwanda cha kutoa Chuma(Nickel) au wanja/kohl au kuanzisha hodhi la kujengea meli za kibiashara,na mfano wake,hakika mambo haya yote yatafanywa na dola wakati itakapokuwa katika baitil-mali kuna mali ya ziada ya kuhudumia sehemu ambazo zitafikwa na madhara kama hazikudumiwa,na ikiwa hakuna mali katika Biatil-mali basi dola haitayafanya haya,na wala haifai kuwekwa kodi kwa ajili ya haya,kwa sababu wislamu hawatafikwa na madhara kwa kutokufanyika haya,kwa sababu kuyafanya haya si wajibu juu yao.

Na juu ya haya ikiwa patapatikana mali katika Baitil-mali,itatumika sehemu yake katika kufanya mambo ya dharura,na pindi ikiwa hakuna mali katika Baitil-mali basi dola itawekakodi kwa waislmu kwa kiwango cha lazima (kutosheleza) kuhudumia na kujenga mambo haya na kuyafanya yapatikane.

6- Huduma za matukio ya Ghafla miongoni mwa Baa la Njaa ,Na matetetmeko na Tufani,au Mashambulizi ya adui,kustahiki kuhudumia mambo haya hayakuzingatiwa/hayakuhesabiwa kuwepo,bali ni katika mambo ya lazima katika hali ya kuwepo mali katika Baitil-mali au kutokuwepo,mali ikiwa ipo katika Baitil-mali,ni wajibu kuitumia wakati huo huo kwa haya mambo ya ghafla ,na ikiwa hakuna mali ,inakuwa ni wajibu/faradhi kwa waislamu na ni

**wajibu ikusanywe toka kwao muda huo huo pasina kuchelewa,ikiwa pataogopewa madhara kwa kuchelewa,Dola itakopa kiasi cha kutosha kuhudumia yale yanayotokea ghafla,kisha itaziba kile ilichokopa kutokana na ile iliokusanywa toka kwa Waislamu,na dalili ya uwajibu wake kwa waislamu ni hadithi :-**

**"ما آمن بي من بات شبعان وجاره جائع إلى جنبه وهو يعلم به"**

**amesema Mtume ( S.a.w) katika yale anayoyapokea toka kwa mola wake "Hajaniamini mimi (Kikweli) Yule ambaye atalala hali ya kuwa ameshiba na jirani yake pembezoni mwake ananjaa na hali ya kuwa analijua hilo" ameipoea Al-bazzar toka njia ya Anas.**

**Na hadithi :-**

**"أيّما أهل عَرْصَةٍ أصبح فيهم امرؤ جائعاً فقد برئت منهم ذمة الله"**

**"watu wa nyumba yoyote ameamka kwao mtu mmoja akiwa na njaa,kwa hakika dhamana ya Mwenyezi Mungu ik mbali nao" ameipokea Imam Ahmad.**

**Hii ni kwa upande wa Baa la njaa.Ama matetemeko ya ardhi na Tufani,kwa hakika dalili za uwajibu wa kuwasidia wenye matatizo ,na uwajibu wa kuondoa madhara kwa waislamu ndio dalili za wajibu wa waislamu kuwahudumia.**

**Hizi ndio sehemu ambazo ni wajibu kwa waislamu kuzihudumia katika hali ya kutokuwepo mali katika Baitil-mali ya waislamu,na ambazo ni wajibu kwa dola isimamie kuweka kodi kwa waislamu kwa ajili ya kuhudumia haya katika hali ya kutokutosheleza mapato ya Baitil-mali na mapato ya kuhifadhi/kulinda toka milki ya uma kwa ajili ya kuhudumia haya,na zitachukuliwa kodi toka kwa waislamu kutoka na yale ya ziada ya kukidhi haja zao za msingi nay ale ya ukamilifu kwa wema.kwa mujibu wa maisha yao ambayo wanaishi,basi Muislamu yeyote atakaekuwa na ziada ya haja zake za lazima na za ukamilifu**

**itachukuliwa toka kwake kodi,na Yule ataekuwa hana ziada ya haja za lazima hatachukuliwa kwake chochote,na hayo ni kutokana na kauli ya Mtume (S.a.w) :-**
**"خير الصدقة ما كان عن ظهر غنى"**
**“Bora ya sadaka ni ile itakayokuwa katika hali ya kutosheka” ameipoke Bukhar toka kwa Abuhureirah .**
**Na “Kutosheka” ni yale anayotosheka nayo mwanaadamu,katika yale ambayo ni kiwango cha kumtosha kukidhi haja zake,Imepokelewa toka kwa Jabir kwamba Mtume (S.a.w) amesema :-**
**وروي عن جابر أن رسول الله صلى الله عليه وسلم قال: "ابدأ بنفسك فتصدّق عليها فإن فَضُلَ شيءٌ فلأهلك، فإن فَضُلَ عن أهلك شيءٌ فلذي قرابتك، فإن فَضُلَ عن ذي قرابتك شيءٌ فهكذا وهكذا ـيقول فبين يديك وعن يمينك وعن شمالك"**
**“Anza kwa nafsi yako ipe sadaka,ikiwa kitazidi kitu basi (Mpe sadaka)Mkeo wako(familia yako) ikiwa kitazidi kitu kwa familia yako,wape jamaa zako wa karibu,ikiwa kitazidi kitu kwa jamaa wa karibu basi ni kama hivi na hivi,-anasema basi mbele yako,na kulia kwako,na kushotoni kwako”**
**Akachelewesha wale ambao ni wajibu kuwahudumia juu ya nafsi yake,na mfano huo kwa kodi,kwa sababu ni mfano wa huduma,na mfano wa sadaka na Mwenyezi Mungu anasema :-**
**{ويسألونك ماذا ينفقون قل العفو}**
[na wanakuuliza watoe nini ? sema : “vilivyokuzidieni” TMQ :2:219] yaani yale ambayo hakuna uzito/tabu katika kuhudumia kwake,nacho ni kile kilichozidti juu ya haja za lazima.na kodi itachukuliwa kwa mali yote iliozidi juu haja za lazima si kwa kile kilichoingia(Mapato)
Na itapangwa kodi kwa kiasi cha haja na kutosheleza kukidhi kile kilichoshindikana/kilichokosekana katika huduma za lazima juu ya sehemu zilizotangulia kutajwa,na wala haizingatiwi katika kuweka kodi kuzui kuzidi kwa Uchumi/mali nyingi,au kuzuia utajiri ,au

kuzuia kuzidi mapato ya Baitil-mali.na haichungwi/haizingatiwi katika kuweka kodi isipokuwa kutosheleza kwake kukidhi huduma za lazima za sehemu hizi,na wala haitachukuliwa zaidi ya hivyo kwa sababu kuchukuwa zaidi inakuwa nidhulma,kwa kuwa si wajibu kwa waislamu kutoa,na dhulma ni kiza siku ya kiyama.

Na wala haifai kwa dola kuweka kodi ambazo si za moja kwa moja(kwa jambo husika),kama vile haifai kuweka kodi katika muundo wa kodi za Mahakama,au juu ya maombi yanayopelekwa serikalini,au juu ya mualama wa kuuza ardhi na kuzisajili,au juu ya vilivyosakafiwa,au juu ya vipimo,au yasiokuwa hayo katika aina za kodi zisizokuwa zilizopita,kwa sababu kuweka kodi hizo ni dhulma iliokatazwa,na ni katika kodi ambayo ameikataza Mtume (S.a.w):-

**"لا يدخل الجنة صاحب مكس"**

**"Haingii Peponi Mtoza kodi"ameipokea ahmad,darimiy na abuu ubaidah.**

MALI ZA SADAKA

ZAKKAH

Sadaka ambazo ndio mapato ya Baitil-mali ndio Zakkah,kama vile hutumika neno Zakkah juu ya sadaka.

Na Zakkah kilugha (Ya kiarabu ) ina maana ya Kukua,na pia huja kwa maana ya Kusafisha,na inakuja katika sheria kwa maana mbili,kwa sababu kuitoa kwake ni sababu ya kupata Baraka mali kama ilivyo katika hadithi :-

**"ما نقص مال عبد من صدقة"**

"Haipungui mali ya mja kwa kutoa sadaka" ameitoa Thirmidhiy,au kwa sababu malipo yanakithiri kwa sababu yake,kwa sababu ni takaso la nafsi kutokana na uchafu wa Ubakhili na takaso la madhambi.

Na maana yake kisheria : "Zakkah ni haki iliokadiriwa ni wajibu katika mali maalum". Nayo ni Ibada miongoni mwa Ibada,na inahesabika ni nguzo katika nguzo za Uislamu,kama Swala,na Swaumu, na Hija.

Na zakkah ni wajibu kwa Waislamu peke yao,na wala haichukuliwi toka kwa wengineo,nayo ni wajibu kwa dalili za kitabu na sunnah.
Ama kitabu ni kauli yak Mwenyezi Mungu Mtukufu :-
**{وآتوا الزكاة}.**
[ Na toeni zaka… TMQ 2:43]
Ama Suna,hakika Mtume (S.a.w) wakati alipomtuma Mua'dh kwenda Yemen alimwambia : -
**"أعلمهم أن الله افترض عليهم صدقة في أموالهم تُؤخذ من أغنيائهم، فترد في فقرائهم"**
"Wafundishe kuwa Mwenyezi Mungu amefaradhisha juu yao (Kutoa) sadaka katika mali zao itakayochukuliwa toka kwa matajiri zao,na kujereshwa kwa masikini wao"ameipokea Ibn Majah na Abu dauda.
**"ما من صاحب ذهب، ولا فضة لا يؤدي منها حقّها إلا إذا كان يوم القيامة صُفِّحتْ له صفائح من نار، فأُحميَ عليها في نار جهنم، فيكوى بها جنبه وجبينه وظهره، كلما بردت أعيدت له في يوم كان مقداره خمسين ألف سنة، حتى يُقضَى بين العباد، فيرى سبيله، إمّا إلى الجنة، وإما إلى النار، قيل: يا رسول الله، فالإبل؟ قال: ولا صاحب إبل لا يُؤدّي منها حقّها، ومن حقّها حلبها يوم وردها، إلا إذا كان يوم القيامة بُطِحَ لها بقاعٍ قرقر أوفر ما كانت لا يفقد منها فصيلاً واحداً، تطؤه بأخفافها، وتعَضّه بأفواهها، كلما مرّ عليه أولاها رُدّ عليه أخراها في يوم كان مقداره خمسين ألف سنة، حتى يُقضى بين العباد، فيرى سبيله، إمّا إلى الجنة وإمّا إلى النار، قيل: يا رسول الله، فالبقر والغنم؟: ولا صاحب بقرٍ، ولا غنمٍ لا يؤدّي منها حقّا، إلا إذا كان يوم القيامة، بُطِحَ لها بقاعٍ قرقرٍ، لا يفقد منها شيئاً، ليس فيها عقصاء، ولا جلحاء، ولا عضباء، تنطحه بقرونها، وتطؤه بأظلافها، كلما مرّ عليه أولاها رُدّ عليه أخراها في يوم كان مقداره خمسين ألف سنة، حتى يُقضى بين العباد، فيرى سبيله، إمّا إلى الجنة وإمّا إلى النار" رواه الخمسة إلا الترمذي.**
Na imepokelewa msisitizo na uzito wa anaezuia zaka,Toka kwa Abu hurairah,toka kwa Mtume (S.a.w) amesema : "Hakuna Mtu yeyote Mwenye Dhahabu,wala Fedha hatoe zaka haki yake isipokuwa ikifika siku ya kiama itatengenezwa(Dhahabu na Fedha na kuwa ) sahani za moto,zitaokwa katika moto wa Jahannamu,atapigwa pasi kwazo mbavuni mwake na usoni mwake na mgongoni mwake,kila mara zinapopoa hurejeshwa tena katika siku ambayo kiwango chake ni miaka khamsini,mpaka pahukumiwe baina ya waja,basi ataona njia yake,ima kwenda peponi au kwenda motoni,pakasemwa,Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu,Vipi kuhusu (Mwenye) Ngamia? Akasema : na wala Mwenye Ngamia hatoe haki yake katika hao ngamia,na miongoni mwa haki zake ni kuwakama siku ya

kunywa kwake,isipokuwa ikiwa siku ya kiama atatupwa katika eneo la tambarare.hakusekani humo ngamia mmoja,anaemkanyaga kwa kwato zake,na anamng'ata kwa mdomo wake,kila wakipita wa mwanzo hurejeshwa juu yake wa mwisho katika siku ambayo kiwango chake ni miaka alfu khamsini,mpaka pahukumiwe baina ya viumbe,basi ataiona njia yake ima peponi au motoni,pakasema : Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu,Vipi (Mwenye) Ng'ombe na Mbuzi akasema : wala mwenye Ng'ombe na wala mwenye Mbuzi hatoe humo haki yake,isipokuwa ikiwa siku ya kiama, atatupwa katika eneo la tambarare.hakitakosekana humu kitu chochote,hamna humo Ng'ombe/Mbuzi (aliepinda mapembe kulelekea masikioni mwake) na Mbuzi asiyekuwa na mapembe,na Ng'ombe/Mbuzi aliyepasuliwa sikio lake,wanampiga kwa mapembe yake,na wanamkanyaga kwa kwazo zao, ,kila wakipita wa mwanzo hurejeshwa juu yake wa mwisho katika siku ambayo kiwango chake ni miaka alfu khamsini,mpaka pahukumiwe baina ya viumbe,basi ataiona njia yake ima peponi au motoni,Imepokewa na Watano isipokuwa Tirmidhi.

Nayo ni faradhi aini kwa kila muislamu,anaemiliki kiwango cha zaidi ya madeni yake,na kupitiwa na mwaka,na wakati wowote itakapowajibika kwa Muislamu basi haitaanguka kwake,na wala hakuzingaziwi kukusanya zaka kwendani na haja za dola na kwa mujibu wa maslahi ya uma,kama mali za kodi ambazo hukusanywa kwa uma,bali hiyo ni haki kwa makundi manane,na ni wajibu ipelekwe kwenye baitil-mali wakati wowote inapowajibu,sawa kuwa kuna haja ua hakuna haja,na zaka sio haki katika haki za Baitil-mali ,na wala sio stahiki yake ,na bila shaka ni hiyo ni haki inayostahiki kwa makundia manane,ambao Mwenyezi Mungu amewabainisha katika aya ya sadaka:-

إِنَّمَا الصَّدَقَاتُ لِلْفُقَرَاء وَالْمَسَاكِينِ وَالْعَامِلِينَ عَلَيْهَا وَالْمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمْ وَفِي الرِّقَابِ
وَالْغَارِمِينَ وَفِي سَبِيلِ اللّهِ وَابْنِ السَّبِيلِ فَرِيضَةً مِّنَ اللّهِ وَاللّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ

*"Wa kupewa sadaka ni mafakiri, na masikini, na wanaozitumikia, na wa kutiwa nguvu nyoyo zao, na katika kukomboa watumwa, na wenye*

*madeni, na katika Njia ya Allah, na wasafiri. Huu ni wajibu uliofaridhiwa na Allah. Na Allah ni Mwenye kujua Mwenye hikima"*. [At-Tawbah: 60]

Na Baitil-mali si chochote ila sehemu ya kuihifadhia tu,ili itumike kwa wale waliobainishwa na aya kwa mujibu wa rai ya Imam na jitihada yake kwa upande wao.

Na ni wajibu kutoa zaka kwa Mwanamme,na Mwanamke,na Mtoto,naMwanawazimu kwa dalili ya hadithi zilizoenea katika uwajibu wa moja kwa moja wa kutoa.

**عن عمرو بن شعيب عن أبيه عن جده قال: "خطب رسول الله صلى الله عليه وسلم الناس، فقال: ألا من وُلِّيَ يتيماً له مال فليتجر له فيه، ولا يتركه فتأكله الصدقة"**

Toka kwa Amri bin Shuayb toka kwa Babayake,toka kwa Babu yake amesema:"Aliwahutuba watu Mtume wa Mwenyezi Mungu

(S.a.w),akasema : Fahamuni kuwa yeyote mwenye kupewa jukumu la kumsimamia yatima mwenye mali basi aifanyie Biashara humu,na wala asiache ikaliwa na sadaka (Zaka)"

**وعن أنس، مرفوعاً: "اتّجروا في أموال اليتامى، لا تأكلها الزكاة"**

Na toak kwa Anas,Marfuuan: "Zifanyieni biashara mali za mayatima,(ili)zisiliwe na zaka",

**وعن القاسم بن محمد قال: "كانت عائشة تبضع أموالنا، ونحن يتامى، وتزكيها"**

Na amepokea Abu Ubaidah na Twabarani na Maliki toka kwa Al-qasim bin Muhammad amesema : alikuwa Aisha ( R) akihifadhi mali zetu,na hali ya kuwa sisi ni mayatima,na akitoa zaka"

**وعن مالك بن أنس أنّه كان يرى أن في مال المعتوه زكاة، وكذلك الزهري.**

Na toka kwa Maliki bin Anas kwamba yeye alikuwa akiona katika mali ya Punguani( Mwandawazimu)inapaswa kutolewa zaka,na pia Azzuhri.

Na toka Ibn Shihab "Kwamba yeye aliulizwa juu ya mali ya Mwendawazimu,je inapaswa kutoa zaka ? akasema: Ndio."ameipokea Ab Ubaida.

Na ni wajibu kutoa zaka katika mali zifuatazo :

1- Mifugo miongoni mwa ngamia,na ng'ombe , na Mbuzi.

2- Nafaka na Matunda.

3- Hela.

4- Vifaa vya Biashara.

Na ni wajibu kutoa zaka katika mali hizi pindi zikifika kiwango,zaidi ya deni,na ikapitiwa juu yake na mwaka,isipokuwa nafaka na matunda kwa sababu zaka yake inakuwa wajibu mara baada ya kuvunwa.

ZAKA YA MIFUNGO

NGAMIA

Kiwango cha mwanzo cha kuzoa zaka ya ngamia ni kuanzia ngamia watano, kwa hadithi Abi said Al-khudriy toka kwa Mtume (S.a.w) "Hakuna (Zaka)Chini kundi la ngamia watano" na Neno "Adhaudu"Ni ngamia kati ya watatu mpaka tisa,basi yeyote mwenye kumiliki chini ya ngamia watano hana zaka inayopaswa kutoa.na mwenye kumiliki ngamia watano wa kufugwa ,wanachungwa sehemu kubwa ya mwaka,basi ni wajibu juu yake atoe zaka ya ngamia mmoja.

Na yanakuwa mafungu ya ngamia na kile cha wajibu kutoa ni kama ifuatavyo :-

1- Ngamia watano zaka yake Mbuzi mmoja.

2- Ngamia kumi zaka yake Mbuzi wawili.

3- Ngamia kumi na tano zaka yake Mbuzi watatu.

4- Ngamia Ishirini zaka yake mbuzi wanne.

Na ziada iliopa kati kati ya hesabu mbili haina zaka ndani yake,pindi ngamia wakizidi ishirini hamna zaka katika hiyo ziada mpaka wakifie ngamia Ishirini na tano,wakifikia Ishirini na tano wataanguka mbuzi,na itakuwa zaka inatokana na ngamia wenyewe,

Toka kwa Allaythi bin sa'ad amesema:

**عن الليث بن سعد قال: "هذا كتاب الصدقة: في أربع وعشرين من الإبل، فما دونها الغنم، في كل خمس شاة".**

"Hiki ni kitabu sadaka:Katika ngamia Ishirini na nne na chini yake zaka yake ni mbuzi,katika kila watano ni mbuzi mmoja"

**وقال الليث: حدثني نافع أن هذه نسخة كتاب عمر بن الخطاب. وعن مالك بن أنس قال: قرأت كتاب عمر بن الخطاب في الصدقة، فإذا فيه: "بسم الله الرحمن الرحيم. هذا كتاب الصدقة. في أربع وعشرين من الإبل، في كل خمس، شاة"**

Na akasema Allythiy :kanielezea Naafi kwamba hii kopi ya kitabu alichiandika Omar bin Khatwab.

Na toka kwa Anas Bin Maliki amesema :Nimesoma Kitabu/barua cha Omar bin Khatwab kinachoelezea sadaka,mara nukakunda ndani yake:Kwa jina Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema,Mwenye Kurehemu.hiki ni kitabu cha sadaka,kitaika ngamia sihirini na nne,katika kila watano ni mbuzi mmoja"

Na pindi wakifikia ngami Ishirini na tano basi yatakuwa mafungu ya viwango,na yale wajibu humu katikaifuatavyo:-

1- Ngamia Ishirini na tano zaka yake ni "Bint Makhadhi" katika ngamia jike,na huyu ni ngamia alifikia mwaka mmoja na ameingia mwaka wa pili,na neon " Makhadhu" ni Mjamzito,yaani Ngamia jike alieingia mida ya kushika mimba.na ikiawa hakuna "Bint Makhadhi" kwa mwenye ngamia,itachukuliwa kwake "Ibnu Labuun Dume "nae ni mwenye miaka miwili na ameingia mwaka wa tatu,

2- Ngamia Thelathini na sita zaka yake ni "Bintu Labun" Jike,na ye mwenye miaka miwili ,na ameunza mwaka wa tatu,ameitwa hivyo kwa sababu mama yake imekurubia sasa kuzaa na kuwa mwenye maziwa.

3- Ngamia Arubaini na sita zaka yake ni "Hiqqah Jike"mwenye kufaa kupandwa na Fahali/Dume,nae ni ngamia mwenye miaka mitatu,na ameingia mwaka wan ne,na maana ya "kufaa kupandwa na Fahali"amestahiki kuingiliwa na Dume.

4- Ngamia sitini na moja zaka yake ni “Jadh’aa”naye ni Yule ambaye amefikia miaka mine,na ameitwa hivyo kwa sababu ameangusha meno yake ya mbele(Mkubwa)

5- Ngamia Sabini na Sita zaka yake ni “Bint Labuuni wawili”

6- Ngamia Tisini na moja zaka yake ni “Hiqqah”wawili wanaofaa kupandwa na dume.

Na ziada iliopo kati kati ya kila hesabu mbili haina zaka ndani yake,na pindi wakizidi ngamia Tisini na moja hamna humo zaka katika hii ziada mpaka wafikie Mia moja na Ishirini na moja,pindi wakifikia hapo hesabu itatofautiana,na watahesabika wote,na watahesabiwa katika kila ngamia Arubaini katika hao “Bint Labun” na katika kila Khamsini “Hiqqah” na vinakuwa viwango,na yale ya wajibu katika hao kama ifuatavyo :-

| | KIWANGO CHA NGAMIA | CHA WAJIBU KUTOA |
|---|---|---|
| 1 | Mia moja na Ishirini | Bint Labuuni watatu |
| 2 | Mia moja na Thelathini | Hiqqah Mmoja na Bint Labuun wawili. |
| 3 | Mia moja na Arubaini | Hiqqah wawili,na Bint Labun Mmoja. |
| 4 | Mia moja na Khamsini | Hiqqah watatu |
| 5 | Mia moja na sitini | Bint Labuuni Wanne. |
| 6 | Mia moja na sabini | Hiqqah Mmoja na Bint labuun Watatu. |
| 7 | Mia moja na Themanini | Hiqqah wawili na Bint Labuun wawili. |
| 8 | Mia moja na tisini | Hiqqah watatu na Bint labuun Mmoja. |
| 9 | Mia mbili | Hiqqah wanne au Bint Labuun watano. |

Na ziada iliopo kati kati ya hesabu mbili hamna zake humo,na dalili ya yote hayo ,

**عن أنس أن أبا بكر كتب له هذا الكتاب، لمّا وجّهه إلى البحرين: "بسم الله الرحمن الرحيم، هذه فريضة الصدقة، التي فرض رسول الله صلى الله عليه وسلم على المسلمين، والتي أمر الله بها رسوله، فمن سُئلها من المسلمين على وجهها فليعطها، ومن سئل فوقها فلا يعط. في أربع وعشرين من الإبل، فما دونها، فمن الغنم، من كل خمس شاة، فإذا بلغت خمساً وعشرين، إلى خمس وثلاثين ففيها بنت مخاض أنثى، فإذا بلغت ستاً وثلاثين، إلى خمس وأربعين ففيها بنت لبون أنثى، فإذا بلغت ستاً وأربعين إلى ستين، ففيها حقّة طروقة الجمل، فإذا بلغت واحدة وستين، إلى خمس وسبعين ففيها جَذَعَة، فإذا بلغت ستاً وسبعين إلى تسعين ففيها بنتا لبون، فإذا بلغت إحدى وتسعين إلى عشرين ومائة ففيها حقتان طروقتا الجمل، فإذا زادت على عشرين ومائة، ففي كل أربعين بنت لبون، وفي كل خمسين حقة، ومن لم يكن معه إلا أربع من الإبل فليس فيها صدقة إلا أن يشاءَ ربُّها، فإذا بلغت خمساً من الإبل ففيها شاة".**

ni yale yaliopokelewa na Anas kwamba Abubakar alimuandikia barua hii,wakati alipomtuma Bahrain : Kwa Jina la Mwenyezi Mungu Mwingi wa Reheme Mwenye kurehemu,Hii ni faradhi ya sadaka/zaka,ambayo ameigiza Mtume wa Mwenyezi Mungu kwa waislamu,na ambayo amemuamrisha Mwenyezi Mungu kwayo Mtume wake,basi Muislamu yeyote anaetakiwa kwa utaraitibu wake basi aitoe,na atakaetakiwa zaidi ya hayo basi asitoe,katika ngamia Ishirini na nne na chini yake itatolewa mbuzi,kwa kila ngamia watano mbuzi mmoja,wakififikia ngamia Ishirini na tano mpaka ngamia Thelathini na tano humu inapaswa kutolewa Bint Makhadh Jike,wakififikia ngamia Thelathini na Sita mpaka arubaini na tano,basi humo inapaswa Bint labuun jike,wakifia arubaini na sita mpaka sitini,basi humo inapaswa kutoa Hiqqah anayestahiki kupandwa na fahali,na wakififikia sitini na moja mpaka sabini na tano humo inapaswa kutoa Jadha'a,na wakififikia sabini na sita mpaka tisini humo inapasa bint labuni wawili,wakififikia tisini na moja mpaka mia moja na ishirini basi ,humo inapaswa kutoa hiqqah wawili wenye kustahiki kupandwa na fahali,wakizidi mia moja na ishirini,basi kwenye kila arubaini ni bint labuuni,na kwa kila khamsini Hiqqah ,na Yule ambaye hana isipokuwa ngamia wanne basi hamna humo zaka isipokuwa atakapotaja mwenyewe,na wakififikia ngamia watano basi humo inapaswa mbuzi mmoja"Ameipokea Bukhari,Abu daud na Thirmidhi.

Ikiwa hautapatikana umri ambao ni wajibu kutoa katika ngamia,na ukachukuliwa umri wa chini yake itampasa mwenye ngamia atoe mbuzi wawili zaidi au Dirham ishirini,na itachukuliwa umri zaidi ya huo atapewa mwenye ngamia mbuzi wawili au Dirham Ishirini,na dirham Ishirini ni sawa na Gram 59.9 za fedha. Na mfano wa hayo:lau kama watakuwa ngamia ni arubaini na sita basi ni wajibu kutoa Hiqqah,ikiwa hakuna Hiqqah kwa mwenye ngamia,lakini anaye Bint labuuni,ni wajibu juu yake atoe zaidi ya bint labuuni mbuzi wawili au dirham ishirini,na ikiwa hana Bint labuuni lakini anaye jadha'a,basi atatoa jadh'aa na atapewa mbuzi wawili au Dirham Ishirini.

**لما روى أنس: "أن أبا بكر كتب له فريضة الصدقة، التي أمر الله رسوله صلى الله عليه وسلم، من بلغت عنده من الإبل صدقة الجذعة، وليست عنده الجذعة وعنده حقة، فإنها تُقْبَل منه الحقة، ويَجْعَل معها شاتين إن استيسرتا له، أو عشرين درهماً، ومن بلغت عنده صدقة الحقة، وليست عنده الحقة، وعنده الجذعة فإنها تُقبل منه الجذعة، ويعطيه المصدّق –جابي الصدقة- عشرين درهماً أو شاتين".**

Kwa yale yaliopokelewa na Anas: "kwamba Abubakar alimuandikia Utaratibu wa faradhi ya sadaka,ambayo Mwenyezi Mungu alimuamuru Mtume wake (S.a.w) Mwenye kufikiwa kwako na zaka ya ghamia atoe Jadha'a,na hana Jadha'a na hana jadha'a na anaye Hiqqah,hakika yake atakubaliwa kutoa Hiqqah na ataweka pamoja naye mbuzi wawili ikiwa itakuwa wepesi kwake au dirhamu Ishirini,na mwenye kufikia kwake atoe zaka ya hiqqah na hana hiqqah ,na anaye jadha'a,hakika atakubaliwa atoe Jadha'a na atapewa na mkusanyaji sadaka dirham ishirini au mbuzi wawili. Ameipoke Bikhari,Abu Daud na Annasai.

Na itachukuliwa sadaka ya Ngamia kwa jinsi yake,na kwa sifa yake,basi itachukuliwa kwa ngamia aina ya Bukhatiy-(wazuri mno na wapya- Wkitokea mji wa Khurasani) na Urabi(Kinyume na Bukhatiy) ,na karima,na kwa ngamia wanene basi wachukuliwe wanene,na wale ngamia waliokonda na wenye kukosolewa watachukuliwa hivyo hivyo,na wala hatachukuliwa ngamia kikongwe,wala mwenye chongo ,wala mgonjwa.

**روي عن النبي صلى الله عليه وسلم قال: "ثلاث من فعلهنّ فقد طَعِمَ طَعْمَ الإيمان: من عبد الله وحده، وأنه لا إله إلا الله، وأعطى زكاةَ مالِهِ طيّبة بها نفسه، رافدة عليه كل**

**عام، ولا يعطي الهرمة، ولا الدّرنة، ولا المريضة، ولا الشرط اللئيمة، ولكن من وسط أموالكم، فإن الله لم يسألكم خيره، ولم يأمركم بشره".**

Imepokelewa toka kwa Mtume (S.a.w)amesema : "Mambo matatu yeyote atakaeyafanya kwa hakika atakuwa ameonya ladha ya imani,mwenye kumuabudu Mwenyezi Mungu peke na kwamba hapana Mola apasaye kuabudiwa kwa haki isipokuwa Mwenyezi Mungu,na akatoa zaka ya mali yake kwa uzuri wa nafsi yake,ikimfikia kila mwaka,na wala hatoe kikongwe,na wala aiswe mchafu,na wala asiwe mgonjwa,na wala mwenye alama mbaya,lakini iwe ni miongoni mwa mali zenu za kati kwa kati,hakika Mwenyezi Mungu hakuombeni kheri zake na wala hakuamrisheni shari zake" Ameipokea Abu Daud.

**NG'OMBE**

**Zaka ya ng'ombe ni wajibu kwa dalili ya sunnah na Ij'mai ya maswahaba.**

**فما روى أبو ذر عن النبي صلى اله عليه وسلم أنه قال" ما من صاحب إبل، ولا بقر، ولا غنم لا يؤدي زكاتها إلا جاءت يوم القيامة أعظم ما كانت، وأسمن، تنطحه بقرونها، وتطؤه بإخفاقها" متفق عليه.**

**Amma sunna,ni kwa yale aliyoyapokea Abudharri toka kwa Mtume (S.a.w) kwamba yeye amesema: "Hakuna mwenye Ngami,wala Ng'ombe,wala Mbuzi hatoe zaka yake isipokuwa watakuja siku ya kiama wakiwa wakubwa kuliko walivyokuwa,na wanene,wakimchoma kwa pembe zake,na wakimkanyanga kwa Kwato zake" Muttafaqun alayh.**

**Na Ij'mai ya maswahaba hakika wao wamekubaliana juu ya uwajibu wa kutoa zaka ya ng'ombe.**

**Na zaka ni wajibu katika ng'ombe wanaofungwa na ambao wanachungwa sehemu kubwa ya mwaka,nao ni wale ambao wanachukuliwa kwa ajili ya kuzaliana na kukua,ama ng'ombe wa kufanya kazi hakika hao hawana zaka.**

**عن علي قال: " ليس في البقر العوامل الصدقة"**

**Toka kwa ally amesema :"hakuna sadaka/zaka kwa ng'ombe wa kufanya kazi"ameipokea Abu ubaida na Baihaqii**

**وعن عمرو بن دينار أنه بلغه أن رسول الله صلى الله عليه وسلم قال: " ليس في الثور المثيرة صدقة" وعن جابر بن عبد الله قال: " لا صدقة على مثيرة" والمثيرة التي تثير الأرض أي تحرثها.**

**Na toka kwa Amri bin Dinar kwamba yeye simemfika habari toka kwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) amesema : "Hakuna zaka katika ng'ombe wanaotifua/wanaolima ardhi"**

**Na toka kwa Jabir bin Abdillah amesema : "Hakuna zaka kwa ng'ombe wanaotifua/lima ardhi,na "Almuthirah"wanaotifua ardhi ni ambao wanatifua ardhi yaani wanailima.**

**Na kiwango cha mwanzo cha wajibu kutoa zaka ni Thalathini,na vinakuwa viwango na yale ya wajibu humo ni kama ifuatayo :-**

1- **Ng'ombe thelathini humo ni ndama wa kiume au wa kike,na ndama ni Yule mwenye mwaka mmoja na kaingia mwaka wa pili,na ameitwa hivyo kwa sababu anakuwa anauwezo wa kumfuata mama yake.**

2- **Ng'ombe arubaini,humo ni ndama "Musinnah"na "Musinnah" ni Yule mwenye miaka miwili na ameingia mwaka wa tatu.**

**ودليل ذلك ما روى النسائي والترمذي " أن النبي صلى الله عليه وسلم بعث معاذا إلى اليمن، وأمره أن يأخذ من البقر من كل ثلاثين تبيعا أو تبيعة، ومن كل أربعين مسنة"**

**Na dalili ni yale yaliopokelewa na Annasai na Tirmidhii "kwamba Mtume (S.a.w) alimtuma Muadhi kwenda Yemen,na akamuamrisha achukue zaka katika ng'ombe kwa kila thelathini Tabia au Tabiatan(ndama duke au jike) na kwa kila arubaini achukue "Musinnah"**

3- **Ng'ombe sitini humo ni kutoa Ndama wawili wa kiume au wa kike.**

4- **Ng'ombe sabini humo ni kutoa Musinnah na Ndama mmoja.**

5- **Ng'ombe Themenini humo ni kutoa "Musinnah" wawili.**

6- **Ng'ombe tisini humo ni kutoa Ndama watatu.**

7- Ng'ombea mia moja humo ni kutoa "Musinnah mmoja na "Tabia"ndama wawili.

8- Ng'ombe mis mojs ns kumi humo ni kutoa "Musinnah"wawili na ndama mmoja.

9- Ng'ombe mia moja na Ishirini hmo ni kutoa "Musinnah"watatu au ndama wanne.

**Na wala hakuna zaka kwa idadi ilipo kati hesabu mbili,**

**لما روى يحيي بن الحكم أن معاذا قال: " بعثني رسول الله صلى الله عيه وسلم أصدق أهل اليمن، وأمرني أن آخذ من البقر من كل ثلاثين تبيعا، ومن كل أربعين مسنة، قال: فعرضوا علي أن آخذ ما بين الأربعين والخمسين، وما بين الستين والسبعين، وما بين الثمانين والتسعين، فأبيت ذلك، وقلت لهم: حتى أسأل رسول الله صلى الله عليه وسلم عن ذلك. فقدمت فأخبرت النبي صلى الله عليه وسلم، فأمرني أن آخذ من كل ثلاثين تبيعا، ومن كل أربعين مسنة، ومن الستين تبيعتين، ومن السبعين مسنة وتبيعا، ومن الثمانين مسنتين، ومن التسعين ثلاثة أتباع، ومن المائة مسنة وتبيعتين، ومن العشرة والمائة مسنتين وتبيعا، ومن العشرين ومائة ثلاث مسنات، أو أربعة أتباع، قال وامرني رسول الله صلى الله عليه وسلم أن لا آخذ فيما بين ذلك"**

**kwa yale yaliopokelewa kwa Yahya bin Al-hakam kwamba Muadhi amesema "lituma Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) nikakusanye sadaka/zaka kwa watu wa Yemen,na akaniamrisha nichukue kwa kila ng'ombe thelaehini ndama mmoja,na kwa kila ng'ombe arubaini nichukue Musinnah,akasema : wakanishauri nichukue kati ya ng'ombe arubaini na khamsini,na kati ya sitina na sabini,na kati ya themanini na tisini nikakataa hilo,na nikawaambia: mpaka nikamuulize Mtume (S.a.w) juu ya hilo,nikarudi nikamueleza Mtume (S.a.w),basi akaniamrisha nichukue kwa kila ng'ombe thelathini ndama mmoja ,na kwa kila ng'ombe arubaini "Musinnah" na kwa ng'ombe sitina ndama wawili,na kwa sabini musinnah na ndama mmoja,na kwa themanini Musinnah wawili,na kwa tisini Ndama watatu,na kwa mia Musinnah mmoja na ndama wawili,na kwa mia moja na kumi Musinnah wawili na ndama mmoja,na kwa mia moja na ishirini Musinnah watatu,au ndama wanne,akasema na aliniamrisha Mtume (S.a.w) nisichukue kati ya hapo"**

**وعن معاذ بن جبل قال: " لم يأمرني رسول الله صلى الله عليه وسلم في أوقاص البقر شيئا"**

**na amepokea Ahmad toka kwa Muadhi Bin Jabal amesema : "Hakuniamrisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) kuchukuwa chochote kwa wale ng'ombe waliopoa kati kati ya hesabu/nisabu mbili.**

**Na Nyati hukmu yake ni hukmu ya Ng'ombe katika zaka,ni nisabu (Kiwango cha kuanza kutoa zaka)yake ni sawa ni nisabu ya ng'ombe,na wakiwa pamoja na ng'ombe basi watahesabiwa pamoja katika idadi.**

**عن مالك بن أنس قال: الجواميس والبقر سواء والبخاتي من الإبل وعرابها سواء، والضأن والمعز في الغنم سواء"**

**Toka kwa Malik Bin Anas amesema : Nyati na Ng'ombe ni sawa sawa,na Ngamia Bukhati na Urabu (aina za Ngamia) ni sawa sawa,na Mbuzi wote ni sawa sawa"**

**عن ابن شهاب أن عمر بن عبد العزيز كتب إلى عماله" أن تؤخذ صدقة الجواميس، كما تؤخذ صدقة البقر".**

**Na toka kwa Ibn Shihab kwamba Omar bin Abdul-aziz aliwaandikia wafanyakazi wake (wakuu wa wilaya na maeneo) wachukue zaka ya Nyati kama inavyochukuliwa zaka ya ng'ombe"**

**MBUZI/KONDOO**

**Zaka mbuzi ni wajibu kwa dalili ya sunnah,na Ij'mai ya maswahaba.ama ni kwa yale aliopokea Abu dhari toka kwa Mtume (S.a.w) kwamba amesema:-**

**فلما روى أبو ذر عن النبي صلى الله عليه وسلم أنه قال: ما من صاحب إبل، ولا بقر، ولا غنم لا يؤدي زكاتها إلا جاءت يوم القيامة أعظم ما كانت، وأسمن، تنطحه بقرونها، وتطؤه بأخفافها".**

**Amma sunna,ni kwa yale aliyoyapokea Abudharri toka kwa Mtume (S.a.w) kwamba yeye amesema: "Hakuna mwenye Ngami,wala Ng'ombe,wala Mbuzi hatoe zaka yake isipokuwa watakuja siku ya kiama wakiwa wakubwa kuliko walivyokuwa,na wanene,wakimchoma kwa pembe zake,na wakimkanyanga kwa Kwato zake" Muttafaqun alayh.**

**Na Ij'mai ya Maswahaba,hakika wao wamekubaliana wote pasina kutokea mwenye Kukhalifu juu ya uwajibu wa kutoa**

zaka katika mbuzi/kondoo,na ni wajibu kutoa zaka katika mbuzi wenye kufungwa ambao wanachungwa sehemu kubwa ya mwaka,ikiwa utapita mwaka mmoja juu ya kufikia kiwango,

عن أبي بكر عن النبي صلى الله عليه وسلم في حديث طويل أنه قال: "....وفي سائمة الغنم إذا كانت أربعين ففيها شاة...."، ولقوله صلى الله عيه وسلم" لا زكاة في مال حتى يحول عليه الحول".

Toka kwa Abubakar,toka kwa Mtume (S.a.w) katika hadithi ndefu kwamba amesema : "…….. na katika Mbuzi wanaofugwa wakifika Arubaini basi humo inapaswa kutoa Mbuzi mmoja……." Na kwa kauli yake Mtume (S.a.w) "Hakuna (Kutoa) zaka katika mali mpaka ipitie juu yake na mwaka ".

Na kiwango cha chini cha mbuzi ni arubaini,ikiwa watapungua chini ya arubaini hata mbuzi mmoja basi haipaswi kutoa zaka,na vinakuwa viwango vya zaka ya mbuzi nay ale ya wajibu humo katika sura ifuatayo :-

1- Mbuzi arubaini,inapasa mbuzi mmoja.
2- Mia moja na Ishirini na moja,inapaswa humo mbuzi wawili.
3- Mia mbili na moja,humo mbuzi watatu.
4- Mbuzi mia nne,humo mbuzi wanne.

Na ziada iliopo kati kati ya hesabu mbili haina zaka,ikiwa watafikia mbuzi mia nne,basi inahesabika katika kila mbuzi mia mbuzi mmoja,na wala hakuna kitu katika ziada mpaka itimie mia nyingine,ikiwa atapungua mbuzi mmoja katika mia basi hakuna zaka,na dalili ya hayo:

ما روى عن محمد بن عبد الرحمن" ان في كتاب صدقة النبي صلى الله عليه وسلم، وفي كتاب عمر بن الخطاب، أن الغنم لا يؤخذ منها شيء فيما دون الأربعين، فإذا بلغت الأربعين ففيها شاة، إلى أن تبلغ عشرين ومائة، فإذا زادت على عشرين ومائة واحدة ففيها شاتان إلى المائتين، فإذا زادت على المائتين واحدة ففيها ثلاث شياه إلى ثلاثمائة. قال: فإذا زادت الغنم على ثلاثمائة فليس فيما دون المائة شيء، فإن بلغت تسعا وتسعين، تى تكون مائة تامة، ثم في كل مائة شاة تامة شاة، ولا تؤخذ هرمة ولا فحل إلا أن يشاء المصدق". وفي كتاب الصدقات الذي عند آل عمر بن الخطاب " فإذا زادت عن ثلاثمائة وواحدة، فليس بها شيء حتى تبلغ أربعمائة شاة ففيها أربع شياه".

Yale toka kwa Muhammad bin Abdir rahmani"hakika katika barua za sadaka ya Mtume (S.a.w) ,na katika barua ya Omar bin Khatwab,kwamba katika zaka ya mbuzi haichukuliwi chochote humo chini ya Arubaini,ikiwa watafikia arubaini basi humo yapasa kutoa mbuzi mmoja,mpaka wafikie mia moja na ishirini,ikiwa watazidi katika mia moja na ushirini mbuzi mmoja basi humo yapasa kutoa mbuzi wawili mpaka wafikie mbuzi mia mbili,ikiwawatazidi mbia mbili mbuzi mmoja basi humo mbuzi watatu mpaka wafikie mbuzi mia tatu.amesema : ikiwa watazidi juu ya mia tatu basi hakuna chini ya mia kutoa zaka ,ikiwa watafikia mbuzi tisini na tisa,mpaka wawe mbuzi mia moja,kisha katika kila mbuzi mia moja mbuzi mmoja,na wala asichukuliwe mbuzi kikongwe ,wala fahali isipokuwa akitaka mtoa sadaka.na katika kitabu cha sadaka ambacho kipo kwa familia ya Omar bin Khatwab "ikiwa watazidi juu ya mia tatu mbuzi mmoja,hamna humo zaka mpaka wafikie mbuzi mia nne basi humo watatolewa mbuzi wanne."Ameiokea Abu ubaid.

**YALE YANAYOHESABIWA NA YANAYOCHUKULIWA NA YASIOCHUKULIWA KATIKA ZAKA YA MBUZI**

Kinahesabika kila anachokimiki muislamu miongoni mwa Mbuzi hata kama watakuwa wakubwa au wadogo,mpaka watoto wa kondoo na watoto wa mbuzi kwa sharti wawe wamezaliwaa kabla ya kupita kwa mwaka.

Na atachukuliwa Jadha'a katika (alifikia umri wa miezi sita) zaka ya mbuzi na atachukuliwa Thaniy(aliyefikia mwaka mmoja) katika kondoo,hakuna tofauti kati ya madume na majike,anaweka akachukuliwa dume na anaweza akachukuliwa jike,na watachukuliwa wa kati na kati na wala hawatachukuliwa wa juu yake zaidi au wa chini yake zaidi.

Na wala hawatachukuliwa watoto wa kondoo na mbuzi wadogo,hakika hao hawatoshelezi katika zaka,kama hivi hatachukuliwa mbuzi aliyezaa hivi karibuni au Yule ambaye anatarajiwa kuzaa hivi karibuni,na wala mbuzi ambaye anafugwa kwa ajili kupata maziwa au kwa ajili ya nyama,wala

**fahali la mbuzi,isipokuwa akijitolea mwenye mbuzi akatoa zaka hiyo atakubaliwa,na atapata malipo ya ziada kwa sababu huyo anapendeza zaidi kwake,na dalili ya hayo :-**

**ما روى بشر بن عاصم عن أبيه أن عمر بن الخطاب استعمل أبا سفيان بن عبد الله على الطائف ومخاليفها، فخرج مصدقا فاعتد عليهم بالغذي- السخلة- ولم يأخذه منهم، فقالوا له: إن كنت معتدا علينا بالغذي فخذه منا، فأمسك حتى لقي عمر فقال:" أعلم أنهم يزعمون أنا نظلمهم أنا نعتد عليهم بالغذي ولا نأخذه منهم" فقال له عمر: " فاعتد عليهم بالغذي، حتى بالسخلة يروح بها الراعي على يده وقل لهم: لا آخذ منكم الربى- الوالدة - ولا المخاض -الحامل- ولا ذات الدر، ولا الشاة الأكولة- التي تسمن للذبح- ولا فحل الغنم، وخذ العناق - مالم تتم سنة من المعز صلى الله عليه وسلم والجذعة، والثنية، فذلك عدل بين غذاء المال- السخال- وخياره"**

**رواه الشافعى ومالك**

**Ni yale aliopokea Asim toka kwa Baba yake kwamba Omar bin Khatwab alimfanya Abusufian Bin Abdlillah katika mji wa Twaif na maeneo yake ya pembezoni,akatoka akikusanya sadaka/zaka,akahesabu kwao Ghadhiy/salikhah (aliynona na anafaa kuchunwa kwa kuliwa) na wala hakuchukuwa kwao,wakwamwambia :ikiwa umetuhesabia hawa walionona wachukuwe,akajizuia mpaka akakutana na Omar akamwambia : "Fahamu ya kuwa wao wanadai sisi tunawadhulumu,kwamba sisi tunahesabu wale walionona na wala hatuchukui hao toka kwao"akasema Omar:"wahesabie hao walionona,mpaka Yule mzuri hasa anaeondoka naye mchungaji mkononi kwake (anapoondoka) na waambie : "Sichukui kwenu nyinyi Mbuzi aliyezaa hivi punde,wala mwenye mimba,na wala mwenye kububujisha maziwa kwa wingi,wala mbuzi anailishwa ili aje achinjwe-ambaye ananenepeshwa ili achiunjwe-,wala fahali la mbuzi,chukuwa "Al-iaqa"(ambaye hajatimiza mwaka katika Mbuzi,na Jadh'a katika kondoo,na chukuwa "Thaniyyah" hivyo ni kati na kati (usawa) baina ya Lishe ya Mali na Ubora wake" Kaipokea Shafii Na maliki**

**na kwa kauli ya Mtume (S.a.w)**

إنما حقنا في الجذعة والثنية

**"Hakika haki yetu ni katika Jadh'aa na Thaniyyah".Ameitaja Ibn Quddama katika Nughni .**

**Na wala usichukue katika zaka kikongwe,na wala mwenye aibu,kwa kauli yake Mwenyezi Mungu :**
**(ولا تيمموا الخبيث منه تنفقون)**
" Na wala Msikusudie kutoa vilivyo vibaya" TMQ 2:267
**ولقوله صلى الله عليه وسلم: " ولا تؤخذ في الصدقة هرمة، ولا ذات عوار، ولا تيس إلا إن شاء المصدق"**
Na kwa kauli ya Mtume (S.a.w) "Na wala msichukue katika sadaka Kikongwe,wala mwenye Chongo.wala Mbuzi alienona/pendeza isipokuwa akitaka Mtoa sadaka" Ameipkea Abuu daud
Ikiwa atakubali mkusanya sadaka kuchukua aina hizi kwa kuwa mbuzi wote ni vikongwe,au wana aibu Fulani, itruhusiwa awachukue.

**HUKMU YA WASHIRAKA KATIKA MBUZI/KONDOO**
Kushirikana au kuchanganya mbuzi wa kufugwa huifanya mali iwe ni ya washirika wawili,au waliochanganya wawili,iwe kama mali ya mtu mmoja katika zaka,sawa itakuwa ni kuchanganya kwa Mifugo yenyewe/vitu,nako ni kuwa mifugo inashirikiana baina yao,kila mmoja kati ya hao wawili ana fungu lake linaloenea pasina kutengwa/kupambanuliwa,kwa mfano hao wawili warithi kiwango Fulani,au wanunue kwa ushirika,au wapewe zawadi,wakawawabakisha hivyo hivyo pasina kutengenisha,wala kugawa,sawa iwe hivyo ,au uwe ni mchanganyiko wa sifa,nao ni kule kuwa mali ya kila mmoja wao inajulikana,wakaichanganya na wakashirikiana-Sawa wamelingana katika kushirikiana au wamezidiana-katika mchungaji na machungio,na fahali na manywaji.
Hakika mbuzi wa kushirikiana au wa kuchanganya vyovyote vile wawavyo wao ni kama mbuzi wa mtu mmoja,wanahesabaiwa hesabu moja,na wanabaki katika hali yake pasina kutenganishwa,au kukusanywa.pindi wakifika arubaini atachukua mkusanyaji mbuzi mmoja tu,na ikiwa watafikia mia moja na ishirini na moja atchukua humo mbuzi wawili,na ikiwa watafikia mia mbili na moja atachukua mbuzi

watatu,na ikiwa watafikia mia nne watachukuliwa mbuzi wanne.
Na kitagawanywa kile alichochukua mkusanyaji sadaka kwa washirika au waliochanganya kwa mujibu wa mafungu yao katika mbuzi,na Yule mwenye wachache atamrejeshea mwenye wengi kwa kile kiwango chake,kwa kauli yake Mtume (S.a.w)
**لقوله النبي صلى الله عليه وسلم " وما كان من خليطين فإنهما يتراجعان بينهما بالسوية".**
“Na wale (Mbuzi) watakaokuwa ni watu wawili walichanganya,hakika hao watarejesheana baina yao kwa sawa sawa”ameipokea Abuu Daud
Na mkusanyaji sadaka atawabakisha mbuzi kama walivyo,na atawahesabu kama walivyo,na wala hairuhusiwi awatenganishe ili achukue kiasi kingi,navyo ni kama itakuwa kwa washirika watatu,waliochanganya wana mbuzi mia moja na ishirini,kila mmoja ana mbuzi arubaini,akakausudia mkusanyi kuwatenganisha ili achukue mbuzi watatu,kwa kila mshirika mbuzi mmoja,haifai kufanya hivyo,na anapaswa awabakishe kama walivyo,na achukue humo mbuzi mmoja tu,
kama vile ambavyo haifai kwa wamiliki wa mbuzi kuwatenganisha wakati wa kufika mkusanyaji kwa kutaka kupunguza zaka yake,au kwa kutokutoa zaka yao,na hali ni kama vile watakapokuwa washirika wawili,wa waliochanganya wawili wana mbuzi mia mbili na moja wakawatenganisha ili watoe mbuzi wawili badala ya watatu,katika hali ambayo kama wale mbuzi wangebaki vile vile pamoja,au kama wanamiliki mbuzi arubaini wakawatengamisha ili wasitoe zaka baada ya kuwatenganisha.
Kama vile ambavyo haifai kuwatenganisha mbuzi waliokusanyika,pia haifai kuwakusanya waliotenganishwa katika hao kwa kutaka kupunguza kile kiwango cha kutoa,nako ni pale watakapokuwa watu wawili wana mbuzi themanini,kila mmoja ana mbuzi arubaini pasina kuchanganya na mwenzie,wala kushirikana,pindi atapokuja mkusanyaji wanawachanganya sawa kwa sawa ili wasitoe zaka isipokuwa mbuzi mmoja tu,badala ya kila mmoja kutoa mbuzi mmoja.

ما رواه سعد بن أبي وقاص، قال: قال رسول الله صلى الله عليه وسلم:" لا يفرق بين مجتمع، ولا يجمع بين متفرق في الصدقة. والخليطان ما اجتمعا على الفحل والمرعى والحوض" وفي رواية: "والراعي".

Na dalili ya kutokufaa kuchanganya,waka kukusanya walio tenganishwa,ni ile alioipokea Sa'd bin Abi waqqaswi amesema: amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) "wasitenganishwe walikusanyika,na wala wasikusanywe waliotawanyikaa katika zaka,na waliochanganywa ni wale wanakusanyika juu ya fahali,machungio,na sehemu ya kumnywea" na katika mapokezi mengine "Na Mchungaji" ameipokea Abu Ubaid.

Na itachukuliwa zaka katika mifugo yenyewe kwa yale ya wajibu kwa Ngamia,au Ng'ombe au Mbuzi,na wala haifai kuchukuwa thamani yake badala ya mnyama mwenyewe,kwa sababu dalili za hadithi zimebainisha kile kinachochukuliwa katika ngamia,na ng'ombe na mbuzi na zikapanga/eleza umri wake.

Na pindi wakifanywa mifugo katika ngamia,na ng'ombe,na nyati,na mbuzi kuwa ni wa biashara,basi zaka yake itakuwa ni zaka ya bidhaa za biashara,sio zaka za mifugo,haitazingatiwa humo idadi,wala umri,na watathaminiwa thamani ya bidhaa za biashara na wala sio zaka ya mifugo,haitazingatiwa humo idadi wala umri,na watathaminiwa thamani ya bidhaa za biashara,kwa thamani ya Dirham kwa fedha au dinari kwa dhahabu,wakifikia thamani yake Dirham 200 za fedha,na ndio kiwango/nisabu ya fedha, yaani gram 595 za fedha kwa msingi kuwa dirham ya fedha inalingana au ni sawa na 2,975 za fedha,au ikafikia thamani yake ni dinari 20 za dhahabu,na ndio nisabu/kiwango cha dhahabu,yaani gram 85 kwa msingi kuwa dinari moja uzito wake gram 4,25 za dhahabu,na ni wajibu humo kutoa robo ya moja ya kumi,nandio kiwango cha wajibu katika bidhaa za biashara.

**ZAKA YA MAZAO NA MIMEA**

Zaka ya Mazao na mimea ni wajibu kwa dalili ya kitabu na sunnah.ama kitabu ni kauli yake Mwenyezi Mungu Mtukufu :-
[Na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake .TMQ 6:141]
(وآتوا حقه يوم حصاده)

Ama Sunnah ni kauli yake Mtume (S.a.w) :-

**فقول النبي صلى الله عليه وسلم" ليس فيما دون خمسة أوسق صدق" متفق عليه.**
**وعن ابن عمر عن النبي صلى الله عليه وسلم قال: " فيما سقت السماء والعيون أو كان عثريا العشر، وفيما سقي بالنضج نصف العشر" أخرجه البخاري.**

[Hakuna chini ya makapu matano(Ya Mazao) Kutoa zaka ] na toka kwa Ibn Omar (amesema) Toka kwa Mtume (S.a.w) amesema [ Katika Mazao (yaliota kwa ) Kunyeshewa na Mvua na Chemchem au yakawa yameota yenyewe zaka yake ni Moja ya kumi,na yale mazao yaliota kwa kumwagiliwa maji zaka yake ni Nusu ya moja ya kumi" ameitoa hadithi hii Imam Bukhari.]

**<u>AINA ZA MAZAO NA MATUNDA AMBAYO NI WAJIBU HUMO ZAKA</u>**

Aina za mazao ni Ngano,Na Shairi,na Tende,na Zabibu,kwa dalili iliopokelewa kwa Abu musa Bin Twalha,(Amesema) Toka kwa Omar kwamba yeye amesema :-

**روى موسى بن طلحة عن عمر أنه قال: " إنما سن رسول الله صلى الله عليه وسلم الزكاة في وهذه الأربعة: الحنطة، والشعير، والتمر، والزبيب".**

[Bila Shaka Mtume (S.a.w) ameweka Utaratibu wa kutoa Zaka katika mazao haya ya aina nne,Ngano,na Shairi,na Tende na Zabibu.Ameipokea Imam Twabaraniy"]

**وعن موسى بن طلحة أيضا قال: " أمر رسول الله صلى الله عليه وسلم معاذ بن جبل -حين بعثه إلى اليمن- أن يأخذ الصدقة من الحنطة، والشعير، والنخل، والعنب"**

Na toka kwa Musa bin Twalha pia amesema :- " Amemuamrisha Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) Muadhi Bin Jabal – wakati alipomtuma kwenda Yemen- achukue zaka kwa mazao ya Ngano,na Shairi,na Tende,na Zabibu.Ameipokea Abu ubaid]

Hadithi hizi zinabainisha kuwa Zaka katika mazao na matunda bila shaka inachukuliwa katika aina hizi nne,Ngano,na Shairi,na Tende,na Zabibu,na wala haichukuliwi toka kwa aina nyingine za mazao na matunda,kwa sababu Hadithi ya mwanzo imeanza kwa neno "Innamaa"(Bila shaka si ninginelo) ambalo kwa mujimu kwa kanuni za Lugha ya kiarabu lina maana ya "Haswru" (Kukidhibiti/kukihusiha kile kilichotajwa tu kwa jambo maalum au sifa maalum).ambayo imeshadidia kudhibiti uwajibu wa zaka katika hizi aina nne za mazao na matunda.

ما أخرجه الحاكم، والبيهقي، والطبراني من حديث أبي موسى ومعاذ حين بعثهما النبي صلى الله عليه وسلم إلى اليمن يعلمان الناس أمر دينهم، فقال:" لا تأخذ الصدقة إلا من هذه الأربعة: الشعير، والحنطة، والزبيب، والتمر"

Pia katika yale yaliopokelewa na Alhakim,na Baihaqii,na Twabarani toka hadithi ya Abumusa na Mua'dh wakatia alipowatuma Mtume (S.a.w) kwenda Yemen kuwafundisha watu dini yao,akasema :- [" Msichukue zaka isipokuwa toka aina hizi nne,Shairi,na Ngano, Zabibu,na Tende"]

Amesema Imam Baihaqii juu ya hadithi hii:wapokezi wake ni wakweli"Thiqatu",nayo ni Hadithi "Muttaswil"Imeungana Sanadi yake,.na hadithi iko wazi ndani kuna Haswru/kudhibiti na kuhusisha kuchukuwa zaka katika mazao na mimea kutoka aina hizi nne,kwa sababu tamko "Illah"(isipokuwa) pindi likitanguliwa na chombo cha kukanusha,au cha kukataza linatoa maana ya kukihusisha kile cha kabla yake juu ya kile cha baada yake,yaani kuhusisha kuchukuwa zaka juu ya aina hizi nne zilizotajwa baada yake,nazo ni Shairi,na Ngano,na Zabibu na Tende.

Na kwa sababu matamko(maneno) Ngano,Shairi,Tende na Zabibu ambayo yamepokelewa katika hadithi hizi ni Majina Jamida(Yasiotoholeka) hayachukuwi matamko yake maana ya neno lingine,si kwa matamshi yake na wala si kwa Mafhumu(maana yake)na wala si kwa kuambanata kiulazima( Ukitaja hili basi huambatana na linguine) kwa sababu hayo si majina ya sifa,na wala si majina ya Maana( Yenye kutoa maana nyingine ) basi yamefupika katika vitu ambavyo imeitiwa kwavyo na kutumika kwa vitu hivyo tu,kwa sababu haitachukuliwa kutokana na matamshi yake maana ya "kuwa ni Chakula"au "Kikavu" au "Kuhifadhika, kwa sababu matamko yake hayaonyeshi juu ya maana hizi na sifa hizi.

Na zitakuwa hadithi hizi ambazo zimefunga (zimedhibiti) uwajibu wa zaka katika aina hizi nne za mazao na matunda zinahusisha matamko ya kiujumla yaliokuja katika hadithi :

" فيما سقت السماء العشر، وفيما سقي بغرب، أو دالية نصف العشر"

"Katika mazao yalinyeshewa na mvua (zaka yake ni ) Moja ya kumi,na yale yalimwagiliwa kwa vyombo au chombe cha kumwagilia (zaka yake ni ) Nusu ya moja ya kumi"

Kwa sababu hii inakuwa maana yake kwamba mazao yalionyeshewa na mvua miongoni mwa ngano,shairi,tende na zabibu zaka yake ni moja ya kumi ,na yale yaliomea kwa kumwagiliwa maji kwa vyombo zaka yake ni nusu ya moja ya kumi.

Na wala si wajibu kutoa zaka katika zisizokuwa aina hizi nne katika mazao na matunda,kwa sababu hii haichukuliwi zaka ya mahindi,Mchele?mpunga,Maharage,na Himsi,na dengu na vinginevyo katika nafaka,na Qat'niyaatu(Dengu,Maharage na Himsi nk),kama vile haichukuliwi zaka ya Matufaha,mapeasi ,darraqu na mish mish ,marumani ,machungwa na ndizi,na aina nyingin za matunda.

Kwa sababu nafaka hizi na matunda haya hayakusanywi na neno Ngano,Shairi,Tende na Zabibu,kama vile ambavyo haikupokelewa dalili sahihi ya kutegemewa,wala Ij'maa,na wala hayaingiwi na Kiasi,kwa sababu zaka ni katika Ibada,na Ibada haziingiwi na kiasi,bali hutokwa tu kwa yale yaliowekwa na dalili,kama vile ambavyo haichukuliwi zaka toka kwenye Mboga mboga kama Matango,Khiyari,yaqtwin,Bilinganya,Maboga,karoti na mengineyo,

**فقد روى عن عمر وعلي ومجاهد وغيرهم أنه ليس في الخضراوات صدقة، رواها أبوعبيد والبيهقي وغيرهما.**

Imepokelewa toka kwa Omar ,Ally na Mijahidi na weengineo kwamba Hakuna zaka katika Mboga mboga,Imepokelewa na Abu Ubaida na Baihaqii na wengineo.

**والحمص، والعدس ،، كما لا تؤخذ من التفاح، والإجاص، والدراق، والمشمش، كالقثاء، والخيار، واليقطين، والباذنجان، واللفت، والجزر، وغيرها،**

نصاب الزروع والثمار

**NISABU(KIWANGO) CHA MAZAO NA MATUNDA**

Hakika nisabu ya chini ya zaka ya mazao na matunda ni wajibu kutoa zaka ni makapu matano,ikiwa Ngano,au Shairi,au Tende au zabibu haikufikia makapu matano hamna zaka humo,

**عن أبي سعيد الخدري قال: قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: " ليس فيما دون خمسة أوسق صدقة" أخرجه البخاري ومسلم.**

kwa yale yalipokelewa toka kwa Abu said Al-khudriy amesema :Amesema Mtume (S.a.w) :"Hakuna Kutoa zaka chini ya makapu matano"Ameitoa Bukhari naMuslim.

**عن محمد بن عبد الحمن أن في كتاب رسول الله صلى الله عليه وسلم، وفي كتاب عمر في الصدقة" أن لا تؤخذ من شيء حتى يبلغ خمسة أوسق" أخرجه مسلم.**

Na kwa yale yaliopokelewa toka kwa Muhammad Bin Abdirrahmani kwamba katika barua ya Mtume (S.a.w) na katika Barua ya Omar katika zaka kwamba pasichukuliwe chochote mpaka kififie makapu matano"ameitoa Muslim.

**روى أبو سعيد، وجابر عن النبي صلى الله عليه وسلم قال: " الوسق ستون صاعا"**

Na Wisqu(Kapu)ni pishi sitini,amepokea Abu Said na Jabir toka,toka kwa Mtume (S.a.w) amesema : "Wisqu ni Pishi sitini" na Pishi ni Vibaba vine,na kibaba ni Ratili moja na Theluthi kwa kipimo cha Baghdadi,na pishi moja ni sawa na kg 2,176,na wisqu moja ni sawa na kg 130,56 za ngano .na juu ya haya unakuwa uzito wa Wisqu tano – na ndio nisabu ya zaka- ya ngano ni kg 652,na uzito huu unatofautiana na uzito wa shairi,na uzito wa tende,na uzito wa zabibu,kwa sababu aina hizi haziko sawa kiuzito kwa kipimo kimoja,na Nisabu inazingatiwa kwa kipimo na wala si kwa uzito kwa kule kuhusiana uwajibuwa zaka kwa hilo,kama zilivyotaja hadithi juu ya hilo.

WAKATI WA KUCHUKUA ZAKA KATIKA NAFAKA NA MATUNDA

Ikiwa nafaka na matunda zitafikia wisqu/makapu matano baada ya kutolewa ardhini,itachukuliwa zaka yake katika nafaka baada ya kuvunwa na kupondwa/kusangwa na kusafishwa,na katika matunda baada ya kukauka na ziwe tende laini/rutwabu ngumu,na zabibu laini ziwe ngumu na wala hakuna sharti la kupitwa na mwaka,bali kuvunwa ,kusafishwa na kukauka kwa ajili ya kauli yake Mwenyezi Mungu mtukufu :-

**( وآتوا حقه يوم حصاده)**

[Na toeni haki yake siku ya kuvunwa kwake TMQ 6:141]

Na kwa sababu sunnah inajulisha kwamba kuchukuwa zaka kunakuwa baada ya kukaushwa tende na zabibu na kugeuka

kuwa tende na zabibu ngumu na baada ya kuvunwa nafaka na kupondwa na kusafishwa.

**KUHESABIWA MATUNDA**

**Ni wajibu kwa Dola itume wahesabuji wanakaowahesabia watu matunda yao miongoni mwa mitende na mizabibu,baada kuonekana kufaa kwake,**

**عن عتاب بن أسيد" أن النبي صلى الله عليه وسلم كان يبعث على الناس من يخرص عليهم كرومهم وثمارهم" رواه أبو داود وابن ماجة والترمذي.**

**kwa yale aliopokea Ut'tab ni Usaid kwamba Mtume (S.a.w) alikuwa aliwatumia watu Yule ambaye atahesabu mizabibu yao na matunda yao" Ameipokea Abu Daud na Tirmidhii na Ibn Majah.**

**وفي لفظ عن عتاب قال: " أمر رسول الله صلى الله عليه وسلم أن يخرص العنب كما يخرص النخل، وتؤخذ زكاته زبيبا، كما تؤخذ زكاة النخل تمرا وقد عمل به النبي صلى الله عليه وسلم فخرص على امرأة بوادي القرى حديقة لها" رواه الأمام أحمد في مسنده وعمل به أبو بكر بعده والخلفاء.**

**Na katika tamko linguine toka kwa Ut'tab amesema: "Ameamrisha Mtume (S.a.w) zihesabiwe zabibu kama vile zinavyohesabiwa tende,na ichukuliwe zaka yake zikiwa ni zabibu zilizokomaa,kama vile zinavyochukuliwa zaka ya tende zikiwa ni tende zilizokomaa na alilifanya hili Mtume (S.a.w) alimhesabia mwanamke wa Bonde la Qura shamba lake,ameipokea Imam Ahmad na alilifanya hili Abubakar na Makhalifa baada yake.**

**Na ni juu ya Mwenye kuhesabu katika kuhesabu aache Theluthi moja au Robo pasina kuihesabu,kwa ajili ya kuwapa wasaa wenye matunda,kwa sababu wabahitaji kuyala na chakula kwa wageni wao,majirani zao,jamaa zao ,marafiki zao,wanapita kwao,na wanaomba ambao wanawaomba,na kwa ajili ya kula ndege ambao wanatua hapo.**

**عن سهل بن أبي حثمة أن رسول الله صلى الله عليه وسلم كان يقول:" إذا خرصتم فخذوا ودعوا الثلث، فإن لم تدعو الثلث فدعوا الربع" رواه أبو داود والترمذي والنسائي.**

**Toka kwa Sahli bin Abi hathma amesema kwamba Mtume (S.a.w)alikuwa akisema : "pindi mtakapohesabu acheni**

**Theluthi, ikiwa hamkuachathelethi basi acheni acheni Robo"ameipokea Abu Daud na Thirmidhiy na Annasai.**

**وعن مكحول قال: " كان رسول الله صلى الله عليه وسلم إذا بعث الخراص قال: خففوا فإن المال العرية، والوطية، والآكلة".**

**Na toka kwa Makhoul amesema: alikuwa Mtume (S.a.w) pindi anapowatuma wahesabuji husema : fanyeni wepesi kwa sababu katika mali kuna cha kuazima,na cha kukanyaga(Wanaotembea)na cha kula"ameipokea Abu Ubaid.**

**Na wala haihesabiwi ngano na shairi ,kwa sababu haikupokelewa hivyo kwa Mtume (S.a.w),na kwa sababu kuhesabu kwake si jambo jepesi kama ilivyo katika tende na zabibu,na kwa sababu matunda ya tende na zabibu yanaliwa yakiwa mateke/laini,-huhesabiwa kwa wenyewe kwa kuwafanuia wepesi kwao,ili wapewe nafasi kwao ya kula matunda na kuyatumia kwa kuuzamau kula au kutoa zawadi au linginelo,kisha wanato zaka katika hayo kwa yale yaliohesabiwa.**

**Na zainahesabiwa tende na zabibu kwa aina zake zote nzuri na mbaya,na zinakusanywa baadhi yake kwa baadhi na wala hazikusanywi tende pamoa na zabibu,kama vile ambavyo haikusanywi ngano na shairi.**

**Na matunda yakifikwa na uharibifu baada ya kuhesabiwa,na kabla ya kukauka,au yakaharibika pasina kufanya uzembe,au yakaibwa kabla ya kukauka,na baada yake,hakuna dhamana kwa mwenyewe na wala si wajibu kutoa zaka isipokuwa yale yaliobaki yakiwa yanafikiwa kiwango.**

## KIWANGO CHA ZAKA AMBAYO HUCHUKULKIWI TOKA KATIKA NAFAKA NA MATUNDA

**Pindi ikitolewa ardhini katika ngano,au shairi au tende au zabibu wisqu/makapu matano itakuwa ni wajibu Ushru/moja ya kumi ikiwa imemwagiwa pasina gharama yoyote,kama vile imenyeshewa na maji ya mbinguni,au mito,au imekuwa mizizi yake ikinywa maji pasina kumwagiwa kama vile mti ambao unapandwa katika ardhi ambayo maji yake yapo**

**karibu na uso wake,au ipo karibu na mto au mfereji na mizizi ya mti anayafikia maji pasina kuhitaji kumwagiliwa.**

**Na ni wajibu kutoa Nusu ya Ushru/nusu ya moja ya kumi wa mazao yalimwagiwa maji kwa gharama kama vile kutumia vyombo na vifaa vya umwagiliaji.**

**عن علي قال: فيما سقت السماء العشر، وفيما سقي بالدوالي والنواضح ونصف العشر"**

**Toka kwa Ally (R ) amesema : katika yale mazao yaliomwagiliwa kwa mvua itolewa Ushru/mija ya kumi,na katika yale yalimwagiliwa kwa vyombo na vyombo vya kumwagiulia nusu ya Ushr"**

**وعن بسر بن سعيد قال: " فرض رسول الله صلى الله عليه وسلم الزكاة فيما سقت السماء، وفي البعل، وفيما سقت العيون العشر، وفيما سقت السواني نصف العشر"**

**Na toka kwa Busra Bin Said amesema : Ameagiza Mtume (S.a.w) zaka katika (Mazao) yalinyeshewa na Mvua ,na katika yaliolowa lowa,na katika yalionyeshewa na Chem chem. Ushru/moja ya kumi,na yale yalio mwagiwa kwa vyombo nusu ya UShru/moja ya kumi"ameipokea Abu ubaid.**

**وعن الحكم بن عتيبة قال: كتب رسول الله صلى الله عليه وسلم إلى معاذ بن جبل وهو باليمن: إن فيما سقت السماء، أو سقي غيلاً العشر، وفيما سقي بالغرب نصف العشر"**

Na toka kwa Al-hakam bin Utaibah amesema :aliandika Mtume (S.a.w) kwa Mua'dh bi Jabali akiwa Yemen: Hakika katika yale yalinyeshewa na mbingu/mvua au yakanyeshewa kwa Ghaylan(ukungu,umande na umajimaji) moja ya kumi,na yaleyalimwagiwa kwa vyombo ni nusu ya Ushru"

Na umwagilaji huu unazinagtiwa katika sehemu kubwa ya mwaka,ikiwa sehemu kubwa ya mwaka yatamwagiliwa pasina gharama itakuwa zaka yake ni nusu ya ushru/moja ya kumi,na ikiwa yatamwagiliwa kwa maji katika sehem kubwa ya mwaka itakuwa zaka yake ni nusu ya Ushru/moja ya kumi,na ikiwa yamemwagiliwa nusu ya mwaka kwa gharama na nusu ya mwaka yakwamwagiliwa bila gharama itakuwa zaka yake ni robo tatu ya ushru/moja ya kumi.

**NAMANA YA KUTOA ZAKA KATIKA NAFAKA NA MATUNDA**

Asili katika zaka ya nafaka na matunda ni kuchukuliwa nafaka na matunda yenyewe ambayo ni wajibu kutolewa zaka,na

yachukuliwe katikati yake na wala sio juu yake,na wala sio mabaya yake,haifai kwa mkusanya zaka akakusudia kuchukuwa mazao namatunda mazuri sana kuliko yote katika zaka,

**لقول النبي صلى الله عليه وسلم" إياك وكرائم أموالهم".**

kwa kauli yake Mtume (S.a.w)"Tahadhari mali zao nzuri"Tirmidhiy

kama vile haiai kwa mwenye mazao /mkulima mwenye nafaka na matunda akusudie kutoa yaliomabaya zaidi kuyatoa katika zaka,kwa kauli yake Mwenyezi Mungu :-

**ولا تيمموا الخبيث منه تنفقون)**

[na wala msikusudie kutoa vilivyo vibaya …TMQ 2:267]

Na kwa katazo la Mtume (S.a.w) la kuchukuwa Alja'ruru(Aina ya tende mbaya) na Rangi mbaya(aina ya tende) katika zaka,Kaipokea Annasai.nazo ni aina mbili za tende,moja wapo inageuka na kuwa ni ganda tupu na nyingine ikitoa matunda/ikikomaa inakuwa mbaya sana.

Na ni ruhusa katika zaka ya nafaka na matunda kuchukuwa thamani –hela au mfano wake badala ya kuchukua nafaka au tunda lenyewe,

**روى عمرو بن دينار عن طاووس أن النبي صلى الله عليه وسلم بعث معاذاً إلى اليمن فكان يأخذ الثياب بصدقة الحنطة والشعير"**

nayo kwa yale alioyapokea Amru bin Dinar toka kwa Twausi kwamba Mtume (S.a.w) alimtuma Mua'dh kwenda Yemen akawa anachukuwa nguo kwa ile zaka ya ngano na shairi"Ameipokea Abu Ubaid.

Na kwa sababu hupatikana aina Fulani ya tende zile tende zake teke teke hazikomai na kuwa tende kamili,na kama vile hupatikana aina za zabibu hazifikii kukomaa zikawa zabibu basi huchukuliwa humo kima/thamani yake,.

Imepokewa toka kwa Muadh katika zaka hiyo hoyo kwamba yeye alichukuwa badala yake bidhaa za biashara,na hilo ni katika kauli yake

**" إيتوني بخميس أو لبيس آخذه منكم مكان الصدقة فإنه أهون عليكم وأنفع للمهاجرين بالمدينة"**

"Niletee Nguo au kivazi nikichukuwe badala ya zaka kwa sababu hilo ni jepesi kwenu na lina manufaa zaidi kwa Muhajirina wa Madina"
Na kwa hakika imepatikana katika sunna toka kwa Mtume (S.a.w) na maswahaba zake ,huwa inakuwa wajibu haki katika mali kisha anaigeuza kwa kitu kingine kile ambacho kinakuwa kukitoa ni chepesi kwa mtoaji kuliko kile cha asili.na katika hayo barua ya Mtume ( S.a.w) kwa Mua'dh bin Jabal katika Jiz'yah kwamba

**"أن على كل حالم دينارا أو عدله من المعافر"**

" Juu ya kila Mtu mzima Balegh Dinar moja au kiwango chake na Mu'arifia (Aina ya Nguo ikitengenezwa Yemen)"Mtume (S.a.w) alichukuwa bidhaa badala ya Kitu chenyewe,yaani alichukuwa nguo badala ya Dhahabu.Kaipokea Abu Daud.

**" أن عليهم الفيء حله في كل عام أو عدلها من الأواقي"**

Na katika hayo yale aliyoyaandika kwa watu wa Najrani,"kwamba wana wao (Ni wajibu wao)kutoa nguo alf mbili kwa kila mwaka (kuilipa dola ya Kiislam) au thamani yake katika vito (Dhahabu) ameipokea Abu Ubaid.
Na ameeleza Ibn Quddamah katika Mughni kwamba Omar ( R ) alikuwa akichukuwa ngamia katika Jiz'yah badala ya Dhahabu na Fedha,kama vile Ally ( R ) alikuwa anachukuwa akichukuwa Sindano,na Kamba na Panga/ala katika Jiz'yah badala ya Dhahabu na Fedha.

زكاة الفضة والذهب

**<u>ZAKA ZA DHAHABU NA FEDHA</u>**

Zaka ya Dhahabu na Fedha,sawa zitakuwa hela(zilizofuliwa) au hazijafuliwa,ni wajibu kwa dalili ya sunnah na Ij'mai ya maswahaba.

Amma sunnah ni yale yaliopokelewa na Abu hurairah ( r )amesema :

**فما روى أبو هريرة قال: رسول الله صلى الله عليه وسلم: "ما من صاحب ذهب، ولا فضة لا يؤدي منها حقه، إلا إذا كان يوم القيامة صفحت له صفائح من نار، فأحمى عليها في نار جهنم، فيكون بها جنبه وجبينه وظهره، كلما بردت أعيدت له، في يوم كان مقداره خمسين ألف سنة حتى يقضى بين العباد، فيرى سبيله إما إلى الجنة، وإما إلى النار" رواه الخمسة إلا الترمذي.**

amesema Mtume (S.a.w) ""Hakuna Mtu yeyote Mwenye Dhahabu,wala Fedha hatoe zaka haki yake isipokuwa ikifika siku ya kiama itatengenezwa(Dhahabu na Fedha na kuwa ) sahani za moto,zitaokwa katika moto wa Jahannamu,atapigwa pasi kwazo mbavuni mwake na usoni mwake na mgongoni mwake,kila mara zinapopoa hurejeshwa tena katika siku ambayo kiwango chake ni miaka khamsini,mpaka pahukumiwe baina ya waja,basi ataona njia yake,ima kwenda peponi au kwenda motoni."Wameipokea wapokezi watano isipokuwa Tirmidhii.

Na toka kwake Mtume (S.a.w) amesema :-

**وعنه صلى الله عليه وسلم قال:" من آتاه الله مالاً فلم يؤد زكاته مثل له يوم القيامة شجاعاً أقرع، له زبيبتان يطوقه يوم القيامة، ثم يأخذ بلهزمتيه، ثم يقول: أنا مالك، أنا كنزك، ثم تلا{ ولا يحسبن الذين يبخلون بما آتاهم الله من فضله هو خيراً لهم، بل هو شر لهم، سيطوقون بما بخلوا به يوم القيامة}، رواه الخمسة إلا أبا داوود.**

Mwenye kujaaliwa mali kisha hakuitolea Zakaah yake itageuzwa (mali hiyo) nyoka mwenye sumu kali ambae kichwa chake hakina manyoya na huku ana alama za vidoto viwili vyeusi kwenye macho yake. Nyoka atamzonga kwenye shingo yake na kumng'ata kwenye mashavu huku akisema: "Mimi ni utajiri wako mimi ndiyo hazina yako" Kisha akasoma: "Wala wasione wale ambao wanafanya ubakhili katika aliyowapa Allaah miongoni mwa fadhila zake kuwa ni bora kwao (kufanya ubakhili). Laa ni vibaya kwao watafungwa kongwa (minyororo inayofungwa kwenye shingo) za yale waliyoyafanyia ubakhili siku ya kiama" [Aali 'Imraan: 180] al-Bukhaariy

Amma Ij'mai : Kwa hakika wamekubaliana maswahaba juu ya uwajibu wa kutoa zaka katika Dhahabu na Fedha pasina kutofautiana.

**<u>KIWANGO CHA NISABU YA FEDHA</u>**

Kwa hakika kiwango cha chini cha wajibu kutoa zaka ni waqia Tano,kwa kauli yake Mtume (S.a.w)

**لقوله صلى الله عليه وسلم: "ليس فيما دون خمس أواق صدقة"، متفق عليه**

"Hakina (wajibu za zaka) chini ya waqia tano"Mutafaqun alayhi. Na kiwango chake kwa kuhesabu ni Dirham Mia

mbili,kwa sababu kila waqia moja ni Dirham Arubaini,Toka kwa Ally Bin Abi Twalib amesema :-

**عن علي بن ابي طالب قال: "وفي كل مائتي درهم خمسة دراهم".**

"Na katika kila Dirham mia mbili (zaka yake ni ) Dirham tano".ameipokea abu ubaid.

**وعن محمد بن عبد الرحمن الأنصاري أن في كتاب رسول الله صلى الله عليه وسلم، وفي كتاب عمر بن الخطاب في الصدقة "والورق لا يؤخذ منه شيء حتى يبلغ مائتي درهم"،**

Na kadhalika imepokelewa toka kwa Muhammad Bin Abdurrahman Al-answary ,kwamba katika barua ya Mtume (S.a.w) na katika barua ya Omar Bin Khatwab katika zaka "Na Fedha haichukuliwi (Zaka) Mpaka ifikie Dirham mia mbili".

Na juu ya haya ikiwa fedha itapungua dirham moja chini ya dirham mia mbili basi si wajibu kutoa zaka,kwa sababu itakuwa ipo chini ya waqia tano,na Mtume (S.a.w) Hakuwajibisha kutoa zaka kwa kile kilichopo chini ya waqia tano.

Na Dirhama ambayo inazingatiwa kuwa ndio Nisabu,Ni dirham ya kisheria ambayo kila kumi katika hizo zinakuwa sawa na uzito wa Mithqali saba kwa uzito wa dhahabu,na kila Dirham katika hizo inakuwa sawa na sehemu ya saba ya kumi ya mithqali(Uzito), na hiyo ndio Dirham ya kisheria ambayo hukadiriwa kwayo katika Nisabu za zaka na viwango vya Jiz'yah na Dia (Fidia) ,na kiwango (Nisabu) ya kukata katika wizi,na yasiokuwa hayo.

Na kiwango cha Dirham kwa gharama zinazotumika hivi ni sawa gm 2.975 na juu ya haya inakuwa nisabu ya zaka ya fedha – ambayo ni dirham mia mbili – ni gm 595.

Na inaukusanywa hapa fedha iliofuliwa kuwa hela na nyinginezo,katika fedha(Tibru) au zilizofuliwa, na ikiwa fedha imeghushiwa kwa kuchanganywa na shaba,au risasi au madini mengine na ile safi ikiafikia kiwango cha Nisabu ya fedha itakuwa ni wajibu kutoa zaka na itatolewa kwa kiwango cha fedha halisi.

## KIWANG CHA WAJIBU KATIKA NISABU YA FEDHA KATIKA ZAKA

Pindi fedha ikifikia kiwango cha zaka na ikapitiwa na mwaka,ni wajibu humo kutoa robo ya moja ya kumi,yaani ni wajibu kutoa Dirham tano katika Nisabu ambayo ni Dirhama mia mbili,na limethibiti hilo kwa sunnah.

**عن أبي بكر الصديق عن النبي صلى الله عليه وسلم انه قال: "في الرقة ربع العشر" والرقة الفضة المضروبة.**

Toka kwa Abubakar Swiddiq,toka kwa Mtume (S.a.w) amesema "Katika Fedha (zaka yake ni )robo ya moja ya kumi" na Riqqah ni fedha iliofuliwa.

**وروى البخاري قول النبي صلى الله عليه وسلم: "فهاتوا صدقة الرقة من كل أربعين درهماً درهماً، وليس في تسعين ومائة شيء".**

Na amepokea Bukhari kauli ya Mtume (S.a.w) : "Leteni zaka ya Fedha kwa kila Dirham arubaini dirham moja,na wala hakuna kitu katika dirhami mia moja na tisini"

**وعن محمد بن عبد الرحمن الأنصاري أن في كتاب رسول الله صلى الله عليه وسلم وفي كتاب عمر في الصدقة "والورق لا يؤخذ منه شيء حتى يبلغ مائتي درهم"**

Na amepokea abu ubaid toka kwa Muhammad ni Abdurrahmani Al-answar kwamba katika barua ya Mtume (S.a.w) na katika barua ya Omar katika zaka "Na fedha haichukuliwi chochote mpaka ifikie dirham mia mbili"

Na Dirham tano za wajibu katika Nisabu ya zaka ni sawa na gm 14.875 kwa sababu Dirham uzito wake ni sawa na gm 2.975.

**KIWANGO CHA NISABU YA DHAHABU NA KINACHOPASWA KUTOLEWA ZAKA**

Hakika Kiwango cha chini cha Dhahabu ambacho ni wajibu humo kutoa zaka ni Dinar Ishirini,ikiwa itapungua chini ya Dinar Ishirini Dinar moja hata kama ni qirat moja si wajibu kutoa zaka.

**عن علي بن أبي طالب قال: " في كل عشرين ديناراً نصف دينار، وفي كل أربعين ديناراً "**

Toka kwa Ally bin Abi twalib amesema "katika kila Dinar Ishirini kuna nusu dinar(Ya zaka)"Ameipokea Abuubaid.

**وعن عمرو بن شعيب عن أبيه عن جده عن النبي صلى الله عليه وسلم قال:"ليس في أقل من عشرين مثقالاً من الذهب صدقة".**

Na toka kwa Amr bin Shuayb toka kwa baba yake toka kwa babu yake toka kwa Mtume (S.a.w) amesema :"Hakuna zaka chini ya Mithqal Ishirini za Dhahabu"

Na itaunganishwa dhahbu baadhi yake kwa baadhi,sahihi na ile yenye kasoro,ilifuliwa na isiofuliwa(mchanga) na ilichongwa na yote itahesabiwa yote hisabu moja.
Ama kile cha wajibu katika Nisabu ya Dhahabu katika zaka ni Robo Dinar,yaani nusu Dinar katika Nisabu ambayo ni Dinar Ishirini,na Dinar moja katika Dinar arubaini kwa ushahidi wa hadithi zilizopita.
Na kile kitakachozidi katika nisabu ya dhahbu na fedha hakika hicho kitakuwa kwa hesabu yake,yaani katika Robo ya Moja ya kumi kwa vyovyote vile itakavyokuwa ziada ni nyingi,au kidogo,nah ii inatofautiana na hukmu ya  Mifungo kwa sababu humo kuna ziada  baina ya hesabu mbili,ziada kati ya Nisabu mbili haina zaka humo,ama dhahabu na fedha kwa kila ziada juu ya Nisabu humo inapaswa kutolewa zaka na wala hamna isipokuwa Nisabu moja,na kile kitakachozidi katika Nisabu Kinachukuwa Hukmu ya Nisabu,na kinachozidi juu ya Nasabu kinachukuwa hukmu ya Nisabu na kinatolewa zaka yake,yaani inachukukiwa humo robo ya Ush'ru(Moja ya kumi).
Ama uzito wa Nisabu ya Dhahabu ambao ni Dinar Ishirini ni gm 85 za dhahabu,na hakika  uzito wa Nusu ni Dinar ya wajibu katika Nisabu ya Dhahabu ni gm 2,125 za dhahabu kwa sababu uzito wa dinar ya dhahabu ni gm 4,25.
Na wala si wajibu kutoa zaka katika Nisabu ya dhahabu na fedha mpaka ipitiwe na mwaka mmoja kamili,na ikawa ni Nisabu kamili toka mwanzoni mwa mwaka mpaka mwisho wake.
Amepokea Tirmidhiy toka kwa Ibn Omar amesema "Mwenye kupata mali , Hakuna zaka katika mali mpaka ipitiwe juu yake na mwaka"
**عن عائشة قالت: سمعت رسول الله صلى الله عليه وسلم يقول: " لا زكاة في مال حتى يحول عليه الحول"**
Toka kwa Aisha ( R ) amesema:Nimemsikia Mtume (S.a.w)"Hakuna zaka katika mali mpaka ipitiwe juu yake na mwaka"
Pindi mtu akimiliki mwanzoni mwa mwaka chini ya kiwango cha Nisabu ya dhahabu au fedha,kisha akapata mali ya

kukamilisha Nisabu kabla ya kumalizika mwaka,hakika mwaka wake unaanza toka wakati wa kukamilisha Nisabu,ikiwa itatimia kupitiwa kwa mwaka itakuwa wajibu kutoa zaka,ama ikiwa Nisabu ya dhahabu au fedha imetimia toka mwanzoni mwa mwaka na ikapatikana ziada katika ya mwaka,ikiwa ziada imetokana na biashara basi itaunganishwa na ile asili,na itahesabiwa mwaka wa ziada sawa na ule mwaka wa asili,kwa sababu ile ziada imekuwa imetokana na kukuwa kwa mali na jinsi yake imekuwa ikifuata hiyo.

Ama ikiwa ziada ni katika jinsi ya Nisabu,lakini imetoakana si kwa njia ya kukuwa kwa mali kama vile imepatikana kwa Mirathi au zawadi,basi ziada hii ni wajibu nayo ipitiwe na mwaka kamili,na wala hainganishwi na ile asili na wala haichukuwi hukmu ya mwaka wake,na kadhalika itakaopkuwa ziada si jinsi ya mali,kama vile akapata ziada ya mifugo,kwa hakika haviunganishwi havikusanywi katika mali yake ya asili dhahbu na fedha,na hapana budi ipitiwe na mwaka kamili mpaka iwajibikiwe kutolewa zaka ikiwa imefikia Nisabu.

Na wala haikamishwi Nisabu ya Dhahabu kwa Fedha na wala Nisabu ya fedha kwa Dhahamu,kwa sababu hizo ni ainambili tofauti,kama vile haikamishwi nisabu ya tende kwa zabibu,na nisabu ya ngamia kwa ng'ombe,kwa sababu hadithi inasema :

" ليس فيما دون خمس أواق صدقة"

"Hakuna zaka chini ya waqia tano"

Na kwa sababu Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) amefanya hivyo ni jinsi mbili tofauti,na akaruhusu kuzidiana baina ya hivyo katika muamalati wa kubadili.

## ZAKA KATIKA HELA ZA KA KARATASI

Hela za makaratasi[Noti] ni karatasi za mali ambazo hutolewa na Dola,na huzifanya na hela zake,huthamiwa kwazo thamani ya vitu vinavyonunuliwa,na malipo ya huduma mbali mbali,na

hela hizi za karatasi zaka yake inakuwa kama zaka ya dhahabu na fedha,na inapitiwa juu yake hukumu za zaka kwa mujibu wa hali yake,na hali hii inaonekana katika aina tatu,nazo :-

1- Hela zaa karatasi za niaba,nazo ni karatasi(Noti) hela zinatolewa na Dola (hela)ambazo zinakweenda kwamfumo wa malipo ya madini,zinalingana na kiwango maalum cha dhahabu,au fedha,na zinakuwa ni niaba yake katika mzunguruko,na zinatumika wakati haja,na karatasi hizi za niaba zinahesabika ni dhahabu au fedha,kwa sababu katika wakati wowote zinabadilishwa kuwa dhahbu au fedha,na inakuwa zaka yake ni ya dhahabu na fedha,basi ikiwa ni niaba ya dhahabu na zikafikia kiwango kinachofanana na dhahabu dinar ishirini –yaani gm 85- na ndio Nisabu ya Dhahabu,ni wajibu kutoa zaka wakati inapopitiwa na mwaka,na ni wajibu kutoa humo Robo ya Ush’ru,na kama zitakuwa ni niaba ya fedha,na zikifikia kiwango ,na zikafikia kiwango kinachofanana cha fedha Dinar mia mbili –yaani gm 595 – na ndio nisabu ya fedha,ni wajibu humo kutoa zaka wakati inapopitiwa na mwaka na ni wajibu humo kutoa Robo ya Ush’ru.na dalili ya uwajibu wa zaka humo ni hadithi zilizotangulia juu ya uwajibu zaka katika dhahbu na fedha kwa sababu ni niaba,na ni wakala wa dhahbu na fedha,na naibu na wakili anachukuwa hukmu ya asili.

2- Hela za karatasi wathiqa(Hati zilizothibishwa au Cheki),nazo ni hela za karatasi zinatolewa na dola ,au moja ya benk zilizothibishwa ambazo zinapewa na dola haki ya kutolewa(kutumika) na zinakuwa na mfuniko(Utepe ,Alama maalum) wa dhahbu au fedha kwa kiwango maalum,thamani ya karatasi hizi ni jina,lenye hadhi kwa dola,au benk ambayo iliotoa dhamana yake,na

Yule aliotoa anachukua ahadi ya kulipa /kutoa thamani yake ya dhahabu au fedha itakayofunika na kukidhi kwa Yule alieichukuwa,na unakuwa utepe wake si kamili ,bali ni kwa kiwango maalum cha thamani yake,yaweza kuwa ni robo tatu au theluthi mbili au nusu au kwa kiwango cha asili mia maalum.

1- Na karatasi hizi zilizothibitishwa zinahesabika ni karatasi niaba ya dhahabu au fedha,kwa sababu wakati wowote zinabadilishwa kwa hizo,na inakuwa zaka yake ni kama zaka ya dhahabu na fedha,na ikiwa imefunikwa kwa dhahabu,na ikawa kifuniko(utepe) wake ni nusu ya kima chake kwa jina mfano, ni wajibu humo kutoa zaka pindi ikifikia Dinar arubaini,na zikafikiwa na mwaka,na inakuwa zaka yake ni katika jinsi yake,na ikiwa haikufikia Dinar arubaini basi hamna zaka humo,kwa sababu inakuwa ni chini ya Nisabu.na ikiwa imefunikwa na (Stika) ya fedha,na ikawa mfuniko wake ni nusu ya thamani yake kijina kwa mfano,ni wajibu humo kutoa zaka pindi ikifikia Dirham mia nne,na zikapitiwa na mwaka,na inakuwa zaka yake ni Dirham kumi toka jinsi yake,na ikiwa itapungua Dirham moja katika mia nne hamna zaka humo,kwa sababu inakuwa ni chini ya nisabu ya fedha.

Na dalili ya uwajibu wa zaka katika hizo ni hadithi hizo hizo zinazojulisha juu ya uwajibu wa kutoa zaka katika dhahabu na fedha,kwa sababu hizo karatasi ni naibu na wakala wa dhahabu na fedha katika kiwango kilichochapwa kwa thamani yake kijna,na ambayo imewajibika humo kutoa zaka,na naibu na wakili anachukuwa nafasi ya asili.

2- Hela za karatasi za kulazimisha,nazo ni karatasi za hela ,zinatolewa kwa kanuni ya dola na inaziingiza katika mzunguruko wa hela,na dola inazifaanya ni hela zinazofaa

kuwa ni thamani ya vitu,na malipo ya huduma na manufaa,lakini hazibadilshwa kwa thamani ya dhahabu na fedha na wala hazina chapa ya dhahabu wala fedha na wala hazidhaminiwi hata kwa tahadhari kwa dhahabu au fedha au hela nyingine zinafunika,na wala hazina karatasi (noti ) hizi thamani yeyote isipokuwa thamani ya kanuni ya dola.

Lakini zama ilipokuwa hela hizi ni za kulazimisha ,imewekwa istlahi kuwa hizi ni hela na thamani ya vitu,na ni malipo kwa kupata manufaa na huduma,na kwa hizo hununuliwa dhahabu na fedha,kama vile ambavyo hutumika kununuliwa bidhaa na vitu,basi zitakuwa imethibitika kwake kuwa ni hela na zenye thamani na ni kitu ambacho kipo katika dhahabu na fedha,zilizofuliwa na kuwa Dinar na Dirham.

Kwa sababu dalili zilizopokelewa katika zaka ya dhahabu na fedha zipo aina mbili:-

Mosi :kuna dalili zimetaja moja kwa moja juu ya dhahabu na fedha kama majina ya Jinsi,yaani katika vitu vya dhahabu na fedha nayo ni majina Jamidah (Yasiotoholeka) haifai kutolea sababu,haifanyiwi kiyasi,kwa sababu hii hakuna zaka katika madini mengine kama vile chuma ,shaba ,nk.

Amepokea Abu hurairah kwamba Mtume (S.a.w) amesema :-

**فما روى أبو هريرة قال: رسول الله صلى الله عليه وسلم: "ما من صاحب ذهب، ولا فضة لا يؤدي منها حقه، إلا إذا كان يوم القيامة صفحت له صفائح من نار، فأحمى عليها في نار جهنم، فيكون بها جنبه وجبينه وظهره، كلما بردت أعيدت له، في يوم كان مقداره خمسين ألف سنة حتى يقضى بين العباد، فيرى سبيله إما إلى الجنة، وإما إلى النار" رواه الخمسة إلا الترمذي.**

amesema Mtume (S.a.w) ""Hakuna Mtu yeyote Mwenye Dhahabu,wala Fedha hatoe zaka haki yake isipokuwa ikifika siku ya kiama itatengenezwa(Dhahabu na Fedha na kuwa ) sahani za moto,zitaokwa katika moto wa Jahannamu,atapigwa pasi kwazo mbavuni mwake na usoni mwake na mgongoni mwake,kila mara zinapopoa hurejeshwa tena katika siku ambayo kiwango chake ni miaka

khamsini,mpaka pahukumiwe baina ya waja,basi ataona njia yake,ima kwenda peponi au kwenda motoni."Wameipokea wapokezi watano isipokuwa Tirmidhii.

Limepokelewa tamko/neno la dhahbu na fedha nayo ni majina Jamidah hayafanyiwi sababu(Hayatoholewi)

Pili :Dalili zinazotamka juu ya uwajibu wa kutoa zaka ya dhahabu na fedha zikiwa kama ni hela ambazo watu wanatumia ikiwa na thamani ya vitu na malipo,na hadithi hizi zinaweza kuchukuliwa humo sababu(Kutohowa) nayo ni kule kuwa hela ya kulipia vitu,basi inakisiwa kwa hizi hela za kulazimisha kwa kuhakika sababu hii humo,na hutekelezwa humo hukmu za zaka ya hela kwa mujibu wa kile kinacholingana nacho katika soko la dhahabu au fedha.

**عن علي بن أبي طالب ( ر ) عن النبي – ص – قال : إذا كانت لك مئتا درهم , وحال عليها الحول , ففيها خمسة دراهم , وليس عليك شيئ – يعني في الذهب – حتى يكون ذلك عشرون دينارا ,وحال عليها الحول , ففيها نصف دينار " رواه أبو داود**

Toka Ally bin Abi Twalib (R ) Toka kwa Mtume (S.a.w) amesema :-

"Ukiwa una Dirham mia mbili,na zikapitiwa na mwaka,basi humo mna Dirham tano za zaka,na wala hupaswi chochote juu yako – yani katika dhahabu – mpaka uwe na Dinar Ishirini,Ukiwa una Dinar Ishirini ,na zikapitia na mwaka basi humo mna nusu Dinar ya zaka" Ameipokea Abu Daud

**( في كل عشرين دينارا نصف , وفي أربعين دينارا دينار )**

Kama vile imepokelewa tena kwa Ally (R ) "katika kila dinar ishirini nusu dinar,na katika kila Dinar arubaini Dinar moja"

**وعن علي ( ر ) قال : قال رسول الله – صلى الله عليه وآله وسلم - ..... هاتوا صدقة الرقة , في كل أربعين درهما, درهما وليس في تسعين ومئة شيئ ,فإذا بلغت مائتين ففيها خمسة دراهم ) رواه البخاري وأحمد .**

Na toka kwa Ally ( R ) amesema : amesema Mtume (S.a.w) ….Leteni zaka ya fedha ,katika kila dirham arubaini dirham moja,na wala hakuna zaka katika mia moja na tisini,na pindi ikifika mia mbili basi humo mna dirhama tano (za zaka) kaipokea Bukhar naAhmad.

**(...... والورق لا يؤخذ منه شيئ حتى يبلغ مئتي درهم )**

Kama alivyopokea Abdurrahmani Al-answary katika barua ya Mtume (S.a.w) na barua ya Omar (r ) katika zaka (…../ na

fedha haichukuliwi humo chochote mpaka ifikie dirham mia mbili.) kaipokea Abu ubaid

Hadithi hizi zimeonyeshajuu ya kutumika(Naqdi) na thamani,kwa sababu matamko ya riqqah (fedha) pamoja na kiambatanisho ( Katika kila Dirham arubaini )na maneno wariqu,dinar na dirham na maneno yanayotumika kutoa maana ya dhahabu na fedha zilizochapwa na kufuliwa,yaani ambayo ni hela na thamani,na kuyatumia maneno haya inaamanisha kuwa kutumika na thamani ndiko kulikokusudiwa katika hadithi hizi,na kwa hizo kumehusiana na hukmu nyingi za kisheria,kama vile zaka,fidia na kafara na kukata kwa mwizi na hukmu nyingine.

Na kwa kuwa karatasi (Noti) hizi la kulazimisha imehakika humo kutumia/kulipa na thamani,basi zinakuwa zimekusanywa na hadithi za uwajibu wa zaka katika dhahabu na fedha,ni wajibu humo kutoa zaka ,kama ilivyokuwa ni wajibu katka dhahabu na fedha,na zitakadiriwa kwa dhahabu na fedha,basi yeyete mwenye kuwa na hizi karatasi za lazima zinazofikia thamani ya dinar ishirini za dhahabu – yaani gm 85- na ndio Nisabu ya dhahabu,au akiwa ana kiasi kinacholingana na thamnai ya dirham mia mbili za fedha – yaani gm 595 za fedha- na zikapitiwa na mwaka,ni wajibu humo kutoa zaka na ni wajibu humo kutoa Robo ya Ush'ru yake.

Na atatoa dhahabu kwa dhahabu,na kwa makaratasi yalioniaba na makaratasi ya hati,na atataoa zaka ya fedha kwa fedha na makaratasi ya niaba na yati,kama vile inatosheleza kutoa zaka ya dhahabu kwa fedha na kwa makaratasi ya lazima,na fedha kwa dhahabu na kwa makaratsai ya lazima,kwa sababu zote ni hela na thamani inatosheleza baadhi yake kwa baadhi ,na inajuzu kutoa baadhi yake kwa baadhi kwa kule kuhakika lengo katika hilo,na imeshapita katika mlango wa zaka ya mazao na matunda dalili za kuchukuwa thamani badala ya kitu chenyewe kilichowajibishwa kutoa zaka.

ZAKA YA BIDHAA ZA BIASHARA

Bidhaa za Biashara:Ni kila kitu kisichokuwa vito kinafanywa kwa ajili ya Biashara kwa kitu hicho kwa kuuza au kununua kwa makusudio ya kupata faida,miongoni mwa vyakula,mavazi,matandiko,vitu vya kutengenezwa,na wanyama,madini,ardhi ,majengo na vinginevyo katika vile ambavyo huuzwa na kununuliwa.

Na bidhaa za biashara ambazo zinafanya kwa ajili ya biashara ni wajibu humo kutoa zaka pasina tofauti kati ya maswahaba,

**عن سمرة بن جندب قال:" أما بعد فإن رسول الله صلى اله عليه وسلم كان يأمرنا أن نخرج الصدقة من الذي نعد للبيع" رواه أبو داود.**

Toka kwa Jundubi bin Junada amesema : "Ama baad,hakika ya Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) alikuwa anatuamrisha kutoa zaka kwa vile ambavyo tunavihesabu kwa ajili ya biashara" kaipokea Abu daud.

**وعن أبي ذر عن النبي صلى الله عليه وسلم قال: " وفي البز صدقته"**

Na toka kwa Abu dhari,toka kwa Mtume (S.a.w) amesema :"Na katika Nguo na vitambaa kuna zaka"kaipokea Daru Qutniy na Baihaqii.

Buzzu: Ni nguo na vitambaa ambavyo hufanyiwa biashara,

**وعن أبي عمرة بن حماس عن أبيه قال:" مر بي عمر بن الخطاب، فقال: يا حماس أد زكاة مالك، فقلت مالي ممال إلا جعاب، وأدم، فقال: قومها قيمة ثم أد زكاتها"**

Na toka kwa Abu Umrah bin Hammas toka kwa baba yake amesema :alipita Umar Bin Khatwab akasema :Ewe Hammas Toa zaka ya mali yako,nikasema Sina mali isipokuwa (nauza) viriba vya kuhifadhia mikuki na mishale na ngozi,akasema : Vithamini kisha toa zaka yake.

**وعن عبد عبد الرحمن بن عبد القارئ، قال" كنت على بيت المالزمن عمر بن الخطاب، فكان إذا خرج العطاء جمع أموال التجار ثم حسبها، شاهدها وغائبها، ثم أخذ الكاة من شاهد المال على الشاهد والغائب"**

Toka kwa Abdurrahmani Bin Abdulqari amesema : "Nilikuwa (nafanya kazi ) katika Baitil-mali zama za Omar Bin Khatwab alikuwa anapotoa sadaka/zaka anakusanya mali za wafanya biashara kisha anazihesabu,zilizokuwepo

na zisizokuwepo kisha anachukuwa ……..kwa shahidi wa mwenye mali kwa alieopo na asiyekuwepo”

**وعن ابن عمر، قال: "ما كان من رقيق أو بز يراد به التجارة ففيه الزكاة"**

Na toka kwa Ibn Omar amesema : “Watumwa wowote wanakaokuwa au Mafurushi ya Nguo wanaokusudiwa Biashara basi humo mna zaka “

Na kwa hakika imepokelewa uwajibu wa kutoa zaka katika Biashara toka kwa Omar,na Mtoto wake na Ibn Abbas ,na Mafuqahaa saba,na Alhassan.na Jabir,na Twaus ,na Annakhay.na Atthaury na Al-awzay,na Shafiiy ,na Ahmad,na Abu ubaid na As’habur ra’ay(Watu wa Rai),na Abu hanifah ,na wengineo.

Na ni wajibu kutoa zaka katika Bidhaa za Biashara pindi thamani yake ikifikia thamani ya Nisabu ya Dhahabu au Nisabu ya Fedha,na zikapitiwa na mwaka.

Pindi akianza mfanya biashara biashara yake kwa mali chini ya Nisabu,na mwishoni mwa mwaka ikawa mali imefikia Nisabu,basi itakuwa si wajibu juu yake kutoa zaka kwa sababu Nisabu yake haijafikiwa /haijazungurukiwa na mwaka,na itakuwa ni wajibu kwa Nisabu yake kutoa zaka baada ya kupitiwa juu yake na mwaka mmoja.

Na pindi atakapoaanza mfanya biashara biashara yake kwa mali inayovuka Nisabu kama vile akianza kwa Dinar alf mbili,na mwishoni mwa mwaka ikakuwa biashara yake na ikawa thamani yake ni Dirham alf tatu,itakuwa ni wajibu juu yake kutoa zaka kwa hizo Dinar alfu tatu na wala sio kwa Dinar alf mbili ambao alianzia,kwa sababu kile kilichoongezaka kinafuata kile alichoanzia,na inakuwa juu ya faida iliopatikana na msingi wake hiyo ndiyo yenyewe juu ya ile asili,mfano wa watoto wa mbuzi na watoto wa kondoo kwani wao wanahesabiwa pamoja na mama yao na wanatolewa zaka pamoja,kwa sababu mwaka wao ndio mwaka wa mama zao,kadhalika faida ya mali,mwaka wake huwa ni mwaka wa mali ya asili ambayo ilomletea faida.

Pindi mwaka ukimalizika atathamini mfanya biashara bidhaa zake za biashara sawa zinakuwa ni wajibu juu yake

kutoa zaka kwa vitu vyenyewe kama vile ngamia,ng'ombe,na mbuzi na kondoo,au zitakuwa si wajibu kutoa zaka kwa dhati ya vitu vyenyewe(Mpaka viwe kibiashara) kama vile nguo na vitu vya kutengenezwa ,au mfano wa ardhi na majengo,na vyote vitathaminiwa kwa thamani moja kwa dhahbu au fedha na itatolewa zaka yake robo ya moja ya kumi ikiwa vitafikia thamani ya Nisabu ya Dhahabu,au Thamani ya Nisabu ya Fedha na kitatolewa kile cha wajibu katika zaka yake kwa hela zinazozunguruka,(zinazotumika).

Na inajuzu kutoa zaka yake kutokana na vitu hivyo,ikiwa hilo litakuwa jepesi,navyo ni kama vile Yule anaefanya biashara ya kuuza mbuzi au ng'ombe,au nguo,yeye anaruhusiwa kutoa zaka yakle hela,na anaweza kutoa mbuzi au ng;ombe au nguo,chochote akitakacho katika hivyo.

Na hutolewa zaka bidhaa za biashara ambazo ni wajibu juu yake kutoa zaka katika dhati ya vitu vyenyewe,kama ngamia,na ng'ombe,na mbuzi (kondoo) (hutolewa zaka za )Bidhaa za Biashara,si zaka ya mifugo,kwa sababu ndio iliokusudiwa kwa kuimilii na wala sio ....... alqaniyah

ZAKA YA DENI

Mwenye kuwa na mali iliofikia Nisabu,na ikapitiwa na mwaka,na alikuwa na deni linalomaliza Nisabu,au linafanya kilichobaki baada ya kulipa deni ni kichache kuliko nisabu,basi hamna zaka juu yake,nayo ni kama vile akimiliki Dinar alf moja,na ana deni la Dinar alf moja,au kama vile akiwa anamiliki Dinar arubaini za dhahabu,na ana deni la Dinar thelathini za Dhahabu,basi katika hali hizi mbili hana zaka juu yake kwa sababu anakuwa si mwenye kumiliki Nisabu.

**عن نافع عن ابن عمر قال: قال رسول الله صلى الله عليه وسلم:" إذا كان لرجل ألف درهم، وعليه ألف درهم، فلا زكاة عليه".**

Toka kwa Nafi'I amesema,toka kwa Ibnu Omar amesema,amesema Mtume (S.a.w) "Pindi akiwa mtu ana Dirham alf moja na anadaiwa Dirham alf moja,basi hana zaka juu yake"ameitaja Ibn Qudama katika Mughniy.

Ama ikiwa mali iliozidi baada ya kutoa deni inafikia Nisabu,ni wajibu juu yake kuitolea zaka,kwa dalili iliopokelewa toka kwa

**لما روى عن السائب بن يزيد قال: سمعت عثمان بن عفان يقول: " هذا شهر زكاتكم، فمن كان عليه دين فليؤده حتى تخرجوا زكاة أموالكم. وفي رواية: " فمن كان عليه دين فليقض دينه، وليزك بقية ماله" قال دلك بمحضر من الصحابة فلم ينكروه، فدل ذلك على اتفاقهم.**

Assaib bin Yazid amesema:Nimemsikia Othman Bin Affan akisema: "Huu ni mwezi wa zaka zenu,yeyote mwenye kuwa na deni alitoe mpaka mtoe zaka za mali zenu.na katika mapokezi mengine "Yeyote mwenye kuwa na deni basi na alilipe deni lake,na atoe zaka mali yake iliobaki"kayasema hayo mbele za maswahaba na wala hawakumpinga,likaonesha hilo juu ya kukubaliana kwao.

Na akiwa mtu anadeni ,ikiwa ana uwezo na wala si mwenye kubani akulipa ,na ni katika uwezo wake kulilipa katika wakati wowote,ni wajibu juu yake atoe zaka yake wakati ikipitiwa na mwaka.

**عن عمر بن الخطاب قال:" إذا حلت الصدقة فاحسب دينك، وما عندك، واجمع ذلك كله ثم زكه".**

Toka kwa Omar Bin Khattwab amesema: "Pindi ikifika sadaka,hesabu deni lako,na vile ulivyo navyo na kusanya vyote hivyo na kisha toa zaka yake"

**وعن عثمان بن عفان قال: " إن الصدقة تجب في الدين الذي لو شئت تقاضيته من صاحبه، والذي هو على مليء، تدعه حياء أو مصانعة، ففيه الصدقة"**

Na toka kwa Othman Bin Affan amesema: "Hakika sadaka/zaka ni wajibu kutolewa katika deni ambalo lau ukitaka utalilipa kwa mwenyewe,na lile lililopo kwa mwenye uwezo unaliachakwa kuona haya au kwa kutendeana (Vizuri) basi humo zaka/sadaka itolewe"

**وعن ابن عمر قال:" كل دين لك ترجو أخذه، فإن عليك زكاته كلما حال الحول".**

Na toka kwa Ibn Omar amesema : "Kila deni lako unalotaraji kulichukuwa,basi ni wajibu juu yako kutoa zaka yake kila mara linapopitiwa na mwaka"

Ama ikiwa deni lipo kwa mtu mzito?kaelemewa,au kwa tajiri anayezuia kulipa,si wajibu kwake kutoa zaka yake isipokuwa baada ya kuipokea,ikiwa atapokea/atalipwa atatoa kila cha wajibu humo kwa miaka yote.

**عن علي في الدين الظنون - الذي لا يدري صاحبه أيصل إليه أم لا- قال: " إن كان صادقا فليزكه إذا قبضه لما مضى".**

Toka kwa Ally katika deni linalotarajiwa-Deni ambalo haijulikani kwa mwenyewe litamfikia au hapana- amesema "akiwa ni mkweli basi atoe zake pale atakapolipata kwa ile miaka iliopita"ameipokea Abu Ubaid.

**وعن ابن عباس في الدين قال:" إذا لم ترج أخذه فلا تزكه، حتى تأخذه، فإذا أخذته فزك عنه ما عليه".**

Na pia imepokelewa toka kwa Ibn Abbas kuhusiana na Deni amesema : "Ikiwa hutarajii kupata deni lako basi usitoe zaka,mpaka ulipate,pindi ukipata basi toa zaka yale ya wajibu".

**MAPAMBO**

Mapambo : Ni yale anayojipamba kwayo mwanamke na kujipambia,miongoni mwa dhahabu ,au fedha katika maungio yake au katika shingo yake au katika masikio yake au katika sehemu nyingine katika sehemu za mwili wake.

Na mapambo hayana zaka,sawa yatakuwa yametokana na dhahabu au ya fedha au toka kwa aina nyingine katika aina za vito kama vile Lulu,yakuti ,zabarjadi na aqiqu na mengineyo katika vito vizuri .sawa mapambo na machache au mengi,yamefikia kiwango/Nisab au yamezidi,kwa hakika hamna zaka katika yote hayo,kwa sababu ni kwa ajili ya matumizi,na anayachukuwa mwanamke kwa ajili ya kuvaa na kiujipamba,na wala si kwa ajili ya kulimbikiza,na wala si kwa ajili ya Biashara.

Ikiwa mapambo ni kwa ajili ya Kulimbikiza au kwa biashara,basi humo inapaswa kutoa zaka.

**عن الليث بن سعد بن أبي الزبير عن جابر عن النبي صلى الله عليه وسلم انه قال" ليس في الحلي زكاة".**

Toka kwa Laith bin Sa'ad bin Abii Zubair toka kwa Jabir (R ) toka kwa Mtume (S.a.w) amesema "Hakuna zaka katika mapambo".ameitaja Ibn Qudamah katika Mughniy.

**عن عمرو بن دينار قال: " سئل جابر بن عبد الله: أفي الحلي زكاة" ؟ قال لا، قيل: وإن بلغ عشرة آلاف؟ قال نعم"**

Toka kwa Amr Bin Dinar amesema : "aliulizwa Jabir bin Abdillah :Je kuna zaka katika mapambo ? akasema

Hapana,pakasemwa hata kama yatafikia tahamani ya( Dinar) alf kumi? Akasema Ndio.

**وعن نافع عن ابن عمر " أنه كان يزوج المرأة من بناته على عشرة آلاف، فيجعل حليها من ذلك أربعة آلاف، قال: فكانوا لا يعطون عنها الزكاة".**

Toka kwa Nafi'i ,toka kwa Ibn Omar "kwamba alikuwa anamuozesha mwanamke katika Mabint zake kwa (Dinar) alf kumi, anafanya mapambo yake ni katika hela hizo kwa alf nne,akasema :walikuwa hawatoi zaka yake"

**وعن عبد الرحمن بن القاسم عن أبيه " أن عائشة زوج النبي صلى الله عليه وسلم كانت تلي بنات أخيها يتامى في حجرها لهن الحلي فلا تخرج من حليهن الزكاة".**

Na toka kwa Abdurrahmani Bin Qassim toka kwa baba yake "kwamba Aisha Mkewe Mtume (S.a.w) alikuwa akiwalea Mabint wa kaka yake mayatima katika hifadhi yake,wana mapambo,alikuwa hatoi zaka ya mapambo yao". Ameitoa Maliki katika Muwat'wa.

Ama hadithi ambazo wametolea hoja wale waliosema uwajibu wa kutoa zaka katika mapambo,kwa hakika matamko yake ,Riqa,awaqii na wariqi(Dhahabu na Fedha)na Dinar yaliopokelewa katika hadithi zinazowajibisha kutoa zaka katika dhahabu na fedha,haikusanyi mapambo.kwa sababu matamko haya hutumika katika lugha ya kiarabu juu ya kuamanisha Dirham na Dinar zilizonakishiwa zenye kutumika kwa watu,nazo ni hela ambazo ni thamani ya vitu,na malipo ya huduma na manufaa,na mapambo na vinginevyo,na lau yangekuwa matamko ya hadithi kwa msemo "pindi ikifikia fedha kiasi kadha basi yapasa kiasi kadha basi mapambo yangekuwa yanakusanywa kwa tamko la Fedha,isipokuwa matamko ya hadithi yamekuja kwa tamko la Riqah,wariqi ,waqiyah na dinar na yote hutumika kwa vile vilivyofuliwa katika fedha na dhahbu na kuwa fedha/hela na mapambo si katika hivyo.

Na hadithi hizi zinahusisha(Zinafunga maana yake ) na hadithi ami( Ya kiujumla)

**" ما من صاحب ذهب ولا فضة لا يؤدي منها حقا إلا إذا كان يوم القيامة صفحت له صفائح من نار".**

“Hakuna mwenye dhahabu wala fedha na wala hatoe zake isipokuwa itakapofika siku ya kiama itatengenezwa vipande vya sahani za moto…”

Ama hadithi ya Amru Bin Shuaib ambayo amepokelewa humo “Kwamba Mwanamke alimuendea Mtume (S.a.w) akiwa na Bint yake mkononi mwake mna Bangili mbili za dhahabu,akasema :Unatoa zaka ya hizi? Akasema Hapana,akasema :hivi inakufurahisha Mwenyezi Mungu akuvishe bangili mbili za moto….”

Hadithi hii,amesema Abu Ubaid : “Hatuijui inapokelewa isipokuwa kwa njia moja kwa Isnad wameizungumizia watu zamani na sasa,basi ikiwa jambo kama lilivyopokelewa na alikuwa Mtume (S.a.w) ameihifadhi,huenda ikawa maana yake ikawa amekusudia zaka ya “Cha kuazima” kama walivyotafsiri wanazuoni ambao tumewataja akiwemo :Said bi Musayyab,na Sha’abii na Alhasan na Qatada katika kauli yao : ni zaka ya A’ariyah (Chenye kuazimwa),na lau ingekuwa ni zaka katika mapambo ni faradhi kama vile ufaradhi wa fedha basi ingekuwa inaenea katika sadaka zote ulimwenguni miongoni mwa vitabu vyake na suna zake “

Amesema Tirmidhiy : “Haijasihi katika mlango huu kitu chochote”.

Ama yale yaliopokelewa toka kwa Aisha katika kauli yake :

**عن عائشة من قولها:"لا بأس بلبس الحلي إذا أعطيت زكاته"**

”Hakuna ubaya kuvaa mapambo ikiwa utatoa zaka yake”

**وقول النبي صلى الله عليه وسلم عندما رآها تلبس فتخات من ورق أي خواتيم كبيرة" هي حسبك من النار"**

Na kauli ya Mtume (S.a.w) wakati alipomuoina anavaa pete kubwa za fedha “hizo zatosha kukupeleka motoni”

Hakika hizo zinachukuliwa kama ilivyochukuliwa hadithi ya Amru bin Shauaib,na hasa hasa kwamba Aisha imepokelewa kwake yale yanayopingana na hayo,

**فقد روى ابن أخيها القاسم بن محمد " ما رأيت عائشة أمرت نساءها ولا بنات أخيها"**

Amepokea mototo wa kaka yake Qassim bin Muhammad “Sikumuona Aisha akiamrisha wanawake wenzake na mabint wa kaka yake(Kutoa zaka ya mapambo”

Na alikuwa akiwapamba mabint wa kaka zake kwa dhahabu na fedha,na wala hatoe zaka yake,na hadithi ya Aisha juu ya pete kubwa ya Fedha,imepokelewa kwa njia ya Yahya bin Ayyub naye ni dhaifu.na hii zaidi ya kuwa pete za fedha haiwezekani uwe uzito wake ni uzito wa Nisabu ya fedha mpaka iwe wajibu kutoa zaka na wala haijapitiwa na mwaka.haya ndio yanatilia nguvu udhaifu wa hadithi hii.

Na ama hadithi ya vidani iliopokelewa toka kwa ummu salama,kwa hakika imepokelewa kwa njia ya Utabu naye ni Maj'hul(Hajulikani hali yake)

Ama hadithi ya Abdulah bin Omar kwamba yeye alikuwa akitoa zaka ya mapambo ya Mabint zake, kwa hakika katika isnadi yake kuna maneno mengi kama ilivyosemwa katika isnadi ya Amru bin Shuaib iliotajwa hapo nyuma.

Na ameonelea juu ya kutokutoa zaka ya mapambo Ibn Omar na Jabir na Anas na Aisha na Asmaa na msimamo huu ameusema Alqasim,na Sha'abii na Qatada na Muhammad bin Ally na Malik na Shafii na Ahmad na Abu Ubaid na Is'haqa na Abu Thaur.

Hii ni katika mapambo ambayo anayachukuwa mwanamke,ikiwa atayachukuwa mwanamme kwa ajili ya kuyatumia yeye,ni haramu juu yake na ni wajibu atoe zaka,ama akiyachukuwa si kwa ajili ya matumizi yake yeye,bali awape au awaazime wake zake,au mabint zake au wa watu wengine ,hamna zaka juu yake,kwa sababu yanakuwa ni ajili ya matumizi yaliruhusiwa,na wala hakuna madhambi juu yake katika hilo, na ikiwa atayachukuwa mapambo kwa ajili ya biashara basi ni wajibu juu yake kutoa zaka.

## <u>KUMPA ZAKA KHALIFAH</u>

Hutolewa zaka sawa itakuwa ni mifugo,mimes na matunda,au vito na bidhaa za biashara kwa Khalifah au wale wanaomuwakilisha miongoni mwa ma-wali na ma-umali ,au Yule anateuliwa katika wakusanyaji zaka na wanaofanya kazi ya kukusanya sadaka.

Amesema:Mwenyezi Mungu Mtukufu :

( خذ من أموالهم صدقة تطهرهم وتزكيهم بها، وصل عليهم إن صلاتك سكن لهم).

"Chukua sadaka katika mali zao,uwasafishe kwa ajili ya hizo (sadaka zao) na kuwataja kwa vizuri (Mbele yangu) na uwaombee dua .Hakika kuwaombea kwako kutawapa utulivu (watengenekewe) na Mwenyezi Mungu ndiye asikiaye na ajuaye" TMQ 9:103

Hakika Mwenyezi Mungu kamuamrisha Mtume wake katika ayah ii achuku sadaka kwa wenye mali,na alikuwa Mtume (S.a.w) akiteua miongoni mwa ma-wali na ma-umali na wakusanyaji zaka kwa wenye mali ,kama vile Mtume (S.a.w) aliteua wahesabuji ili wakahesabu mitende na zabibu,na walikuwa watu wakati wa Mtume (S.a.w) wakimpa zaka yeye (S.a.w) au kwa wale aliowateua miongoni mwa ma-wali na ma-umali na wakusanyaji wa zaka,na hali hii (Utaratibu huu) uliendelea baada yake,siku za ukhalifah wa Abubakar na Omar na Othaman na Ally na wa baada yao.

Amepokea Abu Ubaid toka Ibn Siirin amesema : "Zaka ilikuwa akipewa Mtume (S.a.w) au kwa Yule aliyeamrishwa apewe,na kwa Abubakar au Yule aliyeamrisha apewe,na kwa Omar au Yule aliyeamrisha apewe,na kwa Othman au kwa Yule aliyeamrisha apewe,alipouawa Othman walitofautiana ,wakawa miongoni mwao wanawapa wao(makhalifah) na wengine walikuwa wakiigawa,na alikuwa miongoni mwa wanaowapa bila kugawa ni Ibn Omar"

Na anapewa zaka Khalifah au Yule anaemteua miongoni mwa ma-amir,na ma-wali na ma-umali na wakusanyaji,hata kama watakuwa ni madhalimu,muda wa kuwa hukmu ya Uislamu ndio inayotekelezwa,na hata kama kuna makosa katika utekelezaji.

عن سهيل بن أبي صالح عن أبيه قال: " سألت سعد بن أبي وقاص، وأبا هريرة، وأبا سعيد الخدري، وابن عمر، فقلت: إن هذا السلطان يصنع ما ترون، أفأدفع زكاتي إليهم؟ قال: فقالو كلهم: ادفعها إليهم". وعن أبن عمر قال: "ادفعوها إلى من ولاة الله أمركم، فمن بر فلنفسه، ومن أثم فعليها".

Toka kwa Suhail bin Abi swaleh toka kwa baba yake amesema :"Nimemuuliza Sa'ad bin Abi waqqas na Abu

hurayrah na Abu said Al-khudriy na Ibn Omar ,nikasema :Hakika mtawala huyu anafanya mnavyoviona,je nimpe zaka yangu?akasema : wote wakasema :Mpe ,na toka kwa Ibn Omar amesema "Wapeni zaka watawala wenu wale Mwenyezi Mungu aliwapa usimamizi wa mambo yenu,Mwenye kufanya wema ni kwa ajili yake na Mwenye kufanya madhambi ni kwa ajili ya nafsi yake"

Na kwa hakika zimepokelewa Riwaya kwa maswahaba na taabiina za kuruhusu mtu yeye mwenyewe kusimamia kugawa zaka na kuiweka sehemu yake katika mali zilizokimya,yaani ,.

**فقد روي أي كيسان جاء لعمر بمائتي درهم صدقة، وقال له: " يا أمير المؤمنين، هذه زكاة مالي"، فقال له عمر: فاذهب أنت بها فاقسمها"**

Amepokea Abu ubaid kwamba Kaisana alikuja kwa Omar na Dirham mia mbili za sadaka,akamwambia :Ewe Amir wa waumini,hii ni zaka ya mali yangu,akasema Omar : Nenda nayo wewe ukaigawe"

Kama vile alivyopokea Abu Ubai toka kwa Ibn Abbas kauli yake

**" إذا وضعتها أنت في مواضعها، ولم تعد منها أحدا تعوله شيئا فلا بأس"**

"pindi utakapoiweka wewe sehemu yake,na wala hukumhesabia yeyete unayemhudumia (Hukumpa chochote) hakuna ubaya"

Kama ilivyopokelewa toka kwa Ibrahim na Al-hassan wamesema :

**عن إبراهيم والحسن قالا: " ضعها في مواضعها، واخفها"**

"iweke sehemu yake, na Ifiche " hii ni katika swamit(yenye kunyamaza) yaani katika hela.

Ama mifugo na mazao na matunda hapana budi apewe khalifah,au Yule anaemteua,Abuubakar kawaua wenye kuzuia zaka wakati walipokataa kuwapa zaka ma-wali na wakusanyaji aliowateua,na akasema

**" والله لو منعوني عناقا كانوا يؤدونه إلى رسول الله لقاتلهم عليه".**

"Wallah ikiwa watazuia kunipa kamba ya kufungia mbuzi waliokuwa wakimpa Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) basi ningaliwapiga kwa hiyo"Mutafaqun alayh kwa njia ya Abu huraiarah.

Na Mustahabu kwa anaechukuwa amuombee dua mtoaji kwa kusema :-

" آجرك الله فيما أعطيت، وبارك لك فيما أنفقت، وجعله له طهورا"

"Akulipe Mwenyezi Mungu Ujira kwa ulichokitoa,na akupe baraka katika ulichokitoa na akifanye ni kisafi"

Hata kama mtoaji anampa Khalifah au Yule aliyeteuliwa,amuombee dua mtoaji ,amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu : -

( خذ من أموالهم صدقة تطهرهم، وتزكيهم بها، وصل عليهم، إن صلاتك سكن لهم).

"Chukua sadaka katika mali zao,uwasafishe kwa ajili ya hizo (sadaka zao) na kuwataja kwa vizuri (Mbele yangu) na uwaombee dua .Hakika kuwaombea kwako kutawapa utulivu (watengenekewe) na Mwenyezi Mungu ndiye asikiaye na ajuaye" TMQ 9:103

Toka Abdullah bin Abi Aufah amesema :Baba yangu alikuwa ni katika watu wa kwenye mti,na alikuwa Mtume (S.a.w) pindi watu wakimletea sadaka zao ,husema :"Ewe Mwenyezi Mungu Waingize katika rehma zako familia ya Fulani,basi baba yangu akamletea sadaka yake,akasema :Ewe Mwenyezi Mungu waingize katika rehma zako Familia ya Abi aufaha" Muttafaqun Alayh.

HUKMU YA MWENYE KUZUIA ZAKA

Pindi muislamu atakapomiliki Nisabu,katika mali ambazo ni wajibu kutoa zaka,ni wajibu juu yake atoe kile cha wajibu humu katika zaka,ikiwa atakataa kutoa atapata madhambi makubwa mno,kama ilivyopita katika hadithi zilizopokelewa juu ya maudhui ya mali za zaka,ambazo zinashadidia kupinga juu ya wale ambao hawatekelezi zaka za mali zao.

Na anaekataa kutoa zaka itaaliwa wakia/hali yake,ikiwa alikataa kutoa zaka kwa ujinga wa kutokujua ulazima wake,kwa sababu watu mfano mara nyingi hawajui,atafahamishwa uwajibu wake ,na wala hatakufurishwa na wala hata adhibiwa ,kwa sababu amesameheka(Ana udhuru) itachukuliwa zaka yake.

Na ikiwa atakataa kutoa zaka kwa kupinga uwajibu wake,basi ni Murtadi na atafanyiwa kama wanavyotendewa walioritadi,atatakiwa atubie kwa muda wa siku tatu,ikiwa atatubuia na kurejea kwaMwenyezi Mungu,itachukuliwa zaka yake na ataachwa,na kama si hivyo atauwa,kwa sababu uwajibu wa zaka ni kitu kinachojulikana katika dini kwa dharara(kila mtu anakijua) na dalili za uwajibu wa zaka ziko wazi katika kitabu na sunnah na Ij'mai,na zinakurubia hazifichiki kwa muislamu yeyote Yule.

Na ikia atakataa kutoa zaka na hali ya kuwa anaamini uwajibu wake,itachukukuliwa kwake kwa nguvu,na ikiwa atakataa kundi moja litakataa kutoa zaka kwa Dola,na wakakataa kutii katika uwajibu kwa kutoa zaka,na wakajizuia mahala Fulani na kujiweka hapo ,Dola itawapiga kipigo cha Bughati(Waovu) kama Abubakar na maswahaba walivyowapiga wale waliozuia zaka.

MATUMIZI YA ZAKA

Hakika matumizi ya Zaka Ameyapanga Mweneyzi Mungu Mtukufu katika kitabu chake pale aliposena :-

إِنَّمَا الصَّدَقَاتُ لِلْفُقَرَاءِ وَالْمَسَاكِينِ وَالْعَامِلِينَ عَلَيْهَا وَالْمُؤَلَّفَةِ قُلُوبُهُمْ وَفِي الرِّقَابِ وَالْغَارِمِينَ وَفِي سَبِيلِ اللَّهِ وَابْنِ السَّبِيلِ فَرِيضَةً مِنْ اللَّهِ وَاللَّهُ عَلِيمٌ حَكِيمٌ (التوبة: 60) .

"Sadaka hupewa (watu hawa)Mafakiri na Masikini na Wanazitumikia na wanaotiwa nguvu nyoyo zao,(Juu ya Uislamu) na katika kuwapa Uungwana watumwa,na katika kuwasaidia wenye deni,na katika (Kutengeneza) Mambo alioamrisha Mwenyezi Mungu na katika (Kupewa) Wasafiri (Waliharibikiwa ).Ni faradhi inayotoka kwa Mwenyezi Mungu ,na Mwenyezi Mungu ni Mjuzi (na ) Mwenye Hikima" TMQ 9:60

Aya hii tukufu,imedhibiti matumizi ya zaka katika makundi manane,na kuyafunga juu yake,na kuhusika na hayo tu,haifai kupewa zaka kwa wasiokuwa hawa wa aina nane,kwa sababu aya imeanza kwa chombo cha "Innamaa" ambacho ni chombo cha kudhibiti na kufunga maneno ya baada yake,na imekuja baada yake "Laamu"ya

kumiliki,ikaonyesha kudhibiti kustahiki zaka na kumilikiwa na haya makundi manane ambayo ni haya:-

1- Mafakiri : Nao ni wale ambao haiwafikiii mali ya kukidhi mahitaji yao ya lazima,ambayo ni kula,kuvaa na kulala,basi yeyote Yule ambayo kinaingia kwake kichache cha yale anayoyahitaji cha kukidhi haja zake za msingi,anahesabika ni Fakiri,ni halali juu yake kupewa sadaka na ana haki ya kuchukuwa sadaka,na inaruhusiwa apewe katika sadaka mpaka kiasi cha kukidhi matatizo yake,na umasikini wake.

Na kwa hakika ameharamisha Mwenyezi Mungu kwa matajiri kuchukua sadaka.

**عن عبد الله بن عمرو قال: قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: " لا تحل الصدقة لغني، ولا لذي مرة سوي"**

Toka kwa Abdullah bin Omar amesema : amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) : "Si halali sadaka/zaka kwa Tajiri,na wala kwa mwenye Mirrah(Mwenye Nguvu na uwezo wa kuchuma)"

Ikiwa hakupata cha kuchuma anahesabika ni Fakiri,na Tajiri: ni yule aliyetosheka na Mwenzie,na akapata ziada ya haja zake za lazima,na zimepokelewa hadithi zinazobainisha ni nani Tajiri .

**عن عبد الله بن مسعود قال: قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: " ما من أحد يسأل مسألة، وهو عنها غني، إلا جاءت يوم القيامة كدوحا، أو خدوشا، أو خموشا في وجهه، قيل: يا رسول الله، وما غناه، أو ما يغنيه؟ قال خمسون درهما، أو حسابها من الذهب" رواه الخمسة.**

Toka kwa Abdullah bin Masoud amesema : amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w)"Hakina mtu yeyote anaeomba kitu na hali ya kuwa ana uwezo nacho ,isipokuwa kitakuja siku ya kiama kama vile mti wenye miba,au kitu cha kukwaruza au kukwangua kikimkwangua katika uso wake,pakasemwa ni upi utajiri wake?au kipi kinachomtosha ?akasema Ni Dirham Khamsini au hesabu yaken katika dhahabu".Imepokelewa na Maimam watano.

Basi anaemiki Dirhama Khamsini yaani kiasi kinacholingana gm 148,75 za fedha,au kinacholingana nacho cha dhahabu ikiwa ni ziada ya chakula chake,na mavazi yake,na makazi yake,na huduma za familia yake na watoto wake,na mfanyakazi wake ,anahesabika ni tajiri,na wala haijuzu kuchukuwa katika sadaka/zaka.

2- Masikini : Nao ni wale ambao hawapati chochote,wametulizwa kwa kukosa,na wala hawawaombi watu,amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu : -

**قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: "ليس المسكين الذي يطوف على الناس، ترده اللقمة واللقمتان، والتمرة والتمرتان، ولكن المسكين الذي لا يجد غني يغنيه، ولا يفطن به فيتصدق عليه، ولا يقوم فيسأل الناس". متفق عليه.**

"Si masikini Yule ambayo anarejeshwa na tunge moja na matonge mawili,na tende moja na tende mbili,lakini masikini ni Yule ambaye hampati tajiri wa kumtoshelezea haja zake,na wala hajulikani ili apewe sadaka,na wala hasimami akaomba watu".Muttafaqun alayhi.

Na masikini ni chini ya fakiri kwa kauli yake Allah:-

**(أو مسكينا ذا متربة)**

"Au masikini aliye hohe hahe" TMQ 90:16

Yaani amegandana na mchanga kwa kuwa kwake uchi na kuwa na njaa.

Na masikini ni halali kupewa sadaka,na ana haki ya kuchukuwa sadaka,na inaruhusiwa apewe katika sadaka mpaka kiwango cha kuondoa umasikini wake na kumfanya ajitosheleza kukidhi haja zake.

3- Wanaofanya kazi katika zaka:Hawa ni wale wanaotembea kukusanya zaka na wakusanyaji sadaka,ambao wanateuliwa kukusanya sadaka toka kwa wale waliowajibu kutoa sadaka,au kuzigawanya kwa wanaostahiki,na watapewa kutokana na sadaka hata kama ni matajiri,kwa kule kufanya kazi kwao ya kukusanya sadaka,au kuzigawa,

**عن عطاء بن يسار قال: قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: "لا تحل الصدقة لغني إلا لخمسة: عامل عليها، أو رجل اشتراها بماله، أو رجل له جار فقير تصدق عليه بصدقة فأهداها إليه، أ, غاز، أو مغرم".**

Toka kwa Atwa'a bin yasar amesema :amesema Mtume wa Mwenyezi Mungu :"Si halai kupewa sadaka Tajiri isipokuwa kwa moja ya mambo matano,anayefanya kazi ya kukusanya sadaka,au mtu aliyeinunua kwa mali yake,au mtu mwenye jirani fakiri akapewa sadaka naye akampa zawadi,au Mpiganaji fii sabilillah au mwenye madeni"

**عن بسر بن سعيد " إن ابن السعدي المالكي قال استعملني عمر على الصدقة، فلما فرغت منها، وأديتها إليه، أمر لي بعمالة، فقلت: إنما عملت لله. فقال خذ ما أعطيت، فإني عملت على عهد رسول الله صلى الله عليه وسلم فعملني، قلت مثل قولك، فقال لي رسول الله صلى الله عليه وسلم: إذا أعطيت شيئا من غير أن تسأل فكل وتصدق" متفق عليه.**

Na toka kwa Busru bin said amesema : "Hakika Ibn si'idy al-malikiy amesema:alinipa kazi Omar katika sadaka,nilipomaliza na kumfikishia ,akaamrisha nipewe malipo ya kazi,nikasema :Nimefanya kazi kwa ajili ya Mwenyezi Mungu,akasema chukua ulichopewa,hakika mimi nimefanya kazi zama za Mtume wa Mwenyezi Mungu akanilipa,na nikasema kama ulivyosema,akaniambia Mtume wa Mwenyezi Mungu:Pindi ukipewa chochote pasina kuomba (kuchukue)ukile na (Ukitaka)kitoe sadaka"Muttafaqun alayhi.

4- Wanaotiwa nguvu nyoyo zao,(Juu ya Uislamu) Nalo ni kundi la viongozi au watu wakubwa au waliathirika au mashujaa ambao imani haijakomaa kwao,na anaona Khalifaha au wa-wali wake wapewe katika zaka ili kuzipa ngivu nyiyo zao,au kukomaza Imani zao,au kuwatumia kwa ajili ya maslahi ya Uislamu na waislamu,au ili wawaathiri watu na makundi yao,mfano kule kuwapa kwao Mtume (S.a.w) alipompa Abu sufiani,na Uyainah bin Hisnu,na Al-aqrai bin Habis,na Abbas bin Mirdas na wengineo.

عن عمرو بن تغلب " أن رسول الله صلى الله عليه وسلم أتى بمال، أو سبي فقسمه، فأعطى رجالا، وترك رجالا، فبلغن أن الذين ترك عتبوا، فحمد اله، ثم أثنى عليه، ثم قال: أما بعد، فوالله إني لأعطي الرجل، وأدع الرجل، والذي أدع أحب إلي من الذي أعطي، ولكني أعطي أقواما لما أرى في قلوبهم من الجزع والهلع، وأكل أقواما إلى ما جعل الله في قلوبهم من الغني والخير".

Toka kwa Amru bin Taghlub,kwamba Mtume (S.a.w) aliletewa mali au mateka akagawa,akawapa watu na akaacha kuwapa watu wengine,zikafika habari kuwa wale ambao ameacha kuwapa wamelaumu,akamshukuru Mwenyezi Mungu na akamsifia,kisha akasema Ama Ba'ad,Namuamba Mwenyezi Mungu hakika mimi ninampa mtu na ninaachakumpa mtu,na Yule ninaeachakumpa anapendeza zaidi kwangu kuliko niliempa,lakini mimi nanawapa watu kwa yale ninayoyaona katika nyoyo zao katika hamaki na kupapatikia (Pupa) na ninaacha kuwapa watu kwa yale aliojaalia Mwenyezi Mungu katika nyoyo zao miongoni mwa Utajiri(kutosheka) na kheri .Bukhari.

Hawa wanaopewa nguvu hawapewi zaka isipokuwa watakapokuwa ni waislamu,wakiwa ni makafiri hawatapewa zaka,kwa sababu zaka hapewi kafiri,kwa kauli yake Mtume (S.a.w) Kwa Mua'dh wakati alipomtuma Yemen:-

لقول لرسول صلى الله عليه وسلم لمعاذ حين بعثه إلى اليمن: " فاعلمهم أن الله افترض عليهم صدقة في أموالهم، تؤخذ من أغنيائهم، وتر على فقرائهم".

"wafahamishe kwamba hakika ya Mwenyezi Mungu amefaradhisha sadaka katika mali zao,itachukuliwa kwa matajiri zao na kurejeshwa kwa masikini wao"Bukhari toka kwa Ibn Abbas.

Kama vile hawapewi isipokuwa ile sababu ambayo wanapewa kwa ajili yake ipo,ikikosekana sabau hawatopewa,kama vile alivyokataa Abubaka na Omar kuwapa baada ya Uislamu kupata nguvu na kuenea.

5- Kuwapa Uungwana watumwa:Hawa ni watumwa wanapewa katika zaka ikiwa wameandikishiana na Mabwana zao ili kujikomboa shingo zao,na watanunuliwa toka mali ya zaka na wataachwa huru ikiwa si wenye

kuandikiana na wanaowamiliki.na watumwa hivi sasa hawapo.

6- Wenye madeni :Nao ni wenye madeni ambao wanabeba majukumu ya deni kwa kutengeneza Mahusiano mazuri,au kutoa fidia,au wanabeba madeni kwa kutatua matatizo yao Binafsi.

Ama wale ambao wanabeba madeni kwa kutengeneza mahusiana mazuri,au kulipa fidia basi watapewa katika zaka ,sawa watakuwa ni mafakiri au matajiri,na watapewa kiwango kile tu walichokibeba katika dni pasina Ziada.

**عن أنس أن النبي صلى الله عليه وسلم، قال" " إن المسألة لا تحل إلا لثلاثة، لذي فقر مدقع، أو لذي غرم مفظع، أو لذي دم موجع".**

Toka kwa Anas kwamba Mtume (S.a.w) amesema : “Hakika kuomba hakufai isipokuwa kwa sababu tatu,kwa mwenye Umasikini Mkubwa mno,na kwa mwenye deni lenye kufedhehesha,na mwenye damu(fidia) yenye kuumiza”

**وعن قبيصة بن مخارق الهلالي قال: " تحملت حمالة، فأتيت رسول الله صلى الله عليه وسلم، أساله فيها، فقال: أقم حتى تأتينا الصدقة، فنأمر لك بها، ثم قال: يا قبيصة إن المسألة لا تحل إلا لأحد ثلاثة: رجل تحمل حمالة، فحلت له المسألة حتى يصيبها، ثم يمسك، ورجل أصابته جائحة اجتاحت ماله، فحلت له المسالة حتى يصيب قواما من عيش، أو قال سدادا من عيش، ورجل أصابته فاقة حتى يقول ثلاثة من ذوي الحجا من قومه لقد أصابت فلانا فاقة، فحلت له المسالة حتى يصيب قواما من عيش، أو قال: سدادا من عيش، فما سواهن في المسالة يا قبيصة فسحت يأكلها صاحبها سحتا".**

Na amepokea Muslim na Abu Daud na Nasai toka kwa Qabiswah Bin Mukhariq Al-hilali amesema : “Nilibeba majukumu ,nikamuendea Mtume (S.a.w) Nikimuomba juu ya hili,akaniambia :Subiri mpaka zitufikie sadaka,ili tuamrishe upewe,kisha akasema :Ewe Qabiswah ! Hakika kuomba hakufai isipokuwa kwa moja ya mambo matatu :Mtu kabeba majukumu atahalalikiwa kuomba mpaka ayapate kisha aache,na mtu kafikwa na balaa limeangamiza mali yake,atahalalikiwa kuomba mpaka apate msimamo wa maisha,au kasema kutatua maisha

yake,na mtu kafikwa na umasikini mkubwa mno mpaka wanasema watu watatu wenye akili katika watu wake,kwa hakika kafikwa fualani na tatizo la umasikini mkubwa mno,atahalalikiwa kuomba mpaka apate msimamo wa maisha,au kasema kukidhi maisha yake,yasiokuwa haya ewe qabiswah ni dhulma anakula dhulma mwenye kufanya hivyo.

Ama wale ambao wanabeba madeni kwa kukidhi mambo yao binafsi,watapewa zaka ili kulipa madeni yao ikiwa ni mafakiri,au wakawa si mafakiri lakini hawana uwezo wa kulipa madeni yao,ama wakiwa ni matajiri na wana uwezo wa kulipa madeni yao hawatapewa zaka,kwa sababu si halali kwao.

7- na katika (Kutengeneza) Mambo alioamrisha Mwenyezi Mungu,yaani katika Jihadi na yanayohitajika katika jihadi na yanayosimamia ,miongoni mwa kutengeneza Jeshi,na kutengeneza Viwanda na kutengeneza Silaha,mahala popote ilipopokelewa neno (Fii sabiillah )katika Qur'ani ,hilo linakuwa halina maana zaidi ya maana ya Jihadi,basi hutolewa zaka kwa ajili ya Jihadi na yale yanayolazimiana nayo,na wala hayapangwi kwa kiwango maalum,inajuzu kuitoa zaka yote au baadhi yake kwa ajili ya jihadi kwa mujibu atakavyoona Khalifah maslahi ya wale wanaostahiki kupewa zaka.

**عن أبي سعيد قال: قال رسول الله صلى الله عليه وسلم:" لا تحل الصدقة لغني إلا في سبيل الله..." وفي رواية":....أو لغاز في سبيل الله....).**

Amepokea Abu Daud toka kwa Abu saidi amesema :Amesema Mtume (S.a.w)"Si halali sadaka kwa tajiri isipokuwa akiwa fii Sabillah" na katika mapokezi yake mengine (…au kwa mpiganaji katika Njia ya Mwenyezi Mungu)

8- Wasafiri:Huyu ni Yule aliyekatikiwa na safari ambaye hapati cha kumfikisha mjini kwake,atapewa katika zaka kiwango cha kumfikisha mjini kiwe kidogo au kingi,kama vile atapewa kiasi cha kumtosha katika mahitaji ya njiani

kwake mpaka afike mjini kwake,na atapewa katika zaka hata kama atakuwa ni tajiri mjini kwake,kwa kauli yake Mtume (S.a.w):-

**9- لقول الرسول صلى الله عليه وسلم: " لا تحل الصذقة لغني إلا في سبيل الله، أ, ابن السبيل، أو....".**

“Si halali zaka kwa tajiri isipokuwa akiwa fii sabillah au msafiri au……”ameipokea Abu daud.

Na wasiokuwemo katika makundi haya manane yaliotajwa katika aya haijuzu kuwapa zaka,haitolewi zaka kujenga misikiti,au mahosptali mambo mengine ya kheri au maslahi yeyote ya dola,au uma,kwa sababu zaka ni milki maalum kwa makundi manane,hayashirikiani na humo na wengineo.

Na khalifah ana haki ya kuangalia katika kuyapa haya makundi,kwa mujibu wa vile anavyoona kutahakikisha maslahi ya makundi haya,kama alivyokuwa Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) na makhalifah baada yake wakifanya hivyo,ana ruhusiwa Khalifah kuigawa kwa makundi yote manane ,kama vile ana ruhusa ya kugaia baadhi,ikiwa hayatapatikana makundi haya,basi zaka itahifadhiwa katika baitil-mali,katika ofisi ya sadaka ili ije itumike wakati wa haja katika matumizi yake.

**عن ابن عباس قال عن الصدقة: " إذا وضعتها في صنف واحدد من الأصناف الثمانية أجزأك"**

Toka kwa Ibn Abbas amesema juu ya zaka:”Ikiwa utaiweka katika kundi moja miongoni mwa makundi maneni itakutosheleza”

Na kadhalika amesema Atwa’a,na Al-hassan,

**وعن مالك قال: " الأمر عندنا في قسم الصدقات أن ذلك لا يكون إلا على وجه الاجتهاد من الوالي، ، فأي الأصناف كانت فيه الحاجة والعدد، أؤثر ذلك الصنف بقدر ما يرى الوالي".**

na toka kwa maliki amesema :- Jambo lililopo kwetu katika kugawa zaka kwamba hilo haliwi isipokuwa katika njia ya kujitahidi kwa kiongozi,kwa aina yeyote katika makundi manane litakalokuwa haja kubwa na

Idadi,litapewa kipaumbele kundi hilo kwa kiwango anachokiaona kiongozi.

**HELA KATIKA UISLAM**

Hela : katika lugha hutumika ni neon la kutofautisha Dirham(Hela) na kutoa zile za bandia, na hutumika katika kutoa na kuchukua Dirham,na katika maana hii ni hadithi ya Jabir na Ngamia wake wake,wakati Mtume (S.a.w) alipomnunua toka kwake,akasema : "akanilipa thamani yake" yaani alinipa hela kwa kuwahisha(Si kuchelesha).kama vile hutumika hela kwa maana ya Hela yenyewe.

Na Hutambulishwa Hela kuwa ni kitu ambacho wakubaliana watu kukifanya ni thamani ya Bidhaa,na ni malipo ya juhudi na huduma,sawa zitakuwa ni madini au sio madini,na kwz hizo hukisiwa(hupimiwa) bidhaa zote na Juhudi na huduma.

Na kwa hakika walikuwa watu wanauziana,na kubadilishana Bidhaa kwa kupokeana(Badilishana) kabla ya kufahamika hela,lakini wakati ilipokuwa wakibadishana bidhaa na juhudi(kazi) kwa kupeana(kubadilishana)jambo hili likifunikwa na uzito mwingi,umewekwa kama ni sharti katika muamala wa Kibiashara,makundi ya watu yakafikiri kuchagua bidhaa ya msingi yenye kima(Thamani) yenyewe,na ni nyepesi katika mzunguruko iwe ni kipimo cha kukisiwa bidhaa zote na juhudi zote,wakaweka hela ziwe ndio kipimo cha pekee cha kupimia thamani za bidhaa.na ilipokuwa Dhahabu na fedha ni katika madini yenye thamani yenyewe kidhati kwa wanaadamu toka zamani,wakafanya hela kutoakana nazo,na wakafua kutoakana nazo Dinar na Dirham,na hasa hasa kwa hizo mbili zinasifika kwa unadira wake,kama vile dhahabu inasifika pia kwa kukubali kwenda na wakati.

Dola ya Kirumi na zile zinzoifuata iliiweka dhahabu kuwa ndio msingi wa hela yake,zikafua(Chapisha) kutokana na dhahabu hela ya Hirqiilah[الهرقيلة ] na ikaziweka katika muundo wa vipimo maalum,kama Dola ya Kifursi na Dola zinazoifuata ziliweka Fedha ndio msingi wa hela zake,na ikafua toka hiyo Dirham na wakaziweka katika muundo kwa kipimo maalum,na

zilikuwa Dinar za kirumi zimo katika muundo mmoja hazitofautiani,ama Dirham za kirumi zilikuwa katika miundo na uzito mbali mbali.
Na walikuwa waarabu kabla ya Uislamu,khasa makuraish wakifanya biashara na wale wa jirani zao katika miji na nchi,

**{لإيلاف قُرَيْشٍ إيلافِهم رِحْلة الشتاء و الصيف}**

[Ili kuwafanya Mkuraish waendelee,waendelee na safari zao wakati wa kusi (Kwenda Yemen) na wakati wa Kaskazi (kwenda Shamu,ndio maana tukajaalia Jeshi la Ndovu kushindwa)TMQ 106:1-2]
Na walikuwa wakirudi toka Shamu wakiwa wamebeba Dinar za Dhahabu za Qaisar,na toka Iraq wakibeba Dirham za fedha za Kisrah,na mara chache wakibeba toka Yemeni Dirham za Himyar,Mji wa Hijaz ukawa unafikiwa na Dinar za Dhahabu za Hiraqlah na Dirham za fedha za Sasaniah,isipokuwa wao hawakuwa wakitumia Dirnar na Dirham hizi kwa kuzihesabu (kama hela ) bali walikuwa wakizitumia kwa uzito kwa kuzihesabu ni Vito,yaani Mada ambayo imefuliwa kwa Dhahabu na Fedha,na kwa uwezekano wa kupungua Dinar kwa kuwa mzunguruko wake ni Mwingi,ijapokuw kwa wakati ule zilikuwa zimethiti kiuzito,kwa kuzuia Hadaa wao walikuwa wanakusudia kutazama Uzito,na walikuwa na vipimo maalum vya kupimia,navyo ni Ratili na waqia,na Nashu na Nawatu,na Mithqali,na Dirham na Daaniqu na Habbah.

**[ الرطل والأوقية، والنشّ، والنواة، والمثقال، والدرهم، والدانق، والقيراط، والحبّة]**

Na ilikuwa Mithaqal kwao - ndio msingi wa kipimo- ndio kipimo kinachojulikana,uzito wake ni Qiratu ishirini Mbili isipokuwa habbah moja,kwao wao ulikuwa uzito wa Dirham tano ni sawa na Mithqali saba.
Ulipokuwa Uislamu alikubali Mtume wa Mwenyezi mungu (S.a.w)kutumika kwa hela hizi Dinar na Dirham,na akakubali kuzihesabu ndio hela za kutumia,na kama vile alikubali vipimo ambavyo Maquraish wakipimia kwavyo Dinar na Dirham hizi.

**عن طاووس عن ابن عمر قال: "قال رسول الله صلى الله عليه وسلم: الوزنُ وزنُ أهل مكة، والمكيال مكيال أهل المدينة".**

Toka kwa Twaus,toka kwa Ibn Omar amesema : Amesema Mtume wa Mwenyezi mungu (S.a.w) : “Kipimo Ni cha watu wa Makkah,na Kipimo ni cha watu wa Madina”Ameipokea Abu Daud na Nasai.

**وروى البلاذريّ عن عبد الله بن ثعلبة بن سعير قال: "كانت دنانير هرقل تَرِدُ على أهل مكة في الجاهلية، وترد عليهم دراهم الفرس البغلية، فكانوا لا يتبايعون إلا على أنها تِبْر، وكان المثقال عندهم معروف الوزن، وزنه اثنان وعشرون قيراطاً إلا كسراً، ووزن العشرة دراهم سبعة مثاقيل، فكان الرطل اثني عشر أوقية، وكل أوقية أربعين درهماً، فأقرّ الرسول صلى الله عليه وسلم ذلك، وأقرّه أبو بكر وعمر وعثمان وعليّ".**

Na amepokea Albaladhiry toka kwa Abdullah bin Tha’labah bin Sair amesema : Zilikuwa Dinar za Hiraqlah zikifika kwa watu Makkah katika Ujahilia,na zikiwafika Dirham za Fursi Al-bghliyah,na walikuwa hawazitumii isipokuwa kwa kuzihesabu kuwa ni vito,na ulikuwa Uzito(Mithqali) kwa wao ni yenye kujulikana uzito wake,Uzito wake ni Qiratwi Ishirini na mbili isipokuwa Kasri,na uzito wa Dirham kumi ni Mithqali saba,Ratili moja ilikuwa ni waqiya kumi na mbili,na kila waqiyah moja ni Dirham arubaini,Mtume (S.a.w) akalikubali hilo,na akalikubali Abu bakar na Omar na Othman na Ally.

Na kwa hakika walibaki Waislamu wakitumia Dinar za Hiraqli na Dirham za Kisrah kwa Umbile lake na chapa yake na picha yake kipindi chote cha Uhai wa Mtume (S.a.w) na kipindi chote cha Ukhalifah wa Abubakar,na Siku za Mwanzo za Ukhalifah wa Omar.

Mwaka wa Ishirini wa Hijria,nao ni mwaka wa nane wa Ukhalifah wa Omar,alichapa(alifua) Omar Diham Mpya zipo katika Mundo wa Sasaniyah,na akazibakisha juu ya Umbile lake na Uzito wake wa Kasri,na akabakisha humo picha na maandishi ya Bahlawiyah,na akazidisha juu yake kuandika baadhi ya herufi kwa Lugha ya Kiarabu za kufa mfano “Bismillah” na “Bismirabbiy”.

Na waliendelea Waislam kutumie kutumia Dinar zilizopo katika muundo wa Kirumi na Dirham zikiwa katika Muundo wa Sasaniah pamoja na kuandika baadhi ya maneno ya Kiislamu kwa herufi za kiarabu mpaka wakati wa Abdulmaliki Bin Marwani.

Katika mwaka 75 au 76 Hijria,Abdulmalik alichapisha Dirham na kuziweka katika mfumo maalum wa kiislam,zikibeba matamko ya Kiislam,yaliochapishwa juu ya Dirham kwa hati (Maandishi) ya kufah baada ya kuuacha muundo wa sasaniyah.
Na katika mwaka 77 Hijriyah akachapisha Dinar katik muundo maalum wa kiislam, na yaliochapishwa juu yake kwa hati (Maandishi) ya kufah na ukaachwa muundo wa Kirumi uliokuwepo.na baada ya Abdulmalik kuchapisha Dirham na Dinar kwa Muundo maalum wa kiislam,wakawa Waislamu wana Hela yao maalum yenye Muundo maalum wa Kiislam,na wakaachana na hela za watu wengine.

**UZITO WA DINAR NA DIRHAM**

Hakika uzito wa Dinar haukutofautina katika zama za Ujahilia na wala katika zama za Uislam,Uzito wake ulikuwa umethibiti(Umetulia) na ilikuwa Dinar ya Kirumi ndio hiyo hiyo ilikuwa ikitumika siku za Ujahilia,na siku za Mtume (S.a.w) na Makhalifah baada yake,kisha Abdulmalik akachapisha Bin Marwan Dinar ya Kiislam ikiwa katika uzito huo huo,na ilikuwa Dinar ya Kirumi ikipimwa kwa Mithqal moja,na Mithqal moja ni sawa na Dawaniq kumi,na uzito wake ni Qirati Ishirini au Ishirini na Mbili isipkuwa Kasra moja,na vipimo vyote viwili ni sawa sawa kwa sababu Qirati hutofautiana kidogo,na wakakadiria Mithqal na sawa na punje sabini na mbili za shairi katika ile shairi ya kati na kati ilikatwa ncha zake mbili nyemba nyemba,kama ilivyokadiriwa kwa punje alf sita za Khardali ya bara(Nchi kavu) ya kati na kati.
Na kwa hakika alikubali Mtume (S.a.w) uzito huu wa Dinar,na akauhusisha katika hukumu za zaka,na fidia na kukatwa mkono katika wizi,ukawa ndio uzito wa Kisheria wa Dinar,na ndio uzito huo huo aliutegemea Abdulmalik bin Marwani wakati alipochapisha Dinar za Kiislama,akaifanya ni Mithqal.
Ama Dirhm ilikuwa na uzito toafuti tofauti,na Wafursi (Waajemi) walikuwa na Dirham za aina tatu:-
kubwa:na ulikuwa uzito wake ni uzito wa Mithqal,yaani Qirati Ishirini,na ,

Ndogo:na ulikuwa uzito wake ni nusu ya Mithqal,yaani Qirati kumi.na ya Kati,na zilikuwa kumi katika hizo zina uzito wa Mithqali sita,yaani Qirati kumi na mbili.

Amesema Al-baladhiriy toka kwa Hassan bin Swaleh amesema :-

**روى البلاذريّ عن الحسن بن صالح قال: "كانت الدراهم من ضرب الأعاجم مختلفة، كباراً وصغاراً، فكانوا يضربون منها مثقالاً، وهو وزن عشرين قيراطاً، ويضربون منها وزن اثني عشر قيراطاً، ويضربون بوزن عشرة قراريط، وهي أنصاف المثاقيل".**

"zilikuwa Dirham katika chapa ya waajemi zipo tofauti tofauti,kubwa na ndogo,walikuwa wakichapisha katika hizo Mithqal,nao ni uzito wa Qirati Ishirini,na wakichapisha katika hizo zenye uzito wa Qirati kumi na mbli, na wakichapisha katika hizo zenye uzito wa Qirati kumi,nazo ni nusu ya Mithqal"

**وروى عن غير الحسن بن صالح فقال: "كانت دراهم الأعاجم ما العشرة منها وزن عشرة مثاقيل، وما العشرة منا وزن ستة مثاقيل، وما العشرة منها وزن خمسة مثاقيل".**

Na imepokewa toka kwa aiyekuwa Hassan bin Swaleh aksema:"Zilikuwa Dirham za waajemi kumi katika hizo zina uzito wa Mithqali kumi,na pia zilikuwa kumi katika hizo zina uzito wa Mithqali sita, na pia zilikuwa kumi katika hizo zina uzito wa Mithqali tano.

Na zilikuwa zikiitwa Dirham kubwa kwa jina la "Dirham za Kibaghlia (Nyumbu)" au Nyeusi zenye kutosheleza kwa kule kutosheleza kipimo cha uzito wa msingi wa Dirham,na ni uzito wa Mithqal wa Dhahabu,yaani Dawaniqi nane, na Daniqu moja ni Qirati mbili na nusu,zinakuwa ni Qirati Ishirini,na zilichapwa kwa uzito huu katika zama za sasaniyah na zama za Makhalifah waongofu na zama za Umawiyah.

Na zikitwa Dirham ndogo ambazo n nusu ya Mithaqal kwa jina la "Dirham za Twabaraniy" nasaba ya Twabarstani mahala zilipochapishwa,zikiwa na uzito wa Dawaniq nne, na zinalingana na Qirati kumi.

Na zikiitwa Dirham za kati na kati kwa jina la "Jawariqiyyah"nasaba ya Jawraqan mji zilioshapishwa,na zina uzito wa Dawaniq 4.8 yaani sawa na Qirati kumi na mbili.

Na ulipkuwa Uislam, na ikafaradhishwa zaka katika fedha,na ukaweka Dirham tano kwa kila Dirham mia

mbili,zikazingatiwa Dirham ambazo kila kumi katika hizo ni sawa na uzito wa Mithqal saba,na ndio ambazo zinasemwa kuwa ni uzito wa saba,nazo ni Dirham za kati na kati katika uzito wake kwa upande wa Dirham.

Nako ni kwamba wao walikusanya Qirati za Dirham kubwa na Ndogo na za kati na kati na wakazigawa kwa tatu,yakawa matokeo ni Qirati 14 au Dawaniq sita,na zinakuwa ni sawa sawa na Punje khamsini za shairi,na Khumsi mbili za Punje ya shairi ya kati na kati ilikatwa katika ncha zake mbili,kama vile ambavyo inalingana na mbegu za Khardali alf nne na mia mbili,na ikawa hii ndio Dirham ya kisheria inayozingatiwa katika hukumu za zaka na fidia.

Na ulikuwa uzito huu ndio unaojulukana na kuzingatiwa siku za Mtume (S.a.w),na wakati wa Omar ( R ) alipanga kiwango chake kwa Dawaniq na Qirat kwa kutegemea Hadithi ya Mtume (S.a.w):-

**حديث الرسول صلى الله عليه وسلم "الوزن وزن أهل مكة".**

“Kipimo ni Kipimo cha watu wa Makkah” Kaipokea Abu Daud na Nasai”

Akapanga viwango nvipimo kwa ile hali waliokuwa nayo makuraish wameiweka katika vipimo,na akavikubali Mtume (S.aw) na kipimo hiki huitwa kwa Dirham ya Kisheria,na kwa kipimo hiki zikifungwa hukmu za kisheria katika zaka,fidia na nyinginezo na ndio uzito/kipimo wa Dirham ya kisheria ambayo aliichapa Abdulmalik bin Marwan baada ya kuachana na Dirham za Kiajemi.

Amenakili Al-waqidiy toka kwa Wahbi bin Kaysan amesemea :

**وقد نقل الواقدي عن وهب بن كيسان أنه قال: "رأيت الدنانير والدراهم قبل أن ينقشها عبد الملك ممسوحة، وهي وزن الدنانير التي ضربها عبد الملك.**

“Nimeziona Dinar na Dirham kabla hajaziakishi upya Abdulmalik zikiwa zimefutwa ,na ndizo huo huo uzito wa Dinar ambazo amechapa Abdulmalik”

**وروى أيضاً عن عبد الملك بن السائب عن أبي وداعة السهمي أنه أراه وزن المثقال قال: "فوزنته فوجدته وزن مثقال عبد الملك بن مروان، قال: هذا كان عند أبي وداعة بن ضبيرة السهمي في الجاهلية".**

Pia amepokea toka kwa Abdulmalik Bin Assaib toka kwa Abu wida’a Assahmiy kwamba yeye alimuonyesha uzito wa

Mithqal,akasema :Nikaupima nikaukuta una uzito wa Mithqal ya Abdulmalik Bin Marwan,akasema :Hii ilikuwa kwa Abu zur'at Bin nadhri Assahmiy katika ujahilia.

**وروى البلاذريّ عن عثمان بن عبد الله قال: قال أبي: "قدمت علينا دراهم ودنانير عبد الملك المدينة، وبها نفر من أصحاب رسول الله صلى الله عليه وسلم، وغيرهم من التابعين، فلم ينكروا ذلك"،**

Na amepokea Albaladhiriy toka kwa Othman Bin Abdillah amesema :- amesema Baba yangu :Zilitufikia Dirham na Dinar za Abdulmalik katika mji wa Madina,na walikuwepo kundi la maswahaba wa Mtume (S.a.w) na wengineo katika Ta'biina,hawakulipinga hilo"

**وقال محمد بن سعد: "وزن الدرهم من دراهمنا هذه أربعة عشر قيراطاً من قراريط مثقالنا الذي جعل عشرين قيراطاً، وهو وزن خمسة عشر قيراطاً من إحدى وعشرين قيراطاً وثلاثة أسباع".**

Na amesema Muhammad Bin Sa'ad:Uzito wa Dirham katika Dirham zetu hizi ni Qirat kumi na nne katika Qirat za Mithqali zetu ambao umefanywa ni Qirat Ishirini,na huo ndio uzito wa Qirati kumi na tano,kutokana na Qirati Ishirini na moja na As'baa tatu."

Huu ndio uzito wa Dinar za dhahabu,na Dirham za Fedha,na kiwango kilichopangwa kati ya aina zake,na ili iwe wepesi kwetu kufahamu uzito huu,hapana budi tufahamu viwango vyake vilivyopangwa kwa hesabu ya vipimo vya leo.

Na kwa hakika imewezekana kufahamu uzito huu kwa kina baada ya ugunduzi wa vitu vya kale,na kupata Dinar za Kirumi,na Dirham za Kaisariyah,na Dinar na Dirhama za kiislam,khasa zile ambazo zilichapwa katika siku za Abdulmalik Bin Marwan,na zile ambazo alizichapa katika uzito wa Dinar na Dirham za kisheria.

Na zimepatikana hela nyingi za toka zama za Kiislam,na bado zipo zimehifadhiwa katika majumba ya mambo ya kale,na wamesajili wasimamizi wa majumba haya ya mambo ya kale kuwa hizi hla- baada ya kuzipima na kuzipambanua – uzito wake kwa umakini uliotimia kwa sura ya kukata,na wamekuta kuwa Dinar ya Kiislam ambayo aliichapa Abdulmalik Bin Marwan uzito wake ni Gram 4.25,na ndio uzito wa Sulodios wenyewe,na ndio uzito wa hela ya dhahabu ambayo ilikuwa

imeenea Kwa Warumi,na ndio uzito wa Dinar za kigiriki,ambazo zilitegemea uzito wa Soldios[السوليدوس ] juu ya Uzito wa Dinar ya kirumi,ambayo ilikuwa imeenea siku za ujahilia na Uislamu.

Na kuwa Dinar ndio Mithqal,na mithqal ndio msingi wa vipimo,kuifahamu kunarahisisha kufahamu uzito wa Dirham,na Dawaniq,na Qararitwi,na Habati(Nafaka) kwa upande wake.

Na kwa kuwa Mithqal ni sawa na Gram 4.25,na ni sawa na Dawaniqu nane,basi unakuwa uzito wa Daniqi ya Dhahamu kwa Gram ni 4.25 ambao ni uzito wa Mithaqal ÷ Dawaniq 8=0.53125 grm za uzito wa dawaniqu.

Na kwa kuwa Mithqal ni Qiaratwi Ishirini,basi unakuwa uzito wa Qiratwi kw agrm ni grm 4.25 uzito wa Mithqal ÷ kwa Qiratwi 20=0.2125 grm za uzito wa Qirat.

Na kwa kuwa Mithqal moja ni sawa na Mbegu 72 za Shairi,basi unakuwa uzito wa mbegu moja kwa grm ni :

Grm4.25 za uzito wa Mithaqal ÷ 72 za Mbegu za Shair = grm 0.059 ndio uzito wa mbegu moja ya shairi kwa kiwango cha dhahabu na hii inalingana na Mbegu 83.3 za Khardali.

Na kwa kuwa Dirham moja ni sawa na saba ya kumi ya mithqal,na kila dirham kumi ni sawa na mithqal saba,basi unakuwa uzito wa Dirham kwa gram ni :

Grm 4.25 uzito wa Mithqal × 7/10 = 2.975 grm za fedha ndio uzito wa dirhm.

Au kila Dirham 10 =Mithqal 7 yaani 10 ×2.975= 29,75 grm uzito wa Dirham kumi.

Au kila Mithqal 7 =Dirham 10 yaani 7× 4.25 =29,75 grm uzito wa Mithqal saba.

Na kwa kuwa Dirham moja ni sawa na Dawaniqu sita,basi unakuwa uzito wa Dawaniqu za Fedha kwa Gram ni :-

2.975÷ 6 = 0.495 Grm ndio uzitowa Daniq moja ya fedha.

Na ilipokuwa waqiya ambazo hupimia Dirham kwazo ni sawa na Dirham 40,basi unakuwa uzito wake kwa Gram ni Grm 2.985 (Uzito wa Dirham) × 40 (Dirham,uzito wa waqiya) = Grm 119 uzito wa waqiya za fedha.

Hii ndio hela ambayo ilikuwa ikitumika katika siku za Ujahilia,na huu ndio uzito wake,na Uislamu umeikubali hela hii kama ilivyo,na ukakubali kutumika kwake,na ukaifanya ndio chombo cha mzunguruko wa kihela,na ni kipimo cha kupimia bidhaa na kazi(Juhudi) na vile umekubali vipimo vya watu wa Makkah.

Na pamoja na hayo,hakika Uislam haukulazimisha iwe ndio chombo pekee katika Mzunguruko, wakati ilipopitisha Hukmu za Biashara,kuuza na kununua na kukodisha,bali umempa uhuru mwanadamu abadilishane bidhaa na manufaa na juhudi (Kazi) kwa kitu chochote kitakachotumia kuridhiana juu yake,pasina kulazimisha kitu maalum cha kupitia /kuzungurukia mzunguruko juu yake.

Uislamu umemruhusu mwanadamu anunue Upanga kwa Tende,na Mbuzi kwa ngano,na nguo kwa Dinar,na Nyama kwa Dirham,na afanye kazi siku moja kwa Pishi ya Zabibu,au atengeneze kabati kwa Dinar tano,au ajenge nyumba maalum kwa kulima ardhi maalum.

Kama hivi Uislam umeacha huru kubadilishana watu kama wanavyotaka,na kwa yale yatakayotimia maridhianao baina yao,sawa yatakuwa kwa Bidhaa au kwa juhudi (Kazi ) au kwa Hela.

Na pamoja kuwa Uislam umeacha huru kubadilshana bidhaa watu kwa vile watakavyo,isipokuwa emeweka hela ambazo zinakuwa ndio za kubadilishana kwazo,ukaweka dhahabu na fedha,na ukaziweka kuwa ni kipimo cha hela ambacho hurejeshwa juu yake vipimo vya bidhaa na juhudi,na msingi ambao hupita juu yake Muamalat wote,na ukaziweka katika kipimo maalum ambacho ni kipimo cha watu wa Makkah.(Kipimo ni kipimo cha watu wa Makkah)

Na Uislam Umefungamanisha hukumu za Kisheria kwa Dhahabu na Fedha,kwa kuzizingatia kuwa ni dhahabu na fedha,na kwa kuzizingatia kuwa ni hela,na thamani ya vitu na ni malipo ya juhudi (Kazi) .

Na miongoni mwa Hukumu ni hizi :-

1- Uislam Umeharamisha Kulimbikiza Dhahabu na Fedha,amesema Mwenyezi Mungu Mtukufu :-

{والذين يكنزون الذهب والفضة ولا ينفقونـها في سبيل الله فبشّرهم بعذاب أليم}

"Na wale wakusanyao Dhahabu na Fedha wala hawazitoi katika njia ya Mwenyezi Mungu,wape habari za adhabu inayoumiza (Inayowangoja) TMQ 9:34"

Akaweka uharamu wa kulimbikiza kupo juu ya Dhahabu na Fedha,kwa kuzizingatia kuwa ni Dhahabu na Fedha,na kwa kuzizingatia kuwa ni hela,na chombo cha mzunguruko ( wa matumizi) na kwa hizo mbili hutimia kuuziana na kazi.

2- (Uislam)Umefungamanisha kwa Dhahabu na Fedha hukmu maalum zenye kuthibiti na hazibadiliki zikiwemo :

A- Umefaradhisha Zaka katika Dhahabu na Fedha kwa kuzizingatia kuwa ni Hela,na thamani kwa ajili ya kuuziana,na malipo kwa juhudi(Kazi) na ukabainisha Nisabu(kiango) maalum miongoni mwa Dinar za Dhahabu na Dirham za Fedha.

"في كل عشرين ديناراً نصف دينار وفي كل مائتي درهم خمسة دراهم".

"Katika kila Dinar Ishirini ni Nusu Dinar,na katika kila Dirham Mia mbili ni Dirham Tano"

B- Na wakati Ulipofaradhisha Fidia ukafanya Dhahabu na Fedha ndizo zinazotolewa,na ukabainisha kiwango maalum katika Dhahabu ni Dinar alf moja,na kiwango maalum cha fedha kuwa ni Dirham alfu kumi na mbili.

عن ابن عباس "أن رجلاً من بني عدي قُتِلَ فجعل النبي صلى الله عليه وسلم دِيَتَهُ اثني عشر ألفاً"، أي من الدراهم رواه أصحاب السنن،

"Toka kwa Ibn Abbas kwamba ;Mwanamme mmoja toka kabila la Bani Adiyy aliuawa,akajaalia Mtume (S.a.w) fidia yake ni Kumi na Mbili alf,Yaani za Dirham.Imepokewa na As'habu Sunani."

وعن أبي بكر بن محمد بن عمرو بن حزم عن أبيه عن جده "أن رسول الله صلى الله عليه وسلم كتب إلى أهل اليمن كتاباً، فكان في كتابه "وإن في النفس الدِّيَةَ مائة من الإبل، وعلى أهل الذهب ألف دينار" رواه النسائي.

"Na toka kwa Abubakar Bin Muhammad Bin Amr Bin Hazm,toka kwa Baba yake,Toka kwa Babu yake,Kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.w.a) Aliwaandikia Barua watu wa Yemen,yalikuwemo katika Barua hiyo ni "Na katika Nafsi Fidia yake ni Ngamia Mia moja,na kwa watu wa dhahabu ni Dinar alf moja"ameipokea Annasai".

C- Wakati (Uislamu)Ulipowajibisha Kukata mkono katika wizi,Ulibainisha kiwango ambacho utakatwa mkono wa mwizi kwa upande dhahabu ni Robo Dinar,na katika Fedha ni Dirham tatu,na ukajaalia kiwango hicho kuwa ni kipimo kwa kila kinachoibiwa.

**عن عائشة عن النبي صلى الله عليه وسلم قال: " لا تقطع يد السارق إلا في ربع دينار فصاعداً"،**

"Toka kwa Aisha ( R ) ,Toka kwa Mtume (S.a.w) amesema :"Haukatwi Mkono isipokuwa katika Robo Dinar na kuendelea"Imepokelewa na wapokezi watano.

**وعن ابن عمر "أن رسول الله صلى الله عليه وسلم قطع سارقاً في مِجَنٍّ قيمته ثلاثة دراهم".**

Toka kwa Ibn Omar ,kwamba Mtume wa Mwenyezi Mungu (S.a.w) aliukata mkono wa Mwizi katika Ngao Yenye thamani ya Dirham tatu.Imepokewa na Sheikhani na Abu dawd.

3- Wakati Uislamu Ulipopitisha hukmu za matumizi katika Muamalati wa hela,uliweka katika Dhahabu na Fedha,na Matumizi ni kule kubadilishana hela kwa hela,na kuuza kitu kwa kitu,ima kwa kitu cha jinsi moja kwama kuza dhahabu kwa dhahabu,na kuuza fedha kwa fedha,na ima kwa aina nyingine isio jinsi yake,kama vile kuuza dhahabu kwa fedha,na kuuza fedha kwa dhahabu.

**عن أبي بكرة قال: "نهى النبي صلى الله عليه وسلم عن الفضة بالفضة والذهب بالذهب إلا سواء بسوا، وأمرنا أن نشتري الفضة بالذهب كيف شئنا، ونشتري الذهب بالفضة كيف شئنا"، أخرجه الخاري ومسلم.**

“Toka kwa Abubakar amesema:- Amekataza Mtume (S.a.w) Kuuza fedha kwa fedha na dhahabu kwa dhahabu isipokuwa ziwe sawa kwa sawa,na ametuamrisha tununue fedha kwa dhahabu kwa namna tutakavyo,na tununue dhahabu kwa fedha kwa namna tupendayo”ameitoa Bukhar na Muslim.

Uislamu umeunganisha Hukmu hizi za Kisheria kwa Dhahabu na Fedha,kwa kuwa kwake ni Naqdi na hela za mzunguruko,na ni thamani ya vitu vinavyouzwa,na huko ni kukubali kwa Mtume (S.a.w) kwa kuzifanya dhahabu na fedha kuwa kipimo pekee cha hela ambazo hukadiriwa kwacho thamani ya vinavyouzwa na malipo na juhudi (Kazi).

Na hili linaonyesha juu ya kuzingatia hela katika Uislamu kuwa ni Dhahabu na Fedha,kwa sababu hukumu zote zina uhusiano na hela,zimefungamanishwa na dhahabu na fedha kwa kuzizingatia kuwa ni thamani ya Bidhaa zote na Juhudi,na ni malipo(Hela) katika Mzunguruko,sawa ziwe zimefuliwa au hazikufuliwa.

Lakini Je hii inakusudiwa kwamba haifai kwa waislamu na kwa Dola ya Kiislamu ,kutumia hela zisizokuwa dhahabu na fedha au kubalisha(mzunguruko)kwa zisizokuwa hizo?

Ama kutumia mzunguruko usiokuwa huo,jambo hili ni ruhusa moja kwa moja,na wala hakuna tofauti,kwa sababu kununua na kuuza kulikuwa kunafanyika siku za Mtume (S.a.w) kwa kupokea(Kubadilishana) vitu baadhi yake kwa baadhi,kama vile ambavyo kukifanyika kwa kununua kwa hela miongoni mwa dhahabu na fedha.

Na alikiri Mtume (S.a.w) yote hayo pasina kuzuia,au kupinga,na akaruhusu kuzitumia.

**روى مسلم عن عبادة بن الصامت عن النبي صلى الله عليه وسلم قال: "الذهب بالذهب، والفضة بالفضة، والبُرُّ بالبُرّ، والشعير بالشعير، والتمر بالتمر، والملح بالملح، مِثْلاً بمثل، سواء بسواء، يداً بيد، فإذا اختلفت هذه الأصناف، فبيعوا كيف شئتم، إذا كان يداً بيد"،**

Amepokea Muslim toka kwa Ubadah Bin Swamit,toka kwa Mtume (S.a.w) amesema: “Dhahabu kwa Dhahabu,na Fedha kwa Fedha,na Ngano kwa Ngano, na Shairi kwa Shairi,na Tende kwa Tende,na Chumvi kwa Chumvi,Vilingane sawa kwa sawa,Mkono kwa Mkono (Kupeana kwa

Kupeana)zikitofautiana aina hizi basi uzeni kwa namna mtakavyo,ikiwa Mkono kwa mkono.

Na amepokea Annasai toka kwa Ubadah amesema : "….. Na Tumeamrishwa tuuze Dhahabu kwa Fedha,na Fedha kwa Dhahabu na Ngano kwa Shairi na Shairi kwa Ngano Mkono kwa Mkono,Kwa namna tutakayo".

Ama maudhui ya kuruhusu au kutokuruhusu Waislamu na Dola ya Khilafah kutumia hela isiokuwa ya dhahabu na fedha,ili kufikia hukmu ya hayo hapana budi kuangalia wakia/waqia/hali halisi ya Hela,ambayo ilikuwa siku za Mtume (S.a.w) na kwa kurejea hukmu za kisheria ambazo zimeambatanishwa na dhahabu na fedha.

Ama wakia/hali halisi ya hela ambazo zilikuwa siku za Mtume (S.a.w) kwa hakika hakukuwa na hela iliokuwa inatumika kwa kuizingatia ni hela ambayo zitapimiwa kwayo thamani ya vitu vyote vinavyouzwa,na kuwa ndio malipo ya juhudi isipokuwa dhahabu na fedha,hapakuwa na hela zaidi ya hizo,za madini au zisizokuwa za madini,hapakuwa na hela za shaba au risasi,kama vile hapakuwa na hela za ngozi,au za karatasi,bali ilikuwa dhahabu na fedha peke yake ndio hela zinazotambulika,na ndio inazunguruka kwa waislamu,na ilikuwa kuuza na kununua kunatimia kwa uzito wa hizo,si kwa kuhesabu,kwa kuzingatia hizo ni dhahabu halisi,pindi zinapokuwa zimefuliwa,basi kwa mfanya biashara ambaye ananunua bidhaa kwa dinari ataipima dinar ili ahakikishe kwamba ina uzito uliotimia na wala haukupungua chochote kwa kule kuwa katika mzunguroko,na mwenye kuuza bidhaa kwa Dirham atapima hizo dirham ili ahakikishe kwamba uzito unaohitajika ambao imetimia biashara kwa uzito huo upo.

Na mwenye kuwa na dinar ishirini,na zikapitiwa na mwaka na akakuta uzito wake umepungua Qirati moja hatatoa zaka,kwa sababu hiyo imepungua kiwango cha kutoa zaka (Nisabu) na mwenye kuwa na dirham mia mbili na akazikuta zinapungua Qirat moja hatatoa zaka,kwa sababu zimepungua Nisabu.

Na hii inabainisha kuwa Dhahabu na Fedha kwa vile zilivyo zinahesabika ni hela na thamani,pasina kutazama kuwa zimefuliwa au hazijafuliwa,kwa sababu imekubalika kuzizingatia kuwa hela hupimiwa kwazo bidhaa na juhudi na huduma.akakubali Mtume (S.a.w) kutumika huku,na hela hizi zikabaki ndizo zikitumika katika maisha yote ya Mtume (S.a.w) na ya Makhalifah waongofu baada yake,na siku za Umawiyyah na Abbasiyah,na wala waislam hawakuwa na hela zaidi ya hizo kwa muda wote huo,basi kukiri kwa Mtume (S.a.w) kwa kuwa ni hela na thamani huko ni kukiri kwa wakia wa kile kilichopo,na wala hakuamrisha kuchukuwa nyingine badala yake.

Ama kurejea Hukmu za kisheria ambazo zimeambatanishwa na dhahabu na fedha,kwa hakika inabainika kutokana na haya uharamu wa kulimbikiza haupatikani isipokuwa kwa hizo peke yake pasina mali nyingine,ama mali nyingine inafikirika kuzilimbikiza na wala sio kulimbikiza,Vyakula havikae muda mrefu,na wanyama na mifugo hawakai muda mrefu,na ndege haififikiriki humo kilimbikiza,kwa sababu vinadumu kukuwa,na wakati ilipokuwa kulimbikiza hakuhdihiri isipokuwa katika hela,basi ukaja uharamu wa kilimbikiza kuhusiana na dhahabu na fedha,kwa sababu ilikuwa hakuna kwa waislam hela isipokuwa hizo.

Na kwa hakika hata ikiwa sheria imehusisha na dhahbu na fedha hukmu maalum zenye kuthibiti na hazibadiliki,kama hukmu za fidia na zaka,kwa hakika sheria haikutosha /haikushia na hizo mbili katika hukmu hizo,bali umehusisha fidia na zaka na mali za aina nyingine,umeihuisha fidia pia na Ngamia,Ng’ombe na Mbuzi na kondoo,na vipambo yaani Nguo,na Zaka imewajibishwa katika mifungo miongoni mwa Ngamia,Ng’ombe na Mbuzi na Kondoo,na katika Mimea na Matunda,na Bidhaa za Biashara,kama vile ilivyowajibisha katika Dhahabu na fedha.

Kwa sababu hiyo,hukmu hizi ambazo zimehusishwa na dhahabu na fedha haikuishia hapo tu kwenye dhahabu na fedha,bali pia zimehusishwa na vikine visivyokuwa dhahabu

na fadha,isipokuwa haukuelekea kutumia hela zaidi ya hizo,kwa sababu ya kutokuwepo hela nyingine,ama hukmu za riba na kubadilishana zinazohusiana na hizo,kwani riba inahusiana na hizo na mali nyingine za riba ambazo zimeelezewa na hadithi na kubalishana hakuwi isipokuwa katika hela inayotumika.

Na kutokana Mapitio haya ya hali ya hela,za dhahabu na fedha,ambazo zilikuwa zikitumika katika wakati wa Mtume (S.a.w),na kutokana na mapitio ya Mfumo wa dhahabu na fedha,na faida zake,na mifumo mingine ya hela inapambanuliwa katika haya yafuatayo,inawezekana kufikia kwamba hela ya Dola ya Khilafah Ni dhahabu na fedha kuwa ndio msingi,kwa ajili ya kupimia thamani ya bidhaa na juhudi,na ijapokuwa inafaa kutumia madini mengine pamoja na dhahabu na fedha wakati wa kufua vipande vidogo vidogo kutoka hela za dhahabu na fedha.

MIFUMO YA HELA

Hela zipo aina mbili : Za madini na za Karatasi.

Hela za Madini ni zile ambazo zimetengenezwa kutokana na Madini,kama dhahbu na fedha,shaba na Risasi na Nikali [النيكل ]

Na hela za karatasi ni zile hela ambazo zimetengenezwa kutokana na karatasi,badala ya dhahabu na fedha,au zimefunikwa (Utepe) kwa dhahabu au fedha au vyote viwili kwa pamoja,kufunikwa kwa moja kwa moja,au kwa sehemu Fulani tu,au sio badala ya dhahabu na fedha,na wala hazijafunikwa kwazo.

Na kwa hakika Ulimwengu ulikuwa ukitumia hela za dhahabu na fedha mpaka jirani na vita vya dunia vya kwanza,wakati paliposimamishwa kuzitumia,kisha ulimwengu ulirejea kuzitumia tena hela za dhahabu na fedha kwa kiasi kidogo baada ya vita vya dunia vya kwanza,kisha ukawa utumiaji huu unaisha kidogo kidogo.

Mnamo mwaka 1971 pakafutwa moja kwa moja kabisa matumizi ya hela za dhahabu na fedha,na alipisha sheria ya kufuta rasmi Rais Nickson wa Marekani mnamo tarehe 15/7/1975 fumo wa Broton na Words unaoagiza kufunika Dola

kwa dhahabu,na kuifungamanisha kwao kwa thamani yenye kuthibiti.
Na mfumo wa hela : Ni mkusanyiko wa kanuni ambazo hutimia kwa msingi wake kuweka hela na kuzizingatia katika dola miongoni mwa dola.
Na Mzunguruko wa msingi kwa kila mfumo ni kubainisha umoja wa hela za msingi ambazo zinajisabisha juu yake thamani ya aina nyingine ya hela,kwa mfano ikiwa utaungana msingi wa umoja wa hela kwa kiwango maalum cha dhahabu,utakuwa umoja huu ndio hela ya msingi wa mfumo huu.
Na hutegemea Mfumo wa hela kawaida ambayo huitwa ni kawaida ya hela ya msingi inayochukuliwa humo,ikiwa hela ya msingi ni dhahbu,basi huitwa mfumo huu ni mfumo wa dhahabu,au kanuni ya dhahabu,na ikiwa msingi wa hela ni fedha,huitwa ni mfumo wa fedha,na ikiwa hela ya msingi imetengenezekana kwa vitu viwili – Dhahabu na Fedha – utaitwa mfumo huu kuwa ni mfumo wa Madini aina mbili.
Na ikiwa thamani ya umoja wa hela ya asili haufungamani na mahusiano yaliothibiti kwa dhahabu au fedha,utaitwa mfumo huu kuwa ni mufumo wa kujilazimisha,sawa utakuwa umechukuliwa kutokana na madini,kama madini ya shaba,au umechukuliwa kutokana na karatasi kama hela za karatasi ( Bankanut) [**(بنكنوت)** ]

## MFUMO WA MADINI

Mfumo wa Madini:Ni Mfumo ambao hutengenezeka msingi wa umoja wa hela kwa madini,nao ima uwe umoja wa msingi wake umetengenezeka kutokana na madini aina moja tu,na ima uwe umetengenezeka kwa madini ya aina mbili.
Mfumo wa Madini ya aina moja
Huo ni mfumo wa hela wa madini ambao hutegemea madini ya aina moja,dhahabu au fedha,na mfumo huu unaweza kupatikana katika aina tazo hizi:-

1- Mfumo wa hela zilizofuliwa kwa dhahabu au fedha.

2- Mfumo wa Cheki za dhahabu au fedha.

3- Mfumo kubadili kwa dhahabu au kwa fedha

1- MFUMO WA HELA ZILIZOFULIWA KWA DHAHABU AU FEDHA

Huo ni mfumo ambao huzunguruka vipande vya dhahabu,au vipande vya fedha,zilizofuliwa kwa vipimo na uzito maalum uliothibiti,vinakuwa hivyo ndio vyombo vya mzunguruko wenyewee,na huenda pia pakaingizwa katika mzunguruko pamoja na dhahabu na fedha hela karatasi mbada ya dhahabu au fedha,zikifanana nazo kwa moja kwa moja,na hubadilishwa kwazo katika wakati wowote pasina shrti lolote au kizuizi chochote.

2- MFUMO WA CHEKI ZA DHAHABU AU FEDHA

Ni Mfumo ambao huondolewa vitande vya dhahabu au fedha iliofuliwa huondolewa katika mzunguruko wa hela,na Dola au Benk kuu inahifadhi katika hazina yake vipande vya dhahabu au fedha vilivyofuliwa,na hutoa hela za karatasi zikiwa ni niaba ya dhahabu au fedha,na huziingiza katika mzunguruko,na zinaweza kubadilishwa kwa dhahabu au fedha.

Isipokuwa Dola wakati ilipokusudia mfumo wa Cheki,iliweka uwezekano wa moja kwa moja wa kubadilisha kwa dhahabu au fedha kwa hela za Karatasi,na ukazifanya katika sehemu ndogo sana,na ukatengeneza Cheki za aina kubwa ili asiweze kila mtu kuzinunua ili apate kuhifadhi dhahabu au fedha ya akiba na tahadhari,na ili iweze kuziba upungufu wowote katika bajeti yoyote ya vinavyotolewa,na pia ili iweze kuzuoia kutoroshwa dhahabu au fedha kwenda nje,kwa sababu hii Dola ambayo inatumia mfumo huu, imeweka Idara ya hela na kiasi Fulani cha ukaguzi juu ya harakati za dhahabu na fedha.

3- MFUMO WA KUBADILI DHAHABU AU FEDHA

Ni mfumo ambao unasifikwa kwamba umoja wa hela katika mji ambao inautumia,haujifungi moja kwa moja juu ya msingi wa dhahabu au fedha,isipokuwa hujifunga juu ya msingi wa kufungamana hela yake na hela ya mji /nchi mwingine unaokwenda katika mfumo wa dhahabu au fedha,kama ilivyokuwa inatokea katika kufungamana hela ya Mji/Nchi inayofuatwa na hela ya nchi inayofuata ambao huenda juu ya msingi wa dhahabu au fedha,kama hela ya Syria na Lebanon ambayo ilikuwa imefungamana na hela ya Ufaransa siku za Intidabi/Uchaguzi,na kama hela ya Misri na Iraqi ambayo ilikuwa imefungamana na hela ya Uingereza wakati zilipokuwa chini ya utawala wa Uingereza.

MFUMO WA MADINI AINA MBILI

Ni mfumo ambao inakuwa hela yake ya msingi imetengenezwa kwa Umoja wa aina mbili,dhahabu na fedha,hapana budi katika mfumo huu kupanga kiwango kilichothibiti katika kiwango na uzito kati ya umoja wa dhahabu na umoja wa fedha,ili iwezekane kupima moja wapo kwa nyingine,na kufahamu thamani ya kubadilisha kwazo,na katika mfumo huu huzungurushwa vipande vya umoja wa dhahabu pembezoni mwa vipande vya umoja wa fedha,na miongoni mwa dola zilikuwepo zilizokuwa zikiweka kanuni ya ubadilishaji katika umoja wa dhahabu kwa umoja wa fedha ili iwe bei ya kubadilisha kati yake ni yenye kuthibiti baina yake.

Hakika kutumia mfumo wa dhahabu na fedha kunahitajika kupangwe umoja wake wa msingi wa hela kwa dhahbu na fedha kwa kipimo na kiwango maalum kilichothibiti,na wapewe uhuru watu wa kununua dhahabu na kuuza ,kuingiza na kusafirisha pasina kuwekewa sharti lolote,na wawezeshwe uwezo wa(Wafanyiwe wepesi) kubadilisha hela nyingine

kwenda katika dhahabu na fedha ,na kubadilisha dhahabu na fedha kwenda katika hela nyingine,ili kazi za kibiashara za nje ziwe nyepesi na watu wawezeshwe kubadilisha dhahabu na fedha iliofuliwa kwenda katia cheki na cheki kwenda katika dhahabu na fedha kwa gharama ndogo itakayochukuliwa na ofisi ya kufua katika dola.

**MFUMO WA KARATASI**

Mfumo wakaratasi ni mfumo ambao hutumika katika hela za karatasi kuwa ni chombo cha mzunguruko,na hela za karatasi ni muundo wa cheti au hati yenye kuzunguruka hutolewa kwa alieibeba,na huwakilisha deni maalum katika dhamana ya dola,au utawala wa hela ambao umezitoa ikiwa karatasi hizi ni niaba ya dhahabu au fedha au kama zitakuwa ni karatasi zilizofunikwa utepe wa dhahabu au fedha.

Na hela za karatasi nyingine huwa ni niaba ya dhahabu au fedha iliopo katika hazina ya dola,hulingana nazo kwa ukamilifu,yaani ulie utepe wa dhahabu au wa fedha wa hela hizi za karatasi zilizopo katika mzunguruko,hulingana nazo thamani yake kwa asilimia mia moja,na anaebeba hela hizi za karatasi za niaba ana haki ya kuzibadilisha na kuwa dhahabu au fedha kwa mujibu wa utepe wake kwa wakati wowote atakao pasina sharti lolote au kiwango chochote,na hela hizi niaba za karatasi zinahesabika katika wakia wake ni katika mfumo wa madini,na yote yaliopo katika jambo hili ni kwamba badala ya kuzunguruka dhahabu na fedha halisi zenyewe,karatasi hizi za niaba zinasimama mahala pake katika mzunguruko kwa kuzihesabu ni niaba yake.

Na huenda zikawa hela hizi za karatasi zimefunikwa (kwa utepe) kwa sehemu ya thamani yake kwa kiwango maalum,na huitwa hela hizi za karatasi “Hela za Hati” na pamoja kwamba hazikufunikwa kwa ukamilifu kwa dhahabu au fedha,basi kwa hakika ukweli wa kuziamini hizo kumetokana na ukweli/uaminifu wa upande ambao umezitoa,na unakuwa upande uliofunikwa katika karatasi hiyo kwa dhahabu au fedha

ni hela ilioniaba ya dhahabu au fedha,katika wakati huo huo unahesabika upande uliobaki ambao haulingani na dhahabu au fedha ni hela za karatasi za hati,hutengemea nguvu zake katika mzunguruko kwa uaminifu /ukweli wa watu kwa upande ambao umezitoa.

Na aina ya tatu ya hela za karatasi ambayo haina utepe wowote wa dhahabu au fedha,na wala hizo sio niaba ya dhahabu au fedha,na huitwa ni "Hela za karatasi za Kujifunga" nazo ni hela ambazo hazikubali kubadilishwa kwa dhahabu au fedha,na hutegemea thamani yake kwenye nguvu ya "Usafishaji wa Jumla ambao umewekwa na kanuni,na wala haina thamani yoyote ya kibidhaa kwa dhati yake,na bali inategemea thamani yake kwa kanuni ambayo imeagiza/imepanga kuwa ni hela ya mzunguruko,lau kama itafutwa matumizi yake au watu wakakosa imani nayo inakuwa haina faida yoyote.

KUTOA/KUCHAPISHA HELA

Kila dola katika dola inafaa kuchukuwa umoja maalum,kutokana na kitu maalum,na kukifanya ni msingi ambao hunasibishwa kwa hicho vitu vingine na juhudi,na hupimiwa juu yake,na kuvifua katika umbile maalum,na mfumo maalum,kwa kipimo na kiwango maalum,na zimepita jamii toka zamani kwa kuweka umoja huu wa kipimo katika vitu ambavyo vina thamani ya dhati katika ulimwengu wote,wakaweka dhahabu na fedha kuwa kipimo hunasibishwa kwake bidhaa zote na juhudi,lakini dhahabu na fedha zina thamani ya dhati katika ulimwengu wote,na wakafua kutokana navyo vipande vya hela kwa umbile maalum,na mfumo maalum kwa uzito na kiwango maalum.

Hakika dola ambayo inachukuwa umoja wa dhahabu,au fedha kuwa ndio msingi wa hela yake,(dola hiyo) inakuwa inakwenda katika msingi wa madini,ikiwa itaweka umoja wa dhahabu kuwa ndio msingi wa hela yake ambayo inaifua kuwa hela yake inakuwa inakwenda juu ya kanuni ya dhahabu,au juu ya mfumo wa dhahabu,na ikiwa itaweka umoja wa fedha ndio misingi wa hela yake ambayo unaifua

inakuwa inakwenda juu ya msingi wa kanuni ya fedha,au juu ya mfumo wa fedha, na itaweka umoja wa dhahabu na umoja wa fedha –pembezoni kwa pembezoni – kuwa ndio msingi wa hela yake ambayo unaifua kuwa hela yake,inakuwa inakwenda juu ya kanuni ya dhahabu na fedha au juu ya mfumo wa madini aina mbili.

Ama dola ambayo inachukuwa hela yake ya kuzunguruka katika bidhaa na juhudi,hakika inakuwa inakwenda katika mfumo wa hela za karatasi,ikiwa karatasi ambayo inaichapa,na kuifanya ni hela yake niaba ya dhahabu au fedha,dola inakuwa inakwenda juu ya mfumo wa hela za karatasi zilizoniaba,na ikiwa karatasi ambazo inazichapa na kuzifanya ni hela yake,na zina kifuniko(Utepe) wa dhahabu au wa fedha unalingana na kiwango maalum katika thamani yake,inakuwa inakwenda juu ya mfumo wa hela za karatasi za aina ya hati.

Ama ikiwa karatasi ambayo inaichapa na kuitoa na kuifanya na hela yake sio niaba ya dhahabu au fedha na wala haina kifuniko chochote cha dhahabu au fedha,inatatambuliwa dola hii inakwenda katika muundo wa hela za karatasi za Maamuzi(Kijilazimisha)

Kwa hakika dola ya kirumi ilichukuwa umoja uliothibiti wa dhahabu ulipangwa uzito na kiwango kuwa ndio msingi wa hela yake,na ikafua kwa msingi huu vipande vya dhahabu kwa maumbile maalum,na mfumo maalum iliochora kwa michoro maalum,na ikafanya vipande hivi vya dhahabu vilivyofuliwa ni hela yake,ukaiingiza katika mzunguruko,kwa ajili hii ilikuwa imechukuwa msingi wa dhahabu katika kutoa hela yake , na ikaendea humo katika mfumo wa vilivyofuliwa vya dhahabu.

Ama dola ya Sasaniyah hakika hiyo ilichukuwa umoja wa fedha kuwa msingi wa hela yake na ukaifanya katika vipimo vitatu,na ikafua juu ya misingi huu Dirham( hela) za fedha zikiwa katika maumbile maalum,na mfumo maalum ilizozichora kwa michoro maalum,na ikaweka vipande hivi vilivyofuliwa kuwa ni hela yake ilioiingiza katika

mzunguruko,ikawa kwa ajili hii imechukuwa msingi wa fedha na ikaenda juu ya msingi wa vilivyofuliwa vya fedha.
Ama waislamu,hakika wao walichukuwa umoja wa dhahabu na umoja wa fedha kuwa ndio msingi wa hela yao,wakazitumia pamoja pembeni kwa pembeni,isipokuwa wao walikuwa wanachukuwa Dinar za Kirumi na Dirham za Kifursi(Kaisariyah) kuwa ndio hela zao,na wala hawakufua hela zao maalum,toka siku za Mtume (S.a.w) na Makhalifah baada yake,mpaka siku za Abdulmalik Bin Marwan.
Katika wakati wake alichapisha Abdul malik hela maalum za Kiislam,aliziweka juu ya umbile maalum,na mfumo maalum,alizichora kwa michoro maalum ya kiislam,na akaziweka zimesimama juu ya msingi wa dhahabu na msingi wa fedha,kwa uzito wa Dinar na Dirham za kisheria,kwa ajili hii wanakuwa waislamu wameenda juu ya msingi wa dhahabu na fedha,yaani juu ya msingi wa madini aina mbili.
Na Mwishoni wa siku za Abbasiyah na siku za Azabikah katika Misri,walifua waislamu pembezoni mwa Dhahabu na Fedha (Ilifua)hela za Shaba kwa ajili ya kununua vitu vidogo vidogo kwa kuzingatia kuwa thamani ya Shaba kwa dhati ni dogo,na wala hazikuwa ni niaba ya dhahabu na fedha,na bila shaka zimekuwa zikisimama kwa dhati yake zikitegemea juu ya thamani yake kama shaba,kwa sababu ilikuwa ni ya kununua vitu vidogo vidogo (Visivyokuwa na Maana) isipokuwa pale wakati dhahabu na fedha zilipokuwa chacha katika zama za Atabikah,wakawa wananunua kwa hiyo (Shaba) bidhaa zote vikubwa na vidogo.
Na ulimwengu uliendelea kwenda juu ya msingi wa dhahabu na fedha juu ya msingi wa vilivyofuliwa mpaka mwishoni mwa karne ya Ishirini,na kila dola ikifua hela zake za dhahabu,au za fedha kwa maumbile na mfumo maalum kwa ajili yake,kwa uzito na viwango vilivyothibiti na vilivyopangwa,mpaka pale dola kubwa za kikoloni jirani na vita vya dunia vya mwanzo pale zilipoachana na msingi wa dhahabu na fedha ,na zikachukuwa karatasi za hela za za Maamuzi(Kijilazimisha) kuwa ndio hela zake.

Huu ndio wakia (Hali halisi) ya utoaji wa hela,na ndio wakia ambao kwao walipita waislam juu yake ,katika kuchukuwa hela na kuzitoa ,na wakia wa hukmu ya kisheria wa kuzitoa (Kuchapisha ).

Na juu ya haya,ni wajibu wa waislam ziwe hela zao ni za dhahabu na fedha,na ni juu ya dola ya Khilafah ifanye hela zake ni dhahabu na fedha,na iende juu ya msingi wa dhahabu na fedha,yaani msingi wa madini ya aina mbili,kama ilivyokuwa siku za Mtume (S.a.w),na Makhalifah baada yake.na ni wajibu juu yake ifue Dinar za dhahabu na Dirham za Fedha na izifue kutokana na mada ya dhahabu na fedha khalisi yenye kiwango cha juu,na ifanye Dinar na Dirham zikiwa katika umbile maalum na mfumo hasa maalum wa kiislam katika dola ya Khilafah.

Na ifanye uzito wa Dinar ya dhahabu ndio uzito wa dinar ya kisheria,yaani uzito wa Mithqal,ifue dinar kwa uzito wa gram 4.25 kwa dinar moja,ambao ndio uzito wa Mithqal,na ifanye uzito wa dirham ya fedha ndio uzito wa dirham ya kisheria ambao hutamkwa kuwa ni uzito wa saba,yaani kila dirham kumi katika hizo ni sawa na uzito wa Mithqal saba,ifue dirham kwa uzito wa Gram 2.975 kwa dirham moja.

Na Dola inaweza kufua Dinar za dhahabu na sehemu zake na nyongeza zake kwa sura ifuatayo :-

| ALMAKUKAT-VILIVYOFULIWA | | UZITO WAKE KWA GRAM | |
|---|---|---|---|
| NA | | GRAM | |
| 1 | ROBO DINAR | 1,0625 | NA NDIO AMBAO HUKATWA KWAO MKONO WA MWIZI |
| 2. | NUSU DINAR | 2,125 | NA NDIO KIWANGO CHA WAJIBU KATIKA NISABU YA ZAKA |
| 3. | DINAR | 4,25 | |
| 4. | DINAR TANO | 21,25 | NAZO NI ROBO YA NISABU YA ZAKA. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 5. | DINAR KUMI | 42,5 | NA NDIO NUSU YA NISABU YA ZAKA. |
| 6. | DINAR ISHIRINI | 85 | NANDIO NISABU YA ZAKA. |

Na kwa Mchoro huu dola itakuwa imefua vipande kwa uzito wa Nisabu ya dhahabu,na vipande kwa uzito wa Dinar ambayo ndio msingi wa uzito wa dhahabu,na kipande kwa uzito wa nusu dinar na ndio kiwango cha wajibu katika nisabu ya zaka,na kipande kwa robo Dinar na ndio kiwango ambacho hukwatwa humu mkono wa mwizi.

Kama vile ambavyo dola inaweza kufua Dirham za Fedha na vipande vyake na ziada yake kwa sura (Muundo )ufuatao :-

| ALMAKUKAT-VILIVYOFULIWA | | UZITO WAKE KWA GRAM | |
|---|---|---|---|
| NA | | GRAM | |
| 1 | NUSU DIRHAM | 1,4875 | |
| 2. | DIRHAM MOJA | 2,975 | |
| 3. | DIRHAM TANO | 14,675 | NA NDIO KIWANGO CHA WAJIBU KATIKA NISABU YA FEDHA. |
| 4. | DIRHAM KUMI | 29,75 | |
| 5. | DIRHAM ISHIRINI | 59,50 | |

Kama vile dola itasimamia kufua umoja mdogo mdogo kuliko huo,miongoni mwa fedha,ili kuwepesisha kupata juu ya vitu vidogo vidogo (Visivyokuwa na maana) na kwa kuzingatia kuwa mjumuiko wa umoja huu kunatokana na fedha basi uwe mdogo,na ni vigumu kuamiliana navyo kwa kuzingatia kuwa ni vilivyofuliwa vikiwa safi huongezwa ndani yake sehemu maalum ya madini yasiokuwa na thamani,na kwamba ibainishe kiwango cha fedha ,katika umoja uliofuliwa,kwa namna ya kuzuia ubabaishaji wowote ule ndani yake.

Na ni wajibu kwa dola ya Khilafah ifanye kazi ya kuurejesha Ulimwengu kuamiliana kwa Dhahabu na Fedha mpaka Dola ya

Marekani,(Dola ya Khilafah) iwe ni yenye udhibiti katika hela Ulimwenguni iichezee (Iendeshe ) kwa mujibu wa Maslahi yake.

**<u>KIWANGO CHA DHAHABU NA FEDHA</u>**

Dola ya Kiislamu katika zama zake tofauti tofauti ilikuwa ikihifadhikiwango cha dhahabu na fedha ili ibakie khalisi haina mapungufu yoyote,na ilikuwa ikichunga isafishwe usafi uliotimia,mpaka iwe na kiwango cha hali ya juu,na ilikuwa ikizuia ghishi na hadaa yoyote katika dhahabu na fedha,na ikiweka adhabu kali kwa yeyote Yule anayefanya ghishi katika Dinar au Dirham.

Kwa sababu hii ni wajibu ziwe Dinar na Dirham ziwe khalisi pasina kuchanganywa na madini mengine yeyote yale,na ni wajibu izuiliwe kuzighushi,na pawekwe adhabu kali kwa kila anaichanganya na madini mengine,kwa sababu hiyo ni ghishi,na ghishi ni haramu.

Amesema Mtume (S.a.w) :

**"ليس منا من غش"**

“Si katika sisi yeyote mwenye kutuanyia Ghishi” ameipokea Abu daud na Ibn majah.

Na amepokea Muslim na Tirmidhiy :-

**"من غشنا فليس منا".**

“Yeyote Mwenye Kutufanyia Ghishi si katika sisi”

**<u>UPANDE DHAHABU NA FEDHA</u>**

Ni wajibu kwa Dola ya Khilafah iache huru upande wa kubadilisha dhahabu na fedha pasina kuweka kiwango,basi ibadilishwe dhahabu kwa fedha,na fedha kwa dhahabu kwa kiwango kinachotembea sokoni kwa mujibu wa kilivyowekwa na kinavyohitajika,kama ilivyokuwa hali hii siku za Mtume (S.a.w) na Makhalifah baada yake.

Mtume (S.a.w) Hakupanga kiwango maalum kati ya dhahabu na fedha,na wala hakupanga kiwango maalum cha kubadili ,isipokuwa aliwaachia waislam wauze fedha kwa dhahabu,na dhahabu kwa fedha kwa kiasi watakacho,mkono kwa mkono pasina kupanga kiwango maalum baina yake.

قال صلى الله عليه وسلم: "بيعوا الذهب بالفضة كيف شئتم يداً بيد"

Amesema Mtume (S.a.w) "Uzeni dhahabu kwa fedha kiasi mtakacho mkono kwa mkono" kaipokea Tirmidhiy.

وعن ابن عمر قال: "كنت أبيع الإبل بالبقيع، فأبيع بالدنانير، وآخذ الدراهم، وأبيع بالدراهم وآخذ الدنانير، آخذ هذه من هذه، وأعطي هذه من هذه، فأتيت النبي صلى الله عليه وسلم وهو في بيت حفصة، فقلت: يا رسول الله رويدك أسألك، إنّي أبيع الإبل بالبقيع، فأبيع بالدنانير، وآخذ الدراهم، وأبيع بالدراهم وآخذ الدنانير، آخذ هذه من هذه، وأعطي هذه من هذه، فقال رسول الله صلى الله عليه وسلم: "لا بأس أن تأخذها بسعر يومها ما لم تفترقا وبينكما شيء".

Toka kwa Ibn Omar amesema : "Nilikuwa nauza ngamia katika eneo la Baqii,nauza kwa Dinar na nachukuwa Dirham,na nauza kwa Dirham na nachukuwa Dinar,nachukuwa hizi kwa hizi,na natoa hizi kwa hizi,nikamuendea Mtume (S.a.w)naye yuko nyumbani kwa Hafsah nakasema :Ewe Mtume wa Mwenyezi Mungu Mimi nauza ngamia katika eneo la Baqii, nauza kwa Dinar na nachukuwa Dirham,na nauza kwa Dirham na nachukuwa Dinar,nachukuwa hizi kwa hizi,na natoa hizi kwa hizi,akasema Mtume wa Mwenyezi Mungu "Hakuna ubaya uzichuku kwa bei ya siku yake hiyo,muda wa kuwa hamjaachana na kati yenu kuna kitu" kaipokea Abu Daud.

Na hii si kuuza dhahabu kwa dhahabu ,na fedha kwa feedha,kuuza huku ni wajibu humu viwe sawa sawa **"Sawa kwa sawa" "Mkono kwa Mkono"**

قال صلى الله عليه وسلم: "الذهب بالذهب والفضة بالفضة والبُرُّ بالبُرّ، والشعير بالشعير، والتمر بالتمر، والملح بالملح، مِثلاً بمِثل، يداً بيد، فمن زاد أو استزاد فقد أربى، الآخذ والمعطي فيه سواء" رواه مسلم.

Amesema Mtume (S.a.w) "Dhahabu kwa Dhahabu na fedha kwa fedha,na Ngano kwa ngano,na Shairi kwa Shairi,na tende kwa tende,na chumvi kwa chumvi,sawa kwa sawa,mkono kwa mkono,basi yeyote mwenye kuzidisha au kutaka azidishiwe kwa hakika amefanya(amekula ) riba,mwenye kuchukuwa na mwenye kutoa wako sawa (Katika madhambi)kaipokea Muslim.

Na kiwango cha dhahabu kwa fedha ni chenye kubadilika na si chenye kuthibiti,na kinasimamia kwa upatikanaji kwa

wingi wa dhahabu na fedha na uchache wake,na kwa kuwekwa sokoni na kutafutwa (Kuhitajika).

Na kilikuwa kiwango katika siku za Mtume (S.a.w) ni kiasi cha 1:10,na siku za Omar 1:12,kisha 1:14,na kilikuwa mwaka 1981 kimefikia 1:45,kisha baada ya hapo katika ndani ya miezi michache kilifikia 1:16,kiwango baina yake si chenye kuthibiti.

Kwa sababu hiyo basi kupanga kiwango maalum cha kubadili na chenye kuthibiti kati ya dhahabu na fedha ndani yake kuna madhara,kwa sababu vyote kati ya dhahabu na fedha – ikiwa vitapangiwa bei ya kubadili kwa kiwango cha kanuni –itakuwa katika hatari ya kutofautiana kiwango chake kikanuni.na kiwango cha sokoni,ikiwa kutatokea tofauti hii ndani ya Dola,au katika masoko ya nje,hali hii itapelekea kufichika hela ambayo bei yake imepanda na kutoroshwa nje ya nchi,ikiwa thamani yake ya sokoni nje ya nchi ni kubwa kuliko thamani yake kikanuni ndani ya nchi.

**<u>FAIDA ZA MFUMO WA DHAHABU NA FEDHA</u>**

Wakati ilipokuwa dhahabu na fedha ndio hela inaozunguruka katika ulimwengu hapakuwa na matatizo ya hela hata kidogo ulimwenguni,na matatizo ya hela hayakutoa isipokuwa baada ya ulimwengu kuachana na mfumo wa dhahabu na fedha,wakati dola za kikoloni zilipochezea mifumo ya kikoloni ya ucheumi na kimali ili kumakinika kuutawala ulimwengu,wakatumia hela kuwa ni njia katika njia kikolono,na wakaachana na kanuni ya dhahabu na fedha,na wakageuza hela kwenda katika mifumo mingine,wakizingatia humo wadia(zilizohifadhiwa) vya kubalisha,na hela za kijilazinisha (kujitungia) ambazo hazitegemei dhahabu au fedha katika kiwango cha hela, wakawa wanaichezea hela ya ulimwengu kwa kulingana na maslahi yao,na wakatengeneza migongano ya hela na wakaleta matatizo ya kiuchumi,na wakazidisha kuchapisha hela za kujitungia,hali ambayo ilileta mfumko mkubwa katika hela,na ikapelekea kuporomoka nguvu ya kununua kwa hela na hayakuwa hayo isipokuwa ni matokeo ya kuachana na kanuni ya dhahabu na fedha.

Na kanuni ya dhahabu na fedha ndio pekee yenye uwezo wa kutatua matatizo haya ya hela,na juu ya mfumko huu mkubwa ambao umeenea ulimwenguni,na kuleta utulivu wa hela na kuthibiti kwa bei ya ubadilishaji,na kupatikana maendeleo katika biashara za kimataifa.
Hivyo ni kwa sababu mfumo wa dhahabu na fedha umebeba sifa za kiuchumi nyingi,na miongoni mwazo ni hizi :-

1- Hakika kule kuwa dhahabu na fedha ni bidhaa inayodhibiti katika uzalishaji wake wa kilimwengu gharama za kuichimba na kuitafuta,na kuitafuta kunalingana na kutafuta bidhaa nyingine na huduma,kunafanya kuupatia ulimwengu hela hakupo chini ya dola za kikoloni,kama ilivyo katika mfumo ya hela ya karatasi,ambao dola zinaweza kuweka sokoni hela itakazo kwanjia ya kuzichapisha kwa ziada kila mara zinapotaka kuboresha kipimo cha hela yake na malipo pamoja na dola nyingine.

2- Hakika mufumo wa dhahabu na fedha hautokei kwa ghafla kwa kuzidisha kila kinachozunguruka,kama inavyotokea katika hela ya karatasi,kwa sababu hii hela itakuwa na sifa ya kuthibiti na kutulia,na utazidi uaminifu katika hela hiyo.

3- Hakika mfumo wa dhahabu na fedha inakusanya juu ya kipimo (Mizani ) ya kurekebisha kasoro katika malipo ya dola baina yake pasina kuingiliwa na Benk kuu,kama kuingilia kunakopatikana hivi sasa,kila mara inapovurugika bei kubadili baina ya hela za dola mbali mbali,hakika ziada ya vinavyoingia (mapato) dhidi ya vinatoka kitazidisha mapato ya dola nyingine kutokana na hela ya dola,na itazidisha kutoka dhahabu na fedha nje,na kinachofuata hapo ni kupunguwa kwa bei ndani ya

nchi,kitu ambacho kitazifanya bidhaa za ndani ni rahisi kuliko zinazoletwa kitu ambacho mwishiwe kitapunguza uagizaji.zaidi ya hayo dola itahofia kukosa akiba yake ya dhahabu na fedha,ikiwa itaendelea kuwepo kasoro katika kiwango cha malipo,baina katika kivuli cha mfumo wa karatasi dola huelekea kuzidisha kuchapisha hela kila mara panapotokea mapungufu katika akiba ya malipo(matumizi) kwa sababu hakuna masharti juu ya kuzitoa kwake,jambo ambalo litasababisha kuzidi kwa mfumko,na kuporomoka kwa nguvu za kununua kwa hela.ama mfumo wa dhahabu na fedha kwa hakika dola haiwezi kufanya wasaa katika kutoa karatasi za hela,muda wa kuwa hela inaweza kubadilishwa kwa dhahabu na fedha kwa bei maalum,kwa sababu dola inachelea na kukhofia ikiwa itazidisha katika kutoa hela patazidi hitajio la dhahabu,basi itashindwa kukabiliana na mahitaja haya,au itatolewa nje na itapoteza akiba yake.

4- Hakika kule kuwa dhahabu ni umoja wa hela haudhibitiwi na Dola kunaifanya inakuwa na sifa kubwa kwa kiasi kwamba hakika ya kiwango yaani cha hela katika dola kinatosha yale yanayohitajika sokoni katika mabadilisho yah la,pasina kutazama kule kuwa kwake ni kubwa au kidogo ,kiasi kwamba bidhaa zote zinachukuwa bei ya kubadilisha pamoja nayo.na patazidi uzalishaji katika bidhaa nyingine,na bei zitapungua,baina katika mfumo wa karatasi haipelekei kuzidi hela katika hilo,bali hupelekea kupungua thamani ya kununua katika hela,hali ambayo hupelekea mufumko.na kwa haya inabainika kwamba mfumo wa dhahabu na fedha ndio mfumo unaomaliza tatizo la mfumko,bali mfumo wa karatasi huzidisha makali yake.

5- Hakika mfumo wa dhahabu na fedha unasifika kwa kuwa bei ya kubadilisha hela za dola mbali mbali ni yenye kuthibiti,kiasi kwamba kila hela katika hizo zimekadiriwa kwa kiwango cha umoja maalum katika dhahabu au fedha,kwa sababu hii hakika ulimwengu wote utakuwa una hela moja katika uhakika miongoni mwa dhahabu au fadha kwa vyovyote vile itakavyotofautiana,na ulimwengu wakati huo utapata uhuru wa kibiashara,na kuhama bidhaa na mali baina ya dola mbali mbali ulimwenguni,na utaondoka ugumu wa vipande na hela za nadira,miongoni mwa mambo yatakayopelekea juu yake kuebdelea katika biashara ya kimataifa,kwa sababu wafanya biashara hawachelei kupanua katika biashara za nje,kwa sababu bei ya kubadilisha imethibiti.

6- Hakika mfumo wa dhahabu na fedha unahifadhi kwa kila dola uchumi(Utajiri) wake wa dhahabu na fedha,hakutopatikana kutoroshwa dhahabu na fedha,toka mji mmoja hadi mwingin,na wala dola haitahitaji uchungaji wowote kwa ajili ya kuhifadhi dhahabu yake na fedha zake kwa sababu hazitohama toka kwake isipokuwa thamani ya bidhaa au malipo ya wafanya kazi.

Na faida zote hizi zinapatikana katika mfumo wa madini moja ya dhahabu au fedha,na katika mfumo wamadini aina mbili ya dhahabu na fedha,na huzidishwa hapo kwamba mfumo wa madini aina mbili huzidisha katika ukubwa wa kanuni ya kimadini,hali ambao hupelekea juu yake kuwa mtazamo wa kiujumla wa hela ni mkubwa,na hiyo huiwezesha dola kupokea haja za watu za hela kwa wepesi na urahisi,hali ambayo huleta uwepesishaji mwingi,na kufanya nguvu ya kununua kwa umoja wa hela na kiwango cha bei kinaelekea kwenye daraja kubwa ya kuthibiti.

Hizi ni sifa na faida za kanuni ya dhahabu na fedha,nazo haziepukani na matatizo ,kutokana na matokeo ya ulimbikizaji wa kimataifa,na kupatiakana vikwazo vya kastam,na kuhifadhiwa kiwango kikubwa cha dhahabu na fedha katika hazina za dla kubwa na dola ambazo uwezo wake umezidi uzalishaji,na uwezo wake juu ya kushindana katika biashara za kimataifa,au kuchipukia kwake kwa wanazuoni na wataalamu na Mainjinia,na kuchukua mfumo wa hela ya karatasi za kujilazimisha badala ya dhahabu na fedha.

Na ili dola ambazo zinatumia kanuni ya dhahabu na fedha ziweze kuvuka vikwazo hivi,na matatizo haya – khasa pindi zikibakia dola kubwa za ulimwengu na dola ambazo zina athari katika biashara ya kimataifa zikienda kwa msingi usio kuwa wa dhahabu na fedha – basi ni juu yake ziende juu ya siasa ya kujitosheleza kidhati,ipunguze uagizaji na ifanye juu ya kubadilishana bidhaa ambazo inaziagiza kwa bidhaa zilizopo nchini kwake,si kwa dhahabu,na wala si kwa fedha,kama vile ambavyo ni juu yake ifanye kazi ya kuuza bidhaa zilizopo kwake kwa bidhaa inazozihitaji kwake,au kwa dhahabu na fedha,au kwa hela ambayo ina haja nazo kwa kuagiza vile inavyovihitaji katika bidhaa na huduma.

Na zaidi ya hayo ni juu ya dola ambayo inakwenda kwa kanuni ya madini aina mbili – dhahabu na fedha –ijiepushe na kupanga bei ya kubadili iliothibiti kati ya umoja wa dhahabu na umoja wa fedha,na ni juu yake iache huru bei ya kubadili ,ifuate kugeuka kwa bei kwenyewe, kwa sababu kupanga bei ya kubadiki kumethibiti kati ya umoja wa aina mbili na itapelekea juu yake kufichika umoja wa hela ambazo thamani yake imepanda sokoni juu ya kima (Thamani) yake kikanuni katika mzunguruko,na kubakia umoja wa hela ulio mwepesi,kwa sababu hela rahisi inafukuza hela nzuri katika mzunguruko.

**<u>KUTOSHELEZA KWA DHAHABU ILIOPO ULIMWENGUNI</u>**

Hakika mfumo wa dhahabu ndio mfumo wenye kufaa kuzuia serikali kuzalisha kiwango kikubwa cha hela za karatasi bila kuwepo mlinzi,na ambao unapelekea kuleta mfumko,na mfumo

wa dhahabu unaleta umoja uliothubiti katika kuamiliana kimataifa,jamba ambalo litahamisisha biashara ya kimataifa.

Lakini je dhahabu iliopo hivi sasa ulimwenguni inatosha kuurejesha ulimwengu katika kwenda kutumia kanuni ya dhahabu kama ilivyokuwa zama zilizopitwa ?

Na je inatosha kutoa yale ya lazima katika hela kwa ajili ya miamala ya kibiashara ?

Na Je dola ya khilafah inayo dhahabu ya kuiwezesha kurudi katika kanuni ya dhahabu ?

Na kwa kujibu juu ya maswali haya tunasema : ndio,hakika dhahabu iliopo katika ulimwengu inatosha kuurejesha ulimwengu kwenda juu ya msingi wa dhahabu,na kuna wepesi wa kutosha kutoa yale ya lazima katika hela kufunika(kukidhi) miamala ya kibiashara,na haja za kiuchumi katika ulimwengu,nayo ni kwa sababu zifuatazo :-

1- Kupitia historia ya Mwanaadamu,hayakupata hadhi madini miongoni mwa madini kama ilivyopata hadhi dhahabu ya kushughulikuwa,dhahabu alioitoa mwanaadamu haijaacha kuwa inatumika mpaka leo ,pamoja kwamba imetilewa kabla ya maelf ya miaka,kiasi kwamaba kile kinachotolewa hakimalizwi ule umalizaji ambao utakifanya kikosekane kabisa,bali ilikuwa yale yanayopatikana ni kuibadilisha ima kwa sura ya hela au mapambo,na ima kuingizwa katika kutengenezwa au kuirejesha [إعادة صهره.]

2- Hakika dhahabu katika zama zote zilizopita,mpaka mwishoni mwa karne ya kumi na tisa,ilikuwa ikitosheleza kwa kazi zote za kibiashara,na kukidhi haja zote za kiuchumi katika ulimwengu kwa zama tofauti tofauti pasina kutokea matatizo ya kiuchumi au kimali.na katika kipindi cha karne ya kumi na tisa ambao ilizidi kukuwa kwa uchumi kwa daraja kubwa,ulimwengu ulishuhudia kukuwa na kung'ara

kukubwa kwa uchumi na kupungua kwa bei ,na kuzidi katika malipo(Mishahara) pasina kuhitajia kiwango kikubwa cha hela za dhahabu zilizopo,pamoja na kuzidi kwa bidhaa na huduma.

3- Hakika kilicho muhimu kwa watu sio wingi wa hela kwa hakika,bali uwezo wake wa kununua,na ulikuwa uwezo wa umoja wa dhahabu wa kununua ni mkubwa,na umeleta kuthibiti na kutulia,na ukasababisha wepesi na kung'ara,kwa upande mwingine ilikuwa kuzidisha katika kuchapisha hela za karatasi zisizokuwa za niaba (Ya dhahabu na fedha)ni sababu ya haya matatizo ulimwenguni,miongoni mwa matatizo ya kiuchumi,na mfumko wa mali(Bidhaa) na mfumko ukazidi jambo ambalo limepelekea kupungua thamani ya kununua kwa hela za karatasi.

4- Hakika mfumo wa uchumi ambao hauna ndani yake masharti kama vile kupanga bei,au kulimbikiza,si muhimu humo kiwango cha hela zilizopo humo,kiasi chamba kiwango chochote cha hela kinachozunguruka kitakuwa kinafaa kununua bidhaa na huduma zilizopo sokoni.wakati bidhaa na huduma zilizopo zinapozidi,pamoja na kuthibiti kiwango cha hela inayozunguruka,kwa hakika hili litapelekea kufanya umoja wa hela ni wenye uwezo juu ya kununua kiwango kikubwa cha bidhaa na huduma,na kinyume ni sahihi,yaani pindi kiwango cha bidhaa na huduma kitakapokuwa kichache pamoja na kuthbiti kiwango cha hela,hakika umoja wa hela uwezo wake utakuwa mchache juu ya kununua bidhaa na huduma,na vyovyote vile jambo litakavyokuwa,hakika hela

inayozunguruka itakuwa inatosha katika mzunguruko wa hela kwa vyovyote kitakavyokuwa kiwango chake chenye kuzunguruka.

5- Hakika yale yanayoonekana miongoni mwa upungufu wa dhahabu katika dhahiri bila shaka hayo ni matokeo ya mfumko ulioenea ulimwenguni,na lau kama ulimwengu utarudi katika mfumo wa dhahabu basi ungerudi katika bei ya hela,kitu ambacho kitafanya matumizi makubwa ya dhahabu kupungua,kiasi kwamba dhahabu haitatumika kwa ajili ya Mikopo (Mudharaba-ushirika)ya kibiashara wakati huo,na yote itaelekezwa katika kazi za kibiashara,na haja za kuichumi,kwa sababu kazi za kibiashara ni kwa dhahabu na mikopo(Mudharaba-Ushirika) ni kwa hiyo,itasimama kwa kuwa bei za hela zitapata utulivu,kwa sababu bei ya hela,na kiwango cha baadhi yake kwa baadhi itapangwa kwa dhahabu,kitu ambacho kitafanya hela zote ulimwenguni kana kwamba ni hela moja,na katika yanayopelekea kutokuwezekana kufanya Mudharaba kwa hela hiyo ,na uchache wa faida katika kufanya biashara kwa dhahabu,kwa sababu hii dhahabu itakuwepo kwa wingi,na yatafikichikana yale yaliokuwa yanaonekana kuwa kuna upungufu kwa nje.

6- Sababu hizi zote inabainika kuwa ulimwengu unaweza kurudi kwenye kanuni ya dhahabu,na kwamba inawezekana kwa dhahabu iliopo ulimwenguni kutosheleza haja za hela,na kukidhi kazi za kibiashara,na kutosheleza mali ya lazima kwa haja za kiuchumi.

Ama dola ya khilafah hakika yanayotokea kwake ndio hay ohayo yanayotokea katika dola nyingine,na kwa hakika sababu ambazo zimetajwa katika hayo yaliopita zinabainisha kwamba kwa uwezo wake inaweza kurudi katika kanuni ya dhahabu,na hakika dhahabu iliopo katika miji ya kiislamu na ile iliohifadhiwa katika mabenk na kwenye hazina,humo mna kiwango cha kutosha cha kuiwezesha dola ya Khilafah kurudi kwenye kanuni ya dhahabu.zaidi ya haya kuna kiwango kikubwa cha fedha kilichopo katika miji ya kiislam,( Na ambacho kitakuwa ni umoja wa msingi katika hela ya dola ya Khilafah pamoja na umoja wa dhahabu,kwa sababu dola ya Khilafah inasimama juu ya msingi wa kanuni ya dhahabu na fedha,na juu ya mfumo wa madini ya aina mbili kwa upande wa hela) zikiwepo kwa kiwango kikubwa kitu ambacho kitafanya wepesi kwa dola ya khilafah kurudi katika kanuni ya dhahabu na fedha.

Na zaidi ya hayo,kwa hakika miji ya kiisalam ina mali ghafi nyingi ambazo zinaulazimu uma na dola ya Khilafah uzipate,kitu ambacho kinaufanya hauna haja ya bidhaa nyingine kama hitajio la msingi,au hitajio la dharura,kwa sababu hii inaitosheleza dola ya Khilafah kwa bidhaa zake za ndani pasina kuagiza bidhaa nje ya nchi,kitu ambacho kitafanya dhahahu ilotolewa nje (Kuchimbwa)kwa wingi na kuendelea kubakia ndani ya nchi.

Kama vile ambavyo miji ya kiislamu inamiliki bidhaa muhimu kma vile Mafute(Petroli) inayohitajiwa na miji yote ulimwenguni,na dola ya Khilafaha inaweza kuiuza kwa dhahabu,au kwa bidhaa ambayo dola inahaja nayo,au kwa hela ambazo inazihitaji kuagizia vitu vya lazima miongoni mwa bidhaa na huduma,kama vile ambavyo inaweza kuzuia kuiuza kwa dola yotote ile mpaka ilipe kwa dhahabu na kuuza bidhaa kama hiyo kwa dhahabu.

Itaifanya dhahabu ielekee kwa wingi katika miji,kitu ambacho kitazidisha akiba ya dola ya Khilafah,kutosheka dola na kutokuhitaji kwa dola nyingine kwa bidhaa za ndani,na kumiliki kwake kwa bidhaa wanazozihitaji watu wote,na wanajiandaa kulipa thamani yake kwa dhahabu,kunaihifadhi dhahabu na kutoka kwenda nje pasina sababu nzuri yenye faida na kutazidisha kiwango cha dhahabu katika nchi,kwa sababu hii itaweza kuwa ni yenye athari,na kudhibiti soko hela la kimataifa na kumzuia yeyote kudhibiti hela yake.

Na kwa haya inabainika kwa uwazi wote kwamba Dola ya Khilafah inaweza kurudi kwenye kanuni ya dhahabu na fedha,na kwamba dhahabu iliopo katika miji ya Kiislamu inatosha katika kurudi huku,kama vile ambavyo inatosha kuweka hela za lazima.

## VIPI INATIMIA KUREJEA KWENYE KANUNI YA DHAHABU

**Kwa ajili ya kurejea kwenye kanuni ya dhahabu ni wajibu kuondoa sababu ambazo zimpekea kuacha kutumika kwake,na kuondoa mambo yote yaliopelekea kuporomoka kwak,yaani pafanywe yafuatayo:-**

**1- Kusimamisha uchapishaji wa hela za Karatasi.**

**2- Kuzirejesha hela za dhahabu katika kuamiliana.**

**3- Kuzuia vikwaz vya kastani mbele ya dhahabu,na kuondoa vikwazo vyote vya kuingiza na kusafirisha.**

**4- Kuondoa vikwazo juu kumiliki dhahabu,kuichukuwa,na kuinunua na kuiuza ,na kuamiliana nayo katika mikataba (Ya kibiashara)**

**5- Kuondoa vikwazo juu ya kumiliki hela za msingi katika ulimwengu,na kufanya ushindani huru,mpaka ichukue**

**bei ilithibiti yenyewe kwa upande wa baadhi yake ,na kwa upande dhahabu pasina kuingiliwa na dola kwa kupunguza hela zake au kuzieneza[ تعويمها ]**

**Na wakati wowote dhahabu itakapoachiwa huru basi kwa hakika itakuwa na soko lililofunguka katika kipindi cha muda mfupi,na kufuatia kwamba hela zote za kimataifa zitachukuwa bei cha kubadili iliothibiti kwa upande wa dhahabu,na utakuja kuwa utendaji wa kimataifa ni kwa njia ya dhahabu,na kwa njia yake patapitishwa kufunga mikataba mikubwa ya bidhaa ikikadiriwa thamani yake kwa dhahabu**

Hatua hizi pindi zikisiamamiwa na Dola yenye nguvu,itapelekea kufaulu kwake (na) kuzihamishisha dola nyingine kuzifauta katika hili,hali ambayo itapelekea kuendelea mfumo wa dhahabu ulimwenguni mara nyingine.

Na hakuna dola yenye Umuhimu kuliko dola ya Khilafah ya kulismimamia hili kwa sababu kurudi kwenye Msingi wa Dhahabu na Fedha ni hukmu ya Kisheria kwa upande wake,na Kwa sababu dola ya Khilafah ina jukumu kubwa (Mas'ulah) ulimwenguni ,jukumu la Uongozi na Uchangaji.

Kimetimia kwa Msaada wake Mwenyezi Mungu Mtukufu siku ya Jumatano 19 ya Mwezi wa Rajabu pekee 1402 Hijria,inayonasibiana na 12/Ayari 1982 Miladi.

**Hapa ni mpaka page namba 233 [ 0205 2011]**